**7 MEI, 2026**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA TATU

**Kikao cha Ishirini na Nne – Tarehe 7 Mei, 2026**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tukae.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA: -**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**MHE. BARAKA A. U. MWAMENGO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo Kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni ya

Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI KWA WAZIRI MKUU

**SPIKA:** Maswali kwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Waziri Mkuu, karibu.

Mheshimiwa Agnesta Lambert Kaiza. *(Makofi)*

**MHE. AGNESTA L. KAIZA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwa mwuliza swali namba moja kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, ninampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya, kwa ajili ya kupeleka tabasamu kwa wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunatambua dhamira njema ya Serikali katika kuwaletea maendeleo wananchi, hasa kupitia ujenzi wa miradi mbalimbali ya kimkakati nchini, ikiwemo barabara, bandari, viwanda na viwanja vya ndege. Katika kufanikisha miradi hiyo, Serikali imekuwa ikitwaa maeneo mbalimbali kutoka kwa wananchi ili kufanikisha maendeleo haya. Baadhi ya maeneo ambayo Serikali imeyatwaa yapo Kipunguni, Jimbo ya Segerea, Kilwa, Mwanza Chato, Nachingwea na kwingineko.

Mheshimiwa Spika, maeneo haya wananchi hawajalipwa fidia kwa miaka mingi sana na jambo hili limesababisha adha kubwa sana, ambapo wananchi wanashindwa kuendelea na maisha yao mengine.

Mheshimiwa Spika, ni ipi kauli ya Serikali katika kutatua kero hii, kwa kuwalipa fidia zao wananchi hawa, ili hatimaye nao waweze

kuendelea na maisha mengine ikizingatiwa kwamba, hawajiendelezi katika maeneo hayo? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushuru kwa kunipa nafasi hii niweze kujibu swali la Mheshimiwa Agnesta Lambert. Ni kweli, kumekuwepo na utwaaji wa maeneo kwa ajili ya kutimiza malengo mapana ya Kitaifa kwa masilahi mapana ya Taifa letu, hasa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, jambo la kutwaa maeneo lipo kisheria. Kwa mujibu wa sheria yetu inayoongoza utwaaji wa maeneo, mwananchi anawajibika kuachia maeneo yake ya ardhi ili kuwezesha nchi kutekeleza miradi yenye masilahi mapana ya Kitaifa. Hata hivyo, sheria inayoongoza utwaaji wa maeneo inaelekeza kwamba, mwananchi mwenye eneo lake la ardhi analolimiliki kwa hati, ama umiliki wa asili, anapopisha miradi ya maendeleo anapaswa kulipwa fidia.

Mheshimiwa Spika, swali alilolileta Mheshimiwa Mbunge ni la msingi, na ametaja moja ya eneo la Kipunguni na maeneo mengine, kama alivyoyataja. Imetokea kwa muda mrefu takribani miaka 15 mpaka 20 hivi iliyopita, yamefanyika makosa hayo ya kutwaa maeneo bila kulipa fidia, ambapo yamelimbikiza mzigo mkubwa wa ulipaji wa fidia hizo, hasa maeneo ambayo tayari yamechukuliwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Serikali inachofanya, na kauli ya Serikali ni kwamba, Serikali itaendelea kuheshimu Sheria hiyo ya Utwaaji wa Maeneo kwa kulipa fidia kwa kila mwananchi, ambaye ameachia eneo lake la umiliki lenye hati, ama umiliki wa asili, kwa ajili ya kupisha mradi wa maendeleo wenye maslahi mapana kwa Taifa.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika miaka yake minne, mitano ya mwanzo amelipa fidia maeneo mengi sana ambayo yametwaliwa zamani, ikiwemo kule Liganga, Mchuchuma; ikiwemo kule Engaruka na maeneo ya

viwanja vya ndege. Hata hili la Kipunguni, deni lilikuwa kubwa sana, ninavyokumbuka litakuwa limelipwa linaelekea *halfway*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bado kuna hao wananchi wengine ambao Mheshimiwa Mbunge ameuliza. Ninakumbuka nimewahi kufika pale Kipunguni nikiwa Waziri wa Fedha, nikiwa nimetumwa na Mheshimiwa Rais, kwenda kujionea hali halisi, lakini pia, kuweza kuanza kutekeleza njia ya malipo, na imefanyika kwa kiwango kikubwa, lakini bado kuna sehemu ambayo haijalipwa. Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, Serikali itaendelea kulipa fidia za maeneo ambayo Serikali imeyatwaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utwaaji wa maeneo mengine umekuwa siyo tu kwa ajili ya miradi ya maendeleo, na hapo ndipo ambapo tatizo linapoanzia. Yapo maeneo ambayo yamechukuliwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, lakini bila kufuata utaratibu huu. Yapo maeneo ambayo nimepita hata kwenye ziara nimejionea, lakini yapo maeneo mengine ambayo siyo hata kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, inatokea pana mwananchi anamiliki eneo kihalali na hati anayo, anatokea mwananchi mwingine analitafuta eneo hilo kwa misingi ya uwekezaji ama biashara, anatuma viongozi wa Serikali kwamba, nichukulieni lile eneo ili niweze kutekeleza mradi na inaenda kutumika Sheria ile ya Utwaaji wa Maeneo kwa masilahi mapana ya Taifa. Hilo siyo sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama mwananchi ana miliki eneo lake kihalali na ana hati, siyo uungwana na siyo utaratibu wa kisheria kulitwaa bure ili umpe mwingine ambaye amelitamani eneo hilo. Kama umetamani eneo la mwananchi mwenzako na una shughuli nalo, nenda na fedha, lipia eneo ili na yeye aweze kuendelea na maisha yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukianzisha Kliniki ya Ardhi hapa, utakuta hata Wabunge, wapo ambao maeneo yao yametwaliwa kwa ajili ya kutekeleza shughuli nyingine na fidia bado haijalipwa. Sasa maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kwamba, mwananchi asinyang'anywe ardhi yake anayoimiliki kwa sababu yoyote ile.

Lazima alipwe fidia ili na yeye aweze kubadilisha maisha yake, aweze kupata utajiri kupitia urithi huo alionao ambao wengi wa Watanzania urithi wao ni ardhi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Mafuwe.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE**: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kumwuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni nchini Tanzania kumeibuka watu ambao hatuna hakika kama ni wataalamu, wanatoa elimu ya namna ya ulaji. Utasikia anasema, ili kupunguza kitambi kula hivi, kula hivi, bila kumjua yule anayempa ushauri ana uzito kiasi gani, ana urefu kiasi gani au anafanya shughuli gani? Kwa hiyo, wimbi limekuwa kubwa na wananchi wakati mwingine wanachanganyikiwa na hizi *theory* za ulaji.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali sasa ina mpango gani wa ku-*centralize* utoaji wa elimu kwa watu mahususi wenye taaluma hiyo ili kuondoa mkanganyiko ulioko kwenye jamii yetu sasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Ninatumia fursa hii kujibu swali la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumetokea wimbi kubwa la watoa elimu ya masuala ya lishe na afya. Hii ni kutokana na kukua kwa uelewa, pengine wa masuala ya afya. Kwa sasa tuna wataalamu wengi wanaojua masuala ya afya kutokana na kupanuka kwa elimu ya masuala ya afya kutoka kwenye vyuo vyetu. Kwa sasa ni kweli, wigo wa vyuo vyetu umeongezeka sana.

Mheshimiwa Spika, pili, ni kweli kumeongezeka wimbi hilo la kutoa elimu kwa sababu njia za kutoa elimu zimeongezeka. Zamani ilikuwa chombo cha habari rasmi, itakuwa ni *TV* au ni redio, ambayo ni rasmi. Sasa hivi kila mwananchi anaweza akatoa ujumbe wake pale

pale alipo kupitia mitandao ya kijamii. Kwa hiyo, huu ni wigo mwingine ulioongezeka tofauti na zamani, ambapo kulikuwa na madarasa rasmi, *TV* rasmi na redio rasmi ya Taifa. Sasa kuna njia hii ya mitandao ya kijamii ambako kuna majukwaa mengi, kuna kurasa nyingi ambazo mtu anaweza akatoa elimu yake.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, swali aliloleta Mheshimiwa Saashisha ni la msingi na ni jambo ambalo linatokea. Serikali itaendelea kusimamia sera, sheria, pamoja na miongozo inayohusu afya na masuala ya lishe, ili kuweza kulinda usalama. Kwanza, usahihi wa elimu inayotolewa, na pili, usalama wa wananchi wetu kufuatia kile ambacho kinatolewa kwenye mwongozo huo.

Mheshimiwa Spika, ninatambua tuna Sheria ya Afya, tuna Sera ya Afya, tuna Sera ya Masuala ya Lishe na tuna Miongozo, ambayo inasimamia masuala hayo ya lishe. Mbali na hilo, taaluma ya masuala ya kiafya inatawaliwa pia na mabaraza yanayozisimamia. Ninatumia fursa hii kuwaelekeza wenzetu wa Wizara ya Afya, pamoja na Mabaraza yale yanayosimamia Tasnia hizo za Taaluma ya Afya kuendelea kuzingatia, huku tukifanya tathmini kuhusu uwezekano wa kuratibu masuala ya leseni na vibali kuhusu watoa elimu hiyo ya afya na lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, anachokisema Mheshimiwa Mbunge ninaweza nikatolea mfano kidogo. Zamani Wanyiramba walikuwa wanataniwa kwamba ni watu wanaokula punda. Najua ulikuwa ni utani, na kama ni kula, ni kuonja kidogo. Ikaja ikatokea kwenye hawa watoa elimu waliokuja, sijui ni yupi, akasema kwamba, nyama ya punda inaepusha ugonjwa wa *gout* kwenye magoti.

Mheshimiwa Spika, ghafla tukasikia mnada wa nyama ya punda umejengwa kule kwa wenzetu Wanyaturu, Damankia. Hatujakaa sawa, tukasikia na Wairaq kule Manyara wanatafuta mnada wa nyama ya punda. Hatujakaa sawa, tukasikia Warangi huku Kondoa wanatafuta mnada wa nyama ya punda, na siyo ajabu ukakuta hata kwa Wagogo kuna mnada wa punda. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, la msingi ninalotaka kusisitiza ni kwamba hatuna uhakika kama kweli kile kilichosemwa kwamba ukila nyama ya punda inaepusha ama inatibu *gout*. Hatuna huo uhakika, lakini ndiyo hivyo, yule aliyetoa taarifa ile ameshawachongea punda wetu. Sasahivi ukitafuta punda kule ni shida kuwapata.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jambo aliloleta Mheshimiwa Mbunge, tutazingatia kusimamia miongozo ili taarifa inayotolewa iwe ni ya kweli na imethibitishwa kwamba ni ya kweli, na hakuna madhara kwa kile kilichoshauriwa. Ninakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Rebeca Nsemwa.

**MHE. REBECA S. NSEMWA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa muda wa kuuliza swali. Kwa kuwa, wanawake wengi Tanzania wanaojihusisha na shughuli za kilimo wanapatikana vijijini na wanatumia zana duni za kilimo, je, ni lini Serikali itawasaidia wanawake hawa kwa kuwaunganisha na benki za kilimo ili waweze kupata mikopo yenye riba nafuu na hatimaye waweze kufanya kilimo cha kisasa, chenye tija na kisha Serikali iwasaidie kutafuta masoko ya mazao yao ndani na nje ya nchi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa nafasi niweze kujibu swali zuri la Mheshimiwa Rebeca Nsemwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli katika maeneo mengi yanayojihusisha na kilimo, moja ya wahusika wakuu katika shughuli hiyo ya kilimo ni wanawake na wamekuwa nguzo katika familia nyingi hapa nchini. Kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameuliza, Serikali ina mpango gani wa kuwaunganisha na taasisi za kifedha na pengine taasisi za kifedha zisogee karibu na kule walipo?

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua na inakubaliana na ushauri na wazo zuri lililotolewa na Mheshimiwa Mbunge. Kwa sasa Serikali imekuwa inatumia Benki yetu ya Kilimo, *TADB,* pamoja na

taasisi nyingine za kifedha, ambapo Serikali imetengeneza majukwaa ya kuwaunganisha wakulima, hasa akina mama, waweze kunufaika na mikopo yenye masharti nafuu ambayo itawawezesha kutekeleza shughuli hiyo vizuri. Taasisi nyingine ambazo zimefanya kazi hiyo ni pamoja na wenzetu wa *PAS,* Benki kama ya *CRDB, NMB* na *TCB*.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, Serikali pia, imefanya marejeo kuangalia uwezekano wa mikopo ile inayotolewa ngazi za Halmashauri, kuruhusu wigo wa matumizi yake. Kwa yule ambaye anataka aitumie katika shughuli za kilimo, kwenye ile 4% ambayo inaangukia upande wa wanawake, aweze kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania iko hatua za mwisho pia kukamilisha kampuni ambayo itakuwa inasimamia kutoa dhamana, ambapo kwa zamani ilikuwa chini ya dirisha lile la *Export Credit Guarantee Scheme*. Sasa kuwe na kampuni, ambayo itakuwa na madirisha mbalimbali ya kuweza kusaidia makundi mbalimbali, likiwemo kundi la wanawake, kundi la vijana, kundi la vijana wasomi kutoka vyuo vikuu waweze kupata dhamana kupitia kampuni ambayo itakuwa inadhamini mikopo ili makundi hayo ya akina mama ama vijana yaweze kupata mikopo katika taasisi za kifedha.

Mheshimiwa Spika, hivi tunavyoongea, tayari tuna shilingi bilioni 280 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kwenda kutekeleza jambo hilo. Kwa hiyo, ni jambo ambalo litakamilisha taratibu za kisheria ili kuweza kuhakikisha mwamba linaanza kufanya kazi zake na akina mama waweze kupata mikopo hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kauli ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwamba wapendwa wetu wanapokuwa wamepeleka wagonjwa wao na bahati mbaya wameondokewa na wapendwa wao, basi hospitali zetu za Serikali ziweze kuachia hiyo miili, lakini bado kuna sintofahamu katika hospitali nyingi kuendelea kushikilia ile miili kwa kuwaomba hawa watu

waweze kutoa fedha ili waweze kuachiwa miili ya wapendwa wao. Je, ni ipi kauli ya Serikali?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nijibu swali zuri la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwepo na utamaduni ambao ulijengeka miaka mingi wa kuzuia miili ya wapendwa wetu pale inapokuwa imetokea bahati mbaya amefariki, kwa ajili ya kubishania kuhusu masuala ya kulipia gharama za matibabu zilizofanyika.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitoa ahadi wakati wa kampeni, na waraka ukatolewa na mpaka sasa tunasimamia utekelezaji wake kwamba inapotokea bahati mbaya kama hiyo, fedha isiwe kigezo cha kushikilia mwili wa mpendwa wetu anapokuwa ameshatutoka, hasa tukitambua kwamba kuna baadhi ya imani zetu haziruhusu kukaa na mwili muda mrefu kabla ya kuupumzisha.

Mheshimiwa Spika, kwa swali hili, na kwa maelekezo yale ya Mheshimiwa Rais, nisisitize tena kwenye hospitali zote za umma kuhakikisha kwamba wanatekeleza maelekezo haya, na watekeleze mwongozo ambao umetolewa wa namna ya kutekeleza jambo hili.

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni rahisi tu. Imetokea, mpendwa wetu ametutoka, tunazo kumbukumbu, masuala yote ya kitabibu yamekamilika, waruhusiwe mara moja kuchukua mwili. Kumbukumbu zao zinajulikana, mambo ya *bill* yajadiliwe wakishamaliza suala la kumsindikiza mpendwa wao.

Mheshimiwa Spika, nitoe rai tu kwa Watanzania wote kwamba jambo hili limekuwa likijitokeza kwa sababu ni kweli huwa tuna taratibu za masuala ya uchangiaji wa matibabu. Uchangiaji wenyewe unafuata taratibu hizo ambazo zimeorodheshwa. Unapokwenda hospitalini kuna masuala ya vipimo, kuna masuala ya dawa, pamoja na mambo mengine yanayohusiana na matibabu.

Mheshimiwa Spika, jambo hili, Mheshimiwa Rais amekuja na jawabu la kudumu, ambalo ni Bima ya Afya kwa Wote. Kwa Watanzania wote tupokee dhana hii, tupokee sera hii, tupokee jambo hili na sote tujiunge kwenye suala hili la Bima ya Afya kwa Wote ili tuweze kumaliza kabisa tatizo hili la kudaiana bili, hali ukiwa umeshaondokewa na mpendwa wako.

Mheshimiwa Spika, tukishakuwa na Bima ya Afya kwa Wote, maana yake, masuala haya ya matibabu yatakuwa sasa yanaendeshwa kwa taratibu za bima, ambapo hakutakuwepo na mambo ya kulipialipia kila hatua unapokwenda pale hospitalini. Inakuwa unapata matibabu kwa kutumia utaratibu wa bima ambao ndiyo utaratibu ambao umeonesha mafanikio katika maeneo mengi hapa duniani.

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Janeth Mahawanga.

**MHE. JANETH E. MAHAWANGA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha hivi karibuni, dunia imekumbwa na changamoto ya kisiasa na kiuchumi ukiwemo migogoro ya Kimataifa ambayo imeleta changamoto ya upatikanaji wa mafuta katika nchi nyingi ikiwemo Tanzania. Hali hii imeleta sintofahamu na athari kubwa za kupanda kwa maisha na gharama za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, je, Serikali imechukua hatua gani katika kukabiliana na athari hizi za migogoro ya kidunia na Kimataifa zinazopelekea changamoto ya upatikanaji wa mafuta nchini? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi nijibu swali zuri la Mheshimiwa Janeth Mahawanga, Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kufuatia mambo yanayotokea Mashariki ya Kati, kumekuwepo na madhara hasi kwenye uchumi, na siyo tu kwa Tanzania, ni kwa dunia nzima, nchi zote duniani, zinapata madhara haya; nchi zilizopo kwenye eneo la mapigano, nchi zinazoshiriki kwenye mapigano, na nchi nyingine zote, ikiwemo Tanzania ambayo ina sera yake ya kutokufungamana na upande wowote.

Mheshimiwa Spika, katika madhara hayo, kumekuwepo na kupanda kwa masuala ya bei za mafuta, kupanda kwa gharama za bima, kupanda kwa mnyororo mzima wa *distribution*, mgawanyo wa ugavi, na pia kumekuwepo na mashaka ya uwezekano wa kuadimika kwa bidhaa zenyewe katika nchi mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kuchukua hatua kama nilivyowahi kusema, na Mheshimiwa Waziri wa kisekta amewahi kuisemea pia katika sehemu mbalimbali ya maelezo. Ni kwamba Serikali kwanza imefanya tathmini ya kina kujua ukubwa wa tatizo, madhara ambayo yanajitokeza katika sekta zetu za kiuchumi; na pili, hatua ambazo zinafaa kuchukuliwa ili kuweza kuhakikisha kwamba madhara haya hayawi makubwa zaidi pamoja na kwamba ni kweli madhara yatakuwepo na Tanzania siyo kisiwa.

Mheshimiwa Spika, hatua ya kwanza ambayo Serikali imechukua ni ya kuhakikisha kwamba bidhaa hii haiadimiki. Zipo nchi ambazo tayari matatizo yameshajitokeza ya bidhaa hiyo kuadimika, kwamba hata kama una fedha hupati mafuta.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mkakati kuhakikisha la kwanza bidhaa hii ya mafuta haiadimiki; na pili, Serikali imechukua hatua ya kufanya masuala ya ruzuku ambayo tayari kuna taratibu za namna ya kutekeleza zoezi hilo la ruzuku, ambapo zimekuwepo njia nyingi ambazo zinatumika kwa ajili ya kuweza kuhakikisha tunapunguza makali ya madhara yanayotokana na kile kinachoendelea kule Mashariki ya Kati.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, tunatumia uzoefu tuliofanya jambo la aina hii lilipotokea pale palipokuwepo na mzozo kule Ulaya

Mashariki. Lilitokea jambo lililoleta madhara kama haya, na Serikali iliendelea kutoa ruzuku kwa namna mbalimbali za ruzuku ili kuhakikisha kwamba bei hazipandi hasa kwa nishati hiyo ambayo ni injini ya uchumi wetu.

Mheshimiwa Spika, mbali na hilo, pia Serikali imekaa na wadau, imewasikiliza. Mimi pamoja na Mawaziri wa sekta tulikaa na wadau, wakiwemo wadau wa usafirishaji ili kuweza kujadiliana nao na kuhakikisha tunadhibiti kupanda kwa gharama za usafirishaji ambapo zikipanda gharama hizo kimsingi itakuwa inaashiria pia kupanda kwa gharama za maisha.

Mheshimiwa Spika, tulikubaliana na wasafirishaji kupunguza gharama ambazo wanazipata katika baadhi ya hatua zinazochukuliwa na Serikali, ambazo kimsingi siyo za lazima sana na haziathiri sana mambo ya Serikali ili ikiwa ni namna ya kutoa ruzuku kwamba tukiwapunguzia gharama hizo, wao watatumia hiyo fedha ambayo walikuwa wanalipia katika baadhi ya maeneo yaliyokuwa yanatolewa maelekezo na Serikali, itumike kupunguza bei za gharama za usafiri.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kulikuwepo utaratibu wa mabasi yote yanapokwenda mikoani, lazima yapite kila stendi hata kama hayana abiria wa kushusha. Tumesema hakuna ulazima wa kila basi kupita kila stendi hata kama halina abiria wa kushusha ili kuweza kupunguza gharama kwa mabasi haya na gharama hizo zilizopunguzwa, zitumike kama ruzuku ya kutokupandisha bei.

Mheshimiwa Spika, siyo hilo tu, pia kuna mabasi ambayo yameshatengenezwa ambayo hayana uwezo wa kubeba mzigo mkubwa zaidi ku-*overloads,* kuliko uwezo wake wa jinsi ilivyotengenezwa. Mabasi haya pia kila wakati yalikuwa yanapita kwenye vituo vyetu vya kupima uzito, kwenye *weigh bridge* zetu, yalikuwa yanapita hata kama muundo wa basi lake hauruhusu kubeba mizigo mikubwa iliyopitiliza, wanapanga foleni ndefu, wanachoma mafuta, wanaingia gharama.

Mheshimiwa Spika, tumesema mabasi hayo ambayo kwa utengenezaji wake hayawezi yakabeba mzigo mkubwa kuliko ambayo umekadiriwa, hayana ulazima wa kupita kwenye mizani, yenyewe yatapitiliza moja kwa moja ili kupunguza gharama ya kuchoma mafuta na kupandisha gharama kwa wasafirishaji.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, hata yale ambayo yanatakiwa kupima uzito, tumepunguza vituo vya kupita kupima. Watapita sasa kwenye mizani ya kwanza na ya mwisho kabla hawajamaliza safari yao walikokuwa wanaenda.

Mheshimiwa Spika, hizi zote ni njia mbalimbali za utoaji wa ruzuku, kupunguza gharama ambazo zingeweza kubebwa na mwananchi kwa maana ya madhara ambayo yatakuwa yamejitokeza kutokana na kupanda kwa gharama za mafuta.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya tathmini na kuchukua hatua ili kuweza kuhakikisha bidhaa hii haiadimiki, lakini pia kuhakikisha inaendelea kuwa *affordable*, na himilivu, bei ambazo Mtanzania anaweza akamudu na kuendelea kusukuma uchumi kwa nchi yetu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Nsekela.

**MHE. KHALID M. NSEKELA:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru.
Mheshimiwa Waziri Mkuu, kwanza ninaipongeza Serikali kwa jitihada za makusudi za kuendeleza sekta ya elimu na kuwawezesha vijana kiuchumi na jamii kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni vijana wengi ambao wako Vyuo Vikuu wamekuwa wakipata changamoto sana wanapokuwa wamemaliza, wanakuja kutafuta ajira, wamejikuta hawana ujuzi ambao unaendana na ajira inayotakiwa.

Mheshimiwa Waziri Mkuu, swali langu ni je, Serikali ina mpango gani na mkakati wa kuwezesha taasisi za elimu ya juu, kushirikiana na sekta binafsi ili kuwajengea uwezo vijana ambao wako vyuo vikuu na

kuwaandalia mazingira ya kuwapa ujuzi na uzoefu ili wawe tayari kwa soko la ajira?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, ninamshukuru Mheshimiwa Khalid Nsekela kwa swali zuri ambalo ameliuliza.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kumekuwepo na hiyo changamoto ya vijana kupata shida ya masuala yanayohusiana na ajira baada ya kuwa wamehitimu. Serikali tayari imeshasaini makubaliano ya ushirikiano kati ya Serikali, vyuo vikuu, pamoja na waajiri wakiwemo waajiri wa sekta binafsi, kuweza kuangalia namna nzuri ya kuwaandaa vijana wetu kuingia katika soko la ajira, na kuwa washindani katika masuala haya yanayohusu upatikanaji wa ajira.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya masuala ambayo yapo katika yale makubaliano, na utakumbuka pia hivi majuzi tulipokea andiko moja zuri kutoka kwa Mheshimiwa Selemani Jafo, Mbunge wa Kisarawe ambalo na lenyewe lilikuwa linatoa mawazo na maoni kuhusu ni namna gani vijana wanaweza kupata ajira ndani ya Serikali, na sekta binafsi hasa wanapohitimu vyuo vikuu.

Mheshimiwa Spika, kupitia hilo ambalo nimesema Serikali imeshasaini makubaliano hayo na mawazo haya ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa, likiwemo hili ambalo Mheshimiwa Khalid Nsekela amelitoa kupitia swali lake zuri na mawazo mengine ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa ikiwemo lile alilotoa Mheshimiwa Jafo, Serikali kupitia wataalam wake wanaendelea kuangalia madirisha yote haya ambayo yatawafanya vijana waweze kupata mafunzo, waweze kutumia vizuri fursa zinazopatikana ndani ya Serikali na ndani ya sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ambayo Serikali inayaangalia, mojawapo ni hilo la kupata mafunzo angali wanasoma, waendelee kupata *attachment* za kuweza kujifunza kinachofanyika katika ofisi mbalimbali, zikiwemo za umma na zile za sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, lingine, kama nilivyosema, Serikali inaendelea kufanyia kazi maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais aliyatoa ya kuangalia kuwa na dirisha la wahitimu. Dirisha la wahitimu, tunaangalia kupitia hii kampuni ambayo itaanzishwa ambayo ni *Export Credit Guarantee Scheme*, iweze ku-*guarantee* vijana wetu wanaotoka vyuo vikuu ambao wako na mawazo ya kufanya uzalishaji, lakini wanakosa mitaji, ili waweze kupata mitaji, na wakipata mitaji, tuna uhakika kwamba wataweza kujiajiri na pia kuajiri na wengine.

Mheshimiwa Spika, tunawaza hatua kubwa zaidi ya kubadilisha sheria kutoka kwenye dhamana ambazo zilikuwa zinatambulika zamani, zile ambazo hazihamishiki, kwenda kwenye dhamana zinazohamishika.

Mheshimiwa Spika, chukua mfano mmoja mdogo wa mtu ambaye amepeleka kumsomesha mtoto wake kuanzia *kindergarten*, akaenda *primary*, akaenda sekondari, akaenda mpaka chuo na pengine mpaka vyuo vya nje, amemsomesha shule binafsi, gharama kubwa, mwisho anapomaliza anakuwa na cheti chake na hakitambuliki, lakini kipande cha eneo cha hati ya milioni 15 kinaweza kikadhamini mkopo.

Mheshimiwa Spika, cheti cha chuo kilichogharimu takribani milioni 200 hakiwezi kutambulika na kikatumika kama dhamana. Kwenye sheria tunayopendekeza, tunataka vyeti vya shule vikishathibitishwa na *TCU* viweze kutumika kama dhamana ya kukopa na mhitimu yule aweze kutumia cheti chake kuweza kupata mkopo.

Mheshimiwa Spika, msomi wetu aliyemaliza Famasia, na akapata cheti chake, msomi wetu aliyemaliza *Electrical Engineering* na akapata cheti chake, kukosa vitendea kazi vile vya kuweza ku-*practice* taaluma yake, na cheti anacho kwamba tumlazimishe naye awe na kipande cha ardhi tu ndiyo aweze kukitumia kama dhamana, hili tunaona tunabana wigo wa fursa ambazo vijana wetu wanakuwa wameshapata.

Mheshimiwa Spika, hivyo, haya ni baadhi ya maeneo ambayo wataalamu wetu wanaendelea kuyachambua na Muswada upo, unafanyiwa kazi. Tunaamini utakapokuwa umeiva tutaleta ndani ya Bunge lako Tukufu ili kuweza kuwapa fursa hiyo kubwa vijana wetu waweze kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika masuala ya ajira.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Mkuu, nikushukuru sana kwa majibu sahihi. Waheshimiwa ninamwita Mwenyekiti, kuendelea na shughuli zilizopangwa.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Deodatus P. Mwanyika) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Katibu.

**NDG. JOSHUA CHAMWELA, *ndc* – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Tunaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI. Nimwite sasa Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, Mbunge wa Mtwara Mjini, aulize swali lake.

Na. 267

**Ujenzi wa Shule za Kidato cha Tano na Sita**

**MHE. ARIF S. PREMJI** aliuliza:-

Je, Shule ngapi za kidato cha tano na sita zimejengwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 hadi kufikia robo ya pili?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Waziri. Kwa niaba yake, namwita Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Arif Suleiman Premji, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekuwa ikijenga shule mpya za kidato cha tano na sita au kuongeza miundombinu katika shule za sekondari zilizopo ili kuzipandisha hadhi, kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita, kisha kupata usajili rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali imetoa shilingi billioni 23.8 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 318, mabweni 116, matundu ya vyoo 542 katika shule 68 za sekondari ili kuziongezea uwezo wa kupokea wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Aidha, hadi Aprili, 2026 shule 80 zenye uwezo wa kupokea wanafunzi 6,400 wa kidato cha tano na sita zimesajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi billioni 27.5 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni 273, madarsa 1,094 na matundu ya vyoo 1,645 katika shule 91 za sekondari kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha tano na sita. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Arif Premji, swali la nyongeza.

**MHE. ARIF S. PREMJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Jimbo la Mtwara Vijijini lina kata 21. Katika kata hizo, ni shule moja tu ndiyo ina kidato cha tano na sita. Je, ni upi mkakati wa Serikali kuhusiana na hilo ili kuongeza shule za sekondari katika Jimbo la Mtwara Vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wanafunzi 756 ndio wapo kwenye shule ya *Mustafa Sabodo High School*. Shule hiyo inapitia changamoto ya uzio. Ipi kauli ya Serikali kuhusiana na changamoto hiyo na ambavyo wanaweza wakaitatua? Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba Jimbo la Mtwara Vijijini linahitaji ujenzi wa shule za kidato cha tano na sita. Ni kweli kwamba tulishafanya tathmini na kuona kwamba katika kata zile 21 za Jimbo la Mtwara Vijijini kuna maeneo ambayo tumeshayatambua kwa ajili ya kuanza ujenzi wa madarasa ya kidato cha tano na sita, pia kujenga mabweni na maabara kwa zile shule ambazo zitakuwa na mchepuo wa masomo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mpango ambao tumeweka katika mwaka ujao wa fedha, sehemu mojawapo ambayo tumeipa kipaumbele ni kujenga madarasa ya kidato cha tano na sita katika Jimbo la Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa swali la pili, tunafahamu kuwa zipo shule nyingi ambazo zinahitaji kujenga uzio kwa ajili ya usalama, na ni jambo muhimu, lakini safari ni hatua, na kupanga ni kuchagua. Tumekubaliana kwamba, kwanza tuboreshe miundombinu ya elimu, wanafunzi waingie madarasani. Pili, tutakwenda sasa na mpango wa kujenga uzio katika shule zetu hizo. Kama haitoshi, halmashauri wenyewe pia wanaweza wakaanza kutenga fedha kwa awamu kupitia mapato ya ndani na kuanza kujenga uzio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI kumwelekeza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mtwara Vijijini kuanza kutenga fedha kwenye bajeti zao kwa ajili ya kuanza ujenzi wa *fence* hiyo kwa awamu.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Boniphace Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Tunapoelekea mwaka 2028, wanafunzi wote watamaliza, wale wa darasa la sita na darasa saba na tunaenda kwenye madarasa ya *form four*. Je, Serikali ina mpango gani wa kuona kwamba shule hizi za kidato cha tano na cha sita kuwa na shule za *day* ili kuongeza idadi ya wanafunzi kwenye maeneo yote ambayo wanafunzi wanaongezeka?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya mpango mkakati kwamba tunatambua kuanzia Januari, 2028 tutakuwa na *double cohort,* kwa maana ya wanafunzi wa darasa la sita na la saba mwakani 2027, wote wataingia kidato cha kwanza Januari, 2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kwamba wanafunzi hawa watakwenda mpaka kidato cha nne na tutahitaji ongezeko la madarasa, shule na miundombinu mingine ya kidato cha tano na sita. Ninaomba kumhakikishia Mheshimiwa Boniphace Getere, Mbunge wa Bunda, kwamba Serikali katika mpango huo tumeweka eneo la kuhakikisha kwamba pia tutajenga shule, madarasa na miundombinu kwa kidato cha tano na sita ambazo zitaweza kuwachukua wanafunzi hawa wote ambao wataingia Januari, 2028.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Ester Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuniona. Halmashauri ya Mji wa Tarime tangu kuanza kwake ina shule moja tu ya kidato cha tano na cha sita, ambayo ni ya wavulana tu, ya Tarime Sekondari. Kwa kuwa nimekuwa muda mwingi nikizungumzia kuhusiana na shule ya Mogabiri Sekondari kupandishwa hadhi kuwa ya kidato cha tano na cha sita; na kwa kuwa miundombinu ya ujenzi wa mabweni na madarasa imeshakamilika. Je, Serikali haioni kwamba sasa hivi ni muda mwafaka wa kupandisha hadhi ya elimu katika Mji wa Tarime kwa kuanzisha Shule hii ya Sekondari ya Mogabiri kuwa na kidato cha tano na cha sita ili iweze kutoa elimu kwa wavulana na wasichana ndani ya Mji wa Tarime na wengine kutoka sehemu nje ya Tarime?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa

Mwenyekiti, moja ya vigezo vya kuanzisha shule za Kidato cha tano na sita ni idadi ya wanafunzi wa kidato cha nne ambao wanatarajia kuingia kidato cha tano; pili, ni umbali wa wanafunzi wanaohitaji kuingia kidato cha tano na sita kutoka shule nyingine; na tatu, ni upatikanaji wa eneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaitumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Tarime Mjini na wananchi wa Tarime kwa kujenga miundombinu katika shule hiyo ya kuanzia ili tuweze kupandisha hadhi kuwa kidato cha tano na sita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa suala hilo tumelichukua, tutalifanyia kazi haraka iwezekanavyo ili tuweze kupandisha hadhi shule hiyo baada ya kujiridhisha na vigezo, kufanya tathmini ya vigezo ili wanafunzi wa eneo hilo waweze kupata huduma kidato cha tano na sita.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Anne Malecela.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Pamoja na kwamba Mheshimiwa Waziri amejibu kwa ujumla, lakini ninaomba kuuliza swali. Mimi nina Shule ya Sekondari ya Kimala ambayo ni *high school* ya wasichana tu. Hata hivyo, shule hii iko milimani, na ninakiri kwamba shule hii ni nzuri sana lakini haina uzio, na pale ilipo siyo mahali pazuri sana. Je, Serikali haioni kwamba ni vyema sasa wakaenda kuitembelea ile shule na kuona umuhimu wa kuweka uzio, ukizingatia kwamba ni shule ya wasichana watupu?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi, uzio katika shule zetu ni hitaji muhimu kwa ajili ya usalama wa watoto wetu wa kike, na pia wa kiume. Serikali inatambua umuhimu huo, na ndiyo maana katika kila mwaka wa fedha ziko shule ambazo tumeendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ujenzi wa *fence*, na pia tunaendelea na kujenga miundombinu mingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tumepokea hoja ya mama yangu, Mheshimiwa Anne Kilango Malecela. Tutashirikiana na Halmashauri ya Same kupitia mapato ya ndani ya Halmashauri, na Serikali Kuu tutaona pale ambapo tutapata fursa ya kifedha kwa ajili ya kujenga *fence* hiyo, tutapeleka fedha kuhakikisha kwamba *fence* hiyo inajengwa na kuboresha usalama kwa watoto wetu wa shule hiyo.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea kwenye swali linalofuata, ndani ya Wizara hiyo hiyo.

Na. 268

**Kuongeza Kiwango cha Ufaulu kwa Wanafunzi**

**MHE. JAFARI W. CHEGE** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali isiyondoe mfumo wa wanafunzi kurudi mchana kula nyumbani na kurudi tena shuleni ili kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Jafari Wambura Chege, Mbunge wa Jimbo la Rorya, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa mitaala ya elimu msingi na sekondari, wanafunzi wanapaswa kusoma vipindi sita hadi nane kwa siku kwa shule za msingi, na saba hadi kumi kwa shule za sekondari, kutegemea na ratiba ya siku. Katika kutekeleza takwa hili, halmashauri zimekuwa na ratiba ya watoto kurudi nyumbani kupata chakula na kurudi shule kumalizia vipindi. Aidha, halmashauri nyingine wanafunzi hukamilisha idadi ya vipindi bila kurudi nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Waraka Namba Tatu wa Mwaka 2016 kuhusu utekelezaji wa Elimu Bila Ada, Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe Shuleni wa Mwaka 2021 na Mpango wa Utekelezaji wa Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe Shuleni wa Mwaka 2023 Serikali kwa kushirikiana na wazazi imeweka utaratibu wa kuhakikisha kwamba kila mtoto anapata chakula shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia kuwa hali ya upatikanaji wa huduma ya chakula shuleni inatofautiana kati ya halmashauri moja na nyingine, Makatibu Tawala wa Mikoa wanaelekezwa kufanya tathmini ya utekelezaji wa utoaji wa huduma ya chakula shuleni katika mikoa yao ili kuondoa ratiba ya wanafunzi kurudi mchana kula nyumbani na kurudi tena shuleni,

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jafari Chege.

**MHE. JAFARI W. CHEGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali. Hata hivyo, Mheshimiwa Naibu Waziri atakubaliana na mimi kwamba zama zimebadilika, utaratibu huu wa watoto kurudi nyumbani kwenda kupata chakula, una changamoto nyingi, ikiwemo umbali wa watoto wanakoishi na maeneo ya shule yalipo, ushawishi wanaokutana nao wakati wanarudi nyumbani, na pia kuna maeneo mengine ya vijijini watoto wanaporudi nyumbani ndio wanabadilika kuwa wapishi; wanapika chakula na wanapoaliza ndipo wanarudi shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mikoa iliyobaki na utaratibu huu ni michache, je, ni kwa nini Serikali isifute utaratibu huu na kuhimiza chakula shuleni, kwa maana ya lishe, na watoto wakaendelea kupata chakula shuleni badala ya utaratibu wa zamani wa watoto kurudi nyumbani kwenda kupata chakula?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Sera na miongozo ya elimu inahimiza sana watoto kula shuleni, kwa maana ya lishe kupatikana pale pale shuleni. Hata hivyo, zoezi hili limekuwa likisuasua sana kwa

sababu aidha ya elimu kwa wazazi na changamoto nyingine mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba sasa inajikita kutoa elimu kwa wazazi na maeneo mengine ili angalau jambo hili liwe shirikishi na watoto waweze kupata chakula shuleni badala ya sasa utaratibu ulivyo baadhi ya shule wanakula na maeneo mengine watoto hawapati chakula shuleni?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Jaffari Wambura Chege, Mbunge wa Rorya, kwa kweli amekuwa mfuatiliaji mzuri sana wa sekta ya elimu, na tunapongeza sana wananchi wa Rorya kwa kuwa na msemaji madhubuti na imara kama Mheshimiwa Chege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunalo suala la chakula shuleni, na Serikali hii inatambua umuhimu wa wanafunzi wetu wote kupata chakula na lishe shuleni, na ndiyo maana kupitia Waraka wa Utoaji wa Chakula na Lishe wa Mwaka 2021 ukafuatiwa na Mwongozo wa Usimamizi wa Utekelezaji wa Utoaji wa Chakula na Lishe Mwaka 2023. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kwamba wanafunzi wote wanapata chakula shuleni

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa 64% ya shule zetu za msingi, wanafunzi wote wanapata chakula shuleni. 66.47% ya wanafunzi wa sekondari wanapata vyakula shuleni. Kwa hiyo, kwa wastani kuna zaidi ya kama 36% ya wanafunzi katika shule zetu za msingi na sekondari ambao mpaka sasa hawapati chakula shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi, ma-*DC,* Wenyeviti wa Halmashauri na Madiwani, Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na Mitaa, tumekubaliana kwa maelekezo kwamba tutoe elimu kwa wazazi ili wazazi waone umuhimu wa kuchangia chakula kwa wanafunzi

shuleni, Na wanafunzi wale ile *share* yao ambayo wangeipata wakiwa nyumbani, waipate wakiwa shuleni wakiendelea na masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba niitumie nafasi hii nitoe wito kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, kwamba viongozi wote ngazi za mikoa, ngazi za wilaya, Waheshimiwa Madiwani, Wenyeviti wa Serikali kwenye mikutano yao ya hadhara waendelee kutoa elimu kwa wazazi na walezi kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa kuchangia chakula shuleni ili watoto wetu wasome vizuri katika mazingira bora zaidi ya lishe na afya.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Haidary Sumry.

**MHE. HAIDARY H. SUMRY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Manispaa ya Mpanda inamiliki sekondari mbili za kidato cha tano na sita za Kitaifa; na huko nyuma sekondari hizi zilikuwa na magari kwa ajili ya kuwasaidia watoto wanapopata dharura mbalimbali, lakini sasa hivi sekondari zote hizi hazina magari. Je, ni lini Serikali itapeleka magari kwenye shule hizi za Kitaifa ili kuwasaidia watoto wanapopata dharura? Ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, shule zetu za sekondari za Kitaifa kama ambazo Mheshimiwa Sumry, Mbunge wa Mpanda Mjini amezitaja, ni shule ambazo zina uhitaji wa vyombo vya usafiri. Tumeona mara kadhaa miaka miwili mitatu iliyopita Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, alitoa magari kwenye baadhi ya shule kwa ajili ya kuhakikisha kwamba huduma za usafiri katika shule hizo zinaboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba dhamira ya Serikali ni kuendelea kutafuta fedha, kupata magari ili kuwezesha usafiri katika shule hizo. Tutaendelea kufanya hivyo kwa awamu ili kuhakikisha kwamba huduma za usafiri na usafirishaji katika shule zetu hizo zinaimarika.

Tukifanya hivyo, tutahakikisha pia tunatoa kipaumbele katika shule za Jimbo la Mpanda Mjini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sara Ally.

**MHE. SARA M. ALLY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza. Kutokana na taarifa ya hali ya ufaulu, imeonesha kwamba shule ambazo zinapata chakula shuleni wanafaulu vizuri sana ukilinganisha na shule ambazo wanafunzi hawapati chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na jibu la msingi la Mheshimiwa Naibu Waziri, kwamba 52% bado hawapati chakula shuleni; kwa kuwa Serikali imetoa ada shuleni na michango mingine midogo midogo, je, Serikali haioni kwamba pamoja na maelekezo na waraka huo wa kuelekeza viongozi wa ngazi za mikoa kuhamasisha wazazi kuchangia chakula shuleni imeshindikana; na sasa kuona haja ya kuweka sheria ili watoto hawa wapate usawa katika ufaulu wa masomo yao?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya Mheshimiwa Sara Msafiri, Mbunge wa Jimbo la Mvomero ni muhimu na ya msingi. Hata hivyo, ninaomba nirejee kuweka kumbukumbu sawa kwamba wanafunzi wanaopata chakula shuleni kwa ngazi ya elimu ya msingi ni 64% na ngazi ya elimu ya sekondari ni 66.47%. Maana yake ni kwamba, wastani wa 30% ndio ambao hawapati chakula shuleni, siyo 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ni kweli tunafahamu umuhimu wa chakula shuleni, na kweli takwimu zinaonesha wanafunzi ambao wanapata chakula shuleni wana ufaulu mzuri zaidi kwa sababu ambazo ni za wazi. Ndiyo maana Serikali imetoa mwongozo wa 2021, imetoa utekelezaji wa 2023 na tunaendelea kusimamia kupitia wazazi, viongozi wa mikoa, bodi na kamati za shule kuhamasisha wananchi kuchangia chakula kwa watoto wa shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kuwa na sheria, tumepokea wazo la Mheshimiwa Mbunge, tutafanya tathmini na kuona uwezekano wa kufanya utekelezaji wake.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali linalofuata. Nimwite Mheshimiwa Kenneth Esnest Nollo, Mbunge wa Bahi, aulize swali lake. Mheshimiwa Nollo hayupo, Mheshimiwa Ester Bulaya.

Na. 269

**Ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mtitaa Bahi**

**MHE. ESTER A. BULAYA K.n.y. MHE. KENNETH E. NOLLO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatimiza ahadi ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kata ya Mtitaa Bahi?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Kenneth Esnest Nollo, Mbunge wa Jimbo la Bahi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya Mtitaa kilichopo katika Kata ya Mtitaa Halmashauri ya Bahi ni miongoni mwa vituo vya afya kongwe 205 ambavyo Serikali imevianzisha kwa ajili ya ukarabati na kuviongezea miundombinu ili viweze kutoa huduma ya afya ngazi ya kituo cha afya, ikiwemo huduma ya upasuaji wa dharura kwa wajawazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali kupitia Mradi wa Benki ya Dunia wa Usafi na Afya ya Mazingira *(WASH)* ilitoa shilingi milioni 73.83 kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya majisafi na majitaka pamoja na ujenzi wa choo cha nje kwa ajili ya wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Mtitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa miundombinu ya vituo vya afya kongwe kote nchini. Aidha, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Serikali imetenga shilingi milioni 130 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Afya Babayu katika Halmashauri ya Wilaya ya Bahi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya, kwa niaba. Waheshimiwa mliowasha *mic* mngepunguza.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza. Katika Jimbo la Bunda Mjini kuna Kituo cha Afya cha Bunda Mjini na kinatoa huduma ya afya kwa watu wengi sana kuliko vituo vingine vya afya vyovyote takribani kwenye zile kata saba za Bunda Mjini. Hata hivyo, kuna changamoto ya *OPD* ambapo inahitajika shilingi milioni 182; kuna changamoto ya wodi ya wanawake, wanaume na watoto ambayo ukijumlisha zote gharama yake inayohitajika ni shilingi milioni 695.

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, ni lini sasa Serikali itatoa fedha ili wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini na wa Kata ya Bunda Mjini waweze kupata huduma safi za afya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kama ambavyo kilivyo Kituo cha Afya cha Mtitaa kwa Mheshimiwa Nollo, ndiyo hivyo hivyo Kituo cha Afya cha Manyamanyama, ni cha muda mrefu; na Mheshimiwa Waziri anakijua. Aidha, Manyamanyama ndiyo kata ninayotoka mimi Mbunge na Mbunge wa Afrika Mashariki. Je, ni lini mtakikarabati Kituo hicho cha Afya cha Kata ya Manyamanyama?

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimthibitishie dada yangu Mheshimiwa Ester Bulaya, kwamba tunatambua kwamba Kituo cha Afya cha Bunda Mjini ni kituo ambacho kwa kweli kinahudumia wananchi wengi, wajawazito na wagonjwa wa magonjwa mbalimbali, na ni kituo tegemezi sana kwa wananchi wa Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimeshafanya ziara pale miaka miwili au mitatu iliyopita, na tulikubaliana kwamba Halmashauri walete andiko la mapendekezo. Ninaomba nimhakikishie kwamba walishawasilisha na kimeingizwa kwenye mpango wa vituo ambavyo vina upungufu wa miundombinu. Tutatafuta fedha kwenda kujenga *OPD,* kujenga wodi na baadhi ya miundombinu ambayo Mheshimiwa Mbunge taarifa zake tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie yeye na wananchi wote wa Jimbo la Bunda Mjini kwamba Serikali hii iko kazini. Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, daktari namba moja anajali afya za wananchi wa Bunda na tutahakikisha tunapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, vipo vituo vya afya kongwe na chakavu, na Serikali ilishavitambua vituo vya afya 205 ambavyo ni vya miaka mingi na vinahitaji ukarabati na mara nyingine ujenzi kabisa, kikiwemo Kituo cha Afya cha Manyamanyama, ambako Mheshimiwa Mbunge anatoka na Mbunge wa Afrika Mashariki anatoka. Nimhakikishie kwamba mpango huu tutakwenda kuutekeleza kwa awamu kuhakikisha kwamba vituo vyote chakavu, hospitali na zahanati chakavu zinakwenda kukarabatiwa kwa awamu.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tuulize maswali mafupi sana kwa wachache watakaopata nafasi. Nimekuona Mheshimiwa George Malima.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Je, ni lini Serikali itajenga vituo vya afya kwenye kata za kimkakati; Kata ya Godegode, Berege na Chunyu zilizopo katika Jimbo la Mpwapwa?

**MWENYEKITI:** Ahsante, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Malima alishawasilisha orodha ya kata za

kimkakati. Serikali inaendelea na taratibu za kupata fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo hivyo vya afya.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Sikudhani:

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Afya cha Nampungu ni miongoni mwa vituo vya afya vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru. Kituo kile ni kipya, kilitengewa shilingi milioni 500, zimepelekwa shilingi milioni 250 na kwa sasa kituo kimesimama, hakuna ujenzi unaoendelea. Je, Serikali ina kauli gani katika kuhakikisha kwamba tunapeleka fedha ili ujenzi ukamilike? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ni kweli kwamba viko vituo vya afya ambavyo vilipelekewa fedha kwa awamu mbili; shilingi milioni 500 na shilingi milioni 250. Viko ambavyo vimekamilika vimeanza kutoa huduma na vipo ambavyo bado havijakamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kauli ya Serikali ni kwamba, kwanza Wakurugenzi wa Halmashauri kote nchini ambao walipokea fedha na kujenga vituo vya afya ambavyo havijakamilika, moja wawasilishe taarifa hiyo Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, watenge fedha za mapato ya ndani kwa uwezo wao angalau kukamilisha maeneo ambayo wanaweza kukamilisha ili angalau huduma za wagonjwa wa nje *(OPD)* zianze kwenye vituo hivyo wakati tunaendelea na hatua za ukamilishaji wa miundombinu iliyosalia.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Ninamwita sasa Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, Mbunge wa Mbozi, aulize swali lake.

Na. 270

**Uhitaji wa Chuo Kikuu Songwe**

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga chuo kikuu katika Mkoa wa Songwe?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri, Wanu Hafidh Ameir.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Onesmo Merdson Mnkondya, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongeza fursa za upatikanaji wa Elimu ya Juu na kuchochea maendeleo ya kiuchumi, Serikali inaendelea na kukamilisha ujenzi wa kampasi za taasisi za elimu ya juu katika maeneo mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Songwe una taasisi za Elimu ya Juu ikiwemo Kampasi ya Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(DIT)* ambayo kupitia mradi wa *Technical Education Labour Market Survey,* Serikali inafanya upanuzi wa miundombinu. Upanuzi huu unahusisha ujenzi wa jengo la ghorofa nne la taaluma ambalo litakuwa na madarasa, maabara pamoja na karakana. Lengo ni kuongeza udahili wa wanafunzi katika fani mbalimbali kuanzia ngazi ya cheti hadi *degree*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnkondya, swali la nyongeza.

**MHE. ONESMO M. MNKONDYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru Serikali kwa majibu ambayo imeyatoa kuhusiana na tawi hili la *DIT,* lakini ninaomba niwe na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kufuatia kile kinachofundishwa kwenye chuo hiki ambacho kiko chini ya *Dar es Salaam Institute of Technology – DIT* ambacho kimejikita zaidi kwenye ufundi, ni lini upanukaji wake utalenga taaluma ambazo zitaendana na mazingira ya Mkoa wa Songwe, hasa biashara, kilimo na kadhalika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ili kuusisimua Mkoa wetu wa Songwe, ikizingatiwa ni mkoa mchanga na kuupa uchumi na maendeleo zaidi, ni lini Serikali itajenga chuo kikuu Makao Makuu ya Mkoa wa Songwe ambayo yapo Wilaya ya Mbozi ambapo tayari mahali hapa tuna maeneo ya kuanzia kujenga kama Msense, Mifugo Kata ya Isansa; Zelezeta, *Mbozi Missiyon* Kata ya Igamba; Ipunga pamoja na Hasamba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Onesmo kwa ufuatiliaji wake wa karibu kuhusu kuongeza vyuo vikuu katika Mkoa wa Songwe. Alishawahi kunifuata ofisini akifuatilia suala la Chuo cha *VETA* Songwe ambacho kwa sasa kinaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi, hivi sasa Serikali inaendelea na upanuzi wa chuo hicho, na nia ya kuongeza chuo hiki ni kuongeza udahili wa wanafunzi na taaluma ambazo zitatolewa katika chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, mawazo ya Mheshimiwa Mbunge au ushauri unaenda sambamba na azma ya Serikali katika upanuzi wa chuo hicho. Kwa hiyo, ushauri wake au mawazo yake tumeyapokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kama nilivyoeleza katika swali la msingi, kwa sasa Serikali imeelekeza nguvu katika kutanua vyuo vikuu na kuongeza kampasi katika maeneo mbalimbali ya mikoa ya Tanzania. Mpaka hivi sasa mikoa 16 imeshapata kampasi ya vyuo mbalimbali ikiwemo hii ya *DIT* Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, *UDSM* imepeleka kampasi Lindi na Kagera, *AIA* imepeleka kampasi Manyara, *TIA* imepeleka kampasi Mwanza na maeneo mengine na mikoa mbalimbali ina kampasi mbalimbali za vyuo vya elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Serikali itaendelea kuongeza taasisi hizi kulingana na uwezo na bajeti itakavyoruhusu. Hivyo, pale bajeti itakaporuhusu, basi tutaweza kupeleka chuo kikuu katika Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaomba nimpongeze Naibu Waziri kwa majibu mazuri kabisa ya Waheshimiwa Wabunge. Wilaya ya Kahama ina halmashauri tatu, na iko ukanda wa nchi za *East Africa*. Sasa, Serikali ina mkakati gani wa kuweka kampasi ya chuo kikuu katika maeneo ya halmashauri ya Ushetu, kwa sababu eneo tayari tumetenga zaidi ya heka 800?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi, ni kwamba Serikali ina azma ya kusogeza elimu ya juu ya vyuo katika mikoa yote ya Tanzania. Kama nilivyosema, pale bajeti na uwezo utakaporuhusu, basi Serikali pia itafikiria kupeleka chuo kikuu katika mkoa wa Mheshimiwa Chereheni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sidhani kama tutapata jibu zaidi ya hilo. Kila mkoa utapata chuo kikuu. Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru kwa majibu yako.

Tunaendelea Wizara ya Ujenzi. Ninamwita sasa Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, Mbunge wa Moshi Vijijini, aulize swali lake.

Na. 271

**Ujenzi wa Barabara ya *Moshi International School* – Kibosho kwa Rafael**

**MHE. MORRIS J. MAKOI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itamrejesha mkandarasi wa barabara ya *Moshi International School* - Kibosho kwa Rafael yenye urefu wa kilometa 5.49?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa niaba ya Waziri, Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Godfrey Kasekenya.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, Mbunge wa Moshi Vijijini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara ya *Moshi International School* – Kibosho kwa Rafael, kilometa 7.19, ni sehemu ya barabara ya *Kibosho Shine* – Kwa Rafael – *International School* yenye urefu wa kilometa 25.25 ambapo kilometa 18.06 tayari zimejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali imesaini mkataba kwa ajili ya kazi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa kilometa 7.19 zilizobaki ambapo taratibu za malipo ya awali kwa mkandarasi zinaendelea ili aweze kuendelea na kazi kwa mujibu wa mkataba, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Joseph Morris Makoi.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Kwa sababu sasa tangu Serikali ilipokubali kumleta mkandarasi kufanya

kazi hiyo, ni mwaka wa pili sasa; na kwa vile wananchi ambao waliruhusu maeneo yao barabara ipite waliharibu mazao yao na wengine nyumba zao zilivunjwa wakitarajia kwamba barabara ya lami itajengwa na watanufaika na uwepo wa barabara; na kwa vile mpaka sasa hivi hakuna kinachoendelea na mkandarasi hayupo, je, Serikali iko tayari kuwalipa fidia wananchi wale kwa mazao yao na nyumba zao zilizovunjwa ili itakapojengwa barabara wawe hawakuathirika? Hilo ni swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; katika barabara hiyo iko barabara ya mchepuko ambayo inaenda kwa wawekezaji; mmoja wa mashamba ya maua na mmoja anajenga hospitali ya kitalii ya shilingi bilioni 17. Daraja limekatika na mpaka tunapoongea hakuna mawasiliano. Je, Serikali iko tayari kutumia fedha za dharura ambazo zimetengwa kutokana na hali ya mafuriko na mvua nyingi zilizotokea kurejesha daraja lile ili kuwarejeshea wawekezaji wale moyo wa kuendelea na kazi ya uzalishaji maua pamoja na ujenzi wa hospitali hiyo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kabla Mheshimiwa hajajibu, tusipige makofi swali linapoulizwa, maana linapunguza usikivu hapa mbele. Tumwache mtu aulize swali lake amalize maswali kabisa.

Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Makoi, pamoja na wananchi wa Moshi Vijijini kwamba ni dhamira ya dhati ya Serikali kuijenga hiyo barabara kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbunge ameeleza mara kadhaa kwamba tuna miradi ambayo tulikuwa tumesaini na mingine imeanza, lakini tukawa tumechelewa kulipa *advance* ama hati zile za awali za malipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hao wananchi wasiwe na wasiwasi. Sisi kama tulivyosema kwenye jibu letu la msingi, tunaamini kwamba muda siyo mrefu

tutamlipa huyu mkandarasi malipo yake ya awali ili aweze kurejea na kuanza kufanya hiyo kazi kama ambavyo tumekubaliana kwenye mkataba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali lake la pili, barabara aliyoisema ni barabara ambayo inahudumiwa na wenzetu wa *TARURA* na hata hizi barabara nyingi ambazo tumezifanya tumekuwa tukisaidiana na wenzetu wa *TARURA*. Tumelipokea hilo kuhusu daraja lilivyovunjika na ninaomba nitumie nafasi hii pia kumwelekeza Meneja wa Mkoa wa Kilimanjaro wakisaidiana na meneja mwenzake wa *TARURA* Mkoa wa Kilimanjaro waweze kufika eneo hilo ili waone namna watakavyofanya kulijenga hilo daraja na kurejesha mawasiliano ambayo yamekatika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Barabara ya Busegwe – Kitaramanka ya kilometa 38.5 ambayo inapita katika kata tano za Jimbo la Butiama ni barabara muhimu sana. Barabara hii Mheshimiwa Rais alituahidi kwamba itapata lami. Sasa ningependa kujua Serikali imefikia hatua gani katika maandalizi ya kuifanya ipate lami?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba ahadi za viongozi wa Kitaifa na hasa Mheshimiwa Rais huwa ni maelekezo. Sisi kama Wizara, baada ya kupata hayo maombi tumeshaanza kufanya taratibu. Ninamwomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, bajeti yetu bado haijapitishwa, kwa hiyo, tuna hakika itakuwa kwenye utaratibu wa kufanya mipango ya kuanza kuijenga kama ambavyo Mheshimiwa Rais alitoa hiyo ahadi kwa wananchi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Enock Koola.

**MHE. ENOCK Z. KOOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Barabara kongwe ya Pofo – Mandaka – Kilema ya kilometa

7.2 ilikuwa ahadi ya Mheshimiwa Rais, lakini pia Waziri Mkuu. Sasa barabara hiyo ina hali mbaya sana. Je, ni lini Serikali itaenda kukamilisha ujenzi wa hiyo barabara? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli hii barabara pia ni mojawapo ya barabara ambazo zimekasimiwa kwetu kutoka *TARURA*, na tumekuwa tunaendelea kuzijenga kwa awamu kwa kiwango cha lami. Ninataka nimhakikishie pia Mheshimiwa Mbunge kwamba hata katika bajeti hii ambayo tunaiendea, tumeiweka katika utaratibu wa kuendelea kuijenga kwa awamu kwa kiwango cha lami.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu.

Sasa ni Wizara ya Maliasili na Utalii, nimwite Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan, Mbunge wa Bumbwini, aulize swali lake.

Na. 272

**Wanyama Wenye Vibali vya Kuwindwa kwa Matumizi ya Kijamii**

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN** aliuliza: -

Je, ni wanyama gani wana vibali vya kuwindwa kwa matumizi ya kijamii kwa kuwa nchi yetu ina wanyama wengi katika mapori ya vijijini?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa niaba ya Waziri wa Utalii, Mheshimiwa Silinde.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwindaji kwa matumizi ya kijamii kwa maana ya uwindaji wa kujikimu wa wenyeji, ni moja ya matumizi endelevu ya uvunaji wanyamapori kwa lengo la kutoa fursa kwa wananchi wazawa na wakazi kujipatia kitoweo. Ili kuwezesha wananchi kutumia fursa hiyo, Serikali imetunga Kanuni za Uwindaji wa Kujikimu wa wenyeji za Mwaka 2022 katika Tangazo la Serikali Na. 635 la Mwaka 2022 ambazo zimeainisha taratibu za kufuata ili kuweza kufanya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kanuni hizo zimebainisha jumla ya aina 23 ya jamii za wanyamapori ambao wanaruhusiwa kuwindwa kupitia uwindaji wa wenyeji ambapo kati yao jamii ya mamalia zipo 18 wakiwemo nyati, pofu dume ama mbunju, pongo, digidigi, nyumbu na jamii za ndege aina tano wakiwemo bata, kanga na firigogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua umuhimu wa wananchi kunufaika na rasilimali za wanyamapori, kwani wao ndio walinzi namba moja wa misitu na wanyamapori wetu. Hivyo, Serikali inawaomba wananchi kuzingatia sheria na kanuni zilizopo katika kuwawinda wanyamapori kwa matumizi ya kijamii.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwinyi Ramadhan, swali la nyongeza.

**MHE. MWINYI JAMAL RAMADHAN**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninashukuru kwa kunipa heshima hii kwa kuuliza swali la nyongeza. Kwanza ninamshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali yenye mpango mzuri wa kuwasaidia wananchi kuendelea kutumia maliasili za nchi yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu hayo, ninaomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza. Je, ni taaluma gani iliyoweza kutolewa kwa wananchi ili kuhifadhi zaidi wanyama hawa waliotajwa wasitoweke kwa sababu wana taratibu zao za kuzaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kumekuwa na sheria ya kulinda wanyamapori hawa. Serikali haioni kwamba sheria hizi ambazo na wananchi wanazilalamikia, (wanyama wale ambao wanaudhi, na wananchi wanalalamika juu ya mazao yao ikiwemo tembo, simba na Nyati) sasa umefika wakati Serikali kutoa maelekezo maalum kwa wananchi juu ya utaratibu maalum wa kisheria kuhusu yale malalamiko ambayo yanatolewa hasa kwa fidia, malalamiko juu ya wanyama hawa wanaoharibu mazao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Mwinyi Jamal Ramadhan kwa swali lake zuri la msingi. Ninamwambia tu kwamba, moja, Serikali imekuwa na jitihada kubwa. Kwanza, ni kulinda hawa wanyama wote hatari na hawa wanyama ambao wamekuwa wakitumika kwa ajili ya matumizi ya binadamu na kuna kanuni zake juu ya kuwalinda hawa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, panapotokea eneo limekuwa na shida, Wizara imekuwa ikitumia *TAWA*; yaani kama kuna eneo limevamiwa na tembo, utaona kabisa kunakuwa na operesheni maalum za kwenda kuwaondoa tembo katika eneo husika na kuwarudisha katika maeneo yao. Vilevile, katika maeneo hatarishi, *TAWA* wamekuwa wakifika katika hayo maeneo na kuangalia ni namna gani ambavyo wanaweza kuvuna wale wanyama, kama kuna maeneo wana mamba wamekuwa wakiwavuna na kuwahamishia katika maeneo mengine ambayo hayana watu wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kumekuwa na jitihada kubwa zikiwemo kutoa taarifa kupitia vyombo vya habari, wamekuwa wakielimisha. Pia wamekuwa wakifanya mikutano ya hadhara katika maeneo ambayo yamekuwa na hatari zaidi ya kukutana na hawa wanyama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado Serikali inafanya kazi nzuri kuhakikisha kwamba hakuna athari kubwa kwa wananchi, lakini wakati huo huo tumehakikisha tunaendelea kuwalinda hawa

wanyama kwa faida ya Taifa letu na wananchi katika maeneo husika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninashukuru. Kuna Waheshimiwa mnataka kuuliza maswali Wizara hii, lakini Waziri aliyepo siyo wa Wizara hiyo. Kwa hiyo, ninadhani haitakuwa sawa. Tunakushukuru sana kwa majibu yako.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Tupo katika Wizara hiyo hiyo. Nimwite sasa Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Mwibara, aulize swali lake.

Na. 273

**Kero ya Mamba Wanaodhuru Wananchi – Mwibara**

**MHE. KANGI A. LUGOLA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti kero ya mamba wanaodhuru wananchi katika Jimbo la Mwibara?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola, Mbunge wa Jimbo la Mwibara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kudhibiti mamba katika Jimbo la Mwibara ambapo katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia *TAWA* ilijenga jumla ya vizimba vinne vya kuzuia mamba katika vijiji vya Buzimbwe, Kasahunga, Nampangala na Nyarugoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inaendelea na ujenzi wa vizimba viwili katika vijiji vya Nyamitwebili na Namibu. Aidha, kwa kuwa changamoto hii haiwezi

kwisha kwa mara moja, Wizara kupitia Taasisi ya *TAWA* itaendelea kujenga vizimba kwenye maeneo yenye changamoto za mamba kudhuru watu kwenye Ziwa Victoria katika Wilaya za Jimbo la Mwibara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Wizara imekuwa ikitoa elimu kwa wananchi wa Jimbo la Mwibara ambapo kati ya Mwezi Julai, 2025 hadi Machi, 2026, jumla ya mikutano 12 ilifanyika. Katika mikutano hiyo, wananchi 3,665 ikijumuisha watu wazima 904 na wanafunzi 2,761 walipatiwa elimu ya namna bora ya kutumia vizimba na kuepuka madhara yanayoweza kusababishwa na mamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ili kuongeza wigo wa kutoa elimu kwa wananchi, Wizara ilitoa elimu kwa njia ya redio na televisheni ambapo jumla ya vipindi vitano vya redio na televisheni vitatu vilitolewa. Vipindi hivyo, vilitolewa katika redio za *Bunda FM* na Redio Mazingira, na televisheni ya *Star TV* ambazo zinasikika zaidi katika Kanda ya Ziwa ikiwemo Jimbo la Mwibara.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kangi Lugola, swali la nyongeza.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Serikali na juhudi ambazo Serikali imezifanya kupambana na hawa mamba, lakini nataka kumthibitishia Mheshimiwa Waziri kwamba mamba ni wengi, ni wengi, ni wengi; na hao mamba hawana simile. Ukitisha mamba mmoja, Veronica Marumbo Isige, siku ya mwaka mpya mwanaye amemchinjia mbuzi, ameenda ziwani pale kuchota maji, yeye ndiye akageuka kuwa kitoweo cha mamba mwaka mpya.

**MWENYEKITI:** Swali Mheshimiwa Kangi.

**MHE. KANGI A. LUGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa njia za kupambana na mamba ziko nyingi ikiwa ni pamoja na hivyo vizimba alivyovisema na mamba ni wengi, je, kwa nini Serikali isitumie njia za operesheni maalum ya kuwavuna mamba ikiwa ni pamoja na kukusanya mayai pamoja na vifaranga vya mamba visivyozidi kisheria sentimeta 50?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kwa kuwa wahanga wamekuwa ni wengi; katika kipindi cha miaka miwili walioliwa na mamba na wengine kujeruhiwa wanapata 18; ni lini wahanga hawa kwa sababu imekuwa ni muda mrefu sana, watalipwa malipo yao ya fidia?

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, nami ninampongeza tena Mheshimiwa Kangi Alphaxard Lugola kwa maswali yake mawili ya msingi ambayo yana manufaa makubwa katika jimbo lake. La kwanza, ameuliza kuhusu njia mbadala zikiwemo za kupambana na mamba hasa kufanya operesheni maalumu ya kuvuna mamba hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaja hapa, nilizungumza na Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii na akanithibitishia tu nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba ameshawaelekeza *TAWA* wafike katika eneo lake, wafanye sensa ya mamba na kuhakikisha kwamba katika wale mamba ambao ni wakorofi na wanaleta madhara makubwa kwa wananchi, waweze kuwavuna na kuwahamishia katika maeneo ambayo hayana watu wengi kwa maana hayana athari kubwa kwa wananchi. Kwa hiyo, hilo ni elekezo la Mheshimiwa Waziri na *TAWA* watalitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia kwa wahanga, vilevile Katibu Mkuu wa Wizara amesema walishapokea maombi hayo na yapo katika mchakato, na watakavyomaliza hizi katika hatua za mwisho, watawalipa wale wananchi. Kwa hiyo, namthibitishia tu kwamba yote Serikali imeshayapokea na inayafanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunakwenda Wizara ya Madini. Ninamwita sasa Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

*(Hapa kulikuwa na tatizo la microphone)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa, tupunguze kuwasha zile *mic*.

Na. 274

**Kituo Cha Umahiri Mwakitolyo – Shinyanga**

**MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Kituo cha Umahiri eneo la Mwakitolyo kutokana na ushiriki mkubwa wa wachimbaji wa madini wanawake na vijana?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Steven Lemomo Kiruswa.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Madini, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwanahamisi Athumani Munkunda, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la Mwakitolyo ni moja ya maeneo ambayo Serikali kupitia Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* inapanga kujenga vituo vya mfano vya uchenjuaji madini ya dhahabu kwa kutumia teknolojia ya *Carbon-in-Pulp (CIP)* kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Ujenzi wa vituo hivi ambavyo vingine viko Mikoa ya Geita, Mbeya na Mara ni sehemu ya juhudi za Serikali za kuwaendeleza na kuwakuza wachimbaji wadogo nchini kupitia Shirika la *STAMICO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkandarasi wa kujenga Kituo cha Mwakitolyo ameshapatikana, na taratibu za kimkataba zikikamilika, ujenzi utaanza. Hatua ilivyofikiwa hadi sasa ni kukamilika kwa usanifu wa kituo, na kituo hicho kitakapokamilika, kitakuwa na uwezo wa kuchakata kiasi cha tani 120 kwa siku.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanahamisi, swali la nyongeza.

**MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, ninaipongeza sana Serikali hasa Wizara ya Madini kwa kuendelea kufanya vizuri hasa kwa wachimbaji wadogo, na kwa kweli kutujengea *CIP* kwenye eneo letu la Mwakitolyo, tutakuwa tumewasaidia sana wachimbaji wadogo na hasa wanawake na vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi na jitihada zote ambazo Serikali inafanya ya ujenzi wa *CIP* ambayo itakuwa na uwezo wa kuchakata tani 120 kwa saa, ni uwekezaji mkubwa. Sasa Serikali haioni haja wachimbaji tunaowazungumzia hapa, ambao ni wachimbaji wadogo, ambao hawana uwezo wa kuzalisha mzigo huu utakaochakatwa kwa siku kwa tani 120; ushauri ni kwamba Serikali ije na *CIP* ndogo ndogo ili tuweze kuwasaidia wachimbaji wadogo…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa uliza swali. Umeuliza swali la kwanza. Uliza swali la pili.

**MHE. MWANAHAMISI A. MUNKUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, *CIP* ambazo ninashauri ni zile ndogo ambazo zitawasaidia wachimbaji wadogo tunaowalenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Serikali haioni haja sasa, kwa kuwa ujenzi wa vituo hivyo vya umahiri vinahitaji uwekezaji mkubwa, watumie Vyuo vya *VETA* kama *Centre of Excellence* kwa sababu vyuo hivyo vya *VETA* viko kila halmashauri ndani ya nchi yetu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali limeulizwa moja, la pili ni ushauri.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza Mheshimiwa Mwanahamisi kwa jinsi ambavyo amekuwa mtetezi wa kweli wa wachimbaji wadogo katika masuala ya kusaidia Vituo vya Uchakataji Madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanahamisi, hata mwezi haujaisha aliuliza swali ambalo limekaribia kufanana na hili, na nimelijibu hapa hapa, lakini kwa maswali yake haya mawili ya

nyongeza, moja ni ushauri. Ushauri wake kwamba hiki kituo kinachochakata tani 120 kwa siku siyo kwa saa, huenda hakitatoa huduma kwa wachimbaji wadogo ambao hawawezi kuleta mzigo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mwanahamisi kwamba vituo hivi vinajengwa na Taasisi ya Serikali na haimkatalii mtu yeyote mchimbaji mdogo mzigo wowote anaoleta ili asaidiwe kuchakata. Dhamira ya kweli ya Serikali siyo tu kuwachakatia madini yao, ni kutumia vituo hivyo kuwapa mafunzo ili wale ambao wataweza kufikia vigezo na wakawa na mitaji inayoridhisha, wakaanzisha vya kwao hata vidogo vidogo. Ushauri wake tunaupokea kwamba Serikali iendelee kusaidia utengenezaji wa *CIP* ndogo ndogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami pia ninatoa wito kwa wachimbaji wadogo ambao wanaokuja kwenye vituo vyetu kujifunza, wachukue teknolojia wakazalishe vituo vidogo vidogo vya *CIP*. Ninawapongeza wale wote ambao wameshajifunza pale na wameanzisha maana wako wengi kabisa katika kila mkoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili kuhusu kutumia *VETA* zetu kama mbadala wa maeneo ya kutolea haya mafunzo na kuanzisha *CIP* katika maeneo ya wachimbaji madini, huu ushauri ni mzuri sana, ninampongeza kwa kuishauri Serikali. Hivyo na sisi tutapenda pia kuupokea huo ushauri na kuona namna zile *VETA* zilizoko katika maeneo ya wachimbaji zinavyoweza kuingiza somo la kujenga mitambo ya kusaidia uchakataji. Pale pale wanafunzi wetu wanaosoma kwenye vyuo hivyo wapate hiyo taaluma, na baadaye nao wakawe wachimbaji wanaojua kufanya kazi hizo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri tunakushukuru kwa majibu yako kwa maswali ya Mheshimiwa Mbunge.

Tunakwenda Wizara ya Katiba na Sheria, ninamwita sasa Mheshimiwa Happiness Daniel Ngwando, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

**7 MEI, 2026**

Na. 275

**Kurekebisha Sheria ya Ndoa kwa Kumaliza Kesi za Ndoa Haraka**

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kurekebisha Sheria ya Ndoa pale wanandoa wanapotalikiana ili kumaliza kesi zao haraka?

**MWENYEKITI:** Majibu kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Zainab Athman Katimba.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha Tisa cha Sheria ya Ndoa, Sura 29 kinatafsiri ndoa kuwa ni muunganiko wa mwanamke na mwanume kwa lengo la kuishi pamoja maisha yao yote. Kwa msingi huo, Sheria ya Ndoa imeweka utaratibu wa kuanza kusikilizwa kwa mashauri ya ndoa katika Bodi za Usuluhishi wa Ndoa kabla ya kufikishwa Mahakamani kwa ajili ya maombi ya talaka, lengo likiwa kutafuta suluhu zaidi kuliko kuachana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika juhudi za kuhakikisha usikilizaji na umalizaji wa mashauri, Mahakama ya Tanzania imetoa Mwongozo wa muda wa usikilizaji kesi kulingana na Mahakama ilipofunguliwa. Kwa mujibu wa Mwongozo huo, kesi zinazosikilizwa na Mahakama ya Mwanzo, ukomo wake ni miezi sita; Mahakama ya Wilaya na Hakimu Mkazi ukomo wake ni mwaka mmoja; na Mahakama Kuu ukomo wake ni miaka miwili. Aidha, Mashauri ya Talaka, kwa mujibu wa taratibu yanaweza kusikilizwa na kuamuliwa na Mahakama za Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha taasisi ya ndoa na kuhakikisha migogoro ya ndoa inatatuliwa kwa njia ya usuluhishi, Serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imeanzisha programu ya kuwajengea uwezo Wajumbe wa Bodi za Usuluhishi wa Ndoa Nchini kote. Utekelezaji wa Programu hiyo ulianza rasmi tarehe 8 Aprili, 2026

katika Mkoa wa Kagera. Lengo ni kuhakikisha wanandoa wenye migogoro wanapata suluhu stahiki kabla ya kuwasilisha mashauri yao Mahakamani kwa ajili ya maombi ya talaka.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Happiness Ngwando, swali la nyongeza.

**MHE. HAPPINESS D. NGWANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa makuzi ya mtoto bora mwenye ubongo uliokomaa yanaanzia miaka sifuri mpaka miaka nane, wakati huo mama ndiye mlezi mkuu wa mtoto huyu, wakati anatoka kwenye familia yake anakuwa ameongozana na watoto hawa, je, Serikali haioni haja ya huu muda kuwa mrefu kwa kuwa mgogoro huu hadi unafika Mahakamani umetokea kwa Wajumbe wa nyumba kumi na Mabalozi? Kwa hiyo, mgogoro huu ulishawaka moto muda mrefu. Je, Serikali haioni huu muda wa mwaka mmoja mpaka miaka miwili ni mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa mwanamke ana mchango mkubwa kwenye familia na nyumba zetu, lakini mama huyu pale unapotokea mgogoro anatoka yeye na rambo na watoto, hata alivyochangia kwenye ile familia anakuwa habebi, je, Serikali haioni haja kuepusha migogoro isiyo na lazima, wanandoa hawa wanapogombana kila mmoja aende kwa baba yake na mama yake, mlango ufungwe, ili haki itendeke? Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Majibu, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Happiness, kwa kweli anafanya kazi kubwa sana ya kuwasemea wanawake na watoto siyo tu wa Mkoa wa Ruvuma, lakini wa Tanzania nzima kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la kwanza kwamba muda wa mpaka miaka miwili wa kesi za talaka ni muda mrefu na unaweza ukaleta athari ya mtoto na hasa mtoto wa chini ya miaka minane. Kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi, ni kwamba muda umewekwa mahususi kwa ajili ya kuhakikisha mashauri

mbalimbali yanaisha katika Mahakama ikiwemo mashauri yanayohusiana na masuala ya talaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa muda wa kumaliza Shauri la Talaka katika ngazi ya Mahakama ya Mwanzo ni miezi sita. Ndani ya miezi sita lazima shauri hili liwe limekamilika na maamuzi yametoka, lakini katika ngazi za Mahakama za Wilaya na Mahakama ya Hakimu Mkazi, ni muda wa mwaka mmoja, na katika ngazi ya juu zaidi ambayo ni Mahakama Kuu, ni miaka miwili. Kwa hiyo, mara nyingi kesi za ndoa tunaona zinaisha katika ngazi ya Mahakama ya Mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, yapo mazingira mengine ambayo kesi hizi zinaenda katika ngazi ya juu, na ndiyo maana Mahakama imeweka Mwongozo wa kutaka kuharakisha kesi hizi zisikilizwe kwa wakati ili kuweza kutoa haki hizi kwa wakati na kulinda maslahi ya wanaohusika katika mashauri haya ikiwemo watoto wadogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake sasa la pili ambalo amegusia suala la mwananmke au mke kufukuzwa kwenye nyumba ya ndoa, pindi anapokuwa kwenye shauri linalohusiana na masuala ya talaka, Sheria za Tanzania zinatambua na hasa Sheria ya Ndoa Sura ya 29 hairuhusu mume kumfukuza mke kwenye nyumba ya ndoa. Nyumba ya ndoa imetambulika kabisa kisheria, ni ile nyumba ambayo mume na mke wanaishi. Nyumba hiyo ya ndoa inakuwa na umiliki wa pande zote kwa maana ya mume na mke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mume haruhusiwi kumfukuza mke kwenye nyumba ya ndoa pindi wanapoingia kwenye Shauri la Talaka. Huo ni msingi ambao umewekwa katika Kifungu cha 59 cha Sheria ya Ndoa, lakini tumeona maamuzi mbalimbali yanatolewa na Mahakama kufafanua na kusisitiza msingi huu uliowekwa kwenye Kifungu hiki cha 59. Mathalani kwenye Kesi ya Elizabeth Dikene dhidi ya John Dikene ambayo ni Shauri la Ndoa (Na. 5) la Mwaka 2004. Mahakama imesisitiza msingi wa kwamba mume haruhusiwi kumfukuza mke kwenye nyumba yao ya ndoa wakiwa wako kwenye Shauri la Talaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunafahamu kwenye jamii kunakuwa na changamoto mbalimbali ambazo zinahusisha wanawake kukutana na mazingira kama hayo. Kwa hiyo, wanawake wanapokutana na mazingira kama hayo, wanachoweza kufanya ni kuchukua taratibu za kisheria ambapo anaweza kuwasilisha maombi ya zuio, yaani mhusika, tuseme mke anaweza akaandaa maombi ya dharura Mahakamani *(Chamber Summons)* kwa ajili ya kuiomba Mahakama kuweka zuio la muda *(Temporary Injunction)* ili asifukuzwe. Azuie aidha, kufukuzwa kwenye ile nyumba yao ya ndoa au kuzuia pia nyumba kuuzwa, kwa sababu kuna wakati mwingine unaweza ukashaangaa mpo kwenye Shauri la Talaka, lakini nyumba mnayoishi, yaani nyumba ya ndoa ipo katika kuuzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, utaratibu umewekwa, unaweza ukaomba zuio hilo la muda ili Mahakama iweze kuingilia kati na kuzuia hatua za namna hiyo. Maombi haya yanafanyika kwenye Mahakama, ambapo inasikilizwa…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu yako nadhani ameyaelewa na umempa *reference* nzuri, aende afuatilie. Malizia.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa hiyo, kwa wale wanaohitaji Huduma ya Msaada wa Kisheria, katika kila halmashauri kuna dawati la kutoa Huduma ya Msaada wa Kisheria wafike ili waweze kupatiwa suluhu ya changamoto na hususan kama hii ambayo ameitaja Mheshimiwa Happiness.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na swali letu la mwisho kwa Wizara hii hii. Ninamwita Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini, aulize swali lake.

Na. 276

**Kusimama kwa Ujenzi wa Jengo la Mahakama ya Wilaya – Mbulu**

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mbulu ambao umesimama kwa muda mrefu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama ya Tanzania imeendelea kutekeleza Mpango wa Ujenzi na Ukarabati wa majengo ya Mahakama kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya utoaji haki katika ngazi mbalimbali. Mpango huu unahusisha ujenzi wa majengo mapya pamoja na ukarabati wa majengo yaliyopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utekelezaji wa mpango huo, ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mbulu ulianza katika mwaka wa fedha 2024/2025. Hata hivyo, mradi huo umechelewa kukamilika kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake. Tayari changamoto hizo zimetatuliwa na ujenzi wa jengo hilo unaendelea na unatarajiwa kukamilika ifikapo Novemba, 2026.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zacharia Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi, na ninaishukuru Serikali kwa majibu yake mazuri. Kwa kuwa sasa Serikali imeahidi kukamilisha Mahakama hiyo ya Mbulu ifikapo mwezi Novemba, je, Serikali ina mpango gani wa kuleta samani na vitendea kazi vya kisasa kwenye jengo hilo la Mahakama?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la pili. Kwa kuwa jengo hilo la Mahakama ni la zamani, limechukua miaka mingi na ni chakavu sana na Watumishi wa Mahakama Waandamizi, na Waandamizi wengine hawana majengo ya kuishi, je, Serikali ina mpango gani wa kujenga makazi ya Watumishi wa Mahakama katika Wilaya ya Mbulu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay kwa swali lake zuri la ufuatiliaji wa maendeleo katika Mahakama na hasa katika Wilaya ya Mbulu anayotoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama kwa wakati huu, kama nilivyojibu, inatekeleza mpango wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ambao ni mpango wa miaka mitano, umegharimu mpaka wakati huu jumla ya shilingi bilioni 524.9. Mahakama imekuwa ikifanya maboresho na ujenzi wa katika ngazi mbalimbali ikiwemo katika ngazi ya wilaya. Mahakama ya Wilaya ya Mbulu ni mnufaika wa mpango huu na ndiyo maana tunatarajia mpaka itakapofika Novemba, 2026 itakuwa imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa swali lake la kwanza Mheshimiwa Mbunge kuhusiana na upatikanaji wa samani, vitendea kazi na mifumo yote, pindi ujenzi unapokuwa umekamilika, ninaomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba ukamilifu wa jengo hili la Mahakama ya Wilaya ni pamoja na kuwepo na mifumo yote muhimu inayohitajika kwa ajili ya kutoa huduma hizi za Kimahakama. Kwa hiyo, samani zitapatikana, na mifumo ya ki-TEHAMA yote itakuwepo na rasilimali watu kwa ajili ya kutoa huduma za Kimahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na swali lake la pili ambalo ameuliza kuhusiana na kupatikana kwa makazi kwa ajili ya Watumishi wa Mahakama, kweli katika mpango huu wa kuboresha miundombinu katika Mahakama, Mahakama pia inatazama siyo tu miundombinu ya majengo, lakini pia makazi ya Watumishi katika Mahakama, lakini inafanya hivyo kwa awamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kadiri fedha itakapokuwa inapatikana Mahakama imeweka kipaumbele pia kuzingatia ujenzi wa nyumba za watumishi katika Mahakama na wakati ukifika na fedha ikipatikana Mahakama itafika Mbulu pia kwa ajili ya kujenga makazi hayo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali niweze kuwatambua wageni waliopo ndani ya ukumbi wetu asubuhi hii.

Kwanza kabisa, ni wageni waliokaa Jukwaa la Spika. Wapo wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kama ifuatavyo: -

Tunaye Profesa Carolyne Nombo, yeye ni Katibu Mkuu; Profesa Daniel Mushi, Naibu Katibu Mkuu; Profesa Khamisi Dihenga, ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu; Ndugu Benadetha Ndunguru, ni Mwenyekiti wa Bodi ya Baraza la Taifa la Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi; na Profesa Yunus Mgaya ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ushauri ya *Samia Scholarship. (Makofi)*

Vilevile, tunaye Profesa Makenya Maboko, Mwenyekiti wa Kamati ya Maboresho ya Mitaala; Mheshimiwa Nurdin Babu, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro; Ndugu Daud Mrindoko, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wazazi, Mkoa wa Kilimanjaro; Ndugu Anthony Tesha, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Rombo; Ndugu Seleimen Mfinanga, *MNEC* Mkoa wa Kilimanjaro; na Ndugu Masoud Melimeli, Katibu wa CCM Wilaya ya Rombo. *(Makofi)*

Pia, tunaye Ndugu Raymond Mwangwala, Mkuu wa Wilaya ya Rombo; Ndugu Johari Athumani, Katibu Tawala, Wilaya ya Rombo; Ndugu Gilbert Tarimo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo; na Ndugu Themistocles Isdory, Katibu Mwenezi CCM Wilaya ya Rombo; Sheikh Mlewa Shaban, Sheikh wa Mkoa wa Kilimanjaro; na Ndugu Godfrida Magubo, Kiongozi Ofisi ya Jumuiya ya Madola na Maendeleo *(FCDO)*. *(Makofi)*

Vilevile, tunaye Ndugu Ayub Kafyulilo, Msimamizi wa Masuala ya Elimu kutoka Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Kuhudumia Watoto *(UNICEF);* Dkt. John Lusingu, Mshauri Mkuu wa Elimu kutoka Jumuiya ya Madola na Maendeleo *(FCDO)*; na Ndugu Abdulmalik Mollel, Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Elimu ya Kimataifa. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Profesa Mkenda ni familia yake kutoka Rombo Mkoani Kilimanjaro. Yupo Ndugu Ulirc Mkenda, mdogo wake Mheshimiwa Waziri; Ndugu Saimon Mkenda, mdogo wake Mheshimiwa Waziri; Dkt. Pendo Mkenda, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; Ndugu Mianda Mkenda, mtoto wa Mheshimiwa Waziri; na yupo Kalsta Mkenda, shemeji wa Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Wengine ni wageni watatu wa Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, Naibu Waziri, Elimu, Sayansi na Teknolojia. Hawa ni Mheshimiwa Hamida Mussa Khamis, Mkuu wa Mkoa wa Kusini Kusini Unguja; Mheshimiwa Rajab Ali Rajabu, Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja; Sabrina Ali Mohamedi, Mkurugenzi Mtendaji *Mwanamke Foundation (MIF);* tunaye Ndugu Suleiman Haroub Suleiman, yeye ni Mbunge Mstaafu; na tunaye Ndugu Mwinyi Ahmed Mwinyi yeye ni Mkuu wa Wilaya ya Arumeru. *(Makofi)*

Vilevile, tunaye Ndugu Halid Mbarouk, Mkurugenzi wa Mahusiano ya Benki na Serikali Benki ya *Exim* na Mjumbe wa Baraza Kuu la Taifa (UVCCM); na Ndugu Duraya Sebabili, Mgeni wa Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Tuna Wageni wengine 150 hawa ni Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, hawa ni Wanafunzi na Walimu wa Shule ya Feza kutoka Jijini Dodoma, karibuni sana, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Tunao Wageni wa Waheshimiwa Wabunge wengine. Wapo wageni watano wa Mheshimiwa Maryprisca Winfried Mahundi, Naibu Waziri, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Hawa ni marafiki zake ambao wapo kwenye makundi mawili: kundi la kwanza ni Nasra *House Fashion* na Nasra *Kids Fashion* wanaotoka Mbeya Mwanjelwa na Kariakoo. Tuwaone, wale pale. Karibuni sana. *(Makofi)*

Kundi la pili ni Kampuni ya *Chido Point,* hawa ni wasusi maalumu kutoka Jijini Dar es Salaam; Ndugu Maria Wilson Mwampanga na Ndugu Maria Samwel Moshi kutoka Dar es Salaam. Karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Ibrahim Mohamed Shayo, Ndugu Asnath Adam ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Vilevile, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Haran Nyakisa Sanga kutoka *Aya Sophia Villa* ya Kigamboni Jijini Dar es Salaam.

Tunaye Mgeni wa Mheshimiwa Innocent Lugha Bashungwa, huyu ni Ndugu Joshua Mushenyera, Mpigakura wake kutoka Karagwe Mkoa wa Kagera. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, hawa ni familia yake kutoka Mbozi, Mkoani Songwe. *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Thomas Kitima (Chifu huyu), hawa ni Watumishi wa Umma kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Poa tunao Wageni 11 wa Mheshimiwa Anna Richard Lupembe, hawa ni Wanamaombi wa Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati nikiwatambulisha Wageni kutoka Feza, kuna kijana anaitwa Ndugu Tamimu Hamis Taletale, asimame tumwone. Huyu ni mtoto wa Mbunge mwenzetu Babu Taletale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya Mafunzo. Hawa ni walimu watatu wa Shule ya Msingi Msanga B kutoka Kata ya Msanga Wilaya ya Chamwino, Mkoa wa Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine 84 na walimu 15 kutoka Shule ya Msingi Antonia ya Jijini Dodoma, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wakati nikitambulisha Wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri, nilimwacha mgeni mmoja; huyu ni Ndugu Edward Chibombo, Meneja wa Tawi la Benki ya *EXIM* – Dodoma, karibu sana. *(Makofi)*

Vilevile, katika hawa wanaotoka Feza, tuna kijana anaitwa Sharon Kihenzile; huyu ni mtoto wa Mbunge mwenzetu. Asimame tumwone, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, kuna matangazo mengine. Tangazo la kwanza ni kutoka kwa Katibu wa Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, mnatangaziwa kuwa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania *(TPBA)* kimeandaa Mbio za *Marathon* zinazojulikana kama Wakili *Marathon* 2026. Lengo la mbio hizi ni kukusanya rasilimali fedha ili kusogeza huduma za msaada wa kisheria karibu na wananchi kupitia mfumo wa kidigitali hususan walio katika mazingira ya vijijini, pembezoni mwa mji au miji, wanawake, wazee, watu wenye ulemavu na wagonjwa ambao hukosa fursa ya kuzifikia huduma hizo kwa urahisi.

Waheshimiwa Wabunge, kauli mbiu ya mbio hizo ni 'Kusogeza Huduma za Msaada wa Kisheria Karibu Zaidi na Mtanzania' na zinatarajiwa kufanyika siku ya Jumapili tarehe 31 Mei, 2026 Jijini Dodoma. Usajili wa Waheshimiwa Wabunge na Watumishi wa Bunge utafanyika katika Viwanja vya Bunge kwenye Banda la Usajili *Gazebo* lililopo nyuma ya Ukumbi wa Msekwa. Wabunge wote na Watumishi wa Bunge mnaombwa kushiriki mbio hizi muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo lingine kutoka kwa Katibu wa Bunge. Wote mnatangaziwa kuwa siku ya Jumatatu tarehe 11 Mei, 2026 kutakuwa na semina itakayotolewa na Wizara ya Uchukuzi kuhusu miradi inayotelezwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA),* Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA),* Taasisi za Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC)* na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA)*.

Waheshimiwa Wabunge, Semina hii itafanyika saa saba mchana mara baada ya kusitisha Shughuli za Bunge katika Ukumbi wa Pius Msekwa. Wote mnakaribishwa kuhudhuria semina hii muhimu ili kufahamu miradi mbalimbali inayotekelezwa na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Uchukuzi.

Waheshimiwa Wabunge, tangazo la mwisho kutoka kwa Katibu wa Bunge ni kwamba, wote mnatangaziwa kuwa siku ya Jumamosi tarehe 9 Mei, 2026 kutakuwa na Semina itakayotolewa na Wizara ya Afya kuhusu utekelezaji wa Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote. Semina hii itafanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa saa tano asubuhi. Wabunge wote mnasisitizwa kuhudhuria Semina hii muhimu.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa matangazo kwa sasa, tutaendelea na ajenda yetu.

**MHE. ADO S. ADO:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mwongozo wa Spika, Mheshimiwa Ado.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniona. Ninaomba Mwongozo juu ya suala moja muhimu sana. Leo Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Dugange akiwa anajibu swali dogo la nyongeza kuhusu Kituo cha Afya Nampungu, swali ambalo limeulizwa na Mbunge wa Viti Maalum, Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, kwa maoni yangu, alitoa majibu ambayo yanapishana na swali hilo hilo ambalo mimi nililiuliza wiki tatu zilizopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninauliza, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI wa Afya kwa maana ya upande wa afya Mheshimiwa Dkt. Jafar Seif alisema kwamba Serikali inatambua Kituo cha Afya Nampungu ni kituo cha kimkakati na kwamba maombi ya fedha kwa maana ya shilingi milioni 250 zilizosalia yameshakuwa *processed* na yamewasilishwa Hazina, kinachosubiriwa ni malipo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majibu ya leo yanasema agizo linatolewa kwa Mkurugenzi na kwa Wakurugenzi wote nchini waweze kuwasilisha taarifa hizo, na pia wajipange kutenga fedha kwa yale mambo ambayo yanaweza kugharamiwa na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni majibu mawili tofauti kwa swali lile lile. Sasa *consistency* katika majibu yanayotolewa ni jambo muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Mwongozo wako juu ya suala hili. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Mheshimiwa Ado Shaibu akiomba Mwongozo wa Kiti kuhusiana na swali lililoulizwa leo asubuhi.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 79 ambayo inaruhusu kutoa Mwongozo, nimepokea, maelezo yako, lakini kwa vile Kiti kinahitaji nafasi ya kuweza kupitia *Hansard* ili iweze kutoa Mwongozo ambao utakuwa unafaa katika mazingira haya, kwa hiyo, tutawasiliana na Meza ili tuweze kutoa Mwongozo kwa siku zijazo. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Sasa nimwite Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda aweze kutoa Hotuba yake. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa ninaomba hotuba yangu yote iingizwe kwenye *Hansard* kama ilivyowasilisha Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua na kutoa ushauri wa

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 46, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Fungu 18, Tume ya Taifa ya *UNESCO*, sasa ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio haya ya mapato na matumizi yanayowasilishwa yamelenga katika kuhakikisha uwekezaji katika elimu, sayansi na teknolojia unachangia kujenga rasirimali watu yenye ujuzi, maarifa na ushindani kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena mbele ya Bunge lako Tukufu, kuwasilisha Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Taifa ya *UNESCO* kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika uchaguzi uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindi huu unadhihirisha imani kubwa waliyonayo Watanzania kwa Mheshimiwa Rais na uongozi wake mahiri unaoendelea kuleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Elimu na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Tunaomwombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema na baraka tele katika uongozi wake. Ahadi yetu kwa Mheshimiwa Rais ni kuendelea kufanya kazi kwa bidii na maarifa katika kutekeleza maono yake katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninampongeza Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kuteuliwa na Rais na kupitishwa na Bunge hili Tukufu, kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilala na kwa kupata imani ya Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge hili la Kumi na Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia Mheshimiwa Daniel Baran Sillo kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, ninaomba kutumia nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge; Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso na wewe Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, kwa kuaminiwa katika nafasi hizi muhimu sana katika Bunge hili Tukufu. Mheshimiwa Spika na wasaidizi wake wote wanaliongoza Bunge letu vizuri kwa umakini, umahiri na weledi mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninaomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana, pamoja na Naibu Waziri, Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, kuisimamia na kuiongoza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mwenyekiti wa Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe, na Wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wanaotoa kwetu, hasa katika kuisimamia na kuishauri Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya kazi kubwa ya kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2026/2027. Maoni na ushauri uliotolewa na Kamati umetusaidia sana wakati wa maandalizi ya Bajeti ya Wizara. Ninaiahidi Kamati kuwa, tutaendelea kupokea maelekezo, maoni na ushauri wao na kuufanyia kazi, kwa ajili ya maendeleo ya Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kuwapongeza Mawaziri na Naibu Mawaziri wote walioteuliwa na kuongoza Wizara mbalimbali kwa kuzingatia kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni mtambuka, ninawaahidi kutoa ushirikiano katika kuhakikisha tunatoa huduma na kuleta maendeleo kwa Taifa letu wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, hii ni hotuba yangu ya kwanza kwenye Bunge hili la Kumi na Tatu, ninaomba nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kwao kuwa Wabunge wa Bunge la Kumi na Tatu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni sana Waheshimiwa na ninaomba ushirikiano wenu katika kuendeleza elimu, sayansi na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuwashukuru viongozi wenzangu, watendaji na watumishi wote wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa utendaji mahiri na ushirikiano wanaoutoa katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninamshukuru sana Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, Naibu Waziri, kwa uchapakazi wake na ushirikiano wa hali ya juu anaoutoa katika kuongoza Wizara. Ninamshukuru pia Katibu Mkuu Profesa Caroline Ignatius Nombo na Naibu Makatibu Wakuu, Profesa Daniel Elius Mushi na Dkt. Hussen

Mohamed Omar kwa utendaji kazi wao wenye bidii na weledi mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Rombo kwa kuniamini na kunichagua kuendelea kuliongoza jimbo hilo. Ninawashukuru kwa kuendelea kushirikiana nami katika kuleta maendeleo ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana familia yangu, hususan mke wangu mpendwa Beatrice, kwa kunitia moyo na kuniwezesha kutimiza majukumu yangu kwa umakini, juhudi na ari kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuungana na Wabunge wenzangu wote waliotangulia kutoa salamu za pole kwa Bunge lako Tukufu, kwako wewe binafsi, familia na wananchi wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu. Kwanza, Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, aliyekuwa Mbunge wa Peramiho, aliyefariki tarehe 11 Disemba, 2025. Marehemu Jenista Mhagama aliwahi kuwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, katika mwaka 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ni Mheshimiwa Halima Iddi Nassor, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu, ambaye alifariki tarehe 18 Januari, 2026. Tatu ni, Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi, aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Uratibu, na Wenye Ulemavu na Mbunge wa Jimbo la Ismani, aliyefariki tarehe 25 Machi, 2026. Hakika kuondokewa na viongozi hawa ni pigo kwa familia na Taifa letu kwa ujumla, lakini mchango wao utaendelea kuwa chachu ya maendeleo ya sekta mbalimbali, ikiwepo Sekta yetu ya Elimu. Tutaendelea kuyaenzi maisha yao na kujifunza kutoka kwa uongozi wao mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninatoa pole kwa Watanzania wote walioondokewa na ndugu zao kutokana na maradhi na sababu mbalimbali. Ninawaombea marehemu wote, Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi, Amina!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, ninaomba sasa kutoa Taarifa ya Utelekezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Fungu 46 na Fungu 18, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Taarifa hii inaelezea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Mwelekeo wa Kimkakati wa Sekta ya Elimu katika Kuchangia Maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, idara, vitengo na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zilikadiria kukusanya maduhuli yenye thamani ya shilingi 720,507,879,789.63. Kati ya fedha hizo, shilingi 8,402,257,000 ni makusanyo ya idara na vitengo vya Wizara na shilingi 712,105,622,789.63 ni makusanyo ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli hayo ni ada, malipo ya ushauri elekezi, mchango wa uthibiti ubora wa shule na baadhi ya huduma zinazotolewa na Wizara pamoja na taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo haya yanaonesha mchango mkubwa wa taasisi zilizo chini ya Wizara katika kuongeza mapato ya ndani na kuimarisha uendelevu wa Fedha katika Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara imekusanya jumla ya shilingi 520,140,680,477.35 sawa na 72% ya makadirio, ambapo shilingi 6,868,106,833 zimekusanywa na idara na vitengo; na shilingi 513,272,573,644.35 zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Hali hii inaashiria mwenendo wa kuridhisha wa ukusanyaji wa mapato unaoendana na matarajio ya Serikali licha ya changamoto mbalimbali za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha shilingi 2,826,078,405,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ya Fungu 46, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambapo shilingi 688,614,234,000 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 2,137,464,171,000 zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya

maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18), Wizara iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 3,240,288,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zilizoidhinishwa zimeelekezwa katika maeneo ya kimkakati, ikiwemo kuboresha miundombinu ya elimu, kuimarisha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuongeza upatikanaji wa vifaa vya elimu. Uwekezaji huu unaendelea kuhakikisha kila Mtanzania anapata elimu bora inayomwezesha kushiriki kikamilifu katika uchumi wa Taifa na kuhakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara imetekeleza vipaumbele vitano kwa lengo la kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo pamoja na matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu, ili kuchangia katika maendeleo endelevu ya Taifa. Vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo: -

(a) Kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria, kuandaa miongozo ya utoaji elimu na mafunzo nchini;

(b) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali, ufundi na ufundi stadi katika shule za sekondari na vyuo vya amali;

(c) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu;

(d) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na mwisho,

(e) Kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele hivi vimechaguliwa kwa kuzingatia mahitaji ya Taifa kwenye uchumi wa viwanda, kuongeza

ajira kwa vijana na kuimarisha ushindani wa Kimataifa kupitia elimu, sayansi na teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutekeleza sera, mipango na mikakati mbalimbali inayoimarisha utoaji wa elimu na mafunzo nchini, kwa lengo la kuzalisha rasilimali watu yenye ujuzi na maarifa stahiki yatakayomwezesha Mtanzania kujiajiri au kuajiriwa, pamoja na kuchangia katika maendeleo endelevu ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023, Serikali imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa elimu ya lazima ya miaka 10, ambapo takribani wanafunzi 3,021,177 wanatarajiwa kujiunga na elimu ya sekondari kidato cha kwanza ifikapo 2028. Idadi hiyo inatokana na idadi ya wanafunzi waliopo darasa la tano na darasa la sita kwa mwaka huu 2026, watakaomaliza elimu ya msingi mwaka 2027 na watakaojiunga na elimu ya sekondari mwaka 2028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI, imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya madarasa, maabara, karakana, ununuzi wa vifaa, pamoja na kutoa ajira mpya za walimu, ili kuwezesha mapokezi ya wanafunzi husika. Hatua ya utekelezaji wa elimu ya lazima ya miaka 10 ni ya kihistoria, kwani itaongeza kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa elimu ya sekondari na kuandaa kizazi kipya chenye ujuzi na maarifa na kuendana na lengo Namba Nne la Maendeleo Endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Tanzania umri wa kuanza darasa la kwanza ni miaka sita. Kwa hiyo, mtoto aliyeanza darasa la kwanza akiwa na miaka sita anamaliza darasa la saba akiwa na miaka 13 tu. Huu ni umri ambao mtu hawezi kuajiriwa wala kuajirika. Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023, imerekebisha jambo hili kwa kufanya elimu ya lazima kuwa ni miaka 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, kijana atamaliza elimu ya lazima akiwa na miaka 16. Kwa hiyo, mageuzi ya kufanya elimu ya msingi iwe ni miaka sita, lakini elimu ya lazima iwe ni miaka 10 ni mkakati wa kuhakikisha kijana hawezi kutoka kwenye mfumo wa elimu kabla

hajakaribia umri wa kuajirika na au kujiajiri. Mkakati wa pili unaozingatia fursa katika ajira ni kuanzisha mkondo wa amali katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeendelea na mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353, ambapo tayari imekamilisha kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu na kuandaa Taarifa ya Awali ya Mapitio ya Sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mapitio ya Sheria, Serikali imeandaa viunzi mbalimbali, ili kuendana na mahitaji ya sera, ikiwemo Kiunzi cha Umahiri wa Walimu katika TEHAMA 2026, ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza, Kiunzi cha Kitaifa cha Uanzishaji na Uendelezaji wa Ushirikiano Kati ya Serikali na Wadau wa Teknolojia za Kidigitali katika Sekta ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali pia, imeandaa miongozo mbalimbali ikiwepo miongozo nane ya utoaji wa elimu jumuishi. Miongozo hiyo ni pamoja na Mwongozo wa Sanaa na Michezo Rekebifu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu wa Mwaka 2026, Mwongozo wa Matumizi ya TEHAMA na Teknolojia Saidizi kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalumu wa Mwaka 2026, Mwongozo wa Lugha ya Alama ya Tanzania wa Mwaka 2026 na Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Amali kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu wa Mwaka 2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siku 100 tangu kuapishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alionesha dhamira yake ya dhati ya kuleta mageuzi katika Sekta ya Elimu yatakayokuwa msingi imara kwa wanafunzi kujifunza na kuandaa wahitimu wenye ujuzi na uwezo wa kujiajiri na kuajirika na kushindana katika soko la ajira Kimataifa. Katika kufikia azma hiyo ya Mheshimiwa Rais, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, imeandaa Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wa elimu ya awali na wanafunzi wa darasa la

kwanza na la pili ambao ulizinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tarehe 29 Januari, 2026 Jijini Dar es Salaam. Mpango huu ni hatua ya kimkakati ya kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayefikia darasa la tatu bila kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, imeandaa mkakati wa pamoja kati ya waajiri, vyuo vya ufundi stadi na vyuo vikuu ambao ulizinduliwa na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, tarehe 9 Februari, 2026 Jijini Dar es Salaam. Mpango huo unalenga kuimarisha ushirikiano baina ya Sekta ya Ajira na Viwanda na taasisi za elimu, ili kuandaa wataalamu kulingana na mahitaji, wanafunzi kujifunza kwa vitendo pamoja na kuwezesha wahitimu kujiajiri au kuajiriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matarajio yetu kuwa mpango wa pamoja kati ya waajiri, vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vikuu, utaimarisha ushirikiano na viwanda. Vilevile, utahamasisha waajiri kutoa fursa zaidi za ajira kwa wahitimu na kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi na hivyo kupunguza au kuondoa kabisa changamoto ya kukosekana kwa uwiano baina ya ujuzi na mahitaji ya soko la ajira *(skills mismatch)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imedahili wanafunzi 315,307 kati yao wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi ni 236,199 na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 79,108 sawa na 119% ya lengo la kudahili wanafunzi 265,000. Ongezeko hili la kudahili linaonesha mafanikio makubwa ya Serikali katika kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Hii ni hatua muhimu katika kujenga nguvu kazi yenye ujuzi na inayoongeza ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, ili kuongeza fursa ya amali, ikiwemo ujenzi wa *VETA* 64 za wilaya na chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe, ambapo wastani wa ujenzi umefikia 68%. Mradi huu wa kimkakati utaongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya ufundi katika ngazi ya wilaya, hivyo kuwezesha vijana wengi zaidi kupata ujuzi bila kulazimika kuhama

maeneo yao. Hatua hii pia itaongeza usawa wa upatikanaji wa elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ukarabati wa miundombinu ya vilivyokuwa Vyuo vya Ualimu Mtwara Kawaida na Mtwara Ufundi. Vyuo hivi pia, vimeunganishwa na kuwa Ndaki ya Mtwara ya Ualimu Ufundi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, ambapo ukarabati umefikia 68%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuvipa hadhi vituo vya umahiri, ili kuimarisha utoaji wa mafunzo ya fani za kipaumbele zinazolenga kuzalisha wataalamu waliobobea, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, imekamilisha ujenzi wa jengo lenye kumbi za mihadhara, maabara, ofisi pamoja na kuweka vifaa vya kisasa vya TEHAMA na teknolojia katika Kituo cha Kikanda cha Umahiri katika TEHAMA kilichopo katika Taasisi ya Teknolojia, Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, imeendelea na ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Uchakataji na Utengenezaji wa Bidhaa za Ngozi na Teknolojia Shirikishi katika Kampasi ya Mwanza ya chuo hicho hicho kinachojumuisha mabweni mawili, jengo maalumu la taaluma, jengo la utawala, madarasa na jengo la kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, inatekeleza Mpango wa Kitaifa wa Kuimarisha Elimu ya Ufundi na Umahiri unaolenga kuandaa walimu wenye ujuzi wa kisasa na mbinu shirikishi za ufundishaji, ambao umewezesha walimu 150 wa amali za kihandisi kwenda *New Delhi, India* kwa mwezi mmoja. Walimu hao walipatiwa mafunzo ya umahiri katika ufundishaji wa masomo ya amali katika vyuo vya huko na pia, walipata fursa ya kushiriki mafunzo kwa vitendo katika shule za ufundi na ufundi stadi nchini humo. Hatua hiyo ni ya kimkakati na inadhihirisha dhamira ya Serikali ya kuwekeza katika rasilimali watu na kuhakikisha walimu wanakuwa chachu ya mabadiliko ya elimu na ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, udhibiti ubora wa elimu katika shule za awali, msingi, sekondari, na vyuo vya ualimu ni muhimu katika kuhakikisha elimu inayotolewa katika asasi hizo inazingatia taratibu na miongozo inayotolewa na Wizara. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kuimarisha uthibiti ubora wa shule na vyuo vya ualimu kwa kufanya tathmini ya jumla katika asasi 8,067 zikihusisha shule za awali na msingi, sekondari, vyuo vya ualimu na vituo vya elimu nje ya mfumo rasmi na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi. Aidha, asasi zilizobainika kuwa na upungufu zilipewa ushauri stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuongeza upatikanaji wa vitabu vya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu, ili kufikia lengo la uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi kwa kutekeleza hatua mbalimbali. Serikali imeendelea kutambua na kukuza kazi za uandishi bunifu kwa kuibua vipawa katika uandishi wa Fasihi ya Kitanzania, kuongeza machapisho na kukuza tabia ya usomaji kwa kutekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, imeratibu utoaji wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu, ili kuwatambua waandishi mahiri wa kazi za fasihi, ambapo miswada 260 imepokelewa na kufanyika tathmini katika Duru ya Nne ya utoaji wa tuzo hii. Miswada hiyo 260 imegawanyika kama ifuatavyo: Riwaya miswada 53, Ushairi 83, Hadithi za Watoto 73 na Tamthiliya 48.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miswada hii ilipitiwa na jopo la majaji ambao walichambua na kuchagua mshindi wa kwanza, mshindi wa pili na mshindi wa tatu wa kila nyanja. Washindi hawa watatu kwa kila nyanja walipewa zawadi stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mshindi wa kwanza kwa kila nyanja alipewa zawadi na kutambuliwa kwa tuzo na Muswada wa kila mshindi wa kwanza unachapishwa na kusambazwa kwa wasomaji. Sherehe ya utoaji wa tuzo hii wa duru hii ilifanyika tarehe 13 Aprili mwaka 2026 na hii ni tarehe ambayo Mwalimu Nyerere alizaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Duru ya Nne ya utoaji wa tuzo hii, ambayo ilifanyika tarehe 13 Aprili kama nilivyoeleza, mgeni rasmi

alikuwa Mwalimu Abdilatif Abdalla, ambaye ni mtunzi nguli wa mashairi, Mtafsiri wa Vitabu vya Fasihi Andishi na mshindi wa Tuzo ya Jomo Kenyata ya Fasihi Andishi. Tuzo hii inasimamiwa na Kamati Maalumu inayofanya kazi kwa uhuru, umahiri na weledi, kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, imechapisha na kusambaza nakala 142,000 za vitabu vya washindi wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Vitabu hivyo vimegawanywa katika nyanja kama ifuatavyo: Riwaya nakala 50,000, Ushairi nakala 50,000 na Hadithi za Watoto nakala 42,000. Vitabu hivi vimesambazwa katika shule za sekondari 6,418 na shule za msingi 18,061.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kusimamia matumizi ya teknolojia katika kufundishia na kujifunzia kwa kuimarisha jukwaa la ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wa sekondari; kulifunganisha na teknolojia ya akiliunde kama msaidizi wa mwanafunzi katika kujisomea; kufanya majaribio ya kidijiti na kujipima. Vilevile inaboresha jukwa la shule mtandao kuwa jumuishi ili kuwezesha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kutumia maudhui ya kielektroniki kwa urahisi kupitia TEHAMA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Shindano la Walimu la Stadi za Kufundishia utakaotumiwa na walimu shule za msingi na sekondari kwa masomo yote, ambapo jumla ya walimu 2,800 wamewasilisha *video* za ufundishaji ili kufanyiwa tathmini. Mfumo huu unaongeza ufanisi wa kuwapata walimu mahiri watakaopata zawadi mbalimbali, ikiwemo kurekodi *video* za mfano zitakazotumiwa na walimu wengine katika kufundishia na kujifunzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha upatikanaji wa vifaa kwa walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalumu, ikiwemo kununua na kugawa vifaa vya elimu na saidizi kwa walimu, wakufunzi na walimu tarajali wenye ulemavu. Vifaa hivyo ni pamoja na *computer* mpakato, mashine za kidijiti za kurekodi sauti, *tablets*, mashine za *braille* ya kielektroniki, emboza, mashine za kuongeza sauti na seti za kupima usikivu. Vifaa hivyo vimesambazwa

katika shule za msingi 309, shule za sekondari 629 na vyuo vya ualimu 10. Wanufaika wa vifaa hivyo ni wenye ulemavu wa viungo, wenye changamoto ya uoni, wenye uziwi, wenye ualbino na wenye usikivu hafifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafunzo endelevu ni muhimu katika kuendeleza na kuimarisha utekelezaji wa kazi ya walimu, wakufunzi, wadhibiti ubora wa shule na wasimamizi wa elimu nchini. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imetoa mafunzo mbalimbali ikiwemo kutoa mafunzo kwa walimu na wanafunzi 206,296 kuhusu matumizi ya majukwaa ya kidijiti na maktaba mtandao ili kuwawezesha walimu kutumia maktaba mtandao na nyenzo nyingine za kidijiti katika utekelezaji wa mtaala na imetoa mafunzo kwa walimu 124,601 kwa mchanganuo ufuatao:

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufundishaji wa stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu; usimamizi wa utekelezaji wa mafunzo endelevu ya walimu kazini kwa wakuu wa shule; na mbinu mbalimbali za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji darasani kwa walimu wa shule za msingi na sekondari. Mafunzo haya yanaimarisha umahiri wa walimu na kuongeza ubora wa ujifunzaji darasani. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha mageuzi ya elimu yanafanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imewarejesha wanafunzi 3,467 ikiwemo wanawake 2,062 na wanaume 1,402 waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali, ambao wanaendelea na shule kupitia elimu kwa njia mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imefanya tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa sera na miongozo ya kuwa-*register* shuleni wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali. Tathmini imewezesha kubaini mafanikio katika utekelezaji wa sera na miongozo pamoja na changamoto zinazoweza kuathiri utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha fursa katika elimu ya juu kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa stashahada na shahada kwa kutekeleza yafuatayo: Imeratibu udahili wa wanafunzi 170,916 walioomba kujiunga na elimu ya juu kwa ngazi ya

shahada ya kwanza katika vyuo vya elimu ya juu nchini kwa mwaka wa masomo 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya maombi hayo, waombaji 159,010 sawa na 93% walidahiliwa ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 21,193 ukilinganisha na wanafunzi 137,817 waliodahiliwa katika mwaka wa fedha 2024/2025 na imetoa mkopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu 287,120 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi 245,384 waliopata mikopo kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko ya kasi ya teknolojia hasa katika masuala ya akiliunde *(artificial intelligence)* ni fursa kubwa sana kwa binadamu kuweza kufanya maisha yakawa bora zaidi. Akiliunde itaboresha sana tiba na afya ya binadamu kwa ujumla, itaongeza tija katika kilimo, itaboresha na kuimarisha sana elimu, itabadilisha sana namna nchi inavyoweza kusimamia ulinzi na usalama na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, akiliunde na taaluma kama hizi inakua kwa kasi sana duniani na ni maendeleo ambayo hayaepukiki na hayazuiliki, lakini mabadiliko haya ya teknolojia yanaweza kuwa ni changamoto kubwa na ya kutisha kwa binadamu kama juhudi stahiki zisipochukuliwa za kuielewa, kuimudu na kuisimamia teknolojia hii ya akiliunde na teknolojia zinazoendana nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, kuna uwezekano mkubwa sana wa muundo wa ajira kubadilika sana na kusababisha watu wengi kupoteza ajira kwa sababu ya kasi na ukubwa wa maendeleo ya teknolojia. Akiliunde pia inaweza kuumiza watu na nchi kwa namna nyingi, ikiwa ni pamoja na kugusa mambo ya ulinzi na usalama, kuingilia taarifa za watu bila mipaka na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali, inatambua kuwa ni muhimu kujenga uwezo wa nchi yetu katika kuielewa, kuimudu na kuitumia vizuri teknolojia ya akiliunde na teknolojia kama hizo ili kufanya maendeleo haya yawe fursa badala ya kuwa changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua umuhimu wa kujenga na kuimarisha uwezo wa nchi yetu katika masuala ya akiliunde na

teknolojia za mwelekeo huo, Serikali imeanzisha utaratibu wa kufadhili vijana wa Kitanzania kwenda kusomea mambo ya akiliunde. Moja ya hatua hizi ni kufadhili vijana wa Kitanzania kusoma nje ya nchi katika vyuo vizuri na ambavyo vina utaratibu mzuri wa kutoa taaluma darasani na ujuzi kwa ushirikiano na makampuni ya teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa minajili hiyo, Wizara imeanzisha ufadhili unaojulikana kama *Samia Scholarship Extended Data Science, Artificial Intelligence and Allied Sciences*. Ufadhili huu unaendeshwa kwa uwazi na ushindani na nitarudia, ufadhili huu unaendeshwa kwa uwazi na kwa ushindani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuanzia wanafunzi 50 waliopata ufaulu wa juu zaidi katika matokeo ya kidato cha sita mwaka 2025 kwenye tahasusi za sayansi zinazojumuisha hisabati walichaguliwa kwa ajili ya kupelekwa nje kwa masomo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanafunzi hawa wamechaguliwa kutokana na matokeo yao kuwa bora zaidi kuliko wengine, ni utaratibu wa uwazi na ushindani. Wanafunzi hao walipelekwa kwenye kambi ya mafunzo katika taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela. Kambi hii ya mafunzo ni ya maandalizi ya wanafunzi hawa kabla hawajapelekwa nje kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya wanafunzi hao 50, 16 wameshapelekwa Chuo Kikuu cha Johannesburg kuanza masomo. Wanafunzi 34 waliobaki wameshakubaliwa kujiunga na vyuo vikuu nchini *Ireland*. Kati yao wanafunzi 32 watajiunga na Chuo Kikuu cha Limerick nchini *Ireland* na wanafunzi wawili watajiunga na Chuo Kikuu Kishiriki cha *Dublin* nchini *Ireland*. Wanafunzi hawa wanatarajia kuondoka nchini kuelekea *Ireland* mwezi wa Tisa mwaka 2026 na watakuwa wageni wetu hapa Bungeni, siku ya leo baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanufaika wa mpango wa *Samia Scholarship Extended (SAI+)* wamepata punguzo la ada ya masomo kwa 50% katika Chuo Kikuu cha Limerick nchini *Ireland* kufuatia makubaliano yaliyotiwa saini mwezi Machi, tarehe 26, 2026 Jijini Dar es Salaam. Makubaliano hayo yamelenga kuongeza fursa za elimu ya

juu kwa vijana wa Kitanzania katika fani za kisasa zikiwemo hiyo ya *Science data*, akiliunde na sayansi shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana hao ni sehemu ya wanufaika hawa 50 kama nilivyosema. Kwa upande wa wanafunzi 16 waliokwenda Chuo Kikuu cha Johannesburg nchini Afrika Kusini, makubaliano ya ushirikiano yaliyopo yaliwawezesha kufikiriwa katika kundi la wanafunzi wanaotoka nchi za *SADC* ambao wanalipa ada kiasi kidogo ukilinganisha na ada nyingine; na tumeambiwa kwa ufaulu wao duru nyingine hawatalipishwa ada yoyote kwa sababu tunachukua wale walio bora, waliofaulu vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu ni hatua muhimu katika kuwezesha vijana wenye vipaji kupata elimu na ujuzi unaoendana na mahitaji ya dunia ya sasa ya kidijitali ikiwa ni jitihada ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 inayosisitiza umuhimu wa kuandaa nguvu kazi yenye ujuzi hasa katika maeneo ya sayansi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuwakaribisha wadau wa elimu kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuchangia Mfuko wa *Samia Scholarship* ili kuongeza idadi ya wahitimu katika masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali imeendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza vyuo vikuu ambao wamefanya vizuri zaidi katika masomo ya sayansi na wameenda kusoma masomo ya sayansi. Tunatoa shahada ya Umahiri katika vyuo bora duniani katika fani za *nuclear medicine*, *medical physics, nuclear engineering and power plants and research reactors* kupitia *Samia Scholarship Extended nuclear science*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuimarisha ushirikiano baina ya vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi ambapo kwa kutekeleza hayo, imepokea ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 260 kutoka nchi wahisani kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, Urusi wanafunzi 150, China 49, Hungary 21, Jumuiya ya Madola 11, Misri 10, Algeria Nane, Morocco Nne, Mauritius Nne, Korea Kusini wawili, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomu mmoja. Aidha, imeendelea kutoa ufadhiri kwa wanafunzi 15 kutoka China wanaosoma lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika taasisi za elimu ya juu kwa kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali ikiwemo kuendelea na ujenzi wa majengo mapya 130 yanayojumuisha madarasa, maabara 10 za mihadhara, ofisi, mabweni na vituo vya utafiti katika maeneo 47 ya taasisi 20 zilizotekeleza mradi wa elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi miongozo inayotolewa na mahitaji ya soko la ajira, Serikali imeendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu na taasisi ya elimu ya juu kwa kutoa ithibati kwa programu 233 kati ya 461 zilizofanyiwa tathmini kama ifuatavyo: Astashahada saba, Shahada 193, Shahada ya Uzamili 23 na shahada ya uzamilifu 10.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Serikali imeendelea kuwezesha wahadhiri na watumishi waliopo katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu na muda mfupi kwa wataumishi 1,179 kwa ngazi mbalimbali, astashahada tatu, stashahada 12, shahada ya kwanza 37, shahada ya umahili 422 na shahada ya uzamivu 703 na muda mfupi kwa watumishi 1,289 kwa taasisi za elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti ni nyenzo muhimu katika kuongeza maarifa mapya, kuchochea maendeleo ya uchumi na kutatua changamoto mbalimbali za kijamii. Serikali kwa kutambua umuhimu huo, imeratibu jumla ya miradi 168 ya utafiti na ubunifu ikiwemo miradi 19 ya Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na ubunifu (MAKISATU).

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, imeendelea na utekelezaji wa miradi ya utafiti 261 kupitia taasisi za elimu ya juu na vyuo vya elimu ya ufundi katika maeneo mbalimbali ikiwemo ardhi, ujenzi, maji, tabia nchi, mazingira, kilimo, afya, elimu, viwanda, sayansi ya jamii, teknolojia, biashara na ushirika na uwekezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukabiliana na changamoto za kimazingira na kulipa uwezo Taifa katika maendeleo ya viwanda, uchumi na ustawi wa wananchi kwa ujumla, Serikali imefadhili miradi 39 ya utafiti katika sekta mbalimbali kama vile kilimo, maji, afya, nishati, bioanuwai, mifumo ya miji na utawala bora wa hali ya hewa. Uwekezaji huu utawezesha wanasayansi wa Kitanzania kuendelea na utafiti wa tabianchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza utekelezaji wa Mfuko wa *Samia Innovation Commercialization Fund* unaolenga kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wabunifu ili kuwawezesha kubidhaisha na ubiashalishaji wabunifu na teknolojia za wabunifu wetu. Katika awamu ya kwanza wabunifu saba wamefanikiwa ambapo jumla ya shilingi milioni 767 zimetolewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia taasisi ya elimu ya juu na vyuo vya elimu ya ufundi imechapisha machapisho 1,556 ya kitaaluma katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa ili kuongeza maarifa katika jamii kuhusu namna ya kutatua changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile imeendelea kutoa huduma 230 za ushauri elekezi katika miradi mbalimbali ikiwemo ugani, vyama vya ushirika, matumizi ya udongo, mawe na nyenzo zinazotumika katika ujenzi wa miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kudhibiti na kuimarisha matumizi salama ya mionzi ya *nuclear* hapa nchini kupitia Tume ya Nguvu za Atomu kwa kupima sampuli 31,739 za vyakula na vifaa vya mlolongo wa chakula ili kubaini uwepo wa uchafuzi wa mionzi. Matokeo ya vipimo vya sampuli hizo yalionesha kutokuwepo kwa uchafuzi wa mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* imeendelea kutekeleza majukumu yake ikiwemo kuanzisha kwa utekelezaji wa programu ya *Breach Tanzania* 2025/2026 inayolenga kuwawezesha vijana waliokosa fursa ya elimu kupitia mfumo rasmi kupata stadi za msingi na ujuzi wa ajira na kujiajiri. Aidha, imeendelea na uratibu wa utoaji wa elimu na ushauri wa kitaalamu kuhusu uhifadhi wa maeneo ya urithi wa Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2026/2027, Fungu 46. Katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara imeainisha vipaumbele vya bajeti kwa kuzingatia mahitaji ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, toleo la 2023 inayolenga kuimarisha ubora wa elimu, kukuza ujuzi na kuongeza maarifa. Kutokana na mwelekeo huo, Wizara itaendelea kuweka jitihada kubwa katika maandalizi ya elimu ya lazima ya miaka 10, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, matumizi ya TEHAMA na kuendeleza Sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuendana na mahitaji ya dira 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia itajielekeza kutekeleza vipaumbele vitano kama ifuatavyo: -

(1) Kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria, kuandaa miongozo na kutoa mafunzo nchini;

(2) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali katika shule za sekondari na vyuo vya amali;

(3) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na uwalimu;

(4) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

(5) Kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya Sayansi na Teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itafanya tathmini ya miaka miwili ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 iliyoanza utekelezaji wake mwezi Januari, 2024 na kuzinduliwa rasmi tarehe 1 Februari, 2025. Lengo la kufanya tathmini ni kubaini mafanikio tuliyoyapata hadi sasa pamoja na kubaini vikwazo mbalimbali vinavyoathiri utekelezaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa elimu ya lazima ili kupokea wanafunzi wa darasa la sita na wanafunzi wa darasa la saba kwa wakati mmoja kuingia kidato cha kwanza, mwezi Januari, 2028. Utekelezaji wa jambo hili muhimu unafanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu, TAMISEMI, lakini Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itashirikiana na TAMISEMI hasa katika maandalizi kuandaa miongozo, kutafuta rasilimali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vinavyohitajika kuhamasisha ushiriki wa wadau ikiwemo sekta binafsi pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweka misingi ya kisheria katika utekelezaji wa sera, Serikali itakamilisha mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 na vilevile itakamilisha mapitio ya sheria ya taasisi zilizo chini ya Wizara ikiwemo, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Baraza la Elimu la Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Baraza la Mitihani la Tanzania na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili ziendane na mabadiliko ya sera, sheria na makubaliano ya kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ufanisi na mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Serikali itakamilisha mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia ambayo sasa hivi ni ya mwaka 1996 ili kubaini utoshelevu wake katika mahitaji ya kisayansi, teknolojia na ubunifu wa sasa na baadaye ili kuwezesha nchi kuwa na sera ya kusimamia masuala haya kulingana na vipaumbele vya nchi pamoja na makubaliano ya kikanda na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuongeza fursa katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Serikali itasajili vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 263. Kati ya vyuo hivyo, vya elimu ya ufundi ni 45, vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 152 na shule za sekondari za amali 66 na hivyo kufikisha vyuo 577 vya elimu ya ufundi, vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi kufikisha 1,066 na shule za sekondari za amali kufikia 267.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Serikali itadahili wanafunzi 374,000 wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ambapo kati ya wanafunzi hao, vyuo vya elimu ya ufundi ni 240,000 na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 134,000. Ongezeko la udahili litaongeza idadi ya vijana wenye ujuzi na uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulimwengu wa sasa unahitaji zaidi vitendo kuliko nadharia. Hivyo walimu wa amali ndiyo msingi wa kuandaa vijana wenye uwezo wa kufanya kazi kwa vitendo. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itadahili walimu tarajali 200 katika ndaki ya Mtwara ya Ualimu Ufundi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya na walimu tarajali 1,000 katika Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu hawa wa amali watafundisha katika shule zetu za sekondari za amali na vyuo vya mafunzo vya ufundi stadi na hivyo kuwezesha kuwa na wahitimu wenye uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa na kutatua changamo za kiufundi ambazo ndiyo msingi wa maendeleo ya kiuchumi wa Taifa lolote linalotaka kujitegemea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu mbalimbali ya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuongeza fursa na ubora wa mafunzo kwa kuwezesha ujenzi wa miundombinu katika shule za sekondari za amali pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia kupitia mamlaka ya

elimu Tanzania. Vilevile itaendelea na ujenzi wa vyuo 64 vya mafunzo ya ufundi stadi vya Wilaya pamoja na kile chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Serikali itaendelea na ujenzi wa vyuo vya elimu ya ufundi wa kihandisi wa kati, yaani *polytechnics,* ambapo chuo kama hicho tayari kimekamilika hapa Dodoma, na vyuo kama hivyo vitajengwa katika Mkoa wa Mwanza, Kigoma, Mtwara, Morogoro na chuo kimoja kitajengwa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuandaa programu katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi zinazoendana na mahitaji ya waajiri pamoja na miradi ya kimkakati nchini ikiwemo nishati, TEHAMA na viwanda vya kuongeza thamani, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mkakati wa ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na sekta binafsi pamoja na wadau mbalimbali wa Kitaifa, kikanda na Kimataifa katika utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirikiano huo utawawezesha wanafunzi wengi zaidi wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kufanya mazoezi kwa vitendo viwandani, kuimarisha ushirikiano baina ya sekta ya ajira na taasisi za elimu na kuwezesha vyuo kuandaa wataalamu kulingana na mahitaji na hivyo wahitimu kujiajiri au kuajiriwa kirahisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha mafunzo kwa vitendo katika taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza afua mbalimbali ikiwemo kununua vifaa na kufunga mitambo katika vituo vya umahiri vilivyopo katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile itanunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya *VETA* 145, vyuo vya maendeleo ya wananchi 55 na vyuo tisa vya ufundi stadi na marekebisho kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itatoa mafunzo kuhusu mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa walimu wapya wapatao 1,427 kwa shule za sekondari za amali. Vilevile itatoa mafunzo ya muda mrefu ya ufundi stadi kwa washiriki 15,000 katika vyuo vya maendeleo ya wananchi na washiriki 413 katika vyuo vya ufundi stadi na marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi ni vyuo vya ufundi stadi na marekebisho, kwa sababu vile ni kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalum ya watu wenye ulemavu ili kuwezesha washiriki kupata ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali itatoa mafunzo ya umahiri na mitaala inayozingatia teknolojia kwa watumishi wa *VETA* 6,500, na watumishi wa vyuo vya maendeleo ya wananchi 1,300, na vyuo vya maendeleo ya wananchi. Vilevile itatoa mafunzo ya umahiri na mitaala inayozingatia teknolojia kwa wanafunzi 2,300 kutoka vyuo vya elimu na mafunzo ya elimu stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itabadilisha maudhui ya vitabu vya elimu ya msingi na sekondari kwa kuvifanya kuwa maudhui shirikishi ya kielektroniki yanayojumuisha video, sauti, uhaishaji *(animation)* na majaribio pepe *(virtual simulations)*. Maudhui husika yatasaidia utumiaji wa hapo kwa hapo, ujifunzaji jumuishi kwa masomo ya sayansi, teknolojia na uhandisi na hisabati na matumizi ya rasilimali za *multimedia*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhamasisha usomaji wa jamii, kuboresha huduma za maktaba nchini kwa kutoa huduma za maktaba kwa watumiaji wasiyopungua 800,000 na kununua nakala za vitabu 100,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea na utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania *(Tanzania Teachers Professiyonal Board)* ili kusimamia, kudhibiti, na kulinda taaluma ya walimu nchini, ambapo itaandaa mwongozo wa viwango katika ufundishaji ili kukuza mafunzo endelevu katika taaluma ya ualimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali itaandaa mwongozo wa maadili na mwenendo wa taaluma ya ualimu. Serikali itaanza kutekeleza mpango wa mafunzo kwa vitendo wa mwaka mmoja *(internship)* kwa walimu wa mafunzo ya ualimu. Mpango huu ni muhimu kwa walimu tarajali kwa kuwa utawawezesha kuoanisha nadharia na uhalisia darasani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuwaendeleza kitaalamu na kitaaluma walimu wa shule za msingi na sekondari, wakufunzi wa vyuo vya walimu, wadhibiti ubora wa shule na wasimamizi wa elimu ili kuimarisha utekelezaji katika maeneo mbalimbali kwa kutoa ufadhili wa masomo kwa walimu 1,223 watakaosoma stashahada ya ualimu kwa elimu maalum na kutoa mafunzo kwa walimu 3,000 wa ushauri nasihi wa shule za msingi na sekondari kuhusu malezi, unasihi, stadi za maisha na ulinzi wa mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia watendaji 5,500 pamoja na walimu na wanafunzi kuhusu majukwaa ya kielimu ikiwemo maktaba mtandao na jukwaa la umma ili kujifunza mitandaoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma ya ubainishaji na upimaji pamoja na utoaji wa elimu nyumbani kwa wanafunzi kwa kutoa mafunzo kwa wakufunzi 1,000 kutoka *VETA* za mikoa na vyuo vya maendeleo ya wananchi kuhusu namna ya kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum; na Maafisa Elimu Maalum 52, Maafisa Uthibiti Ubora 52 na Wakuu wa Shule 52 kuhusu ubainishaji na upimaji wa wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi za fasihi hutumika kama kielelezo cha maisha, maadili na historia ya jamii. Kwa mantiki hayo, Serikali itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Waandishi Bunifu kwa lengo la kuhamasisha na kukuza tasnia ya uandishi kwa kazi za fasihi ya Kiswahili ikiwemo riwaya, hadithi fupi na ushairi. Utoaji wa tuzo hizi huhamasisha na kuwajengea uwezo waandishi chipukizi na kuchagiza ukuaji wa sekta ya uandishi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya nje ya mfumo rasmi inatoa fursa kwa wale waliokosa nafasi katika mfumo rasmi kutokana na sababu mbalimbali. Njia hiyo ya elimu inatoa fursa ya kupata maarifa na stadi za maisha kulingana na mahitaji. Kwa umuhimu huo, Serikali itaendelea kuimarisha elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi kwa kuongeza udahili kwa wanafunzi wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala kutoka 14,765 mwaka 2025/2026 hadi 16,000 katika mwaka 2026/2027. Aidha, itaongeza idadi ya vijana watakaopata stadi za maisha, ujuzi na elimu ya msingi kutoka vijana 16,732 kwa mwaka 2026 hadi vijana 22,500 mwaka 2027 kupitia programu ya elimu changamani kwa vijana walio nje ya mfumo rasmi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kufanya upimaji na tathmini ya kubaini umahiri wa wanafunzi katika kumudu masomo ya elimu msingi, elimu sekondari na ualimu kupitia Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuongeza fursa kwa wanafunzi wa elimu ya juu kwa kuratibu udahili wa wanafunzi 180,000 wanaotarajia kuomba kujiunga na programu mbalimbali za shahada ya kwanza katika vyuo vya elimu ya juu. Vilevile itaongeza idadi ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 252,773 mwaka 2025/2026 hadi wanafunzi 292,981 kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi waliosoma masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati kwa kutekeleza yafuatayo: Itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati kwa kupitia *Samia Scholarship;* itatoa ufadhili kupitia programu ya Samia *Extended Scholarship*, *Data Science, Artificial Intelligence Plus* kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu wa masomo ya sayansi katika matokeo ya kidato cha sita kutoka wanafunzi 50 kwa mwaka 2025/2026 hadi wanafunzi 100 ili kujiunga na shahada ya kwanza katika vyuo bora vilivyopo nje ya nchi kwa ajili ya kusoma fani za sayansi ya data, sayansi shirikishi na akili unde. Itaendelea kuwezesha ufadhili wa masomo katika eneo la sayansi na teknolojia ya *nuclear* kwa wanafunzi wa shahada ya umahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha ushirikiano wa kikanda na Kimataifa katika utekelezaji wa elimu ya juu, Serikali itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 15 raia kutoka China wanaosoma lugha ya Kiswahili Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kukuza na kubiasharisha lugha ya Kiswahili, na wanafunzi wawili raia wa Oman na wanafunzi watano raia wa Hungary kusoma katika vyuo vikuu nchini kulingana na mikataba na utaratibu uliopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vikuu na taasisi za sayansi na teknolojia kwa kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali, kukamilisha ujenzi na ukarabati wa vyumba vya semina, kumbi za mihadhara, madarasa, ofisi, maabara, maktaba pamoja na miundombinu mingine katika taasisi 21 za elimu ya juu kupitia mradi wa elimu ya juu kwa mageuzi ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuimarisha ithibati na udhibiti ubora katika taasisi za elimu ya juu ikiwemo kufanya tathmini na kutoa ithibati ya programu 300 za masomo mbalimbali katika vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile itakagua na kufanya tathmini na ufuatiliaji kwa vyuo vikuu 25 kwa lengo la kuendeleza ubora wa elimu kwa kuzingatia utoshelevu wa miundombinu, mafunzo, wanataaluma, utawala na uendeshaji na kutoa ushauri stahiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaongeza ufadhili wa miradi ya utafiti na ubunifu kutoka 80 hadi 109 inayozingatia maeneo ya kipaumbele ili kutatua changamoto za mabadiliko ya hali ya hewa, Uchumi wa Buluu, uvuvi, maji, kilimo, afya na viwanda. Vilevile Serikali kupitia Taasisi ya Elimu za Juu na Elimu ya Ufundi itafanya miradi ya utafiti 1,390 katika maeneo mbalimbali afya, elimu, biashara, kilimo, uongozi, ushiriki katika teknolojia ya uvuvi, ardhi, mazingira na usanifu majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itachapisha machapisho 2,497 katika majarida ya Kimataifa ili kuimarisha usambazaji wa maarifa, uhamasishaji wa mijadala ya kitaaluma na kuhakikisha matokeo ya

kazi za tafiti yanatumika katika kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itazijengea uwezo maabara za taasisi tano za utafiti na maendeleo ili zitumike kama maabara za rufaa za utafiti na ubunifu wa viwanda. Vilevile itaimarisha mahusiano kati ya taasisi za utafiti na maendeleo, taasisi za elimu ya juu na viwanda ili kuchochea mchango wa utafiti na ubunifu katika kutekeleza Dira ya Taifa ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kuhamasisha wabunifu na kuongeza idadi ya kampuni wanufaika wanaoweza kupokea mikopo kupitia Mfuko wa Ubiasharishaji wa Samia *(Samia Innovation Commercialization Fund).* Aidha, itaviwezesha vyuo vitano vya maendeleo ya wananchi kuwa vituo vya ubunifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaimarisha udhibiti na utafiti kimkakati unaolenga kuongeza wigo wa matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii, kwa kuendelea kudhibiti matumizi ya mionzi nchini kwa kukagua vituo 900 vyenye vyanzo vya mionzi ili kuwaweka salama wagonjwa, wafanyakazi, jamii, na mazingira. Vilevile itapima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,110 wanaofanya kazi kwenye mazingira ya vyanzo vya mionzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2026/2027 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18), imepanga kutekeleza yafuatayo: Kwanza, kukamilisha taratibu za kuhakikisha maeneo tarajiwa na yale yaliyo katika orodha ya awali ya *UNESCO* yaingie katika orodha ya *UNESCO*; pili, kuimarisha utekelezaji wa program za *UNESCO* katika sekta za elimu, sayansi, utamaduni na mawasiliano kwa kuzingatia ajenda ya maendeleo endelevu; na tatu, kukuza ushiriki wa Tanzania katika majukwaa ya Kimataifa ya *UNESCO* ili kulinda na kutetea maslahi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na

Teknolojia, kwa uchapakazi na umakini wake na ushirikiano mkubwa anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kumshukuru Katibu Mkuu, Profesa Caroline Nombo; Naibu Katibu Mkuu, Profesa Daniel Mushi, na Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Hussein Omar kwa kunipa ushirikiano mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba kutoa shukrani za dhati kwa Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi na watumishi wote kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa juhudi na ufanisi. Pia ninapenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, waalimu, wanafunzi na wadau wote wa elimu kwa ushirikiano wao katika kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki na menejimenti za shule, vyuo, na taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ninaomba nirudie tena. Aidha, ninapenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki na mameneja wa shule, vyuo na taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunawashukuru washirika wa maendeleo na wadau wote wa elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa mipango ya miradi ya elimu, sayansi na teknolojia. Ninaomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Afrika Kusini, *Brazil*, Canada, China, Ethiopia, Finland, *Hungary*, India, *Ireland, Israel, Italy, Japan*, Kenya, Korea ya Kusini, Mauritius, Misri, Norway, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki na Uswisi. Aidha, ninatambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kuyashukuru mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yanayochangia kufanikisha miradi na program

za elimu, sayansi na teknolojia ambayo ni Pamoja na Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Africa, British *Council, Campaign for Female Education, Christian Social Services Commissiyon, Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty Organization, Foreign Common Wealth and Development Office, Global Partnership for Education, Inter University Council for East Africa, International Atomic Energy Agency, Japan International Cooperation Agency, Jumuiya ya Madola, Karibu Tanzania Organisation, Korea International Cooperation Agency (KOICA), Swedish International Development Cooperation Agency (SIDA), Tanzania Education Network/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Umoja wa Nchi za Ulaya (EU), United Nations Development Programme (UNDP), UNESCO,* na *UNICEF*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi ya fedha. Ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yaliyoainishwa katika mwaka wa fedha 2026/2027, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Fungu 46, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 2,394,423,829,000 kwa mchanganuo ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi 697,841,881,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya Wizara ambapo shilingi 648,082,352,000 ni kwa ajili ya mishahara, na shilingi 49,759,529,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Shilingi 1,696,581,948,000 zinaombwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo shilingi 1,337,249,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 359,332,948,000 ni fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 3,866,993,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni shilingi 1,335,020,000 na matumizi mengineyo ni shilingi 2,531,973,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, ninaomba sasa Bunge lako Tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara, Fungu 46 na Fungu 18, yenye jumla ya shilingi 2,398,290,822,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.moe.go.tz).

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA BAJETI YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA PROF. ADOLF F. MKENDA (MB) AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo iliyochambua na kutoa ushauri wa makadirio ya mapato na matumizi ya FUNGU 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na FUNGU 18 - Tume ya Taifa ya UNESCO, sasa ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2025/26. Aidha, ninaomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2026/27.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** makadirio haya ya mapato na matumizi yanayowasilishwa yamelenga katika kuhakikisha uwekezaji katika elimu sayansi na teknolojia unachangia kujenga rasilimaliwatu yenye ujuzi, maarifa na ushindani kwa maendeleo endelevu ya Taifa letu.

**Pongezi na Shukrani**

3. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama tena

mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha utekelezaji wa Mpango naBajeti ya mwaka wa fedha 2025/26 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Tume ya Taifa ya UNESCO kwa mwaka wa fedha 2026/27.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuchaguliwa kwa kishindo katika uchaguzi uliofanyika tarehe 29 Oktoba, 2025. Ushindi huu unadhihirisha imani kubwa walionayo Watanzania kwa Mheshimiwa Rais na uongozi wake mahiri unaoendelea kuleta mageuzi makubwa katika Sekta ya Elimu na maendeleo ya Taifa kwa ujumla. Tunamuombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema na baraka tele katika uongozi wake. Ahadi yetu kwa Mheshimiwa Rais ni kuendelea kufanya kazi kwa bidii na maarifa katika kutekeleza maono yake katika sekta ya elimu.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninaomba nitumie fursa hii kumpongeza **Mheshimiwa Dkt. Emmanuel John Nchimbi,** kwa kuchaguliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Uchaguzi Mkuu uliofanyika tarehe 29 Oktoba 2025. Ninampongeza pia **Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi**, kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi la Zanzibar. Aidha ninampongeza **Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb)**, kwa kuteuliwa na Rais na kupitishwa na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nikupongeze wewe binafsi **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb)**, kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ilala na kwa kupata imani ya Waheshimiwa Wabunge kuwa Spika wa Bunge hili la 13. Nampongeza pia **Mheshimiwa Daniel Baran Sillo (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, naomba

kutumia nafasi hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, **Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb), Mheshimiwa Cecilia Daniel Pareso (Mb)** na **Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb**) kwa kuaminiwa katika nafasi hizi muhimu sana katika Bunge Tukufu. Mheshimiwa Spika na wasaidizi wako wote mnaliongoza Bunge letu vizuri, kwa umakini na umahiri na weledi mkubwa.

**7.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee ninaomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan** kwa kuendelea kuniamini na kunipa dhamana mimi pamoja na Naibu Waziri, **Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir (Mb)** katika kuisimamia na kuiongoza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa **Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko (Mb),** Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo; Makamu Mwenyekiti **Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe (Mb)** na wajumbe wote wa Kamati kwa ushirikiano wanaoutoa kwetu, hasa katika kuisimamia na kuishauri Wizara katika utekelezaji wa majukumu yake mbalimbali. Kamati imefanya kazi kubwa ya kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2025/26 na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka 2026/27. Maoni na ushauri uliotolewa na Kamati umetusaidia sana wakati wa maandalizi ya bajeti ya Wizara. Ninaiahidi Kamati kuwa tutaendelea kupokea maelekezo, maoni na ushauri wao na kuufanyia kazi kwa ajili ya maendeleo ya sekta yetu ya elimu.

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninaomba kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Mawaziri wote walioteuliwa kuongoza Wizara mbalimbali. Kwa kuzingatia kuwa masuala ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni mtambuka, ninawaahidi kutoa ushirikiano katika kuhakikisha tunatoa huduma na kuleta maendeleo kwa Taifa letu wakati wote.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa hii ni hotuba yangu ya kwanza kwenye Bunge hili la 13, ninaomba nitumie fursa hii kuwapongeza waheshimiwa wabunge wote kwa kuchaguliwa na kuteuliwa kwao kuwa wabunge wa Bunge la 13 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni sana waheshimiwa na naomba ushirikiano wenu katika kuendeleza elimu, sayansi na teknolojia.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuwashukuru viongozi wenzangu, watendaji na watumishi wote wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara, kwa utendaji mahiri na ushirikiano wanaoutoa katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Kipekee, namshukuru sana **Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir,** Naibu Waziri, kwa uchapakazi wake na ushirikiano wa hali ya juu anaoutoa katika kuiongoza Wizara. Namshukuru pia Katibu Mkuu, **Profesa Carolyne Ignatius Nombo** na Naibu Makatibu Wakuu, **Profesa Daniel Elius Mushi** na **Dkt. Hussein Mohamed Omar** kwa utendaji kazi wao wenye bidii na weledi mkubwa.

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninaomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Rombo kwa kuniamini na kunichagua kuendelea kuliongoza jimbo hilo. Nawashukuru kwa kuendelea kushirikiana nami katika kuleta maendeleo ya jimbo letu na Taifa kwa ujumla.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaishukuru sana familia yangu, hususan mke wangu mpendwa **Beatrice,** kwa kunitia moyo na kuniwezesha kutimiza majukumu yangu kwa umakini, juhudi na ari kubwa.

**Salamu za Pole**

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kuungana na wabunge wenzangu waliotangulia kwa kutoa salamu za pole kwa Bunge lako Tukufu, kwako wewe binafsi, familia na wananchi wote kwa kuondokewa na wapendwa wetu; kwanza, **Mheshimiwa Jenister Joachim Mhagama** (aliyekuwa Mbunge wa Peramiho) aliyefariki tarehe 11 Desemba, 2025. Marehemu Jenister

Mhagama aliwahi kuwa Naibu Waziri, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi Mwaka 2014 - 2015.

Pili, **Mheshimiwa Halima Idd Nassor** aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum ambaye alifariki tarehe 18 Januari, 2026 na Tatu **Mheshimiwa William Vangimembe Lukuvi** aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu) na Mbunge wa Jimbo la Ismani aliyefariki tarehe 25 Machi, 2026. Hakika kuondokewa na viongozi hawa ni pigo kwa familia na taifa letu kwa ujumla lakini mchango wao utaendelea kuwa chachu ya maendeleo ya sekta mbalimbali ikiwemo elimu. Tutaendelea kuyaenzi maisha yao na kujifunza kutoka kwa uongozi wao mzuri. Vilevile, natoa pole kwa Watanzania wote waliondokewa na ndugu zao kutokana na maradhi na sababu mbalimbali.

Ninawaombea marehemu wote, Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi, Amina!

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya utangulizi huo, ninaomba sasa kutoa taarifa ya utelekezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46 na 18) kwa Mwaka wa Fedha 2025/26, na Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/27. Taarifa hii inaelezea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/26 na mwelekeo wa kimkakati wa sekta ya elimu katika kuchangia maendeleo ya Taifa.

## B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2025/26 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI

### Ukusanyaji wa Maduhuli

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, idara, vitengo na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zilikadiria kukusanya maduhuli yenye thamani ya **Shilingi 720,507,879,789.63.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi**

**8,402,257,000.00** ni makusanyo ya idara na vitengo vya Wizara na **Shilingi 712,105,622,789.63** ni makusanyo ya taasisi zilizo chini ya Wizara. Vyanzo vya maduhuli hayo ni: ada, malipo ya ushauri elekezi, mchango wa uthibiti ubora wa shule na baadhi ya huduma zinazotolewa na Wizara pamoja na taasisi zake. Makusanyo haya yanaonesha mchango mkubwa wa taasisi zilizo chini ya Wizara katika kuongeza mapato ya ndani na kuimarisha uendelevu wa kifedha wa Sekta ya Elimu.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 520,140,680,477.35** sawa na asilimia 72 ya makadirio ambapo **Shilingi 6,868,106,833.00** zimekusanywa na idara na vitengo, na **Shilingi 513,272,573,644.35** zimekusanywa na taasisi zilizo chini ya Wizara. Hali hii inaashiria mwenendo wa kuridhisha wa ukusanyaji wa mapato unaoendana na matarajio ya Serikali licha ya changamoto mbalimbali za kiuchumi.

**Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo**

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka wa Fedha 2025/26 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha **Shilingi 2,826,078,405,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo ya FUNGU 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ambapo **Shilingi 688,614,234,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,137,464,171,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO - FUNGU 18 Wizara iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 3,240,288,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** fedha zilizoidhinishwa zimeelekezwa katika maeneo ya kimkakati ikiwemo kuboresha miundombinu ya elimu, kuimarisha ubora wa ufundishaji na ujifunzaji pamoja na kuongeza upatikanaji wa vifaa vya elimu. Uwekezaji huu unaendelea kuhakikisha kila Mtanzania anapata elimu bora inayomuwezesha kushiriki kikamilifu katika uchumi wa Taifa na kuhakikisha kuwa hakuna anayeachwa nyuma.

## Matumizi ya Kawaida

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara kupitia Fungu 46 ilikadiria kutumia jumla ya **Shilingi 688,614,234,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 635,249,992,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na taasisi zake, ambapo **Shilingi 109,268,953,000.00** ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa idara na vitengo katika wizara na **Shilingi 525,981,039,000.00** kwa ajili ya mishahara ya watumishi katika taasisi zilizopo chini ya Wizara. Aidha, matumizi mengineyo ni **Shilingi 53,364,242,000.00** ambapo kwa idara na vitengo vya Wizara ni **Shilingi 37,510,134,348.00** na taasisi zilizo chini ya Wizara ni **Shilingi 15,854,107,652.00**. Fungu 18 Tume ya Taifa ya UNESCO ilikadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 3,240,288,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,538,096,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,702,192,000.00** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Aprili, 2026 Wizara kupitia Fungu 46 imepokea jumla ya **Shilingi 554,655,889,627.34** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 81 ya bajeti ya **Shilingi 688,614,234,000.00 .** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 511,604,132,973.88** ni fedha za mishahara na **Shilingi 43,051,756,653.46** ni fedha za matumizi mengineyo. Aidha, kupitia Tume ya UNESCO - Fungu 18, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 2,583,188,234.87** sawa na asilimia 79.8 ya fedha ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,132,078,000.00** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,453,110,234.87** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

## Miradi ya Maendeleo

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,137,464,171,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo

ambapo **Shilingi 1,186,987,965,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 950,476,206,000.00** ni fedha za nje.

**23.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia Aprili, 2026, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 1,159,010,684,656.03** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 54 ya bajeti iliyotengwa. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 760,812,513,258.53** ni fedha za ndani, sawa na asilimia 60 ya bajeti, na **Shilingi 398,198,171,397.50** ni fedha za nje sawa na asilimia 42.

## C. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA FUNGU 46

**24.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara imetekeleza vipaumbele vitano kwa lengo la kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo pamoja na matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchangia katika maendeleo endelevu ya taifa. Vipaumbele hivyo ni kama ifuatavyo:

(a) Kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria, kuandaa miongozo ya utoaji elimu na mafunzo nchini;

(b) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali (ufundi na ufundi stadi) katika shule za sekondari na vyuo vya amali.

(c) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu;

(d) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

(e) Kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

**25. *Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele hivi vimechaguliwa kwa kuzingatia mahitaji ya Taifa kwenye uchumi wa viwanda, kuongeza ajira kwa vijana na kuimarisha ushindani wa kimataifa kupitia elimu, sayansi na teknolojia.

**a. Kuendelea na Utekelezaji wa Sera na Mitaala, Mapitio ya Sheria na Kuandaa Miongozo ya Utoaji Elimu na Mafunzo**

**26. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza sera, mipango na mikakati mbalimbali inayoimarisha utoaji wa elimu na mafunzo nchini kwa lengo la kuzalisha rasilimaliwatu yenye ujuzi na maarifa stahiki yatakayomwezesha mtanzania kujiajiri au kuajiriwa pamoja na kuchangia katika maendeleo endelevu ya Taifa.

**27. *Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, Serikali imeendelea na maandalizi ya utekelezaji wa elimu ya lazima ya miaka 10 ambapo takribani wanafunzi **3,021,177** wanatarajiwa kujiunga na elimu ya sekondari kidato cha kwanza ifikapo Januari, 2028. Idadi hiyo inatokana na idadi ya wanafunzi waliopo darasa la tano na darasa la sita mwaka 2026 watakaojiunga na elimu ya sekondari mwaka 2028. Kwa msingi huo, Serikali, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeendelea na ujenzi wa miundombinu ya madarasa, maabara, karakana na ununuzi wa vifaa pamoja na kutoa ajira mpya za walimu ili kuwezesha mapokezi ya wanafunzi husika.

**28. *Mheshimiwa Spika,*** hatua ya utekelezaji wa elimu ya lazima ya miaka 10 ni ya kihistoria, kwani itaongeza kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa elimu ya sekondari na kuandaa kizazi kipya chenye ujuzi na maarifa na kuendana na Malengo ya SDG 4). Hapa Tanzania umri wa kuanza darasa la kwanza ni miaka sita. Kwa hivyo mtoto aliyeanza darasa la kwanza akiwa na miaka sita anamaliza darasa la saba akiwa na miaka kumi na tatu; huu ni umri ambao mtu hawezi kuajiriwa wala kujiajiri. Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la 2023 imerekebisha jambo hili kwa kufanya elimu ya lazima kuwa ni

miaka kumi, hivyo kijana atamaliza elimu ya lazima akiwa na miaka kumi na sita. Kwa hiyo mageuzi ya kufanya elimu ya msingi iwe ni miaka sita lakini elimu ya lazima iwe ni miaka kumi ni mkakati wa kuhakikisha kijana hawezi kutoka kwenye mfumo wa elimu kabla hajakaribia umri wa kuajirika na au kujiajiri. Mkakati wa pili unaozingatia fursa katika ajira ni kuanzisha mkondo wa amali katika shule za sekondari.

**29. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea na mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura ya 353 ambapo tayari imekamilisha kukusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu na kuandaa taarifa ya awali ya mapitio ya sheria.

**30. *Mheshimiwa Spika,*** sambamba na mapitio ya Sheria, Serikali imeandaa viunzi mbalimbali ili kuendana na mahitaji ya sera kama ifuatavyo:-

(i) imeandaa Kiunzi cha Taifa cha Tathmini ya Elimu (*Tanzania National Education Assessment Framework*) kinacholenga kuwa na mfumo mmoja wa tathmini wenye uwiano katika ngazi zote za elimu;

(ii) imeandaa Kiunzi cha Taifa cha Mitaala (*National Curriculum Framework*) kinacholenga kuandaa wahitimu wenye ujuzi, maadili na uwezo wa kuchangia katika uchumi;

(iii) imeandaa Kiunzi cha Umahiri wa Walimu katika TEHAMA 2026 (*ICT Competency Framework for Teachers*) ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia;

(iv) imeandaa Kiunzi cha Kitaifa cha uboreshaji wa Vituo vya Walimu (*Teacher Resource Centers* – TRC) ili vitumike kama kumbi za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) na Teknolojia za Kidijitali (*DigiSTEM Hubs*); na

(v) imeandaa Kiunzi cha Kitaifa cha Uanzishaji na Uendeshaji wa Ushirikiano kati ya Serikali na Wadau wa Teknolojia za Kidijitali katika Sekta ya Elimu (*National edTech Partnership and Adoption Framework*–NEPAF).

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, pia imeandaa miongozo mbalimbali ya utoaji wa elimu na mafunzo nchini ili iendane na Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na kuongeza kasi katika utekelezaji wake. Miongozo hiyo ni kama ifuatavyo: -

(i) Mwongozo wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA) Ngazi ya Shule na Vituo vya Walimu wa Mwaka 2025 kwa ajili ya kuweka utaratibu madhubuti wa utoaji wa mafunzo endelevu ya walimu kazini na kuimarisha umahiri wa walimu;

(ii) Mwongozo wa Kitaifa wa Kuongeza Fursa za Ufadhili wa Masomo Ndani na Nje ya Nchi 2025 kwa ajili ya kuweka utaratibu madhubuti utakaowezesha kuongeza idadi ya watanzania wanaonufaika na fursa za ufadhili katika maeneo ya kimkakati ikiwemo akili unde, udaktari bingwa, uhandisi wa ndege, meli, treni, magari na maeneo mengine muhimu kwa maendeleo ya nchi;

(iii) Miongozo miwili yenye lengo la kuchochea maendeleo ya sayansi, teknolojia na ubunifu nchini ambayo ni: Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Vituo vya Ubunifu na Teknolojia vya Mkoa (*Regional Innovation and Technology Support Centres*); na Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Maabara za Rufaa za Taifa za Utafiti na Ubunifu wa Viwanda (*National Reference Industrial Research and Innovation Laboratories*); na

(iv) Miongozo nane ili kuwezesha utekelezaji wa elimu jumuishi ambayo ni: Mwongozo wa Sanaa na Michezo Rekebifu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum wa Mwaka 2026; Mwongozo wa Matumizi ya TEHAMA na Teknolojia Saidizi kwa

Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum wa Mwaka 2026; Mwongozo wa Lugha ya Alama ya Tanzania wa Mwaka 2026; Mwongozo wa Matumizi ya Braille ya Kiswahili katika Taasisi za Elimu wa Mwaka 2026, Mwongozo wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2026; Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma kwa Wanafunzi, Walimu na Wakufunzi wenye Mahitaji Maalum wa Mwaka 2026; Mwongozo wa Uendeshaji, Uratibu na Usimamizi wa Mafunzo kazini kwa Walimu na Watumishi Mwega wa Elimu Maalum na Jumuishi wa Mwaka 2026; na Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Amali kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum wa Mwaka 2026. Lengo la miongozo hii ni kuwezesha utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 inayosisitiza utoaji wa elimu katika mazingira jumuishi.

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika siku 100 tangu kuapishwa kwa **Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais** alionesha dhamira yake ya dhati ya kuleta mageuzi katika sekta elimu yatakayokuwa msingi imara kwa wanafunzi kujifunza na kuandaa wahitimu wenye ujuzi na uwezo wa kujiajiri na kushindana katika soko la ajira kimataifa. Katika kufikia azma hiyo ya Mheshimiwa Rais, Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imetekeleza yafuatayo:

(i) imeandaa Mpango Mkakati wa Kisayansi wa Kujenga Umahiri wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) kwa watoto wa elimu ya awali na wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili ambao ulizinduliwa rasmi na **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania** tarehe 29 Januari, 2026 jijini Dar es Salaam. Mpango huu ni hatua ya kimkakati ya kuhakikisha hakuna mwanafunzi anayefika darasa la tatu bila kumudu stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Bila msingi imara wa KKK hakuna elimu bora; na

(ii) imeandaa mpango wa pamoja kati ya waajiri, vyuo vya ufundi stadi na vyuo vikuu ambao uliozinduliwa na **Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi** tarehe 9 Februari, 2026

Jijini Dar es Salaam. Mpango huo unalenga kuimarisha ushirikiano baina ya sekta ya ajira/viwanda na taasisi za elimu ili kuandaa wataalamu kulingana na mahitaji, wanafunzi kujifunza kwa vitendo pamoja na kuwezesha wahitimu kujiajiri au kuajiriwa na kuanzisha miradi binafsi.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** ni matarajio yetu kuwa mpango wa pamoja kati ya waajiri, vyuo vya ufundi stadi na ufundi na vyuo vikuu utaimarisha ushirikiano na viwanda. Utahamasisha waajiri kutoa fursa zaidi za ajira kwa wahitimu na kutoa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa vyuo vyetu vya ufundi na taasisi za elimu ya juu, na hivyo kupunguza au kuondoa kabisa changamoto ya kukosekana kwa uwiano baina ya ujuzi na mahitaji ya soko la ajira (skills mismatch).

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na mpango huo, Serikali imeandaa mikakati mbalimbali ikiwemo:

(i) Mkakati wa Kitaifa wa Umataifishaji wa Elimu wa Mwaka 2025 kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kuandaa wahitimu wenye maarifa, stadi, ujuzi na umahiri unaokidhi viwango na mahitaji ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Aidha, mkakati huo utachangia katika kuimarisha uandaaji wa mitaala na mazingira ya kufundishia na kujifunzia ili kuvutia wanafunzi na wanataaluma kutoka nje ya nchi pamoja na ushirikiano wa taasisi za nje ya nchi;

(ii) Mkakati wa Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika Elimu na Mafunzo ili kuongeza mchango na ushiriki wa sekta binafsi katika sekta ya elimu;

(iii) Mkakati wa Kitaifa wa Ugharamiaji na Utoaji Motisha katika Masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (*National STI Financing and Incentivization Strategy*), kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ugharamiaji na motisha katika Sayansi, Teknolojia Ubunifu ili kuongeza mchango wa masuala hayo katika utekelezaji wa

Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa ujumla; na

(iv) Mkakati wa Wizara wa Usawa wa Kijinsia wa Mwaka 2025/26 - 2029/30 utakaotekelezwa kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya masuala ya jinsia na wadau mbalimbali wa elimu kwa lengo la kuimarisha mifumo itakayowezesha ufikiaji wa usawa wa kijinsia na Elimu Jumuishi.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekubaliana na mabalozi wanaoiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali kutafuta fursa na rasilimali kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa elimu, sayansi na teknolojia ikiwemo suala la umataifishaji elimu.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Takwimu wa Sekta ya Elimu (*Education Sector Management Information System* – ESMIS) ambao umewezesha ufungamanishaji wa mifumo mbalimbali iliyo chini ya Wizara nyingine na hivyo kuwezesha upatikanaji wa takwimu zote za sekta katika eneo moja. Aidha, mfumo huo umeshaanza kukusanya takwimu za elimu za mwaka 2026.

### b. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali katika Shule za Sekondari na Vyuo vya Amali

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuongeza fursa na ubora wa mafunzo ya amali kwa shule za sekondari na vyuo vya amali ili kuongeza uwezo wa nchi kuandaa wahitimu wenye ujuzi na maarifa ya kazi. Azma hiyo imetekelezwa kwa kuongeza udahili wa wanafunzi, kuongeza usajili wa shule/vyuo, ujenzi wa miundombinu na kutoa mafunzo kwa walimu na wakufunzi. Hatua hii pia inalenga kupunguza pengo kati ya elimu na ajira kwa kuhakikisha wahitimu wanakuwa tayari kujiajiri au kuajiriwa mara baada ya kuhitimu.

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imedahili wanafunzi 315,307 (wanawake 147,977 na wanaume 167,330) kati yao wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi ni 236,199 na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 79,108 (wanawake 29,170 na wanaume 49,938) sawa na asilimia 119 ya lengo la kudahili wanafunzi 265,000 (elimu ya ufundi 190,000 na mafunzo ya ufundi stadi 75,000). Ongezeko hili la udahili linalozidi lengo linaonesha mafanikio makubwa ya Serikali katika kuongeza fursa za upatikanaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Hii ni hatua muhimu katika kujenga nguvu kazi yenye ujuzi na kuongeza ajira kwa vijana.

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, ongezeko la udahili linatokana na kuongezeka kwa idadi ya vyuo elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 1,414 (vyuo vya elimu ya ufundi 527 na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 887) mwaka 2025 hadi kufikia vyuo 1,446 (vyuo vya elimu ya ufundi 532 na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 914) mwaka 2026.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, pia imedahili jumla ya vijana 1,606 wanaotoka katika mazingira magumu katika vyuo vya VETA. Vilevile, imedahili jumla ya wanafunzi 132 wenye mahitaji maalum (wanaume 66 na wanawake 66); na imerasimisha ujuzi kwa wanagenzi 656 (wanawake 384 na wanaume 272) kupitia programu mbalimbali zinazotolewa na VETA. Programu hizi zina mchango mkubwa katika kuwawezesha vijana hususan wanawake kupata ujuzi na kujitegemea kiuchumi.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2025/26 Serikali imesajili vyuo 140 vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ambapo vyuo vya elimu ya ufundi 13 na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 127. Vilevile, imeanzisha programu 153 (programu za muda mrefu 76 na za muda mfupi 77) na idara 37 katika vyuo vya elimu ya ufundi kama ifuatavyo: masomo ya biashara, utalii na mipango 17, afya na sayansi shirikishi 3, na sayansi na teknolojia shirikishi 17. Hatua hii inaendelea kuimarisha mfumo wa utoaji elimu ya ufundi nchini kwa

kuongeza fursa za upatikanaji wa mafunzo yenye ubora na yanayozingatia mahitaji ya soko la ajira.

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuongeza miundombinu ya shule za sekondari za amali ambapo kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania imewezesha ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa katika shule 35 za sekondari za amali. Kati ya hizo, shule 14 zimekamilika na kuanza kutumika, shule tano zipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji na shule 16 zipo katika hatua za awali za ujenzi. Aidha, imewezesha ujenzi wa maabara za TEHAMA katika shule 10 za sekondari ambazo ni Nyakato, Rugambwa, Maruku, Bukara, Bwiru Wavulana, Semkiwa, Simbani, Kwaluguru, Rafsanjani na Jitegemee pamoja na kuweka vifaa vya TEHAMA ikiwemo kompyuta za mezani 213 na kompyuta mpakato 24.

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji huu katika miundombinu na TEHAMA unaongeza ubora wa ujifunzaji na kuwajengea wanafunzi uwezo wa kutumia teknolojia katika maisha yao ya kila siku na katika ajira.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuongeza fursa za elimu ya amali kama ifuatavyo:-

(i) imeendelea na ujenzi wa VETA 64 za wilaya na chuo kimoja cha Mkoa wa Songwe ambapo wastani wa ujenzi umefikia asilimia 68 kwa vyuo 64 vya wilaya na asilimia 68 kwa chuo cha Mkoa wa Songwe. Aidha, hatua ya ujenzi kwa kila chuo imebainishwa katika **kiambatisho Namba 1** na **2**. Mradi huu wa kimkakati utaongeza fursa ya upatikanaji wa elimu ya ufundi katika ngazi ya wilaya, hivyo kuwezesha vijana wengi zaidi kupata ujuzi bila kulazimika kuhama maeneo yao. Hatua hii pia itaongeza usawa wa upatikanaji wa elimu nchini.

(ii) imeendelea na ukarabati wa miundombinu ya vilivyokuwa vyuo vya Ualimu Mtwara Kawaida na Mtwara Ufundi ambavyo vyuo hivi pia vimeunganishwa na kuwa Ndaki ya Mtwara ya Ualimu Ufundi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ambapo ukarabati umefikia asilimia 69;

(iii) imeendelea na ujenzi wa karakana ya uzalishaji (*industrial workshop*) katika Chuo cha Ufundi Arusha kwa lengo la kuongeza ufanisi wa mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi ikiwemo matumizi ya mashine za kisasa katika kutengeneza bidhaa mbalimbali ambapo ujenzi umefikia asilimia 43;

(iv) imekamilisha ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 80, kuchimba kisima na kusambaza maji katika Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Malya; na

(v) imeendelea na ujenzi wa hosteli mbili (moja ya wanaume na nyingine ya wanawake) zenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 768 kila moja na bwalo katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume ambapo ujenzi umefikia asilimia 52 kwa hosteli na asilimia 91 kwa bwalo. Vilevile, inaendelea na ujenzi wa jengo la ukumbi wa mihadhara na bwalo katika Kampasi ya Pemba ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 75. Aidha, imeendelea na ujenzi wa maktaba itakayotumiwa na wanafunzi 2,500, ukumbi wa mihadhara utakaoweza kuhudumia wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja, pamoja na madarasa na ofisi katika Kampasi ya Kivukoni ambapo ujenzi umefikia asilimia 41 kwa maktaba na asilimia 70 kwa madarasa na ofisi.

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kuboresha vituo vya umahiri kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa mafunzo ya fani za kipaumbele ili kuvipa hadhi ya kuzalisha wataalam waliobobea kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imekamilisha ujenzi wa jengo lenye kumbi za mihadhara, maabara na ofisi pamoja na kuweka vifaa vya kisasa vya TEHAMA na teknolojia katika Kituo cha Kikanda cha Umahiri katika TEHAMA (*Regional Flagship ICT Center* - RAFIC) kilichopo katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam - DIT kwa lengo la kutoa mafunzo ya kitaalam na ubobezi katika TEHAMA;

(ii) imeendelea na ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Uchakataji na Utengenezaji wa Bidhaa za Ngozi na Teknolojia Shirikishi (*Centre of Excellency in Leather Products and Allied Technologies* - CELPAT) katika Kampasi ya Mwanza unaojumuisha mabweni mawili, jengo la taaluma, jengo la utawala, madarasa ambapo ujenzi umefikia asilimia 92 na ujenzi wa jengo la kiwanda umefikia asilimia 67; na

(iii) imekamilisha ujenzi wa miundombinu na kuendelea na ufungaji wa mitambo ya kuzalishia umeme (*hydropower plant*) kwa ajili ya kuzalisha umeme, kufundishia na kujifunzia ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 99 katika Chuo cha Ufundi Arusha Kampasi ya Kikuletwa.

**46. *Mheshimiwa Spika,*** vituo hivi vina nafasi muhimu katika kuandaa wataalam wabobezi watakaoweza kushindana katika soko la ajira la kikanda na kimataifa. Hii ni hatua ya kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha maarifa na ubunifu barani Afrika.

**47. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha ithibati na uthibiti ubora ili kuhakikisha vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na shule za sekondari za amali zinazingatia viwango vya ubora katika uendeshaji na utoaji wa mafunzo kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imehakiki mitaala 114 kati ya mitaala 230 iliyowasilishwa na vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ikiwemo mitaala 87 ya elimu ya ufundi na mitaala 27 ya elimu ya mafunzo ya

ufundi stadi kwa lengo la kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanaendana na soko la ajira;

(ii) imetoa ithibati kwa vyuo 50 (Elimu ya Ufundi 19 na Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi 31) kati ya 70 vilivyolengwa ili kuwezesha wanafunzi kupata mafunzo yenye ubora unaokusudiwa na unaoendana na mahitaji ya soko la ajira; na

(iii) imefanya ufuatiliaji na tathmini ya ubora wa elimu katika vyuo vya elimu ya ufundi 106 na shule za sekondari za amali 38. Katika ufuatiliaji huo, ushauri kuhusu namna ya kuboresha utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ulitolewa ili kuongeza ufanisi. Aidha, vyuo ambavyo havikukidhi vigezo vilishauriwa namna ya kufanya maboresho na vingine vilifutiwa usajili na kusimamishwa kudahili wanafunzi ili kuvipa nafasi ya kurekebisha mapungufu yaliyobainika.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kutekeleza mikataba ya ushirikiano 49 baina ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, viwanda na taasisi za ndani na nje ya nchi ili kuwezesha vyuo kuandaa wataalamu kulingana na mahitaji, wanafunzi kujifunza kwa vitendo na wahitimu kujiajiri au kuajiriwa na kuanzisha miradi binafsi.

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** ushirikiano huu kati ya vyuo na viwanda unaimarisha uhusiano kati ya elimu na soko la ajira, na kuwezesha wanafunzi kupata uzoefu wa vitendo kabla ya kuhitimu. Huu ndiyo msingi wa kuandaa wahitimu wanaokidhi mahitaji halisi ya uchumi.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, inatekeleza mpango wa kitaifa wa kuimarisha elimu ya ufundi na umahiri unaolenga kuandaa walimu wenye ujuzi wa kisasa na mbinu shirikishi za ufundishaji ambapo imewezesha walimu 150 wa amali za kihandisi kwenda **New Delhi, India** kwa mwezi mmoja. Walimu hao walipatiwa mafunzo ya umahiri katika

ufundishaji wa masomo ya amali katika vyuo vya huko na pia walipata fursa ya kushiriki mafunzo kwa vitendo katika shule za ufundi na ufundi stadi nchini humo. Hatua hiyo ni ya kimkakikati na inadhihirisha dhamira ya Serikali ya kuwekeza katika rasilimaliwatu kwa kuhakikisha walimu wanakuwa chachu ya mabadiliko ya elimu na ajira kwa vijana.

**51. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuwaendeleza kitaalamu na kitaaluma watumishi 658 wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kuwapa mafunzo mbalimbali kwa mchanganuo ufuatao: mafunzo ya muda mrefu watumishi 240 (wanawake 72 na wanaume 168) na ya muda mfupi watumishi 418 (wanawake 150 na wanaume 268). Hatua hii itaongeza uwezo wa taasisi kutoa mafunzo yenye ubora wa juu na yanayokidhi mahitaji ya sasa ya teknolojia na uchumi.

**52. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kugharamia mafunzo kwa vitendo viwandani kwa wanafunzi 1,822 (wanafunzi 411 wa Chuo cha Ufundi Arusha, wanafunzi 873 wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, na wanafunzi 538 wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya). Mafunzo haya ya vitendo yanaongeza uwezekano wa wahitimu kupata ajira au kujiajiri kwa kuwa yanawawezesha kupata uzoefu wa moja kwa moja katika mazingira ya kazi.

**53. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imegharamia huduma ya chakula kwa wanafunzi 15,435 (wanafunzi 12,843 wa vyuo vya maendeleo ya wananchi, wanafunzi 815 wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, wanafunzi 1,275 wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, na wanafunzi 502 wa Chuo cha Ufundi Arusha).

**54. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali, imeendelea kutoa vifaa ikiwemo mitambo na mashine pamoja na zana za kufundishia na kujifunzia za kisasa katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuimarisha ufundishaji na kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

**c. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu**

**55.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imeendelea kuongeza fursa za elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imesajili shule 671 kwa mchanganuo ufuatao; awali pekee 23 zisizo za serikali, awali na msingi 401 (Serikali 179 na zisizo za Serikali 222), Sekondari 245 (Serikali 194 na zisizo za Serikali 51), na vyuo viwili vya ualimu (Serikali kimoja na kisicho cha Serikali kimoja); na

(ii) imedahili wanafunzi 12,554 katika vyuo vya ualimu (wanawake 7,375 na wanaume 5,179) kati yao wanafunzi wa vyuo vya ualimu vya Serikali ni 7,157 (wanawake 3,326 na wanaumme 3,831) na visivyo vya Serikali ni 5,397 (wanawake 4,049 na wanaume 1,348).

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeendelea kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya elimu ikiwemo ujenzi wa mabweni sita katika shule za sekondari, madarasa 128 (sekondari 62 na msingi 66), bwalo la chakula, nyumba ya mwalimu, na kukarabati shule mbili za sekondari. Ujenzi wa miundombinu hiyo itasaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, pia imeendelea kuimarisha miundombinu katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendelea na ujenzi wa vituo vitatu vya mfano vya Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana walio Nje ya Shule - IPOSA ambapo ujenzi katika Mkoa wa Manyara umefikia asilimia 96, Tanga asilimia 75, na Shinyanga asilimia 90;

(ii) imekamilisha ukarabati wa hosteli ya wanafunzi wa Elimu ya Watu Wazima katika kampasi ya Morogoro yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 60. Aidha, inaendelea na ujenzi wa hosteli katika kituo cha elimu ya watu wazima mkoa wa Iringa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 80 ambapo ujenzi umefikia asilimia 60. Vilevile, imeanza ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 80 katika Mkoa wa Katavi, Simiyu na Ruvuma ambapo ujenzi umefikia asilimia 10; na

(iii) imeendelea na ujenzi wa maktaba ya mkoa wa Mwanza yenye uwezo wa kuhudumia watumiaji 1,000 ambapo ujenzi umefikia asilimia 30. Vilevile, imeendelea na ukarabati wa maktaba ya mkoa wa Mara, Mtwara na Tanga ambapo ukarabati umefikia wastani wa asilimia 78.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** uthibiti ubora wa elimu katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu ni muhimu katika kuhakikisha elimu inayotolewa katika asasi hizo inazingatia taratibu na miongozo inayotolewa na Wizara. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kuimarisha uthibiti ubora wa shule na vyuo vya ualimu kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imefanya tathmini ya jumla katika asasi 8,067 kati ya 6,962 zilizolengwa ikihusisha shule za awali na msingi ni 5,700, shule za sekondari ni 2,317, vyuo vya ualimu 19, vituo vya elimu nje ya mfumo rasmi 22 na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi tisa. Aidha, asasi zilizobainika kuwa na upungufu zilipewa ushauri stahiki;

(ii) imefanya ufuatiliaji katika asasi 689 (awali na msingi 546; sekondari 142, na chuo cha maendeleo ya wananchi kimoja) kati ya 1,260 zilizolengwa kuhusu utekelezaji wa ushauri uliotolewa wakati wa tathmini ya jumla. Katika ufuatiliaji asasi zilizobainika kuwa changamoto mbalimbali zilipewa ushauri wa kitaalam na kitaaluma na kuwekwa katika mpango wa ufuatiliaji; na

(iii) imenunua na kusambaza magari matatu kwa ajili ya Halmashauri ya Missenyi, Mbarali na Namtumbo ili kuimarisha utendaji wa majukumu ya wathibiti ubora wa shule.

**59. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuongeza upatikanaji wa vitabu vya elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu ili kufikia lengo la uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imechapa na kusambaza nakala 4,845,490 za vitabu vya kiada vya darasa la tano kwa masomo ya Hisabati, Sayansi, Kiingereza, Kiswahili, Jiografia na Mazingira, Historia ya Tanzania na Maadili na Sanaa, Kiarabu na Michezo katika shule za msingi kwa uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi 1:3. Vilevile, imechapa na kusambaza jumla ya nakala 6,887,325 za aina 27 ya vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha pili katika shule za sekondari ambapo uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi kwa masomo ya sanaa ambayo ni: Business Study, Geography, Kiswahili, English, Historia ya Tanzania na Maadili ni 1:3 yaani kitabu kimoja wanafunzi watatu; na kwa masomo yote ya sayansi uwiano ni 1:1. Vitabu hivi vimeandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa mtaala;

(ii) imechapa na kusambaza nakala 3,000 ya vitabu vya kiada aina 10 vya darasa la tano na nakala 31,520 ya vitabu vya kiada aina 22 vya kidato cha pili kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Vitabu hivi vimesambazwa kwa uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1) mtawalia;

(iii) imechapa na kusambaza nakala 9,600 za aina saba za vitabu vya kiada vya maandishi ya Breili darasa la tano na nakala 8,362 ya aina 19 za vitabu vya kiada vya maandishi ya Breili kidato cha pili kwa ajili ya wanafunzi wasiyoona kwa uwiano wa kitabu kimoja mwanafunzi mmoja (1:1) mtawalia;

(iv) imechapa jumla ya nakala ya vitabu 6,990,588 vya nyongeza (replenishment). Kati ya vitabu hivyo, vitabu 776,782 ni vya elimu ya awali, vitabu 4,460,768 ni vya elimu ya msingi na vitabu 1,753,038 ni vya Sekondari na hivyo kufikia uwiano wa wastani wa kitabu kimoja wanafunzi watatu (1:3);

(v) imeandika aina 45 za vitabu vya sekondari mkondo wa amali kwa ajili ya wanafunzi wa kidato cha tatu. Aidha, jumla ya nakala 17,775 zimechapwa na kusambazwa kwa uwiano wa Kitabu kimoja mwanafunzi mmoja (1:1). Vitabu hivi vimelenga kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya amali katika shule za sekondari; na

(vi) imetoa ithibati kwa miswada ya vitabu vya ziada aina 42 kati ya vitabu 55 vilivopokelewa kutoka kwa wachapishaji binafsi kwa lengo la kukuza tasnia ya uchapaji na uandishi wa vitabu nchini.

**60.** ***Mheshimiwa Spika***, imefanya utafiti wa mnyororo wa uandaaji, usambazaji, utunzaji na utumiaji wa vitabu vya kiada katika elimu ya msingi na sekondari ili kubainisha mahitaji, maandalizi, usambazaji, utunzaji na matumizi ya vitabu vya kiada vinavyotolewa na Serikali. Utafiti huo umewezesha kubaini changamoto zilizopo ikiwemo vitabu kutofika shuleni kwa wakati, utunzaji na uhifadhi wa vitabu hivyo ambapo mapendekezo yalitolewa ili kuboresha ufanisi katika upatikanaji na matumizi bora ya vitabu vya kiada.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kutambua na kukuza kazi za uandishi bunifu kwa kuibua vipawa katika waandishi wa fasihi ya Kitanzania, kuongeza machapisho na kukuza tabia ya usomaji kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imeratibu utoaji wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu ili kuwatambua waandishi mahiri wa kazi za fasihi ambapo miswada 260 imepokelewa na kufanyiwa tathmini katika duru ya nne ya utoaji wa Tuzo hii. Miswada hiyo 260 imegawanyika kama ifuatavyo; riwaya 53, ushairi 86,

hadithi za watoto 73 na tamthiliya 48. Miswada hii ilipitiwa na jopo la majaji ambao walichambua na kuchagua mshindi wa kwanza, mshindi wa pili na mshindi wa tatu kwa kila nyanja.

Washindi hawa watatu kwa kila nyanja walipewa zawadi stahiki. Mshindi wa kwanza katika kila nyanja alipewa zawadi na kutambuliwa kwa Tuzo na mswada wa kila mshindi wa kwanza unachapishwa na kusambazwa kwa wasomaji. Sherehe ya utoaji wa Tuzo hii hufanyika tarehe 13 Aprili ya kila mwaka; hii ni tarehe ambapo Mwalimu Nyerere alizaliwa. Katika Duru ya Nne ya Utoaji wa Tuzo hii, ambayo ilifanyika tarehe 13 Aprili, 2026, Mgeni Rasmi alikuwa ni **Mwalimu Abdilatif Abdalla** ambaye ni mtunzi nguli wa mashairi, mtafsiri wa vitabu vya fasihi-andishi na mshindi wa Tuzo ya Jomo Kenyatta ya fasihi-andishi. Tuzo hii inasimamiwa na kamati maalum inayofanya kazi kwa uhuru, umahiri na weledi kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania.

(ii) imechapa na kusambaza nakala 142,000 za vitabu vya washindi wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu kwa Mwaka wa Fedha 2024/25. Vitabu hivyo vimegawanyika kwa nyanja kama ifuatavyo; riwaya nakala 50,000, ushairi nakala 50,000 na hadithi za watoto nakala 42,000. Vitabu hivi vimesambazwa katika shule za sekondari 6,418 na shule za msingi 18,061; na

(iii) imeratibu mashindano ya uandishi wa insha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambapo wanafunzi 475 wa shule za sekondari walishiriki. Lengo la mashindano hayo ni kuwajengea wanafunzi umahiri katika stadi za uandishi. Aidha, imeratibu uandishi wa insha ya SADC kwa wanafunzi 328 wa shule za sekondari ambapo washindi 10 waliopatikana insha zao zitashindanishwa katika ngazi ya Kikanda.

***62. Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kuhamasisha jamii katika usomaji na uandishi bunifu kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imetoa huduma ya kuazima na kusoma vitabu ndani ya maktaba kwa watumiaji 403,462 wakiwemo wenye mahitaji maalumu 4,392 (wanawake 2,088 na wanaume 2,304). Vilevile, imehamasisha ushiriki wa jamii katika matumizi ya maktaba na kusajili wanachama wapya 1,820; na

(ii) imeendelea kutoa huduma za maktaba kwa njia ya kidigiti ambapo watumiaji 540 wamefikiwa na huduma hiyo.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuimarisha matumizi ya Teknolojia katika kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeimarisha jukwaa la ujifunzaji na ufundishaji kwa wanafunzi wa sekondari kwa kulifungamanisha na teknolojia ya akili unde kama msaidizi wa mwanafunzi katika kujisomea, kufanya majaribio ya kidijiti na kujipima. Aidha, msisitizo umewekwa katika matumizi ya akili unde kama nyenzo ya kujifunza na kujijengea umahiri na si kama njia ya kumpatia mwanafunzi majawabu ya moja kwa moja;

(ii) imeboresha jukwaa la shule mtandao (Online Public School) kuwa jumuishi ili kuwezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kutumia maudhui ya kielektroniki kwa urahisi kupitia TEHAMA. Aidha, imehaulisha masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi, hisabati, jiografia na english ya kidato cha kwanza na cha pili kuwa maudhui shirikishi yanayojumuisha sauti na picha (audio-visual), maudhui ya sauti, maabara mtandao (virtual laboratories), video za maelekezo (instructional videos) na video za kufundishia darasani. Hatua hii imelenga kuongeza wigo wa upatikanaji wa maarifa na kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia duniani; na

(iii) imejenga jukwaa la kidijiti kwa ajili ya maudhui ya elimu ya msingi darasa la I hadi V kupitia mfumo wa shule mtandao katika Taasisi ya Elimu Tanzania ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA. Hatua hizi zinafanya elimu ya

Tanzania kuendana na mabadiliko ya kidijitali duniani na kuwajengea wanafunzi uwezo wa kutumia teknolojia katika kujifunza na kufanya kazi.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imekamilisha ujenzi wa mfumo wa shindano la walimu la stadi za kufundishia utakaotumiwa na walimu wa shule za msingi na sekondari kwa masomo yote ambapo jumla ya walimu 2,800 wamewasilisha video za ufundishaji ili kufanyiwa tathmini. Mfumo huo umeongeza ufanisi wa kuwapata walimu mahiri watakaopata zawadi mbalimbali ikiwemo kurekodi video za mfano zitakazotumiwa na walimu wengine katika kufundishia na kujifunzia.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuimarisha upatikanaji wa vifaa kwa walimu na wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imenunua na kugawa vifaa vya kielimu na saidizi kwa walimu, wakufunzi na walimu tarajali wenye ulemavu. Vifaa hivyo ni pamoja na kompyuta mpakato 688, mashine za kidigiti za kurekodi sauti 377, tablets 196, mashine za Breili ya kieletroniki 19, emboza sita, mashine za kuongeza sauti saba na seti za kupima usikivu vinne. Vifaa hivyo, vimesambazwa katika shule za msingi 309, shule za sekondari 629, na vyuo vya ualimu 10. Wanufaika wa vifaa hivyo ni wenye ulemavu wa viungo 342, wenye changamoto ya uoni 312, wenye uziwi 155, wenye ualbino 190 na wenye usikivu hafifu 198;

(ii) imenunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi na walimu wenye mahitaji maalum ikiwemo *laptops* 270, vitimwendo 20, Breille mashine 100, *tablets* 180, shime sikio 100 na kuvisambaza katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 145, vyuo vya maendeleo ya wananchi 55 na vyuo tisa vya ufundi stadi na marekebisho na wenye ulemavu ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi hao;

(iii) imetoa vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum 1,127 (wanawake 475 na wanaume 652) wanaosoma katika taasisi za elimu ya juu. Vifaa hivo ni pamoja na fimbo za kutembelea 42, vinasa sauti 22, vifaa vya kusaidia kusikia 27, kisoma biti 10, viti vya magurudumu tisa, kofia pama 13, losheni ya kujikinga na jua 13, magongo ya kutembelea nane, kompyuta mpakato 65, perking braille nane, bajaji tisa, tablets 37 na miwani tatu;

(iv) imegharamia ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi 110 wenye mahitaji maalum pamoja na vifaa 122 vya utafiti kwa wanataaluma ili kuhakikisha ya kuwa watu wenye mahitaji maalum wanapata fursa sawa za elimu katika elimu ya juu.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imenunua vifaa vya kujifunzia na kufundishia katika vyuo 34 vya ualimu na vifaa vya maabara katika vyuo 13 vya Serikali. Vilevile, imegharamia huduma ya chakula kwa wanafunzi 12,343 wa vyuo vya ualimu 34 vya Serikali.

**67.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea na utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya Kitaalamu ya Walimu kwa kuweka mifumo na taratibu mbalimbali za utendaji wa Bodi hiyo ikiwemo:-

(i) ujenzi wa mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu;

(ii) kuandaa moduli za mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania ambazo ni moduli ya usajili na utoaji wa leseni kwa walimu na moduli ya usimamizi wa utoaji wa mafunzo endelevu kwa walimu; na

(iii) kuandaa muundo wa mwongozo wa viwango vya ufundishaji kwa walimu.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo endelevu ni muhimu katika kuendeleza na kuimarisha utendaji kazi wa walimu, wakufunzi, wathibiti ubora wa shule na wasimamizi wa elimu nchini. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(i) imetoa mafunzo kwa walimu na wanafunzi 206,296 kuhusu matumizi ya majukwaa ya kidijiti na maktaba mtandao ili kuwawezesha walimu kutumia maktaba mtandao na nyenzo nyingine za kidijiti katika utekelezaji wa mtaala;

(ii) imetoa mafunzo kwa walimu 124,601 (wa shule za serikali 121,494 na zisizo za serikali 3,107) kwa mchanganuo ufuatao: 34,305 kuhusu ufundishaji wa stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, wakuu wa shule 379 kuhusu usimamizi na utekelezaji wa Mafunzo Endelevu ya Walimu Kazini (MEWAKA), 89,917 kuhusu mbinu mbalimbali za kuboresha ufundishaji na ujifunzaji darasani wakiwemo 49,000 wa shule za msingi za Serikali, 37,810 wa shule za sekondari za Serikali na 3,107 wa shule za sekondari zisizo za Serikali;

(iii) imetoa mafunzo kwa walimu 6,024 wa shule za awali na msingi kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia kupitia mpango wa shule salama kwa lengo la kuboresha huduma za malezi, ushauri na unasihi shuleni;

(iv) imetoa mafunzo kwa viongozi wa elimu 5,297 (wanaume 3,663 na wanawake 1,634) kuhusu utekelezaji wa Mwongozo wa Motisha kwa Walimu kwa mchanganuo ufuatao; maafisa elimu kata 3,876, wakurugenzi wa halmashauri 137, maafisa elimu wilaya 363, maafisa elimu taaluma 363, wathibiti ubora wa shule wa wilaya 184, makatibu wa tume ya walimu 153, maafisa utumishi 172, maafisa elimu mkoa na maafisa taaluma 49; kwa lengo la kuimarisha utaratibu wa kutoa motisha kwa walimu katika halmashauri;

(v) imetoa mafunzo kwa walimu 1,964 na wasimamizi wa elimu 676 kuhusu ufundishaji wa somo la elimu ya biashara,

mafunzo kwa walimu 317 kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji, mafunzo kwa walimu 302 na maafisa elimu kata 248 kuhusu tathmini ya ujifunzaji, na mafunzo kwa walimu 165 wa Hisabati na Sayansi na wasimamizi 65 kuhusu ufundishaji wa masomom hayo;

(vi) imetoa mafunzo ya uongozi bora kwa maafisa elimu mkoa 26, maafisa elimu wilaya 182 na maafisa elimu kata 1,960 kwa lengo la kuimarisha umahiri katika kusimamia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023;

(vii) imetoa mafunzo ya muda mrefu kwa walimu 1,972 katika kozi za Astashahada, Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu na Uthibiti Ubora wa Shule katika Kampasi za Bagamoyo, Mbeya na Mwanza kupitia Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu – ADEM; na

(viii) imetoa mafunzo kwa walimu 149 na viongozi 207 wa Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana walio Nje ya Shule -IPOSA kuhusu kufundisha, kuanzisha na kuendeleza vituo vya IPOSA katika wilaya ya Kasulu, Kakonko na Sumbawanga na namna ya kupata wanufaika wa mradi.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo haya yanaimarisha umahiri wa walimu na kuongeza ubora wa ujifunzaji darasani. Hii ni hatua muhimu katika kuhakikisha mageuzi ya elimu yanafanikiwa.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum, Serikali imetekeleza yafuatayo:-

(i) imetoa mafunzo kwa watekelezaji wa elimu jumuishi 224 wa shule za msingi kuhusu kuwabaini na kutoa huduma jumuishi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(ii) imetoa mafunzo kuhusu utambuzi na ubainishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum kwa waratibu wa elimu jumuishi 26 kutoka vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vya maendeleo ya wananchi 35. Aidha, imetoa mafunzo kwa watendaji 51 kutoka katika vyuo vikuu saba vya umma kuhusu ujumuishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(iii) imetoa mafunzo kwa walimu wa shule za msingi na sekondari 350, wakufunzi 50 kutoka vyuo vya ualimu, wahadhiri wa vyuo vikuu 74 na wanafunzi 200 kutoka taasisi za elimu ya juu kuhusu matumizi ya TEHAMA na teknolojia saidizi;

(iv) imetoa mafunzo kwa wanafunzi 205 wa elimu ya juu kuhusu huduma za upatikanaji wa huduma za usaidizi ili waweze kujifunza kwa ufanisi na imetoa mafunzo kwa wakutubi 19, maafisa TEHAMA 19, maafisa maabara 19 kutoka taasisi za elimu ya juu kwa lengo la kuboresha utoaji wa huduma kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; na

(v) imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia saidizi kwa wanafunzi 100 na watumishi 35 wenye mahitaji maalum katika taasisi 19 za elimu ya juu kwa lengo la kuimarisha matumizi ya teknolojia saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa walimu 1,223 wanaosoma stashahada ya ualimu wa elimu maalum ili kuongeza idadi ya walimu wenye umahiri wa kufundisha elimu jumuishi kwa shule za awali na msingi.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, pia imeendelea kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mipango na miongozo inayotolewa na Wizara ili kuhakikisha elimu ya msingi, sekondari na ualimu inatolewa kwa ufanisi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imefanya ufuatiliaji wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la elimu jumuishi na mawasiliano ya kitaalam ya Lugha ya Alama ya Tanzania kwa walimu wa vyuo vya ualimu vya Serikali 34 na visivyo vya Serikali 13 kwa lengo la kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa darasa jumuishi katika shule za msingi;

(ii) imefanya tathmini ya matumizi ya TEHAMA na teknolojia saidizi katika shule 15 za msingi zinazopokea wanafunzi wenye uziwi- kutokuona kwa lengo la kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji kwa kundi husika. Changamoto zilizobainishwa zimetatuliwa kwa kununua vifaa vya TEHAMA na teknolojia saidizi 10,601 ili kuwawezesha wanafunzi wenye mahitaji maalum kujifunza kwa ufanisi;

(iii) imefanya ufuatiliaji katika shule kongwe 27 za msingi na 26 za sekondari zinazotoa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na kutoa ushauri wa namna ya kuboresha huduma na utoaji wa elimu kwa wanafunzi;

(iv) imefanya ufuatiliaji wa ujenzi wa karakana 27 zilizojengwa kwa ajili ya Mpango wa Elimu Changamani kwa Vijana Walio Nje ya Shule-IPOSA katika mikoa wa sita ambayo ni Manyara, Shinyanga, Simiyu, Singida, Pwani na Tanga inayotekeleza programu ya IPOSA na kutoa ushauri ili kuimarisha utoaji wa mafunzo;

(v) imefanya ufuatiliaji katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 18 na vyuo vya maendeleo ya wananchi tisa kwa lengo la kubaini mahitaji ya ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum na kutoa ushauri stahiki;

(vi) imefanya ufuatiliaji wa vitabu vya darasa la VII vilivyosambazwa na Taasisi ya Elimu Tanzania kwa lengo la kupata taarifa kuhusu usambazaji, mapokezi na matumizi ya vitabu husika katika ngazi za mikoa, halmashauri na shule za awali na msingi;

(vii) imefanya ufuatiliaji katika vyuo vya ualimu 23 (vyuo vya Serikali saba na visivyo vya serikali 16) vinavyotoa mafunzo ya ana kwa ana kwa walimu wanaojiendeleza. Aidha, ufuatiliaji ulibaini kwamba kuna uhitaji wa walimu kujiendeleza katika ngazi ya stashahada, hivyo serikali imeanzisha programu ya masafa kwa lengo la kuwawezesha walimu kujiunga na mafunzo pasipo kuathiri majukumu yao;

(viii) imefanya tathmini ya moduli 39 zitakazotumika kuendesha mafunzo kwa walimu kazini ili kuimarisha utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu;

(ix) imefanya tathmini ya moduli 15 za MEWAKA zinazohusu matumizi ya teknolojia katika elimu kwa lengo la kupima ubora, uhalisia na ufanisi wake katika kuwawezesha walimu wa elimu ya sekondari kuimarisha umahiri wao wa matumizi ya teknolojia na mbinu za kufundishia na kujifunzia;

(x) imefanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo ya uongozi na usimamizi kwa ajili ya wakuu na makamu wakuu wa shule za sekondari kupitia Wakala wa Maendeleo ya Elimu - ADEM ili kuimarisha usimamizi wa shule. Tathmini itasaidia kuboresha mbinu za kufundisha, kushauri, kusimamia mitaala na kuweka mkakati wa kuandaa mafunzo; na

(xi) imefanya tathmini ya utekelezaji wa mafunzo ya amali kwa shule za sekondari 201 zilizoteuliwa kwa kuzingatia matakwa ya sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la mwaka 2023. Tathmini hii imeonyesha kuwa zaidi ya asilimia 75 ya wanafunzi katika shule zinazotekeleza mkondo wa amali wamepokea vyema mpango huo na wako tayari kusoma fani mbalimbali zinazotolewa na shule hizi. Hatua hii inaonesha dhamira ya Serikali ya kuhakikisha hakuna mtoto anayekosa haki ya elimu. Elimu ni haki ya kila Mtanzania, si fursa ya wachache.

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuongeza fursa za elimu kupitia vituo vya utoaji wa elimu kwa njia mbadala

kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imewezesha kurejesha wanafunzi 3,467 ikiwemo wanawake 2,062 na wanaume 1,405 waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujauzito ambao wameendelea na shule kupitia elimu kwa njia mbadala (Altenative Education Pathway);

(ii) imetoa mafunzo kwa vijana 16,732 walio nje ya shule kupitia Mpango wa Elimu Changamani (Intergrated Program for Out of School Adolescent -IPOSA);

(iii) imeendesha vipindi vya ana kwa ana na programu huria na masafa kwa jumla ya wanafunzi 2,486 (wanaume 1,183 na wanawake 1,303) kama ifuatavyo: Astashahada 172 (wanawake 87 na wanaume 85), Astashahada Ufundi 100, Stashahada 1,537 (wanawake 836 na wanaume 701) na Shahada 777 (wanawake 380 na wanaume 397); na

(iv) imeendelea kuboresha utoaji wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala na kuongeza fursa za programu za elimu ya kisomo (kusoma, kuandika, kuhesabu na kisomo cha kujiendeleza) katika vituo 191 vya elimu ya watu wazima na waliokosa elimu kwa njia ya mfumo rasmi katika mikoa 26 ya Tanzania Bara ambapo hatua ya I na II ya mitihani ya majaribio ilifanyika kwa wanafunzi 5,438 (wanawake 3,761 na wanaume 1,677).

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imefanya tathmini ya matokeo ya utekelezaji wa sera na miongozo ya kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali (Impact Assessment of School Re-Entry Policies in Mainland Tanzania - 2025). Tathmini husika imewezesha kubaini mafanikio katika utekelezaji wa sera na miongozo pamoja na changamoto zinazoweza kuathiri utekelezaji.

**75. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imefanya utafiti kuhusu changamoto ya mdondoko wa wanafunzi katika shule za msingi na sekondari nchini 2025 (Understanding the Problem of School Dropouts in Tanzania's Primary and Secondary Schools). Utafiti umebaini sababu za wanafunzi kukatiza masomo na kutoa mapendekezo yatakayoisaidia kuweka mikakati na afua za kudhibiti tatizo la mdondoko wa wanafunzi.

**76. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuwezesha upimaji na tathmini kwa wanafunzi na watahiniwa wa elimu ya msingi, sekondari na vyuo vya ualimu kupitia Baraza la Mitihani la Taifa kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) imeendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne wa mwaka 2025 kwa wanafunzi 1,490,314 (wasichana 780,541 na wavulana 709,773) sawa na asilimia 94.10 ya wanafunzi 1,583,686 (wasichana 818,673 na wavulana 765,013) waliosajiliwa. Aidha, katika upimaji huo wanafunzi 1,324,970 (wasichana 703,287 na wavulana 621,683) walifaulu sawa na asilimia 88.91;

(ii) imeendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi 2025 kwa watahiniwa **1,146,231** (wasichana ni 626,147 na wavulana ni 520,084) sawa na asilimia 97.77 ya watahiniwa **1,172,324** waliosajiliwa (wasichana 637,162 na wavulana 535,162) ambapo watahiniwa **937,581** (wasichana 508,477 na wavulana 429,104) sawa na asilimia 81.80 walifaulu mtihani huo;

(iii) imeendesha upimaji wa Kidato cha Pili kwa wanafunzi **819,012** (wasichana ni 461,318 na wavulana ni 357,694) sawa na asilimia 91.13 ya watahiniwa **898,718** waliosajiliwa (wasichana 497,891 na wavulana 400,827). Aidha, idadi ya wanafunzi waliofaulu walikuwa **710,118** kati yao wasichana ni 395,238 na wavulana ni 314,880;

(iv) imeendesha Mtihani wa Kidato cha Nne wa mwaka 2025 kwa watahiniwa **578,400** sawa na asilimia 97.08 ya

watahiniwa 595,810 waliosajiliwa. Watahiniwa **543,414** walifaulu sawa na asilimia 94.15 kati yao wasichana ni 288,015 na wavulana ni 255,399; na

(v) imesajili watahiniwa 133,749 kwa ajili ya Mtihani wa kuhitimu Kidato cha sita wa mwaka 2026. Vilevile, imesajili watahiniwa 10,725 wa Mtihani wa Elimu ya Ualimu wa mwaka 2026.

**77.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali, imefanya utafiti katika shule 45 za msingi katika halmashauri 10 za mikoa mitano ambayo ni Kigoma, Dar es Salaam, Mtwara, Songwe na Morogoro kuhusu matumizi ya kiongozi cha mwalimu katika kufundishia na kujifunzia stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Matokeo ya utafiti yatasaidia kuimarisha ujifunzaji na ufundishaji wa stadi za KKK nchini na kutekeleza mipango mahususi iliyowekwa katika mpango wa kuhakikisha kuwa kila mtoto anayeingia darasa la tatu, anajua kusoma, kuandika na kuhesabu.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kutumia majukwaa mbalimbali ya kitaifa na kimataifa kuhamasisha na kutoa elimu kwa umma kuhusu elimu jumuishi na elimu ya watu wazima kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imetoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa uandikishaji watoto wenye ulemavu, mabadiliko ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 na mitaala iliyoboreshwa ya mwaka 2023 pamoja na utekelezaji wa shule ya nyumbani (home schooling) kupitia maadhimisho ya siku ya watu wenye ulemavu, siku ya viziwi, wenye ualbino, fimbo nyeupe na braille kitaifa ambapo watu 8,201 walishiriki;

(ii) imeendesha Kongamano la Kitaifa la Elimu Jumuishi lililojumuisha washiriki 420 ikiwemo wanafunzi wenye ulemavu 220 na wasiyo na ulemavu 170 kutoka taasisi 19 za elimu ya juu, walezi 10 wa wanafunzi wa vyuo vikuu, waratibu 20 wa elimu jumuishi katika vyuo vikuu kwa lengo kuwajengea

uelewa wa elimu jumuishi na namna bora ya kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum katika taasisi zao; na

(iii) imefanya Maadhimisho ya Siku ya Kisomo Kimataifa na Juma la Elimu ya Watu Wazima tarehe 15-19/09/2025 Mkoani Katavi ambapo takribani washiriki 1,000 walihudhuria. Lengo la maadhimisho hayo ni kuhamasisha jamii kutumia fursa mbalimbali za elimu zinazotolewa na Serikali ili kunufaika kiuchumi na kijamii.

## d. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuimarisha fursa katika elimu ya juu kwa kutoa mikopo kwa wanafunzi wa stashahada na shahada kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imeratibu udahili wa wanafunzi 170,916 (wanawake 78,021 na wanaume 92,895) walioomba kujiunga na elimu ya juu kwa ngazi ya shahada ya kwanza katika vyuo vya elimu ya juu nchini kwa mwaka wa masomo 2025/26. Kati ya maombi hayo, waombaji 159,010 (wanawake 74,973 na wanaume 84,037) sawa na asilimia 93 walidahiliwa ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 21,193 ikilinganishwa na wanafunzi 137,817 waliodahiliwa mwaka 2024/25;

(ii) imetoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu 284,487 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi 245,384 waliopata mikopo mwaka 2024/25 ambapo wanafunzi wa mwaka wa kwanza ni 106,606 (wanawake 50,060 na wanaume 56,546), Shahada ya kwanza ni 94,451 (wanawake 45,092 na wanaume 49,359), stashahada 11,844 (wanawake 4,863 na wanaume 6,981), na shahada za juu 311 (wanawake 105 na wanaume 206). Vilevile, imetoa mikopo kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo 177,881 (wanawake 80,901 na wanaume 96,980) ambapo shahada ya kwanza 170,942 (wanawake 78,244 na wanaume 92,698) shahada za Juu 110 (wanawake 38 na wanaume 72) na stashahada 6,829 (wanawake 2,619 na wanaume 4,210); na

(iii) imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 180.8** kutokana na mikopo iliyoiva kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu sawa na asilimia **82** ya lengo la kukusanya **Shilingi Bilioni 220,273,850,000.00**.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** mabadiliko ya kasi ya teknolojia, hasa katika masuala ya akili-unde, yaani artificial intelligence, ni fursa kubwa sana kwa binadamu kuweza kufanya maisha yakawa bora zaidi. Akili-unde itaboresha sana tiba na afya ya binadamu kwa ujumla, itaongeza tija katika kilimo, itaboresha na kuimarisha sana elimu, itabadilisha sana namna nchi zinavyoweza kusimamia ulinzi na usalama na kadhalika. Akili-unde na taaluma kama hizi inakuwa kwa kasi kubwa sana duniani, na ni maendeleo ambayo hayaepukiki na hayazuiliki. Lakini mabadiliko haya ya teknolojia yanaweza kuwa ni changamoto kubwa na ya kutisha kwa binadamu kama juhudi stahiki zisipochukuliwa za kuielewa, kuimudu na kuisimamia teknolojia hii ya akili-unde na taknolojia zinazoendana nayo. Kwa mfano, kuna uwezekano mkubwa sana wa muundo wa ajira kubadilika sana na kusababisha watu wengi kupoteza ajira kwa sababu ya kasi na ukubwa wa maendeleo ya taknolojia.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Akili-unde pia inaweza kuumiza watu na nchi kwa namna nyingi, ikiwa ni pamoja na kugusa mambo ya ulinzi na usalama, kuingilia taarifa za watu bila mipaka na kadhalika. Serikali inatambua kuwa ni muhimu kujenga uwezo wa nchi yetu katika kuielewa, kuimudu na kutumia vizuri teknolojia ya akili-unde na teknolojia kama hizo ili kufanya maendeleo haya yawe fursa badala ya kuwa changamoto.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kujenga na kuimarisha uwezo wa nchi yetu katika masuala ya akili-unde na teknolojia za mwelekeo huo, Serikali imeanzisha utaratibu wa kufadhili vijana wa Kitanzania kwenda kusomea mambo ya akili-unde. Moja ya hatua hizi ni kufadhili vijana wa Kitanzania kusoma nje ya nchi katika vyuo vizuri na ambavyo

vina utaratibu mzuri wa kutoa taaluma darasani na ujuzi kupitia ushirikiano na makampuni ya teknolojia. Kwa minajili hiyo, Wizara imeanzisha ufadhili unaojulikana kama Samia *Scholarship Extended*, DS/AI+. Ufadhili huu unaendeshwa kwa uwazi na ushindani. Kwa kuanzia wanafunzi 50 waliopata ufaulu wa juu zaidi katika matokeo ya kidato cha sita mwaka 2025 kwenye tahasusi za sayansi zinazojumuisha hisabati walichaguliwa kwa ajili ya kupelekwa nje kwa masomo.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wanafunzi hawa wamechaguliwa kutokana na matokeo yao kuwa bora zaidi kuliko wengine kwa utaratibu wa uwazi na ushindani. Wanafunzi hawa walipelekwa kwenye kambi ya mafunzo katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela iliyopo Arusha. Kambi hii ya mafunzo ni ya maandalizi ya wanafunzi hao kabla hawajapelekwa nje kusoma. Aidha, kati ya wanafunzi 50 waliochaguliwa, kumi na sita wameshapelekwa Chuo Kikuu cha Johannesburg kuanza masomo. Wanafunzi 34 waliobaki wameshakubaliwa kujiunga na vyuo vikuu nchini Ireland. Kati yao wanafunzi 32 watajiunga na Chuo Kikuu cha Limerick nchini Ireland na wanafunzi wawili watajiunga na Chuo Kikuu Kishiriki cha Dublin nchini Ireland. Wanafunzi hawa wanatarajia kuondoka nchini kuelekea Ireland mwezi wa tisa mwaka huu.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** wanufaika wa Mpango wa Samia Scholarship Extended DS/AI+ wamepata punguzo la ada ya masomo kwa asilimia 50 katika Chuo Kikuu cha Limerick nchini Ireland kufuatia makubaliano yaliotiwa saini Machi 26, 2026 jijini Dar es Salaam. Makubaliano hayo yamelenga kuongeza fursa za elimu ya juu kwa vijana wa Kitanzania katika fani za kisasa ikiwemo Sayansi ya data, Akili unde na Sayansi Shirikishi. Vijana hao ni sehemu ya wanufaika 50 wa mpango huo wa ufadhili unaolenga kukuza rasilimaliwatu wenye ujuzi wa hali ya juu katika sekta ya teknolojia. Kwa upande wa wanafunzi 16 waliokwenda Chuo kikuu cha Johannesburg nchini Afrika Kusini, makubaliano ya ushirikiano

yaliyopo yaliwawezesha kufikiriwa katika kundi la wanafunzi wanaotoka nchi za SADC ambao wanalipa kiasi kidogo cha ada ukilinganisha na wanafunzi wanaotoka nchini za kigeni.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** mpango huu ni hatua muhimu katika kuwawezesha vijana wenye vipaji kupata elimu na ujuzi unaoendana na mahitaji ya dunia ya sasa ya kidijitali ikiwa ni jitihada ya utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo ya mwaka 2014, Toleo la 2023 inayosisitiza umuhimu wa kuandaa nguvu kazi yenye ujuzi hasa katika maeneo ya sayansi.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kuwakaribisha wadau wa elimu kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuchangia mfuko wa Samia Scholarship ili kuongeza idadi ya wahitimu katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa elimu ya juu kama ifuatavyo:-

(i) imetoa ufadhili wa masomo kupitia SAMIA skolashipu kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza 936 (wanawake 288 na wanaume 648) na wanaoendelea wanafunzi 850 (wanawake 325 na wanaume 525) wa shahada ya kwanza na shahada ya uzamili 66 (wanawake 24 na wanaume 42);

(ii) imetoa ufadhili kwa wanafunzi wanne wanaosoma Shahada ya Umahiri katika vyuo bora duniani katika fani za: *Nuclear Medicine* (1), *Medical Physics* (2), na *Nuclear Engineering/Power Plants and Research Reactors* (1) kupitia SAMIA *Scholarship Extended* (*Nuclear Science*). Lengo likiwa ni kuongeza wataalamu katika eneo hilo nchini; na

(iii) imetoa ufadhili kwa wanafunzi 10 wasichana wenye ufaulu wa juu katika mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita katika masomo ya sayansi kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuimarisha ushirikiano baina ya vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imepokea jumla ya vijana wa mafunzo kwa vitendo 19 na wakufunzi watano kutoka India, Palestina, Yemen, Tunisia, Ujerumani, Austria, Jamhuri ya Czech, Uhispania, Uswisi na Iran. Vijana hao walipata mafunzo katika taasisi mbalimbali ikiwemo Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Baraza la Mitihani la Tanzania, na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa lengo la kubadilishana uzoefu katika fani za afya na sayansi shirikishi, sayansi ya viumbe, sayansi ya tiba na sayansi ya kompyuta na namna ya kuwahudumia makundi maalum;

(ii) imepokea ufadhili wa masomo kwa wanafunzi 260 kutoka nchi wahisani kama ifuatavyo: Urusi (150), China (49), Hungaria (21), Jumuiya ya Madola (11), Misri (10), Algeria (8), Morocco (4), Mauritius (4), Korea ya Kusini (2) na Shirika la Kimataifa la Nguvu la Atomiki (1) (International Atomic Energy Agency- IAEA); na

(iii) imeendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 15 kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha uhusiano wa kiutendaji kati ya Kamati 33 za Ushauri wa Viwanda (*Industrial Advisory Committees*) kwa kutoa ushauri kuhusu maboresho ya mitaala, mahitaji ya ujuzi kazini na mwelekeo wa sekta za uzalishaji. Vilevile, mikataba 250 ya ushirikiano (MoUs) imesainiwa kati ya vyuo vikuu na wadau wa viwanda na sekta binafsi kwa ajili ya kuimarisha mafunzo kwa vitendo, tafiti shirikishi, ubunifu na uhamishaji wa teknolojia. Kupitia ushirikiano huu, wanafunzi 154,417 wamepatamafunzo kwa vitendo viwandani na wahadhiri 612 wamepata uzoefu wa kazi viwandani uliosaidia kuboresha mbinu za ufundishaji

na kuongeza uhalisia wa maudhui ya kitaaluma kulingana na mahitaji ya soko la ajira.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika taasisi za elimu ya juu kwa kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) imeendelea na ujenzi wa majengo mapya 130 yanayojumuisha madarasa, maabara, kumbi za mihadhara, ofisi, mabweni na vituo vya utafiti katika maeneo 47 ya taasisi 20 zinazotekeleza mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi ambapo majengo mapya matano yamekamilika na ujenzi wa majengo mengine umefikia wastani wa asilimia 57.6. Vilevile, imekarabati miundombinu 18 ya kufundishia na kujifunzia na kuweka vifaa vya kisasa katika majengo 36 (Taarifa ya hatua za ujenzi katika kila taasisi ni kama ilivyobainishwa katika **Kiambatisho Na. 3**). Kampasi hizi zitakapokamilika zitatoa mafunzo ya ujuzi ili kuandaa wahitimu wenye ujuzi unaotakiwa na soko la ajira ndani na nje ya nchi;imeendelea na ujenzi wa maktaba ya kisasa yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 1,500 kwa wakati mmoja katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa ambapo ujenzi umefikia asilimia 48. Aidha, inaendelea na ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 276 kwa kila bweni ambapo wastani wa hatua ya ujenzi umefikia asilimia 58;

(ii) imeendelea na ujenzi wa awamu ya kwanza wa hosteli yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500 katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ambapo ujenzi umefikia asilimia 81;

(iii) imeendelea na ujenzi wa jengo la utawala lenye uwezo wa kuchukua watu 1,800 kwa wakati mmoja ambapo utekelezaji umefikia asilimia 90 katika Chuo Kikuu Mzumbe kampasi kuu. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa jengo la taaluma Tegeta ambapo ujenzi umefikia asilimia 18;

(iv) imeendelea na ujenzi wa ofisi ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu Dodoma ambapo ujenzi umefikia asilimia 84;

(v) imeendelea kuboresha miundombinu ya usambazaji wa maji safi katika Chuo Kikuu cha Dodoma ambapo ujenzi wa tanki la maji katika ndaki ya elimu umefikia asilimia 90. Vilevile, imeunganisha miundombinu ya majitaka katika Hosteli 10 Ndaki ya Elimu na mabweni 3 Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu katika chuo hicho. Aidha, imeendelea na ujenzi wa bweni moja lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 240 kwa wakati mmoja mkoani Iringa umefikia asilimia 26;

(vi) imekamilisha ujenzi wa jengo la TEHAMA lenye uwezo wa kuchukua watu 750 kwa mara moja pamoja na usimikaji wa mifumo ya TEHAMA, jengo la taaluma lenye uwezo wa kuchukua watu 2,000 kwa mara moja, na hosteli moja yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 212 kwa wakati mmoja. Aidha, imeendelea na ujenzi wa jengo la maktaba lenye uwezo wa kuchukua watumiaji 2,500 kwa wakati mmoja ambapo ujenzi umefikia asilimia 75.3 katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi;

(vii) imeendelea na ukarabati wa jengo la utawala wing A na B katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania ambapo ukarabati umefikia asilimia 78 na inaendelea na ujenzi wa ofisi ya taaluma katika kituo cha uratibu Pemba ambapo ujenzi umefikia asilimia 70;

(viii) imeendelea na ukarabati wa jengo la Tume ya Sayansi na Teknolojia ambapo ukarabati umefikia asilimia 97;

(ix) imekamilisha ujenzi wa jengo la utawala katika Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu Nyerere;

(x) imekarabati hosteli tano za wanafunzi katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya;

(xi) imekamilisha upanuzi wa Hosteli ya Dkt. J.P.J. Magufuli (Blocks A na E) kwa kuongeza ghorofa mbili ambao umeongeza malazi kwa kwa wanafunzi 576 na imeendelea na uwekaji wa samani katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na

(xii) imekamilisha ujenzi wa jengo la auxiliary police katika Kampasi ya Solomon Mahlangu kwa ajili ya kuimarisha usalama chuoni. Aidha, imeendelea na ukarabati wa miundombinu katika bweni namba moja na saba katika Kampasi ya Edward Moringe na bweni katika kampasi ya Solomon Mahlangu na nyumba tano za watumishi katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ambapo ukarabati umefikia asilimia 95.

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeanza maandalizi ya ujenzi wa Kituo cha Umahiri cha Magonjwa ya Moyo (awamu ya II) katika Kituo cha Taaluma ya Afya cha Mloganzila. Aidha, wanataaluma 15 wamepata ufadhili wa kusoma kwenye magonjwa ya moyo na mishipa ya damu ambapo ngazi ya umahiri ni 10 na uzamivu ni watano.

**92.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inakidhi miongozo inayotolewa na mahitaji ya soko la ajira, serikali imeendelea kusimamia na kuthibiti ubora wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu na taasisi ya elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imetoa ithibati kwa programu 233 kati ya 461 zilizofanyiwa tathmini kama ifuatavyo: astashahada saba, shahada 193, shahada ya uzamili 23, na shahada ya uzamivu 10;

(ii) imetathmini na kutambua tuzo 1,240 zilizokidhi vigezo kati ya tuzo 1,636 za waombaji waliosoma vyuo vikuu vya nje ya nchi kama ifuatavyo: Astashahada ya Uzamili mmoja, cheti sita, stashahada 63, shahada 681, stashahada ya uzamili 14, shahada ya uzamili 394 na shahada ya uzamivu 81;

(iii) imetathmini usajili wa vyuo vikuu vya nje ya nchi kwa maombi ya wanafunzi 1,570 waliodahiliwa katika vyuo hivyo na kutoa hati ya kutokuwa na pingamizi (No Objection Certificate) kwa wanafunzi 1,472 waliodahiliwa katika vyuo vinavyotambulika kama ifuatavyo: cheti wawili, diploma 135, cheti cha uzamili mmoja, shahada 1,189, shahada ya uzamili 123, na shahada ya uzamivu 22; na

(iv) imefanya ukaguzi kwa mawakala nane wanaohusika kupeleka wanafunzi kusoma katika vyuo vya nje ya nchi kwa lengo la kuwasajili na kuhuisha usajili wa leseni za uwakala.

**93. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuimarisha matumizi ya Teknolojia katika kufundisha na kujifunza katika taasisi za elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imeboresha miundombinu ya mawasiliano, teknolojia na habari katika taasisi 19 za elimu ya juu kwa kuziwezesha kutumia mfumo wa "moodle" kama njia muhimu ya kuendesha programu. Aidha, taasisi tano zimeongeza kasi ya mtandao wa intaneti katika kampasi ili kuongeza ufanisi na taasisi tatu zinaendelea na ujenzi wa studio za "multimedia" kwa ajili ya kuendesha kozi na mafunzo;

(ii) imeanzisha multimedia studio katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela ili kuimarisha utekelezaji wa mafunzo ya kielektroniki katika kufundisha na kujifunza; na

(iii) imesajili mifumo miwili ya kanzidata ya rasilimali za maktaba ambayo ni EBSCOhost na Emerald Insight ili kuwezesha upatikanaji maarifa kwa njia ya kielektroniki kwa wanafunzi katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

**94. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuimarisha masuala mtambuka ikiwemo mazingira, masuala ya kijinsia na elimu ya afya katika taasisi za elimu ya juu kwa kutoa mafunzo

kwa wanafunzi 34,000 kuhusu umuhimu wa kuimarisha maadili na kupinga ukatili wa kijinsia ili kufanya vyuo kuwa sehemu salama ya kuishi, kufanya kazi na kupata ujuzi na mafunzo.

**95. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imeendelea kuwezesha wahadhiri na watumishi waliopo katika vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kwa kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 1,179 (astashahada 3, stashahada 12, shahada ya kwanza 37, shahada ya umahiri 422 na shahada ya uzamivu 703) na muda mfupi kwa watumishi 1,289 wa taasisi za elimu ya juu. Aidha, imewezesha wafanyakazi 295 wa taasisi za elimu ya juu kushiriki katika Shirikisho la Michezo ya Mashirika ya Umma (SHIMUTA) kwa lengo la kuboresha afya za watumishi.

**e. Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili Kuchangia Upatikanaji wa Maendeleo Endelevu**

**96. *Mheshimiwa Spika,*** utafiti ni nyenzo muhimu katika kuongeza maarifa mapya, kuchochea maendeleo ya uchumi na kutatua changamoto mbalimbali za kijamii. Serikali kwa kutambua umuhimu huo imetekeleza yafuatayo:-

(i) imeratibu jumla ya miradi 168 ya utafiti ikiwemo miradi 19 ya Mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu - MAKISATU. Kati ya miradi hiyo 14 imekamilika. Miradi hii, imelenga kutoa suluhu za changamoto katika sekta muhimu za kilimo, afya, maji, nishati, uchumi wa buluu, mabadiliko ya tabia nchi, elimu, viwanda na teknolojia mpya;

(ii) imeendelea na utekelezaji wa miradi ya utafiti 261 kupitia taasisi za elimu ya juu na vyuo vya elimu ya ufundi katika maeneo ya ardhi, ujenzi, maji, tabianchi, mazingira, kilimo, afya, elimu, viwanda, sayansi ya jamii, teknolojia, biashara, ushirika na uwekezaji kwa lengo la kubaini changamoto na kutolea utatuzi katika sekta husika;

(iii) imekamilisha utafiti kuhusu maendeleo ya teknolojia ya kuwezesha ufanisi wa matumizi ya maji ya mvua na umwagiliaji rahisi. Kukamilika kwa utafiti huo, umewezesha wananchi wa Magugu Babati kupata ujuzi wa kutumia maji ya mvua katika kilimo cha mpunga. Aidha, Chuo cha Ufundi Arusha kinaendelea na utafiti wa "Taswira za Mavuno ya Mpunga" kwa kutumia taarifa za satelite; na

(iv) imeendelea kuimarisha makundi ya utafiti (research clusters) kwa kutoa mafunzo kwa viongozi wa makundi hayo kuhusu majaribio ya teknolojia ya kuvuna senene katika wilaya nne za mkoa wa Kagera ambazo ni Muleba, Bukoba vijijini, Bukoba Manispaa, Misenyi na Kyerwa. Teknolojia hiyo imesaidia kuongeza mavuno ya Senene na uchumi kwa wavunaji.

**97. *Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto za kimazingira na kuimarisha uwezo wa Taifa katika maendeleo ya viwanda, uchumi na ustawi wa wananchi kwa ujumla Serikali, imefadhili miradi 39 ya utafiti katika sekta mbalimbali ikiwa ni pamoja na kilimo, maji, afya, nishati, bioanuwai, mifumo ya miji na utawala bora wa hali ya hewa. Miradi hii, inatekelezwa na watafiti 281 kutoka vyuo vikuu, taasisi za utafiti na taasisi zingine za maarifa kote nchini. Uwekezaji huu utawezesha wanasayansi wa Kitanzania kuendeleza utafiti wa hali ya hewa na ubunifu ili kukabiliana na changamoto za kimazingira na kuimarisha uwezo wa Taifa katika maendeleo ya viwanda, uchumi na ustawi wa wananchi kwa ujumla.

**98. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha nchi inaendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani pamoja na kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye ya sayansi, teknolojia na ubunifu, Serikali imeendelea kutekeleza yafuatayo:-

(i) imefanya tathmini ya maudhui ya Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (1996), Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo (2010), Sera ya Taifa ya Baioteknolojia (2010), Sera ya Taifa ya Teknolojia (2013) na kuandaa taarifa ya mapendekezo inayobainisha umuhimu wa kuwa na sera moja

inayoakisi hali halisi na mahitaji ya sasa ya sayansi, teknolojia na ubunifu;

(ii) imeendeleza bunifu saba kupitia Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ambazo ilioneshwa katika maonesho mbalimbali. Bunifu hizo zinajumuisha mita ya umeme ya watumiaji wengi (multitenant electric meter), mtambo wa kuzalisha haidrojeni (*hydrogen fuel electrolyser*), fimbo ya wasiyoona (*blind stick*), mashine ya kieletroniki ya kutotolesha vifaranga (*electronically controlled incubator*), mashine ya kukata nyasi inayotumia nishati ya jua (*solar-powered grass cutter*), mashine ya kufua ya kukanyaga (*pedaled washing machine*) na mbolea ya akwaponi (*aquaponic fertilizer production system*). Bunifu hizo zinatarajiwa kubiasharishwa na kutoa fursa za ajira kwa watanzania; na

(iii) imekamilisha maandalizi ya zana za kufanyia tathmini ya uwezo wa Taasisi za Umma za Utafiti na Maendeleo kwa lengo la kubaini changamoto, mahitaji na hatua za kuziimarisha ili kuongeza mchango wake katika utafiti, ubunifu na uchumi wa viwanda kuelekea utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050.

**99.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali, imewezesha kuibiasharisha bunifu tano kupitia Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) ikiwemo mashine ya kusafishia mafuta ya kula, mashine ya kukaanga nafaka mbalimbali, taa za urembo, mashine ya kuchakata chakula cha wanyama na jiko linalotumia nishati safi. Vilevile, imewezesha bunifu nne zilizoendelezwa kuingia sokoni na hivyo kuongeza idadi ya ubunifu na teknolojia zilizoingia sokoni kutoka 42 hadi 46. Aidha, imefanya ufuatiliaji wa miradi 19 ya ubunifu iliyobainishwa na kuendelezwa kupitia MAKISATU na kubaini miradi hiyo inaendelea kuimarika kuelekea hatua ya ubiasharishaji.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imekamilisha Mfumo wa Taifa wa kukusanya, kuhifadhi na kuchakata taarifa za

masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ambapo taarifa za watafiti 2,220 na wabunifu 480 zinapatikana katika mfumo huo. Aidha, vibali vya utafiti 797 vimetolewa kupitia mfumo huo. Ukusanyaji wa taarifa zaidi za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu unaendelea kwa kushirikiana na vyuo vikuu, taasisi za maendeleo ya utafiti pamoja na vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeanza utekelezaji wa Mfuko wa 'Samia Innovation Commercialization Fund', unaolenga kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa wabunifu ili kuwezesha ubidhaishaji na ubiasharishaji wa bunifu na teknolojia za wabunifu wetu. Katika awamu ya kwanza wabunifu saba wamenufaika ambapo jumla ya Shilingi milioni 767 zimetolewa.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeimarisha ushirikiano na taasisi za utafiti na ubunifu ambapo kupitia ushirikiano huo jumla ya miradi 28 ya tafiti na ubunifu ilipokea **Shilingi bilioni 3.1** kwa ajili ya utekelezaji. Wadau hao ni pamoja na NORAD - Norway, Sida - Sweden, *National Research Foundation* -Afrika Kusini na *International Development Research Centre* - Canada.

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuwaibua, kuwatambua na kuwaendeleza wabunifu wa ndani ili kuimarisha kazi zao pamoja na kuwaunganisha na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa lengo la kukuza ubunifu wao kufikia hatua ya kuingizwa sokoni. Katika kutekeleza azma hii, jumla ya wabunifu 74 wameunganishwa na wadau mbalimbali wa maendeleo kwa lengo la kukuza ubunifu wao kufikia hatua ya kuingizwa sokoni na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa na kuboresha maisha yao kwa ujumla.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali imewasilisha hati miliki saba za ubunifu BRELLA ambapo hatimiliki mbili zimeshatangazwa na tano zinaendelea kufanyiwa kazi. Hatimiliki hizo zinatarajiwa kuendelezwa na kugeuzwa kuwa

kampuni changa (*startups*) kupitia mchakato wa uhaulishaji teknolojia. Ubunifu huo ni: Mfumo wa kiteknolojia wa kufuatilia ubora wa hewa katika Mkoa wa Dar es Salaam; Filamu ya kibaiolojia kwa ajili ya kufungashia bidhaa, inayotengenezwa kwa kutumia mwani aina ya Ulva lactuca; Mfumo mahiri wa kifaa cha mkononi kwa ajili ya huduma za LUKU; Programu ya Sitiolojia ya Macho inayotumia Akili Unde (AI) kubaini tatizo la upofu wa macho unaosababishwa na ugonjwa wa kisukari (*Diabetic Retinopathy*); Mfumo wa *GEOAMIS* kwa ajili ya uchakataji wa data na utabiri wa mafuriko; Roboti ya Akili Unde (AI) Rafiki kwa ajili ya elimu na huduma shirikishi kwa wazee; na Kifaa cha mkononi cha kufuatilia na kutabiri ukame.

**105. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kugharamia vigoda viwili vya utafiti na vituo vya umahiri katika taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela na Chuo kikuu cha Sokoine cha Kilimo chini ya mpango wa "*The O.R. Tambo Africa Research Chairs Initiative* - ORTARCHI" ambapo Serikali imetekeleza yafuatayo:

(i) imesimamia na kuendeleza kigoda cha utafiti cha *O.R-Tambo Africa Research Chairs Initiative* - ORTARCHI katika masuala ya (*Nano science na Nano technology*). Aidha, vituo viwili vya umahiri *Water Infrastructure and Sustainable Energy Future* na CREATES (*Food and Nutritional Science*) vimendelea kutekeleza shughuli za utafiti na ubunifu kupitia mpango wa uendelevu;

(ii) imeshirikiana na kampuni za Illumina na Sciex kufanya uchambuzi wa mlolongo wa jeni (whole genome sequencing) wa virusi vya African Swine Fever Virus (ASFV) vilivyopatikana kwenye kupe wanaohusishwa na nguruwe mwitu ambao umewezesha kubaini namna ya kujikinga na ugonnjwa unaotokana na virusi hivyo kwa jamii inayozunguka eneo la Serengeti;

(iii) imechapisha machapisho tisa ya kitaaluma katika majarida ya kimataifa;

(iv) imewezesha watafiti kuwasilisha matokeo ya tafiti zao katika mikutano ya *International Federation of Biosafety Associations* (IFBA), *Global Management and Development for Health* (MDH), Bioanuwai na Uhifadhi, na Chuo Kikuu cha Manchester;

(v) imewezesha kubaini tiba ya magonjwa ya wanyama kama *African Swine Fever Virus*, *Pest des Petits Ruminants, Leptospira, na Lumpy Skin* na kufanya uchambuzi wa vinasaba vya vimelea husika;

(vi) imeshirikiana na kampuni ya *Hester Bioscience Ltd* iliyopo Kibaha inayojihusisha na utengenezaji wa chanjo ambapo iliwezesha;

(a) kugundua milipuko ya virusi kwa kuku inayosababishwa na virusi vya *Newcastle Disease* na *Infectious Bursal Disease*,

(b) kubuni chanjo ya DNA inayolingana na *genotipu* ya virusi vya *Newcastle* kwa kutumia sampuli zilizokusanywa Tanzania; na

(c) kutoa mafunzo ya utafiti kwa wanafunzi 25 wa ngazi za uzamili na uzamivu.

**106. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usambazaji wa maarifa, uhamasishaji wa mijadala ya kitaaluma na kuhakikisha matokeo ya kazi za utafiti yanatumika katika kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi kwa maendeleo endelevu ya Taifa, Serikali imechapisha machapisho **1,556** ya kitaaluma kupitia Taasisi za Elimu ya juu na vyuo vya elimu ya ufundi katika ngazi ya Kitaifa na Kimataifa kwa lengo la kuongeza maarifa katika jamii kuhusu namna ya kutatua changamoto mbalimbali.

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza maarifa ya watanzania ya utatuzi wa changamoto na kuongeza tija katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, Serikali kupitia Taasisi za elimu ya juu na Taasisi za Sayansi na Teknolojia imeendelea kutoa huduma **230** za ushauri elekezi katika miradi mbalimbali ya maendeleo katika maeneo yafuatayo; ugani, vyama vya ushirika, matumizi ya udongo, mawe na nyenzo zinazotumika katika ujenzi wa miundombinu mbalimbali pamoja na kupima ubora wa maji. Aidha, imetoa huduma za usanifu na usimamizi wa miradi mbalimbali ya ujenzi na ukarabati, michoro ya usanifu na maandalizi ya makadirio ya gharama za ujenzi. Vilevile, imeendelea kutoa elimu ya ushirika na jamii kwa washiriki 15,987 (wanaume 11,088 na wanawake 4,899).

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kutoa mafunzo kwa wadau na kufanya maadhimisho mbalimbali ili kukuza maendeleo ya utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu kwa kutekeleza yafuatayo:

(i) Imetoa mafunzo kwa wahariri 197, wakaguzi 110 wa majarida na watafiti 250 kuhusu mbinu bora za uchapaji wa tafiti za kisayansi kwa lengo la kuimarisha ubora wa majarida ya kisayansi na ushirikiano na mashirika ya kimataifa yanayoorodhesha majarida;

(ii) imeendesha kongamano la siku tatu la wadau kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali katika Elimu, Mwongozo wa Kitaifa wa Elimu ya Kidijitali katika Shule na Vyuo vya ualimu, Mwongozo wa Kitaifa wa Elimu ya Kidijitali katika Shule na Vyuo vya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Mwongozo wa Kitaifa wa Elimu ya Kidijitali katika Vyuo Vikuu, Mwongozo wa Kitaifa wa Akili Unde katika Elimu ili kuimarisha uratibu na utekelezaji wa miongozo hiyo na kujenga uelewa wa pamoja ambapo takribani wadau 280 walishiriki;

(iii) imeendesha warsha kwa maafisa waandamizi 23 kutoka wizara mbalimbali za kisekta kwa lengo la kuimarisha uelewa kuhusu mawanda na utekelezaji wa masuala ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu; na

(iv) imefanya Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake na Wasichana katika Sayansi yaliyofanyika tarehe 11 Februari 2026 katika Kituo cha Mikutano cha Jakaya Kikwete, Jijini Dodoma yaliyohudhuriwa na washiriki takribani 2,800. Maadhimisho hayo yalijumuisha uzinduzi wa Kampeni ya Bara la Afrika (*Africa Educates Her*) inayolenga kuondoa vikwazo kwa watoto wa kike kupata fursa za elimu bora.

**109. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kudhibiti na kuimarisha matumizi salama ya mionzi ya nyuklia nchini kupitia Tume ya Nguvu za Atomu ili kutumia teknolojia husika katika masuala ya kijamii na kiuchumi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imepima sampuli 31,739 kati ya sampuli 25,000 za vyakula na vifaa vya mlolongo wa chakula zilizolengwa ikiwa ni sawa na asilimia 126.9 ya lengo ili kubaini uwepo wa uchafuzi wa mionzi. Kati ya sampuli hizo, sampuli 7,763 zilihusu bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, sampuli 20,951 zilihusu bidhaa za kusafirisha nje na sampuli 3,025 zilihusu mbolea, tumbaku na vifaa vya mlolongo wa chakula. Matokeo ya vipimo vya sampuli hizo yalionesha kutokuwepo kwa uchafuzi wa mionzi;

(ii) imefanya upimaji wa uthibitisho wa vifaa 40 ambapo kutoka Tume ya Nguvu ya Atomu ni 22, *Chrysos Corporation* 8, *PCS Energy Company* 2, MSA *Laboratories* 2, Tanzania *Steel Pipe* 1, Bugando *Medical Centre* 1, *Nuctech Company Limited* 1, Bulyanhulu *Medical Centre* 1, *GO Shuqing* 1 na *Bottles Company Limited* 1 na kubaini kuwa vifaa vyote vipo salama kwa matumizi;

(iii) imepima wafanyakazi 1,358 wanaofanya kazi katika mazingira yenye mionzi kutoka katika vituo 226 ikilinganishwa na lengo la kupima wafanyakazi 1,050. Aidha, wafanyakazi wotewaliofuatiliwa waligundulika kupata dozi za mionzi kati ya *milisiveti* 0.1 hadi 3.0 (mSv) kutokana na kazi wanazofanya. Kiasi hicho cha mionzi kipo ndani ya ukomo salama wa kisheria unaokubalika wa milisiveti 5 kwa kipindi cha miezi sita;

(iv) imepima jumla ya sampuli za mazingira 244 kati ya 400 zilizolengwa sawa na asilimia 61 kwa lengo la kubaini kiwango cha mionzi. Sampuli hizo zilitolewa na wanafunzi wa vyuo vikuu, makampuni binafsi na watafiti wa kisayansi. Upimaji huu umebaini viwango vya mionzi kuwa ndani ya viwango vinavyokubalika kimataifa kwa sampuli zote;

(v) imesajili vituo vipya vya mionzi 44 kati ya 50 viliyolengwa sawa na asilimia 88 na hivyo kufikia jumla ya vituo vya mionzi 1,734 vilivyosajiliwa. Aidha, imesajili vyanzo vipya vya mionzi 95 kati ya 100 vilivyolengwa sawa na asilimia 95. Usajili wa vituo hivi utawezesha serikali kufanya udhibiti wa athari za mionzi kwa wananchi;

(vi) imesajili wasimamizi 219 waliokidhi vigezo vya kusimamia matumizi ya mionzi ioni (*ioninzing radiation*) kwa wagonjwa na kusimika (installation), kufanya matengenezo na kuendesha vifaa vya mionzi; na imekagua vituo 415 kati ya vituo 425 vinavyotumia vyanzo vya mionzi ioni na isiyo ionishi ambapo vituo 371 vilikuwa kwenye kanzidata na vituo 44 vilikuwa vipya kwa lengo la kuimairisha udhibiti wa athari za mionzi kwa wananchi.

**110. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, imeendelea kuimarisha matumizi ya teknolojia ya nyuklia katika kuongeza tija katika sekta ya kilimo, tiba, afya na ufugaji kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) imeanzisha mradi wa utunzaji wa mazao mbalimbali kwa njia ya mionzi (*Enhancing industrialization through establishment of multipurpose irradiation facility*) unaotekelezwa na Tume ya Nguvu ya Atomu - Dar es Salaam;

(ii) imeanzisha mradi wa kuboresha mbegu ya mpunga kwa kutumia teknolojia ya nyuklia ili kukabiliana na ugonjwa wa mabaka ya mpunga (Rice Blast) na uvumilivu wa chumvi (Salinity Tolerant) unaotekelezwa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar (ZARI);

(iii) imeanzisha mradi wa kuongeza na kuboresha tiba ya saratani kwa kutumia mionzi (*Expanding and improving nuclear medicine and radiotherapy services*) unaotekelezwa katika taasisi ya Saratani ya *Ocean Road*, Hospitali ya Bugando, Hospitali ya KCMC, Hospitali ya Benjamin Mkapa na Hospitali ya Mnazi Mmoja iliyopo Zanzibar;

(iv) imeanzisha mradi wa kuimarisha huduma za uhimilishaji kwa njia ya bandia (*Artificial Insemination*) na matumizi ya mbinu ya upimaji wa kingamwili kwa kutumia ya mionzi ya nyuklia (*Radio immunoassay*) kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa unaotekelezwa katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo; na

(v) imeanzisha mradi wa kutekeleza mbinu ya kuachilia wadudu dume tasa (*Sterile Male Insect Technique*) ili kupunguza kuzaliana kwa wadudu waharibifu ikiwemo inzi wa matunda unaotekelezwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Zanzibar.

**111. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO, imeendelea kutekeleza yafuatayo:-

(i) imeanza utekelezaji wa Programu ya BRIDGE Tanzania 2025–2029, kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima inayolenga kuwawezesha vijana waliokosa fursa za elimu kupitia mfumo rasmi kupata stadi za msingi na ujuzi katika Wilaya za Masasi,

Geita na Kaskazini "A" Unguja. Kupitia programu hii, jumla ya vijana 200 wamenufaika;

(ii) imetoa mafunzo kwa Taasisi tano ambazo ni makumbusho ya Taifa ya Tanzania, makumbusho ya Zanzibar, Idara ya Misitu Zanzibar, Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro na Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA kuhusu uhifadhi wa maeneo ya Urithi wa Dunia, ili kuhakikisha yanaendelea kukidhi vigezo vya kimataifa (*Outstanding Universal Valu*e) na yanabakia katika hali ya uasili kama inavyoainishwa katika Mkataba wa UNESCO wa mwaka 1972);

(iii) imeendelea kushiriki kikamilifu katika kamati na majukwaa ya kimataifa ya UNESCO na kufanikisha uteuzi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mjumbe wa Baraza la Kimataifa la Uratibu la Programu ya Mtu na Mazingira (MAB-ICC) ya UNESCO kwa kipindi cha 2025-2029. Uteuzi huo umeongeza hadhi ya Tanzania kama kinara wa uhifadhi wa mazingira na maendeleo endelevu barani Afrika na kuimarisha utekelezaji wa hifadhi zake kwa kuzingatia viwango vya kimataifa;

(iv) imewezesha Tanzania kuchaguliwa kuwa mjumbe wa kamati ya urithi wa dunia kwa kipindi cha miaka minne (2025–2029). Uteuzi huo umeongeza ushawishi wa Tanzania katika maamuzi yanayohusu utekelezaji wa Mkataba wa Urithi wa Dunia wa 1972, pamoja na kuongeza fursa na uwezekano wa Tanzania kuongeza maeneo mapya katika orodha ya urithi wa dunia;

(v) imewasilisha Makao Makuu ya UNESCO nyaraka za maombi ya kuanzisha hifadhi mbili za miamba duniani (UNESCO *Global Geoparks*) katika maeneo ya Arusha (Arusha UNESCO Global Geopark) na Kilimanjaro (Kilimanjaro UNESCO *Global Geopark*) ambayo yamebainika kuwa na urithi wa kijiolojia wenye thamani ya kimataifa;

(vi) imeendelea kuratibu na kufanya tathmini ya utekelezaji wa mikataba na makubaliano ya kimataifa ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia, hususan katika sekta za Mawasiliano na Habari, Elimu, na Maendeleo Endelevu kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji wenye tija na unaoendana na vipaumbele vya kitaifa;

(vii) imefanya tathmini mbili za elimu ya habari na mawasiliano zilizowahusisha wadau 70, vyombo vitatu vya habari na chuo kimoja cha uandishi wa habari katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro na Manyara. Tathmini hizo zimeonesha kuongezeka kwa uelewa wa wadau kuhusu viwango na miongozo ya kimataifa, hususan katika uthibitishaji wa taarifa, mapambano dhidi ya habari bandia na matumizi sahihi ya majukwaa ya kidijitali;

(viii) imesimamia utoaji wa elimu na uhamasishaji dhidi ya ukatili wa kijinsia mtandaoni katika vyuo vya VETA Kihonda, Morogoro School of Journalism, St. Joseph College na Lakewood Vocational Training Centre mkoani Morogoro. Zaidi ya wanafunzi 1,200 wamefikiwa kupitia semina na kampeni za redio, hivyo kuongeza uelewa kuhusu madhara ya ukatili huo na namna ya kujikinga;

(ix) imetoa mafunzo kwa vijana 40 wa Mchinga, Mkoa wa Lindi katika ujasiriamali rafiki kwa mazingira na kuwapatia mashine za kisasa za kutengeneza tofali za interlock. Hatua hii imezalisha ajira, kuongeza kipato cha vijana na kuimarisha uchumi wa jamii huku ikihifadhi mazingira; na

(x) imeshiriki mkutano mkuu wa 43 wa UNESCO uliofanyika Samarkand, Uzbekistan na kuchangia kupata hadhi ya Kiswahili kutambuliwa kama lugha rasmi ya mikutano ya UNESCO, hatua muhimu inayoendeleza hadhi ya lugha ya taifa na utamaduni wa Tanzania kimataifa.

## D. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/27 (FUNGU 46)

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara imeainisha vipaumbele vya bajeti kwa kuzingatia mahitaji ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 (Toleo la 2023) inayolenga kuimarisha ubora wa elimu, kukuza ujuzi na kuongeza maarifa. Kutokana na mwelekeo huu, Wizara itaendelea kuweka jitihada kubwa katika maandalizi ya elimu ya lazima ya miaka 10, elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika elimu na kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuendana na Dira 2050.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itajielekeza kutekeleza vipaumbele vitano kama ifuatavyo:-

(i) Kuendelea na utekelezaji wa sera na mitaala, mapitio ya sheria, kuandaa miongozo na kutoa mafunzo nchini;

(ii) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali katika shule za sekondari na vyuo vya amali;

(iii) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu;

(iv) Kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa elimu ya juu; na

(v) Kuimarisha uwezo wa nchi katika utafiti, matumizi ya sayansi, teknolojia na ubunifu ili kuchochea ujenzi wa uchumi wa viwanda.

**a. Kuendelea na utekelezaji wa Sera na Mitaala, Mapitio ya Sheria, Kuandaa Miongozo na Kutoa Mafunzo Nchini**

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itafanya tathmini ya miaka miwili ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 iliyoanza utekelezaji wake Januari, 2024 na kuzinduliwa rasmi tarehe 1 Februari 2025. Lengo la kufanya tathmini ni kubaini mafanikio tuliyoyapata hadi sasa pamoja na kubaini vikwazo mbalimbali vinavyoathiri utekelezaji wake. Aidha, tathmini itawezesha kubuni mikakati itakayohakikisha kuwa sera na mitaala iliyoboreshwa inaleta matokeo yaliyokusudiwa.

**115.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali, itaendelea na maandalizi ya utekelezaji wa elimu ya lazima ya miaka 10 ili kupokea wanafunzi wa darasa la sita na la saba kwa wakati mmoja mwezi Januari 2028. Utekelezaji wa jambo hili muhimu unafanywa na OWM-TAMISEMI lakini Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itashirikiana na TAMISEMI hasa katika maandalizi kuandaa miongozo, kutafuta rasilimali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa na vinavyohitajika, kuhamasisha ushiriki wa wadau ikiwemo sekta binafsi pamoja na kutoa mafunzo kwa walimu.

**116.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali itaendelea kutoa elimu kwa umma na watendaji kuhusu Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 na mitaala iliyoboreshwa kwa ngazi ya elimu ya msingi, sekondari, ualimu, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na elimu ya juu. Utoaji wa elimu kwa umma kuhusu sera ya elimu na mafunzo utasaidia wazazi/jamii, watendaji na wanafunzi kushiriki kikamilifu na kuimarisha utekelezaji wake.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuweka misingi ya kisheria katika utekelezaji wa sera, Serikali itakamilisha mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353. Vilevile, itakamilisha mapitio ya sheria ya Taasisi ya Elimu Tanzania, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Bodi ya Huduma za Maktaba, Mamlaka ya Elimu Tanzania,

Baraza la Elimu la Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Baraza la Mitihani la Tanzania, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ili ziendane na Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 na Sheria za kikanda na kimataifa. Vile vile, mapitio ya Sheria ya Tume ya Nguvu ya Nyuklia ili kutenganisha majukumu ya urekebu na uhamasishaji wa matumizi salama ya nyuklia.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, Serikali itaendelea kuandaa na kuhuisha mikakati, viunzi, na miongozo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) itafanya mapitio ya Mkakati wa Kitaifa wa Kisomo na Elimu kwa Umma (*National Adult Literacy and Mass Education Rolling Strategy* - NALMERS) kwa lengo la kuimarisha ushiriki wa umma katika kupata maarifa, ujuzi na stadi za maisha kupitia elimu ya watu wazima.

(ii) itaandaa na kusambaza Kiunzi cha Taifa cha Elimu Jumuishi ili kuwezesha utekelezaji wa elimu jumuishi;

(iii) itaandaa Mwongozo wa Kitaifa wa Uendelezaji wa wakufunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na wafanyakazi wasiyo wakufunzi;

(iv) itahuisha Mwongozo wa Uanzishaji na Uendelezaji wa Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ili kuimarisha usimamizi na uratibu wa programu za elimu ya watu wazima;

(v) itahuisha Mwongozo wa Ushauri Nasaha na Ulinzi wa Mtoto kwa Wanafunzi wa Shule na Vyuo ili kuimarisha huduma ya ushauri na malezi kwa wanafunzi; na

(vi) itahuisha Mwongozo wa Kitaifa wa Huduma za Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Shule za Msingi ili kuimarisha utaratibu kwa wajasiriamali wanaouza vyakula

katika maeneo ya shule na kuanzisha bustani za mazao lishe shuleni.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ufanisi na mchango wa sayansi, teknolojia na ubunifu katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, serikali itakamilisha mapitio ya Sera ya Sayansi na Teknolojia (1996) kwa lengo la kuwa na sera inayoendana na mahitaji ya nchi katika sayansi, teknolojia, ubunifu na utafiti. Vilevile, itakamilisha mapitio ya muundo na majukumu ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia.

**b. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Mafunzo ya Amali katika shule za Sekondari na Vyuo vya Amali**

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kuongeza fursa katika elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itasajili vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi 263 kati ya hivyo vyuo vya elimu ya ufundi ni 45; vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 152 na shule za sekondari za amali 66 na hivyo kufikisha vyuo 577 vya elimu ya ufundi; vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 1,066; na shule za sekondari za amali 267; na

(ii) itadahili jumla ya wanafunzi 374,000 wa elimu ya ufundi na mafunzo na ufundi stadi ambapo wanafunzi wa vyuo vya elimu ya ufundi ni 240,000 na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi ni 134,000 sawa na ongezeko la asilimia 19 ikilinganishwa na udahili wa wanafunzi 315,307 waliodahiliwa mwaka 2025/26. Ongezeko la udahili wa wanafunzi wa vyuo vya ufundi kutaongeza idadi ya vijana wenye ujuzi na uwezo wa kujiajiri na kuajiriwa.

**121.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha kuwa Mafunzo yanayotolewa yanakidhi mahitaji ya soko la ajira kitaifa na kimataifa, Serikali itatoa ithibati kwa vyuo vya elimu ya ufundi

152 na hivyo kufikisha vyuo 395 vilivyopata ithibati. Aidha, itatoa ithibati kwa programu 211 za elimu ya mafunzo ya ufundi stadi (VET) na mitaala 300 iliyoandaliwa na vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi.

**122. *Mheshimiwa Spika,*** ulimwengu wa sasa unahitaji zaidi vitendo kuliko nadharia hivyo walimu wa amali ndio msingi wa kuandaa vijana wenye uwezo wa kufanya kazi kwa vitendo. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itadahili walimu tarajali 200 katika vilivyokuwa vyuo vya ualimu Mtwara Kawaida na Mtwara Ufundi ambavyo kwa sasa vimeunganishwa na kuwa ni Ndaki ya Mtwara ya Ualimu Ufundi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya na walimu tarajali 1,000 katika Chuo cha Walimu wa Ufundi Stadi Morogoro.

**123. *Mheshimiwa Spika,*** walimu hawa wa amali watafundisha katika shule zetu za sekondari za amali na vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi na hivyo kuwezesha kuwa na wahitimu wenye uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa na kutatua changamoto za kiufundi ambazo ndio msingi wa maendeleo ya kiuchumi wa taifa lolote linalotaka kujitegemea.

**124. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuongeza fursa na ubora wa mafunzo kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itawezesha ujenzi na upanuzi wa miundombinu katika shule 30 sekondari za amali pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia. Vilevile, itafanya ukarabati wa maabara tano, mabweni matano katika shule za sekondari na madarasa 30 katika shule za msingi na sekondari kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania;

(ii) itaendelea na ujenzi wa vyuo 64 vya mafunzo ya ufundi stadi vya wilaya pamoja na chuo kimoja cha mkoa wa Songwe;

(iii) itaendelea na ujenzi wa vyuo vya elimu ya ufundi wa kihandisi wa kati, yaani polytechnics. Tayari chuo kama hicho kimekamilika hapa Dodoma. Vyuo vingine kama hivyo vitajengwa katika mikoa ya Mwanza, Kigoma, Mtwara na Morogoro na chuo kimoja kama hicho kitajengwa Zanzibar.;

(iv) itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa miundombinu katika Chuo cha Elimu ya Ufundi Dodoma;

(v) itaendelea na ujenzi wa maktaba itakayotumiwa na wanafunzi 2,500 na ukumbi wa mihadhara utakaotumiwa na wanafunzi 1,000 kwa wakati mmoja katika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Kivukoni;

(vi) itaendelea na ujenzi wa jengo la hosteli ya wanafunzi yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 500 (wanawake 360 na wanaume 140) katika chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Pemba;

(vii) itaendelea na ujenzi wa mabweni mawili yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 1,536 (wanaume 768 na wanawake 768) na ujenzi wa madarasa mawili yenye uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 162 na ofisi 19 za walimu katika chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere Kampasi ya Karume;

(viii) itajenga maabara ya udongo itakayowezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo masuala ya udongo katika sekta ya ujenzi na utunzaji wa mazingira. Maabara hii, itaongeza uwezo wa kuhudumia wanafunzi kulingana na mahitaji katika Chuo cha Ufundi Arusha;

(ix) itaendelea na ujenzi wa ofisi ya makao makuu ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi na itaanza ujenzi wa ofisi ya Mamlaka ya Elimu ya Tanzania - Dodoma.

**125. *Mheshimiwa Spika***, Serikali, itaendelea na ukarabati wa miundombinu katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kama ifuatavyo:-

(i) itafanya ukarabati na upanuzi wa vyuo vinne vya mafunzo ya ufundi stadi na Chuo cha Ualimu wa Mafunzo ya Ufundi Stadi Morogoro;

(ii) itaendelea kukamilisha ukarabati wa miundombinu ya kilichokuwa Chuo cha Ualimu Mtwara Kawaida na Mtwara Ufundi ambavyo kwa sasa ni Ndaki ya Mtwara ya Ualimu Ufundi ya Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya;

(iii) itakarabati miundombinu katika vyuo vitano vya ufundi stadi na marekebisho kwa watu wenye ulemavu na kuimarisha matumizi ya nishati mbadala ya kupikia katika vyuo 54 vya maendeleo ya wananchi;

(iv) itakarabati karakana katika vyuo vya maendeleo ya wananchi 55, vyuo vya mafunzo vya Wizara ya Kilimo vinne, vyuo vya ufundi vya maendeleo ya jamii vinne, taasisi za mafunzo za Wizara ya Afya nne na Chuo cha Maendeleo ya Michezo cha Malya. Vilevile, itaendelea na ukarabati wa nyumba 10 za watumishi katika vyuo vya maendeleo ya wananchi; na

(v) itakarabati na kufanya upanuzi wa karakana za kujifunzia katika taasisi zinazotekeleza Mradi wa Kukuza Stadi za Kazi kwa ajili ya Shughuli za Kuzalisha na Kukuza Uchumi (Education and Skills for Productive Job – ESPJ II). Taasisi hizo ni: Chuo cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, VETA, Chuo cha Bahari Dar es Salaam (Dar es Salaam Marine Institute), Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (Livestock Institutions Training Agency), Chuo cha Taifa cha Utalii (National College of Tourism), Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (National Institute of Transport), Wakala ya Elimu na Mafunzo ya Uvuvi

(Fisheries Education Training Agency) na Vyuo vya Mafunzo vya Wizara ya Kilimo.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika, Serikali itakamilisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme kwa kutumia nguvu za maji kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa vitendo katika kituo cha mafunzo Kikuletwa. Aidha, itakamilisha ujenzi wa karakana ya uzalishaji (industrial workshop) kupitia mradi wa Khun International Projects katika Chuo cha ufundi Arusha.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** elimu ya amali ni njia ya kimkakati ya kugeuza nguvu kazi kuwa mtaji wa Kitaifa ili nchi iweze kuwa na nguvu kazi yenye ujuzi inahitaji programu zenye ubora, kwa msingi huo Serikali itatekeleza yafuatayo:-

(i) itaandaa vigezo vya umahiri katika programu 50 za mafunzo yanayotolewa na vyuo vya elimu ya ufundi ili kuandaa wataalamu na mitaala kulingana na mahitaji ya soko la ajira;

(ii) itaandaa programu 10 mpya za mafunzo ya ufundi stadi ili kuweza kutumika katika shughuli ya utoaji mafunzo katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi;

(iii) itaanzisha programu tatu za umahiri (centres of excellence) katika vituo vitatu katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi vitakavyobainishwa; na

(iv) itafanya ufuatiliaji na tathmini katika vyuo vya elimu ya ufundi 572, vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 887, vyuo vya maendeleo ya wananchi 55 na shule za sekondari 201 zinazotoa elimu ya amali kuhakiki ubora wa elimu.

**128.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha ulinganifu na mwendelezo wa elimu na ujuzi katika ngazi zote za elimu, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mfumo wa Taifa wa Sifa Linganifu (Tanzania National Qualification Framework).

**129. *Mheshimiwa Spika,*** mfumo huu unatoa mwongozo wa viwango vya elimu na ujuzi vinavyotambulika kitaifa na kimataifa, jambo linalorahisisha ulinganifu wa vyeti na kuunganisha mfumo wa elimu rasmi na isiyo rasmi, hivyo kutoa fursa kwa watu wengi zaidi kupata stahiki za kitaaluma. Aidha, inarahisisha uhamaji wa wanafunzi na wafanyakazi kati ya sekta mbalimbali za elimu, ikiwemo kutoka mafunzo ya ufundi kwenda elimu ya juu. Vilevile, mfumo unachochea ubora wa elimu kwa kuweka vigezo vya lazima vinavyopaswa kufuatwa na taasisi zote za mafunzo nchini.

**130. *Mheshimiwa Spika***, ili kuandaa programu katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi Stadi zinazoendana na mahitaji ya waajiri na sekta nyingine pamoja na miradi ya kimkakati nchini ikiwemo, nishati, TEHAMA na viwanda vya kuongeza thamani. Aidha, Serikali, itaendelea na utekelezaji wa mkakati wa ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na sekta binafsi na wadau mbalimbali wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika utoaji wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi. Vilevile, itaendelea kutekeleza hati za makubaliano 49 za ushirikiano na sekta, viwanda na mashirika katika utoaji wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi.

**131. *Mheshimiwa Spika,*** ushirikiano huu, utawezesha wanafunzi wengi zaidi wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kufanya mazoezi kwa vitendo viwandani, kuimarisha ushirikiano baina ya sekta ya ajira na taasisi za elimu na kuwezesha vyuo kuandaa wataalamu kulingana na mahitaji na hivyo wahitimu kujiajiri au kuajiriwa.

**132. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali, itaendelea kugharimia wanafunzi 2,095 kutoka taasisi tatu za elimu ya juu (Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya 702, Chuo cha Ufundi Arusha 520, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam 873) katika mafunzo kwa vitendo kwa ajili ya kuimarisha ujuzi. Vilevile, itagharamia huduma ya chakula kwa wanafunzi 18,903 (Chuo kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya wanafunzi 750,

Chuo cha Ufundi Arusha wanafunzi 750, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi 15,500, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam wanafunzi 1,490 na Vyuo vya Ufundi Stadi na Marekebisho kwa Watu wenye Ulemavu wanafunzi 413).

**133. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itawezesha upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika taasisi za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuimarisha mafunzo kwa vitendo kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itanunua vifaa na kufunga mitambo katika vituo vya umahiri ambavyo ni Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Ufundi Arusha na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji.

(ii) itanunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya VETA 145, vyuo vya maendeleo ya wananchi 55 na vyuo tisa vya ufundi stadi na marekebisho kwa watu wenye ulemavu;

(iii) itanunua vifaa vya maabara na karakana katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya; na

(iv) itaweka samani na vifaa saidizi katika Chuo cha Ufundi Arusha -Kituo cha Mafunzo Kikuletwa.

**134. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itatoa mafunzo kwa walimu, washiriki na wanafunzi wa shule za sekondari za amali na vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi kama ifuatavyo:-

(i) itatoa mafunzo kuhusu mbinu za kufundishia na kujifunzia kwa walimu wapya wapatao 1,427 (amali 207 na biashara 1,220) wa shule za sekondari za amali;

(ii) itatoa mafunzo ya muda mrefu ya ufundi stadi kwa washiriki 15,000 katika vyuo vya maendeleo ya wananchi 55 na washiriki 413 katika vyuo vya ufundi stadi na marekebisho kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha

washiriki kupata ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kushiriki katika shughuli za kiuchumi; na

(iii) itatoa mafunzo kwa wanagenzi 3,000 kupitia utaratibu wa urasimishaji ujuzi usiyo rasmi (Recognition to Prior Learning - RPL) kwa lengo la kuwatambua na kuwaongezea ujuzi pamoja na kuwapa tuzo (vyeti vya kuhitimu ujuzi).

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali itatoa mafunzo ya ulezi (mentorship) kwa wajasiriamali 4,000 kupitia programu ya Intergrated Training for Enterpreneurship Promotion - INTEP na watumishi kutoka katika kampuni 30 kupitia programu ya Skills Enhancement Program -SEP kwa lengo la kuwaongezea ujuzi.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, Serikali itaendelea kuwaendeleza watumishi wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi pamoja na vyuo vya maendeleo ya wananchi kwa kuwapa mafunzo mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) itatoa mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 270 (wanawake 87 na wanaume 183) na muda mfupi 608 (wanawake 269 na wanaume 339) wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi ili kuimarisha weledi katika utendaji;

(ii) itatoa mafunzo ya umahiri na mitaala inayozingatia teknolojia kwa watumishi wa vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 6,500 na watumishi wa vyuo vya maendeleo ya wananchi 1,300 na kuwezesha mafunzo ya vitendo viwandani kwa watumishi 155 (vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi 100 na vyuo vya maendeleo ya wananchi 55);

(iii) itatoa mafunzo ya umahiri na mitaala inayozingatia teknolojia kwa watumishi 2,300 kutoka Vyuo vya elimu na mafunzo ya ufundi (Wakala wa Taasisi za Mafunzo ya Mifugo, Wakala wa Taasisi za Elimu na Mafunzo ya Uvuvi, Taasisi za Mafunzo ya Afya, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Chuo cha Ufundi Arusha, Vyuo vya

Ufundi vya Maendeleo ya Jamii, Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Chuo cha Bahari Dar es Salaam, Taasisi za Mafunzo ya Kilimo na Chuo cha Taifa cha Utalii) na mafunzo ya vitendo kupitia viwanda kwa watumishi 100; na

(iv) itatoa mafunzo kwa njia ya masafa (e-learning), kufunga mbao janja (smartboards) katika kumbi 10 za midhadhara, na kununua kompyuta 80 kupitia Chuo cha Kumbukumbu cha Mwalimu Nyerere ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA.

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** mafunzo ya mara kwa mara yanawawezesha watumishi kuzingatia viwango vya ubora vinavyokubalika kitaifa na kimataifa, kuendana na kasi ya mabadiliko ya teknolojia na kuimarisha mbinu za ufundishaji na tathmini. Aidha, mafunzo yanachochea ubunifu na weledi kazini, hali inayosaidia kuzalisha wahitimu wenye ujuzi stahiki unaokidhi mahitaji ya soko la ajira na maendeleo ya viwanda.

**c. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu**

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kushirikiana na sekta binafsi katika kuongeza fursa za elimu ya awali, msingi, sekondari na ualimu kwa kusajili shule za msingi na sekondari 793 kwa mchanganuo ufuatao: awali pekee 25, awali na msingi 432 (Serikali 302 na zisizo za Serikali 155), sekondari 266 (Serikali 213 na zisizo za Serikali 53), elimu ya lazima 70 (Serikali 45 na zisizo za Serikali 25) na chuo cha ualimu kimoja.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kuongeza fursa katika vyuo vya ualimu na Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu kwa kudahili wanafunzi 11,244 katika vyuo vya ualimu vya serikali na visivyo vya serikali. Vilevile, itadahili wanafunzi 2,221 watakaosoma Stashahada ya Uongozi na Usimamizi wa Elimu, na Uthibiti Ubora wa Shule katika Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu kampasi ya Bagamoyo, Mwanza na Mbeya;

na itaanza kutoa shahada ya uongozi na usimamizi wa elimu kwa walimu 109 watakaojiunga na chuo.

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itaendelea kuongeza miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi na sekondari kwa kuwezesha ujenzi wa madarasa 1,360 kwa ajili ya utekelezaji wa elimu ya miaka 10 ya lazima, mabweni 17 kwa shule za sekondari 17, nyumba 33 za walimu. Aidha, itawezesha ujenzi wa vituo 50 vya walimu (Teachers Resource Centres) katika halmashauri za wilaya.

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya ualimu kwa kujenga nyumba tatu za wakufunzi katika Chuo cha Ualimu Sumbawanga, Mhonda na Dakawa. Aidha, itakarabati miundombinu katika vyuo nane vya ualimu ambavyo ni: Chuo cha Ualimu Ilonga, Nachingwea, Morogoro, Bustani, Korogwe, Tukuyu, Vikindu na Bunda. Vilevile, itakamilisha ujenzi wa miundombinu na kukarabati nyumba 10 za watumishi katika Chuo cha Ualimu Mpwapwa na Kleruu.

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali itajenga kituo maalum kwa ajili ya shughuli mbalimbali za utafiti wa kielimu na utunzaji wa nyaraka na taarifa mbalimbali za kielimu ikiwemo mitihani na upimaji wa kitaifa na kuweka vifaa katika Baraza la Taifa la Mitihani Tanzania.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuhakikisha elimu inayotolewa katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu inazingatia taratibu na miongozo, Serikali itatekeleza yafuatayo:-

(i) itafanya tathmini ya jumla katika asasi 7,412 ikiwemo shule za awali na msingi 5,371, sekondari 1,711, vyuo vya ualimu 76; vyuo vya maendeleo ya wananchi 54, na vituo 197 vya elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi;

(ii) itafanya tathmini ya ufuatiliaji katika asasi 1,444 (sawa na asilimia 20 ya shule zilizofanyiwa tathmini ya jumla mwaka 2025/26) ambapo shule za awali na msingi 1,014, shule za sekondari 404, vyuo vya ualimu 16; na vyuo vya maendeleo ya wananchi 10;

(iii) itafanya tathmini ya utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa wa mwaka 2023 katika shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu; na

(iv) itajenga ofisi za uthibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Mji Ifakara na Nkasi. Aidha, itakarabati ofisi za uthibiti ubora wa shule katika Halmashauri ya Mji Kibaha na Chalinze.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** Uthibiti ubora wa shule unahakikisha kuwa viwango vya kitaaluma na mitaala vinazingatiwa ipasavyo, kubaini changamoto za ufundishaji na miundombinu katika shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Aidha, Uthibiti Ubora wa Shule unahakikisha kuwa walimu wanatumia mbinu bora za ufundishaji.

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea na utekelezaji wa Mkakati wa kitaifa wa Kisayansi wa kuimarisha stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK) ambapo itatoa mafunzo kwa wakufunzi 1,326 kuhusu matumizi ya mbinu bunifu za ufundishaji ili kuhakikisha kila mtoto wa Kitanzania anamudu stadi za msingi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu afikapo darasa la tatu.

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali itaendelea kuimarisha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1) katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itaandaa, kuchapa na kusambaza nakala 8,000,000 za vitabu vya kiada na kiongozi cha mwalimu kwa mchanganuo ufuatao: nakala 3,102,263 kwa shule za msingi

darasa la VI, nakala 338,838 za vitabu vya sekondari kidato cha nne mkondo wa amali na nakala 4,558,899 za vitabu vya kidato cha tatu mkondo wa jumla kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mtaala ulioboreshwa; na

(ii) itaandaa, kuchapa na kusambaza nakala 51,000 za vitabu vya kiada katika maandishi yaliyokuzwa na breli kwa elimu ya msingi darasa la VI 23,000 na sekondari kidato cha nne 2,000 mkondo wa amali na kidato cha tatu 26,000 mkondo wa jumla kwa ajili ya wanafunzi wenye uoni hafifu na wasiyoona kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** kuimarisha uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi wa shule za msingi na sekondari ni msingi muhimu katika kuinua ubora wa elimu kwa kuwa kila mwanafunzi anapata fursa sawa ya kujifunza, kuongeza ari ya kujisomea kwa kujitegemea, na kuwapa walimu nyenzo rafiki za kufundishia ili kufikia malengo ya mtaala.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaboresha maudhui ya vitabu vya elimu ya msingi na sekondari kuwa maudhui shirikishi ya kielektroniki yanayojumuisha video, sauti, animation na majaribio pepe (*virtual simulations*). Maudhui husika yatasaidia tathmini za papo kwa papo, ujifunzaji jumuishi kwa masomo ya sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati kidato cha tatu na matumizi ya rasilimali za multimedia.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali itaendelea kuhamasisha usomaji kwa jamii na kuboresha huduma za maktaba nchini kwa kutoa huduma za maktaba kwa watumiaji wasiyopungua 800,000 na kununua nakala za vitabu 100,000. Aidha, itaendesha programu nne za uhamasishaji kwa wasomaji wa maktaba kupitia maktaba za mikoa 22, wilaya 19 na kata mbili.

**150. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea na utekelezaji wa majukumu ya Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania (*Tanzania Teachers Professiyonal Board*) ili kusimamia, kudhibiti na kulinda taaluma ya ualimu nchini ambapo itaandaa mwongozo wa viwango katika ufundishaji ili kukuza mafunzo endelevu katika taaluma ya ualimu. Vilevile, itaandaa Mwongozo wa Maadili na Mwenendo wa Taaluma ya Ualimu.

**151. *Mheshimiwa Spika***, vilevile, Serikali itaanza kutekeleza mpango wa mafunzo kwa vitendo wa mwaka mmoja (internship) kwa wahitimu wa mafunzo ya ualimu. Mpango huo, ni muhimu kwa walimu tarajali kwa kuwa utawawezesha kuoanisha nadharia na uhalisia wa darasani. Mafunzo yatawajengea ujuzi wa kufundisha, kumudu darasa, kuimarisha mbinu za kufundisha na uelewa wa maadili ya kazi kupitia usimamizi wa walimu wazoefu.

**152. *Mheshimiwa Spika***, Serikali, itaendelea kuwaendeleza kitaalamu na kitaaluma walimu wa shule za msingi na sekondari, wakufunzi wa vyuo vya ualimu, wathibiti ubora wa shule na wasimamizi wa elimu ili kuimairisha utendaji katika maeneo mbalimbali kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itaendelea kutoa ufadhili wa masomo kwa walimu 1,223 watakaosoma Stashahada ya Ualimu wa Elimu Maalum;

(ii) itatoa mafunzo kwa walimu 3,000 wa ushauri na unasihi wa shule za msingi na sekondari kuhusu malezi, unasihi na ulinzi wa mtoto; na

(iii) itatoa mafunzo kazini kwa watendaji 5,500 ikiwemo walimu shule za awali, msingi na sekondari, wathibiti ubora, maafisa elimu kata na wakufunzi wa vyuo vya ualimu. Vilevile, itatoa mafunzo kwa walimu na wanafunzi kuhusu majukwaa ya kielimu ikiwemo maktaba mtandao na jukwaa la umma la kujifunza mtandaoni (Online Public School).

**153. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kuimarisha utoaji wa elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum ikiwa ni pamoja na kuimarisha huduma ya ubainishaji na upimaji na utoaji wa elimu nyumbani kwa wanafunzi kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 50 kuhusu haki na wajibu wa watu wenye ulemavu;

(ii) itatoa mafunzo kwa wakufunzi 100 kutoka VETA za mikoa na vyuo vya maendeleo ya wananchi kuhusu namna ya kuwahudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum;

(iii) itatoa mafunzo kwa maafisa elimu maalum 52, maafisa uthibiti ubora wa shule 52 na wakuu wa shule 52 kuhusu ubainishaji na upimaji wa wanafunzi;

(iv) itawezesha upatikanaji wa huduma saidizi kwa watumishi 40 wenye mahitaji maalum katika ngazi zote za elimu; na

(v) itawezesha ushiriki wa watumishi 40 katika maonesho, sherehe na maadhimisho mbalimbali ya watu mahitaji maalum.

**154. *Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha ufundisha mahiri Serikali, itaratibu shindano la stadi za ufundishaji, ujifunzaji na ufaraguzi wa zana kwa walimu wa shule za awali, msingi na sekondari. Uhamasishaji wa ufundishaji ni msingi muhimu wa kuongeza ufanisi wa ujifunzaji, kwani unawawezesha walimu kutumia mbinu mbalimbali na shirikishi zinazozingatia teknolojia ili kuwajengea wanafunzi ujuzi wa kutatua changamoto za maisha halisi. Vilevile, mashindano haya ni njia mojawapo ya kutoa motisha kwa walimu katika kutumia mbinu sahihi za ufundishaji na ujifunzaji.

**155. *Mheshimiwa Spika,*** uandishi wa insha kwa wanafunzi ni nyenzo muhimu katika kukuza uwezo wao wa kufikiri kwa

kina, kujenga hoja zenye mantiki, na kuboresha stadi za mawasiliano kwa lugha sanifu. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali itendelea kutaratibu shindano la uandishi wa insha kwa Nchi za Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kwa wanafunzi 2,000 wa shule za sekondari. Mashindano haya huwapa wanafunzi jukwaa la kutoa maoni yao kuhusu masuala mbalimbali ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa.

**156.** ***Mheshimiwa Spika***, kazi za fasihi hutumika kama kielelezo cha maisha, maadili, na historia ya jamii. Kwa mantiki hiyo, Serikali itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi bunifu kwa lengo la kuhamasisha na kukuza tasnia ya uandishi wa kazi za fasihi ya kiswahili ikiwemo riwaya, hadithi fupi na ushairi. Utoaji wa tuzo hizi huhamasisha na kuwajengea uwezo waandishi chipukizi na kuchagiza ukuaji wa sekta ya uandishi nchini. Kwa kushirikiana na Idara za Fasihi katika vyuo vikuu, Serikali itaandaa warsha na makongamano juu ya uandishi bunifu ili kukuza vipaji vya waandishi chipukizi na hata kufanya Tuzo hiyo kuwa na mtazamo wa kimataifa.

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** Elimu nje ya mfumo rasmi ina inatoa fursa kwa wale waliokosa nafasi katika mfumo rasmi kutokana na sababu mbalimbali, Njia hii ya elimu inatoa fursa ya kupata maarifa na stadi za maisha kulingana na mahitaji. Kwa umuhimu huo, Serikali itaendelea kuimarisha elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itaongeza udahili wa wanafunzi wa elimu ya sekondari kwa njia mbadala kutoka 14,765 mwaka 2025/26 hadi 16,000 mwaka 2026/27);

(ii) itaongeza idadi ya vijana watakaopata stadi za maisha, ujuzi na elimu ya msingi kutoka vijana 16,732 mwaka 2026 hadi vijana 22,500 mwaka 2027 kupitia Programu ya Elimu

Changamani kwa Vijana walio Nje ya Mfumo Rasmi (*Integrated Program for Out of School Adolescents* – IPOSA);

(iii) itakamilisha ujenzi wa jengo la utawala la Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima kituo cha Morogoro na kuanza ujenzi wa jengo la utawala katika kituo cha Mwanza; na

(iv) itaendelea kufanya maadhimisho ya siku ya kisomo kimataifa na juma la elimu bila ukomo.

**158.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kuendesha programu mbalimbali za kuwajengea umahiri walimu na viongozi wa elimu katika nyanja za usimamizi na uongozi wa walimu kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itatoa mafunzo ya muda mfupi kwa viongozi wa elimu kuanzia ngazi ya shule, kata, halmashauri na wizara wapatao 6,702 kuhusu uongozi na usimamizi wa elimu;

(ii) itaendelea na awamu ya pili katika ujenzi wa jengo la kumbi changamani lenye uwezo wa kuhudumia watu 650 kwa pamoja katika kampasi ya Bagamoyo; na

(iii) itaandaa mfumo wa kujifunzia mtandaoni (*e-learning systems*) pamoja na ununuzi wa seva, kompyuta 52 na printa 5 ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika mafunzo na huduma nyingine za Wakala wa Maendeleo ya Uongzi wa Elimu.

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kufanya upimaji na tathmini ya kubaini umahiri wa mwanafunzi katika kumudu masomo ya elimu ya msingi, sekondari na ualimu, kupitia Baraza la Mitihani Tanzania kama ifuatavyo:-

(i) itasimamia Uendeshaji wa Upimaji wa Darasa la Pili kwa wanafunzi 2,009,331 wa shule za msingi Oktoba, 2027;

(ii) itaendesha upimaji wa kitaifa wa Darasa la Nne

kwa wanafunzi 2,110,451 ambapo upimaji huo utafanyika Novemba, 2026. Lengo la upimaji ni kubaini umahiri wa mwanafunzi katika kumudu masomo yanayofundishwa darasa la Tatu na la Nne;

(iii) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 1,384,342 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo Septemba, 2026;

(iv) itaendesha Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili kwa wanafunzi 838,199 ambapo upimaji huo utafanyika mwezi Novemba, 2026;

(v) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Kidato cha Nne kwa wanafunzi 703,800 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Novemba, 2026; na

(vi) itaendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Kidato cha Sita kwa watahiniwa 139,800 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo mwezi Mei, 2027 na itaendesha Mtihani wa Ualimu Mei, 2027 kwa walimu tarajali 12,400.

**160.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kuimarisha mafunzo endelevu kazini kwa kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 61 (wanaume 34 na wanawake 27) na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 568 (wanaume 269 na wanawake 299) kutoka Wakala wa Uongozi na Maendeleo, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Tanzania, Taasisi ya Elimu Tanzania na Baraza la Mitihani Tanzania kwa lengo kuongeza uwezo wa taasisi hizo kutoa huduma zenye ubora na stahiki kwa jamii.

### d. Kuongeza Fursa na Kuimarisha Ubora wa Elimu ya Juu

**161.** ***Mheshimiwa Spika***, Serikali, itaendelea kuongeza fursa kwa wanafunzi wa elimu ya juu kama ifuatavyo:-

(i) itaratibu udahili wa wanafunzi 180,000

wanaotarajiwa kuomba kujiunga na programu mbalimbali za shahada ya kwanza katika vyuo vya elimu ya juu;

(ii) ita ongeza idadi ya wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 252,773 mwaka 2025/26 hadi 292,981 mwaka 2026/27 (mwaka wa kwanza 111,692 na wanaoendelea 181,289); na

(iii) itaendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Stashahada 24,978 (mwaka wa kwanza 14,000 na wanaoendelea 10,978) katika fani za sayansi na ufundi na kubuni vyanzo vingine vya fedha kwa ajili ya kuongeza idadi ya wanufaika wa mikopo na hivyo kuongeza fursa za elimu ya juu.

**162. *Mheshimiwa Spika*,** Serikali, itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi waliosoma masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itatoa ufadhili kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu katika masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) kupitia SAMIA Skolashipu kutoka wanafunzi 2,630 mwaka 2025/26 hadi wanafunzi 2,738 mwaka 2026/27 (wanafunzi 1,000 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 1,738 wanaoendelea);

(ii) itatoa ufadhili kupitia programu ya Samia Extended Scholarship DS/AI$^{+}$kwa wanafunzi wenye ufaulu wa juu wa masomo ya Sayansi katika matokeo ya Kidato cha Sita kutoka wanafunzi 50 mwaka 2025/26 hadi wanafunzi 100 (mwaka wa kwanza 50 na wanaoendelea 50) ili kujiunga na shahada ya kwanza katika vyuo bora vilivyo nje ya nchi kwa ajili ya kusoma fani za sayansi data, sayansi shirikishi, na akili-unde;

(iii) itaendelea kuwezesha ufadhili wa masomo katika eneo la sayansi na teknolojia ya nyuklia kwa wanafunzi 12 wa shahada ya umahiri;

(iv) itaendelea kuwezesha wanafunzi wa kike 200 kushiriki mafunzo ya awali ya masomo ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM) katika Chuo Kikuu Huria cha Tanzania; na

(v) itatoa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi wa kike 11 wenye ufaulu wa juu katika masomo ya Sayansi waliohitimu mitihani ya kitaifa ya kidato cha sita na shahada za awali kupitia Chuo Kikuu Dar es Salaam.

**163. *Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha ushirikiano wa kitaifa, kikanda na kimataifa katika kuendeleza elimu ya juu Serikali, itaendelea kutoa ufadhili kwa wanafunzi 15 raia kutoka China wanaosoma Lugha ya Kiswahili katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa lengo la kukuza na kubiasharisha Lugha ya Kiswahili, wanafunzi wawili raia wa Oman na wanafunzi watano raia wa Hangaria kusoma katika vyuo vikuu nchini kulingana na mikataba na utaratibu.

**164. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kuimarisha ukusanyaji wa mikopo iliyoiva kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo ukaguzi wa waajiri, ulipaji wa adhabu, kuunganisha mifumo ya Bodi na ile ya wadau muhimu pamoja na kuwezesha utambuzi wa wanufaika wapya wa mikopo 42,000 na ukusanyaji wa **Shilingi bilioni 236** za mikopo iliyoiva.

**165. *Mheshimiwa Spika***, Serikali, itaendelea kuboresha Mazingira ya kufundishia na Kujifunzia katika vyuo vikuu kwa kujenga na kukarabati miundombinu mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) itakamilisha ujenzi na ukarabati wa vyumba vya semina, kumbi za mihadhara, madarasa, ofisi, maabara, maktaba pamoja na miundombinu mingine katika taasisi 21 za elimu ya juu kupitia mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi;

(ii) itaendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika chuo Kikuu Dodoma ikiwemo ujenzi wa maabara ya anatomia, uunganishaji wa mtandao wa huduma ya maji katika visima vitano na kukamilisha ujenzi wa bweni moja lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 240 wanaotumia hospitali ya rufaa ya mkoa wa Iringa kufanya mafunzo kwa vitendo katika fani za udaktari wa binadamu;

(iii) itaanza ujenzi wa maktaba ya kisasa awamu ya nne yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,500 pamoja na hosteli mbili zenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 300 kila moja katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa;

(iv) itakamilisha ujenzi wa jengo la utawala Kampasi ya Oswald Mang'ombe katika Chuo Kikuu cha Kilimo na Teknolojia cha Mwalimu J.K.Nyerere;

(v) itajenga maabara na madarasa ya shule ya sekondari ya mafunzo kwa vitendo katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam;

(vi) itaendelea na ujenzi wa kituo cha uratibu wa mafunzo Pemba - Zanzibar katika Chuo Kikuu Huria Tanzania Kampasi ya Pemba, ujenzi wa kituo cha Tanga na Tabora pamoja na kukarabati majengo matatu ya kituo cha mkoa wa Shinyanga, Singida, Dodoma na Mbeya ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa makujumu ya Chuo Kikuu Huria Tanzania;

(vii) itaendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa hospitali ya kisasa na Kituo cha Umahiri cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya damu, madarasa, Ofisi, mabweni, maabara, jengo la TEHAMA na maktaba katika Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili kampasi ya Mloganzila, Kigoma na Muhimbili ili kuimarisha utoaji wa mafunzo ya fani za kipaumbele. Vilevile, imeendelea na ujenzi wa kliniki ya uporoto;

(viii) itaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa jengo la maktaba lenye uwezo wa kuhudumia wasomaji 2,500 katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, Kampasi ya Moshi; na

(ix) itaanza ujenzi wa jengo la taaluma lenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 2,000 kwa wakati mmoja na ujenzi wa karakana moja ili kuimarisha utoaji wa mafunzo kwa vitendo katika programu za sayansi, teknolojia na uhandisi katika Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kuboresha miundombinu katika Taasisi za Sayansi na Teknolojia kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kufundishia (Teaching Factory) katika Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela;

(ii) itaanza ujenzi na ukarabati katika vyuo vinne vya Umahiri na Ubunifu na Uhaulishaji wa Teknolojia ambavyo ni Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume, Chuo cha Ufundi Arusha, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya pamoja na uwekaji wa vifaa;

(iii) itakamilisha ujenzi wa hosteli yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500 katika taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela;

(iv) itakarabati karakana na maabara na kuweka vifaa vya maabara katika Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam;

(v) itakarabati karakana katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya Ndaki ya Mtwara ya Ualimu Ufundi; na

(vi) itakamilisha ujenzi wa maabara, ofisi na vifaa vya mradi wa irradiator katika ofisi za Dar es Salaam na kuweka

vifaa vya maabara katika kanda nne za Tume ya Nguvu za Atomu.

**167.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea kuimarisha ithibati na uthibiti ubora katika taasisi za elimu ya juu kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itafanya tathmini na kutoa ithibati ya programu 300 za masomo mbalimbali katika vyuo vikuu. Vilevile, itakagua na kufanya tathmini na ufuatiliaji kwa vyuo vikuu 25 kwa lengo la kuendeleza ubora wa elimu kwa kuzingatia utoshelevu wa miundombinu, mafunzo, wanataaluma, utawala na uendeshaji, na kutoa ushauri stahiki;

(ii) itafanya ukaguzi wa utekelezaji wa mitaala 60 na kuhuisha ithibati ya vyuo vikuu vinne;

(iii) itafanya ukaguzi wa asasi 10 zinazoratibu udahili wa wanafunzi wanaokwenda kusoma nje ya nchi kwa lengo la kuzitambua na kuzisajili. Vilevile, itafanya tathmini ya usajili wa vyuo vikuu vya nje ya nchi kwa maombi ya wanafunzi 2,000 wanaotarajiwa kuomba udahili katika vyuo hivyo kwa lengo la kutoa taarifa za uhakika kuhusu ithibati ya vyuo husika; na

(iv) itafanya maboresho ya Mfumo wa Ukusanyaji na Uchakataji wa Taarifa zinazohusu Vyuo Vikuu (University Information Management System-UIMS) na Mfumo wa Menejimenti ya Programu za Masomo (Programmes Management System-PMS) kwa lengo la kuimarisha ufanisi wa huduma zitolewazo katika elimu ya chuo kikuu.

**168.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali itaendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vikuu kwa kuendelea kununua vifaa kama ifuatavyo:-

(i) itaendelea kununua vifaa saidizi kwa wanafunzi 855 wenye mahitaji maalum katika vyuo vikuu vya umma ili

kuboresha mazingira ya ufundishaji na ujifunzaji na kuwawezesha kujifunza kwa ufanisi;

(ii) itanunua vifaa vya maabara, kompyuta 20, na samani ikiwemo viti 122 na meza 122 kwa ajili ya Chuo Kikuu cha Dodoma ili kuimarisha matumizi ya mifumo ya kidijitali katika ufundishaji na usimamizi wa shughuli za kitaaluma;

(iii) itanunua vifaa vya TEHAMA, vitabu na majarida, na vifaa vya maabara ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika Chuo Kishiriki cha Elimu Mkwawa;

(iv) itanunua vifaa vya kufundishia na kujifunzia, na samani ikiwemo kompyuta, printer, viti, na meza katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kampasi kuu kuboresha mazingira ya kufundishia, kujifunzia na endeshaji.

**e. Kuimarisha Uwezo wa Nchi katika Utafiti, Matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ili Kuchochea Ujenzi wa Uchumi wa Viwanda**

**169.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaongeza ufadhili wa miradi ya utafiti na ubunifu kutoka 80 hadi 109 unaozingatia maeneo ya kipaumbele ili kutatua changamoto za mabadiliko ya tabianchi, uchumi wa bluu, uvuvi, maji, kilimo, afya, na viwanda.

**170.** ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali kupitia taasisi za elimu za juu na elimu ya ufundi itafanya miradi ya utafiti 1,390 katika maeneo mbalimbali ikiwemo afya, elimu, biashara, kilimo, uongozi, ushirika, teknolojia, uvuvi, ardhi, mazingira na usanifu majengo.

**171.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usambazaji wa maarifa, uhamasishaji wa mijadala ya kitaaluma na kuhakikisha matokeo ya kazi za utafiti yanatumika katika kutatua changamoto za kijamii na kiuchumi, Serikali itachapisha machapisho 2,497 katika majarida ya Kitaifa na Kimataifa.

**172. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, kupitia taasisi za elimu ya juu na elimu ya ufundi zitatoa huduma za ushauri 313 katika maeneo mbalimbali ikiwemo ujenzi, utafiti, ushirika, kilimo, utunzaji wa chakula, uvuvi, uongozi, mazingira, udongo, kokoto na lami, kupima ubora wa maji, usanifu na usimamizi majengo.

**173. *Mheshimiwa Spika,*** itaendelea kuhamasisha Taasisi za Elimu ya Juu na Taasisi za Utafiti na Maendeleo kufanya tafiti za kimkakati katika sekta zenye mchango mkubwa kwenye kukuza uchumi na kuboresha maisha ya jamii kwa kutoa tuzo kwa watafiti watakaochapisha matokeo ya utafiti katika majarida yenye hadhi ya juu kimataifa.

**174. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itajengea uwezo maabara za taasisi tano (5) za utafiti na maendeleo ili zitumike kama maabara za rufaa za utafiti na ubunifu wa viwanda. Vilevile, itaimarisha mahusiano kati ya taasisi za utafiti na maendeleo, taasisi za elimu ya juu na viwanda ili kuchochea mchango wa utafiti na ubunifu katika utekelezaji wa Dira ya Taifa 2050.

**175. *Mheshimiwa Spika,*** itaongeza uwekezaji katika miundombinu ya kitaifa ya utafiti na ubunifu ili kuchochea uvumbuzi na ubiasharishaji wa teknolojia zinazoibuliwa nchini.

**176. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, itamarisha ushiriki wa sekta ya umma na binafsi katika kuongeza mchango wa utafiti na ubunifu kwenye maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza yafuatayo:-

(i) itaimarisha madawati ya Sayansi na Teknolojia katika halmashauri 184 ili kubaini na kuendeleza bunifu kutoka kwa wazawa ziweze kuchangia katika maendeleo ya uchumi.

(ii) itaanzisha dawati la kusajili mikataba nane ya Uhawilishaji wa Teknolojia na kuwezesha matumizi ya

teknolojia tatu kutoka kwenye miradi ya kimkakati ya kitaifa kwenda sekta ya uzalishaji;

(iii) itaanzisha jukwaa la mtandaoni kwa ajili ya usajili wa Watanzania waishio nje ya nchi (Diaspora) wenye utaalamu katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

(iv) itaanzisha kituo katika chuo kimojawapo cha VETA kwa ajili ya kuatamia, kuendeleza ujuzi na ubunifu kwa wanafunzi na wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi (*Vocational Incubation Centre*) na itaanzisha Jukwaa la Taifa la Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;

(v) itaimarisha uwezo wa waratibu wa madawati na majukwaa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kutoka halmashauri 76 hadi 184; na

(vi) itaratibu maadhimisho ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu kupitia wiki ya kitaifa ya elimu, ujuzi na ubunifu na siku ya kimataifa ya wanawake na wasichana katika sayansi.

**177. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itakamilisha maandalizi ya Taifa ya Mahitaji ya Teknolojia katika sekta mbalimbali (National Technology Roadmap-2050).

**178. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaendelea Kuhamasisha wabunifu na kuongeza idadi ya makampuni/wanufaika wanaoweza kupokea mikopo kupitia mfuko wa kibiasharisha ubunifu wa Samia (Samia *Innovation Commercialization Fund*). Aidha, itawezesha vyuo vitano vya Maendeleo ya Wananchi (FDC) kwa vituo vya ubunifu.

**179. *Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaimarisha ubunifu na uuzaji wa matokeo ya tafiti kwa kusajili hati miliki tano na kugeuza bunifu mbili kuwa biashara ili kuimarisha uhamishaji wa teknolojia kwa viwanda na jamii kwa lengo la kuongeza bidhaa

na teknolojia bunifu zinazotatua changamoto za jamii, kuchochea ukuaji wa uchumi, na kuongeza matumizi ya tafiti katika Maendeleo.

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali, itaimarisha uthibiti na utafiti wa kimkakati unaolenga kuongeza wigo wa matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza yafuatayo:-

**181.**

(i) itaendelea kudhibiti matumizi ya mionzi nchini kwa kukagua vituo 900 vyenye vyanzo vya mionzi ili kuwaweka salama wagonjwa, wafanyakazi, jamii na mazingira;

(ii) itapima na kudhibiti viwango vya mionzi kwa wafanyakazi 2,110 wanaofanya kazi kwenye mazingira ya vyanzo vya mionzi ili kuwalinda na madhara yatokanayo na vyanzo vya mionzi sehemu za kazi;

(iii) itasimamia kituo maalumu kilichopo Dar es Salaam cha kupima hewa katika anga kwa lengo la kudhibiti uchafuzi unaotokana na majaribio ya silaha za nyuklia duniani ili kuhakikisha hali ya usalama wa hewa katika anga dhidi ya uchafuzi wa mionzi;

(iv) itaendelea kukusanya na kusafirisha mabaki sita ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika na kuyahifadhi katika kituo maalumu cha mabaki ya mionzi (*Central Radioactive Waste Management Facility*) ili kuiweka nchi salama dhidi ya athari za mionzi kwa kukusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika na kuyahifadhi katika kituo maalumu cha kuhifadhi mabaki ya mionzi (*Central Radioactive Waste Management Facility*);

(v) itaendelea na usimamizi na uratibu wa karibu wa mradi maalumu (*Rays of Hope - Bankable Project*) unaolenga kupanua huduma za uchunguzi na matibabu ya saratani nchini kutoka vituo viwili Hospitali ya Ocean Road-Dar es

Salaam na Hospitali ya Bugando-Mwanza hadi kufikia vituo sita nchini;

(vi) itaendelea na ujenzi wa maabara moja na ofisi moja katika kanda ya mashariki (mkoa wa Dar es Salaam) kwa lengo la kusogeza huduma za udhibiti na uendelezaji wa teknolojia ya nyuklia kwa wananchi;

(vii) itakamilisha taratibu za uanzishwaji wa kituo cha mafunzo ya muda mfupi na umahiri ya ulinzi na usalama wa kinyuklia ili kuongeza wataalam wa kinga na usalama wa mionzi pamoja na wataalam wa kutengeneza vifaa vinavyotumia teknolojia ya mionzi hospitalini (x-ray machine), viwandani (nuclear gauges), kwenye barabara (troxler) na maeneo mbalimbali katika sekta ya ujenzi, sekta ya migodi na madini; na

(viii) itaendelea na upimaji wa sampuli 50,000 za chakula na mbolea zinazoingia na kutoka nchini, na sampuli za maji kwenye visima, wasambazaji na wamiliki wa viwanda ili kubaini endapo kuna uchafuzi wa mionzi kwa ajili ya kuwalinda wananchi dhidi ya madhara yatokanayo na mionzi.

## E. MPANGO WA TUME YA TAIFA YA UNESCO (FUNGU 18)

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2026/27 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO imepanga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

**a. Kukamilisha taratibu za kuhakikisha maeneo tarajiwa na yale yaliyo katika orodha ya awali ya UNESCO yaingie katika orodha ya UNESCO.**

(i) kuratibu maandalizi na uwasilishaji wa nyaraka muhimu kama vile nomination dossiers, ramani za mipaka na mipango ya usimamizi wa maeneo husika;

(ii) kuendelea na uhakiki na uhuishaji wa orodha ya awali (Tentative List) ya maeneo yanayopendekezwa kuingizwa katika orodha ya UNESCO, pamoja na kuhakikisha maeneo mapya yenye vigezo vinavyokidhi hadhi ya urithi wa dunia yanatambuliwa, kuandaliwa na kuwasilishwa kwa kuzingatia miongozo na taratibu za kimataifa;

(iii) kuimarisha uratibu kati ya taasisi za kitaifa, wadau na jamii zinazozunguka maeneo husika ili kuhakikisha usimamizi endelevu, ulinzi na uhifadhi wa maeneo hayo unazingatia viwango vinavyotakiwa na UNESCO; na

(iv) kuandaa na kutekeleza programu za mafunzo na uhamasishaji kwa wadau mbalimbali kuhusu taratibu, vigezo na umuhimu wa kuingiza maeneo katika orodha ya UNESCO ili kuongeza uelewa na ushiriki katika mchakato huo.

**b. Kuimarisha utekelezaji wa Programu za UNESCO katika sekta za Elimu, Sayansi, Utamaduni na Mawasiliano, kwa kuzingatia ajenda ya maendeleo endelevu.**

(i) kuimarisha ushirikiano kati ya taasisi za kitaifa, wadau wa maendeleo na mashirika ya kimataifa ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa programu za UNESCO nchini; na

(ii) kuandaa na kutekeleza programu za uhamasishaji na mafunzo kwa wadau mbalimbali kuhusu dhana ya maendeleo endelevu na mchango wa programu za UNESCO katika kufikia malengo hayo.

**c. Kukuza ushiriki wa Tanzania katika majukwaa ya kimataifa ya UNESCO, ili kulinda na kutetea maslahi ya Taifa;**

(i) kuratibu ushiriki wa Tanzania katika majukwaa ya kimataifa ya UNESCO, ikijumuisha mikutano, makongamano na vikao vya kisheria na kisera ili kuhakikisha maslahi ya Taifa yanawakilishwa na kutetewa ipasavyo;

(ii) kuratibu na kuandaa misimamo ya kitaifa kuhusu masuala ya elimu, sayansi, utamaduni na mawasiliano kabla ya kushiriki katika majukwaa ya UNESCO ili kuongeza ushawishi na mchango wa Tanzania katika maamuzi ya kimataifa;

(iii) kukuza ushirikiano na nchi wanachama na wadau wengine wa UNESCO ili kujenga mitandao ya kimkakati itakayosaidia kulinda na kuendeleza maslahi ya Tanzania katika ngazi ya kimataifa; na

(iv) kufuatilia utekelezaji wa maazimio na makubaliano yanayofikiwa katika majukwaa ya UNESCO na kuhakikisha yanatekelezwa kwa kuzingatia vipaumbele vya maendeleo ya Tanzania.

## F. SHUKRANI

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kutumia fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir (Mb),** Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa uchapakazi na umakini wake na ushirikiano mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu na kufikia malengo ya Wizara. Aidha, napenda kumshukuru tena Katibu Mkuu Profesa Carolyne Ignatius Nombo, Naibu Makatibu Wakuu, Profesa Daniel Elius Mushi na Dkt. Hussein Mohamed Omar kwa kunipa ushirikiano. Vilevile, ninaomba kutoa shukrani zangu kwa Kamishna wa Elimu, wakurugenzi, wakuu wa taasisi na watumishi wote kwa kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa juhudi na ufanisi.

**184.** ***Mheshimiwa Spika,*** naishukuru kwa dhati familia yangu kwa kuendelea kunipa ushirikiano na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa utulivu.

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** pia ninapenda kuwashukuru viongozi wa vyama vya wafanyakazi, walimu, wanafunzi, na wadau wote wa elimu kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa

majukumu yangu. Aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wamiliki na mameneja wa shule, vyuo na taasisi binafsi ambao wamekuwa wakishirikiana na Serikali katika kutoa huduma ya elimu na mafunzo nchini.

**186. *Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninawashukuru washirika wa maendeleo na wadau wote wa elimu ambao wamechangia kufanikisha utekelezaji wa mipango na miradi ya elimu, sayansi na teknolojia. Naomba kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Afrika Kusini, Brazil, Canada, China, Ethiopia, Finland, Hangaria, Ireland, India, Israel, Italy, Japan, Kenya, Korea ya Kusini, Mauritius, Misri, Norway, Sweden, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Urusi, Uturuki, Uswisi. Aidha, natambua pia mchango wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika.

**187. *Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kushukuru Mashirika ya Kitaifa na Kimataifa yaliyochangia kufanikisha miradi na programu za Elimu, Sayansi na Teknolojia ambayo ni pamoja na: Baraza Kuu la Waislam Tanzania (BAKWATA), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *British Council, Campaign for Female Education* (CAMFED), *Christian Social Services Commissiyon* (CSSC), *Comprehensive Nuclear–Test - Ban Treaty Organisation* (CTBTO), *Deutscher Akademischer Austauschdienst* (DAAD), *Foreign, Commonwealth and Development Office* (FCDO), *Global Partnership for Education* (GPE), *Inter University Council for East Africa* (IUCEA), *International Atomic Energy Agency* (IAEA), *Japan International Cooperation Agency* (JICA), Jumuiya ya Madola, Karibu Tanzania Organization (KTO), *Korea International Cooperation Agency* (KOICA), *Swedish International Development Agency* (SIDA), *Tanzania Education Network*/Mtandao wa Elimu Tanzania (TEN/MET), Umoja wa Nchi za Ulaya, *United Nations Development Programme* (UNDP), *United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization* (UNESCO) na *United Nations International Children's Emergency Fund* (UNICEF).

## G. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2026/27

**188.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha utekelezaji wa malengo yaliyoanishwa kwa mwaka wa fedha 2026/27, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,394,423,829,000.00** kwa mchanganuo ufuatao:-

**(i)** **Shilingi 697,841,881,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ya Wizara ambapo **Shilingi 648,082,352,000.00** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 49,759,529,000.00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo; na

**(ii)** **Shilingi 1,696,581,948,000.00** zinaombwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 1,337,249,000,000.00** ni fedha za ndani na **Shilingi 359,332,948,000.00** ni fedha kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18) inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 3,866,993,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Mishahara ni **Shilingi 1,335,020,000.00** na Matumizi Mengineyo ni **Shilingi 2,531,973,000.00**

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa heshima kubwa naomba sasa Bunge lako tukufu likubali kupokea, kujadili na kupitisha Makadirio ya Bajeti ya Wizara (Fungu 46 na Fungu 18) yenye jumla ya **Shilingi 2,398,290,822,000.00**

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza.

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara https://www.moe.go.tz

**WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Hoja imetolewa na hoja imekubaliwa. Ninamwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Bunge, ya Elimu, Utamaduni na Michezo; na kwa niaba yake na atawasilisha ni Mheshimiwa Asha Juma Ferouz.

**MHE. ASHA J. FERUZ K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Bunge, Elimu, Utamaduni na Michezo ninaomba sasa niweze kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2025/2026; pamoja na maoni ya Kamati na ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya kwanza. Kwa kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) kwa mwaka wa fedha 2025/2026, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii ni matokeo ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha tarehe 9 hadi 27 Machi, 2026, kutokana na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya sekta zilizo chini ya Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba taarifa yote ya Kamati iingie kwenye Kumbukumbu Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ilivyowasilishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muundo wa taarifa. Sehemu hii inabainisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Lengo ni kuliwezesha Bunge

kufuatilia mtiririko wa taarifa na kuonesha taarifa inavyozingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa taarifa. Kwa maelezo hayo, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambapo ni sehemu ya kwanza inatoa maelezo ya jumla na kuonesha msingi, mbinu na wigo wa kazi ya Kamati katika kufanyia kazi makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya pili inabainisha matokeo ya uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Sehemu ya tatu inabainisha maoni na ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa Kamati kuchambua taarifa ya utekelezaji wa makadirio ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Fungu 46) ni masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge 2025, kifungu cha 5(g) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kikisomwa pamoja na kifungu cha 7 (1, a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinaipa Kamati hii jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, kanuni ya 120(2) ya Kanuni za Bunge ilitaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kama ilivyofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema asubuhi ya leo taarifa hii iliwekwa Mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 121(5) ya Kanuni za Bunge, na sasa ninawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Bunge kama nilivyoeleza hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbinu zilizotumika; Kamati imebainisha mbinu mbalimbali zilizotumika zikiwemo kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa majibu na mawasilisho ulifanyika kwa kufanya ulinganisho kimaudhui na uhalisia. Haya yote yamefanikisha kupatikana kwa taarifa hii ambayo inabainisha maoni na ushauri wa kufanyiwa kazi katika hoja hii inayohusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wigo na mipaka ya taarifa; wigo na mipaka ya taarifa hii unalenga kuongoza mjadala, kuonesha uwajibikaji wa kibajeti na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatengwa kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na mahitaji halisi ya wananchi. Kwa kuhusianisha maelezo hayo na Dira, ninaomba kurejea maneno halisi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, nanukuu: *"Tanzania inalenga kuwa na mfumo wa elimu jumuishi unaoandaa wananchi kwa ujuzi na maarifa yanayohitajika katika uchumi wa kisasa na kimataifa."* (uk.32). Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, taarifa hii inagusa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Maudhui yake yanahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati Bunge linapitisha bajeti ya Wizara hii. Eneo lingine la taarifa hii linagusa makadirio ya maduhuli, ulinganisho wa vipaumbele na matarajio ya wananchi katika bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili. Uchambuzi na Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Maelezo ya jumla. Sehemu hii inafafanua mambo makuu mawili: Kwanza ni uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na pili ni uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sehemu ya kwanza, maelezo yametolewa kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, uchambuzi wa mwenendo na ukusanyaji wa maduhuli, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utekelezaji wa majukumu na mipango ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Tarehe 24 Machi, 2026, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka

wa fedha 2026/2027. Aidha, uchambuzi wa Kamati ulizingatia mambo matano yafuatayo:

(i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(ii) Utekelezaji wa Kazi zilizopangwa;

(iii) Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iv) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo na

(v) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzingatiaji wa ushauri wa Kamati; wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na sehemu nyingine, utekelezaji wake ni endelevu kama inavyobainishwa katika Kiambatisho namba mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji wa maduhuli; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi bilioni 720.507. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2026, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 438.207, sawa na 61% ya malengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Kamati imebaini kwamba upangaji wa lengo la makusanyo ulizingatia hali halisi. Hata hivyo, upangaji wa lengo la makusanyo kwa taasisi zilizo chini ya Wizara hii unahitaji tathmini kidogo. Kwa upande wa mchango wa makusanyo baina ya Idara na Vitengo kwa upande mmoja na taasisi kwa upande mwingine, hali halisi ilizingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilitembelea miradi sita iliyopo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia pamoja na kupokea taarifa ya upatikanaji

wa fedha kwa ajili ya miradi na kuchambua utekelezaji wake. Ufafanuzi zaidi kuhusu miradi unaambatanishwa pamoja katika taarifa hii, kiambatisho namba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Waziri ilionesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ambapo ni 66.6% ya kipindi cha utekelezaji, Wizara ilikuwa imepokea 42% ya fedha zote za miradi. Uchambuzi zaidi ulionesha mambo yafuatayo:-

(i) Hali ya jumla ya upokeaji wa fedha za kugharimia miradi imekuwa hafifu, jambo linalochelewesha ukamilishaji wa baadhi ya miradi ikiwemo Mradi wa Ujenzi wa *VETA* 64 za Wilaya na Moja ya Mkoa wa Songwe;

(ii) Msukumo mkubwa katika kukamilisha miradi unatolewa zaidi na Serikali kuliko wabia wa maendeleo na wahisani, jambo ambalo linapaswa kuzingatiwa kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2026/2027 ili utekelezaji wa miradi ushirikishe wadau; na

(iii) Mwenendo wa utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na upatikanaji wa fedha. Kwa mfano, utekelezaji wa Mradi Namba 4397, Ujenzi wa Chuo cha Elimu ya Ufundi Stadi *VETA* – Gairo unasuasua kutokana na kuchelewa kwa fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa kuchelewa kunaathiri ukamilishaji wa miradi kwa wakati. Aidha, usimamizi wa ujenzi wa *VETA* 64 za Wilaya utazamwe upya kwani unaweza kuwa na mchango mkubwa katika kusuasua kwa miradi hiyo na katika kulinda viwango na thamani ya fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa majukumu. Maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yanapatikana katika Randama ya Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (uk. 34-68) na Fungu 18 – Tume ya Taifa ya *UNESCO* (uk. 4-10).

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya uchambuzi yalionesha mambo yafuatayo:-

(i) Baadhi ya kazi zilizopangwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 zinaendelea kufanyika hadi sasa na kwa sehemu kubwa ni endelevu;

(ii) Baadhi ya kazi zimetekelezwa zikiwa zinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile ongezeko la mahitaji ya miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu, ongezeko la mahitaji ya walimu hususan masomo ya Sayansi na Amali, wahadhiri na wakufunzi; na

(iii) Sehemu kubwa ya kazi zilizotekelezwa zinaendana na vipaumbele vilivyoainishwa na Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano wa kazi zinazoendelea ni kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali (Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi) katika shule za sekondari na vyuo vya amali. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Serikali inaendelea kuwezesha ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa katika shule 19 za amali kati ya shule 35 zilizolengwa kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania. Utekelezaji wa malengo haya hauridhishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa upatikanaji wa fedha. Kamati ilifanya uchambuzi wa mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa kuangalia matumizi ya kawaida, matumizi ya mishahara, matumizi ya gharama za uendeshaji na matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo. Njia zilizotumika kufanya uchambuzi ni kuweka data katika jedwali na kukokotoa asilimia. Matokeo ya uchambuzi yalionesha kuwa Wizara imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kulingana na bajeti iliyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla upatikanaji wa fedha kwa Wizara hii unahitaji juhudi za ziada, kuwezesha wastani wa 52.4% ya fedha ambazo hazijafika zipatikane ifikapo tarehe 30 Juni, 2026. Kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imewajibika ipasavyo na Bunge litakuwa limetoa mwongozo wake inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; Kamati ilichambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Wakati wa uchambuzi, Kamati ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:

(i) Makadirio ya mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na uzoefu uliopatikana kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(ii) Makadirio ya matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi uliofanywa na Kamati ulizingatia pia Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu 2025/2030. Na hapa nanukuu: "CCM inaamini kuwa rasilimali watu ndio rasilimali kuu katika kuleta maendeleo. Ili kutumia rasilimali hiyo kikamilifu, Taifa halina budi kuinoa ili kuimarisha mchango wake katika kuchochea maendeleo. Nyenzo muhimu ya kuinoa rasilimaliwatu ni elimu. Hivyo, CCM itaendelea kuwekeza katika kupanua fursa na kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote. Lengo ni kuhakikisha kuwa mfumo wa elimu unazalisha wahitimu wenye maarifa na ujuzi stahiki na uwezo wa kushindana kimataifa." (uk.23). Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ahadi hiyo, tathmini ya Kamati inajenga msingi unaozingatia dhamira ya Serikali kuinoa rasilimali watu kwa kutumia elimu. Kwa sababu hiyo, taarifa hii inabainisha matokeo ya uchambuzi katika maeneo yafuatayo:

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya mapato. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa uzoefu wa ukusanyaji wa mapato uliopatikana 2025/2026 umezingatiwa inavyostahili katika kupanga mchango wa mapato ya Wizara kwa Idara, Vitengo na Taasisi zake. Hali hiyo inaashiria taratibu bora za upangaji wa makadirio ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi wa Kamati umeonesha kuwa makadirio ya makusanyo yameongezeka kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na vyanzo vyote vya mapato kwa mwaka wa fedha ulioisha vinaendelea kuwa vile vile. Hali hii inaonesha kuwa Wizara inaweka juhudi stahiki katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi ya maendeleo. Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya shilingi trilioni 1.692 kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo kwa Fungu 46 iliyokusudiwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo:

(i) Bajeti inayoombwa imepungua kwa 21% kwa upande mmoja na taarifa ya utekelezaji ilionesha baadhi ya miradi inaelekea kukamilika kwa upande mwingine;

(ii) Ugharimiaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani umeongezeka kwa 12%. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii; na

(iii) Fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimepungua kwa 62%. Serikali iangalie jitihada zaidi katika kuvutia ushirikiano na wadau wengine kuwekeza katika elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla uzoefu wa upatikanaji wa fedha za nje kwa mwaka wa fedha unaokwisha umezingatiwa inavyostahili. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia zaidi fedha za ndani katika bajeti ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makadirio ya matumizi ya kawaida; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaomba jumla ya shilingi trilioni 2.388 kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Wizara ambapo 29% ya fedha hizo ni makadirio ya matumizi ya kawaida. Matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa Wizara imejipanga kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa hati idhini. Mpango huo unaendana na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu 2025 - 2030 na lengo la Serikali lililoelezwa kwa mujibu wa Katiba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Taifa ya *UNESCO* (Fungu 18). Tume ya Taifa ya *UNESCO* inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi bilioni 2.866 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli na vipaumbele vya Tume hii. Kati ya fedha hizo, 46.6% inakadiriwa kutumika kwa ajili ya mishahara na 54.4% ni kwa ajili ya kugharimia uendeshaji wa Tume. Kiasi cha fedha kilichopangwa kwa ajili hiyo kinatokana na mtazamo wa shughuli za Tume pamoja na njia zitakazotumika kutekeleza shughuli zilizopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tatu, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya uchambuzi, ninaomba kutoa maoni ya Kamati kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi. Maoni haya yanajenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokukamilika kwa ujenzi wa Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* 64 vya Wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe kunatokana na mtiririko mdogo wa fedha na ni jambo linaloathiri manufaa yanayolengwa kupatikana kutokana na ujenzi wa vyuo hivyo.

(ii) Kutokutolewa kwa fedha za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa ukamilifu kunaathiri lengo la Serikali la kutoa mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuwapunguzia vikwazo vya kiuchumi katika kupata elimu bora. *(Makofi)*

(iii) Baadhi ya Vyuo Vikuu vinavyotoa kozi za afya kutokuwa na hospitali za mafunzo kwa vitendo *(teaching hospitals)* kunaathiri ufanisi wa elimu ya tiba na huduma za afya kwa ujumla kutokana na wanafunzi kukosa fursa kwa vitendo *(hands-on experience)* katika mazingira halisi ya hospitali. *(Makofi)*

(iv) Ongezeko la wanafunzi linalosababisha uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi ufikie 1:3 hadi 1:5 unaweza kurekebishwa. Marekebisho yanayowezesha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja yatawezekana iwapo fedha za uchapaji zitapatikana kulingana na

mahitaji, pamoja na usimamizi mzuri wa usambazaji wa vitabu kwa wakati na kuwafikia walengwa.

(v) Utaratibu uliopo wa ruzuku ya shilingi 1,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa ajili ya wathibiti ubora *(Capitation grants)* kupitia TAMISEMI kwa shule za msingi na sekondari unaleta urasimu usiyokuwa na sababu na kuathiri utekelezaji mzuri wa majukumu ya wadhibiti ubora.

(vi) Upungufu wa bajeti kwa ajili ya kuimarisha mafunzo ya walimu kazini hususan walimu wa lugha ya alama ambapo kwa sasa ni wachache na hawakidhi mahitaji halisi, utaathiri ubora wa elimu inayotolewa katika ngazi zote hasa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

(vii) Utekelezaji wa tamko la kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali unahitaji ongezeko la bajeti ili kutengeneza mazingira wezeshi kulingana na mahitaji yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wa Kamati. Kwa kuzingatia maoni ya Kamati ambayo ni mtazamo wa jumla kuhusu mambo yaliyotajwa hapo juu, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali itoe fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)* 64 vya Wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe. Aidha, Kamati inashauri Serikali iajiri watumishi, inunue vitendea kazi na kujenga karakana. Hatua hii itawezesha vijana wengi kupata ujuzi stahiki wa ufundi na kuingia kwenye soko la ajira jambo litakalopunguza changamoto ya ajira nchini.
Ushauri huu unaendana na mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais wakati wa Hotuba yake akizindua Bunge la Kumi na Tatu, nanukuu: *"Vilevile, tutasimamia mpango wetu wa kuhakikisha kila Wilaya ina chuo cha VETA chenye vifaa stahiki vya mafunzo kwa vitendo."* (Uk.12) mwisho wa kunukuu.

(ii) Serikali itoe fedha zote za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa wanafunzi wote wenye sifa za kupata mikopo hiyo ili kutimiza azma ya Serikali ya kuwapunguzia vikwazo vya kiuchumi wanufaika wengi zaidi katika kupata elimu bora.

(iii) Serikali iandae mkakati wa kuviwezesha Vyuo kuwa na hospitali za mafunzo kwa vitendo *(teaching hospitals)* kwenye Vyuo Vikuu vyote vinavyotoa kozi za Afya nchini. Aidha, Serikali ihakikishe kuna utoshelevu wa hospitali za mafunzo kulingana na idadi ya wanafunzi na ihakikishe wanafunzi wanapatiwa mafunzo ipasavyo ili kuwajengea umahiri unaostahili.

(iv) Serikali iendelee kutenga fedha za uchapaji wa vitabu kulingana na mahitaji ili kuimarisha uwiano wa kitabu na mwanafunzi hadi kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1). Aidha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia isimamie kikamilifu usambazaji wa vitabu hivyo na kuhakikisha vinawafikia walengwa kama ilivyokusudiwa.

(v) Serikali ifanye jitihada za kuhamisha *capitation grants* ya shilingi 1,000 kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi na sekondari kwa mwaka, kutoka Fungu 56 - TAMISEMI ambalo halihusiki na Udhibiti Ubora wa Shule na kupeleka Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambalo linahusika na Udhibiti Ubora wa Shule.

(vi) Serikali iendelee kutenga bajeti kwa ajili ya kuimarisha mafunzo kazini hususan walimu wa lugha ya alama, ili kuwawezesha walimu hao kuwa sehemu ya kukuza ujumuishaji, mtazamo chanya na mazingira rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Ushauri huu unaendana na mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais wakati wa Hotuba yake akizindua Bunge la Kumi na Tatu, nanukuu:

*"Tunapotekeleza maendeleo jumuishi, tutaendeleza jitihada tulizozianza za kuweka miundombinu na vifaa kwa*

*wanafunzi wenye mahitaji maalum; pamoja na hao, tutaendeleza fursa muhimu ya kuwasomesha na kujiendeleza kwa watoto wenye magojwa adimu (rare diseases) wanaohudumiwa majumbani.*" (uk.12) mwisho wa kunukuu.

(vii) Bajeti iongezwe kwa ajili ya utekelezaji wa tamko la kuwarejesha shuleni wanafunzi walio nje ya mfumo rasmi *(IPOSA)* kwa kuzingatia uhamasishaji wa jamii, kuboresha mazingira rafiki ya ujifunzaji, miundombinu inayozingatia jinsia, pamoja na upatikanaji wa huduma za ushauri na unasihi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; ninachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Ninawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Ninaomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninapenda kumshukuru Mheshimiwa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wasaidizi wake, Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, Naibu Waziri na Profesa Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, ninapenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongozwa na Katibu wa Bunge, ndugu Baraka Ildephonce Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili liijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu,

Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 KAMA YALIVYOWASILISHA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia **(Fungu 46)** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2026/2027. Taarifa hii ni matokeo ya shughuli za Kamati kwa kipindi cha tarehe 09 hadi 27 Machi, 2026 kutokana na uchambuzi wa makadirio ya mapato na Matumizi ya Sekta zilizo chini ya Kamati hii.

### 1.2 Muundo wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inabainisha mtiririko wa maudhui pamoja na kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 ya Kanuni za Bunge kuhusu muundo wa Taarifa yoyote ya Kamati inayowasilishwa Bungeni. Lengo ni kuliwezesha Bunge kufuatilia mtiririko wa taarifa na kuonesha taarifa inavyozingatia masharti ya Kanuni za Bunge kuhusu

muundo wa Taarifa. Kwa maelezo hayo, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu ambazo ni:

(i) Sehemu ya **Kwanza** inatoa maelezo ya jumla na kuonesha Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi ya Kamati katika kufanyia kazi makadirio ya mapato na Matumizi ya Wizara hii;

(ii) Sehemu ya **Pili** inabainisha matokeo ya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027; na

(iii) Sehemu ya **Tatu** inabainisha Maoni na Ushauri wa Kamati na kumalizia kwa hitimisho.

## 1.3 Msingi, Mbinu na Wigo wa Kazi

### 1.3.1 Msingi wa Taarifa

**Mheshimiwa Spika,** msingi wa Kamati kuchambua taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia **(Fungu 46)** ni masharti ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Kifungu cha 5 (7) (g) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7 (1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, kinaipa Kamati hii jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Aidha, Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Bunge ilitaka makadirio haya yajadiliwe na Kamati kama ilivyofanyika.

**Mheshimiwa Spika**, mapema asubuhi ya leo, taarifa hii iliwekwa mezani kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (5) ya Kanuni za Bunge. Na sasa, nawasilisha taarifa hii kwa mujibu wa Kanuni ya 121 (9) ya Kanuni za Bunge kama nilivyoeleza hapo awali.

### 1.3.2 Mbinu Zilizotumika

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebainisha mbinu zilizotumika kufanyia kazi hoja hii kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 145 (a) (iii) ya Kanuni

za Bunge. Lengo ni kuiwezesha Taarifa hii kuwa rejea madhubuti, inayosaidia mjadala wa Bunge kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara. Kwa kufanya hivyo, Kamati inajenga msingi wa uadilifu uliozingatiwa ili kupata maoni na ushauri wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitumia mbinu mbalimbali za uchambuzi zikiwemo kupokea maelezo ya Waziri, kuhoji mambo yaliyojitokeza na kupokea majibu ya mtoa hoja. Uchambuzi wa majibu na mawasilisho ulifanyika kwa kufanya ulinganisho kimaudhui na uhalisia. Haya yote yamefanikisha kupatikana kwa taarifa hii ambayo inabainisha maoni na ushauri wa kufanyiwa kazi katika hoja hii inayohusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

### 1.3.3 Wigo na mipaka ya Taarifa

**Mheshimiwa Spika**, kama inavyofahamika, lengo la taarifa hii ni kulipatia Bunge tathmini ya kina na yenye ushahidi kuhusu makadirio ya mapato na matumizi yaliyowasilishwa na mtoa hoja. Madhumuni yake ni kuongoza mjadala, kuonesha uwajibikaji wa kibajeti na kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatengwa kwa kuzingatia vipaumbele vya kitaifa, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na mahitaji halisi ya wananchi. Kwa kuhusianisha maelezo hayo na Dira, naomba kurejea maneno halisi ya Dira;

***Nanukuu***:
*"Tanzania inalenga kuwa na mfumo wa elimu jumuishi unaoandaa wananchi kwa ujuzi na maarifa yanayohitajika katika uchumi wa kisasa na kimataifa." (uk.32)*. **Mwisho wa kunukuu.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa msingi huo, taarifa hii inagusa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Maudhui yake yanahusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo, ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa ushauri uliotolewa na Kamati wakati Bunge linapitisha bajeti ya Wizara hii. Eneo lingine la taarifa hii linagusa makadirio ya maduhuli, ulinganisho wa vipaumbele na matarajio ya wananchi na bajeti inayoombwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

## SEHEMU YA PILI 2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA2025/2026

### 2.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, sehemu ya pili ya Taarifa hii inatoa maelezo kamili kuhusu mambo yote yaliyochambuliwa na Kamati. Sehemu hii itakuwa na maelezo kuhusu mambo makuu mawili. Mambo hayo ni: -

(i) Uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026; na

(ii) Uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi huo ulifanyika kwa ulinganisho kama ilivyoelekeza Kanuni ya 120 (1) na (2) ya Kanuni za Bunge na ni uchambuzi unaojenga msingi wa maoni na ushauri wa Kamati.

### 2.2 Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** ili kukidhi masharti ya Kanuni za Bunge, tarehe 24 Machi, 2026, Kamati ilipokea taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

Madhumuni yalikuwa ni kuliwezesha Bunge kulinganisha dhamira yake wakati wa kupitisha bajeti na matokeo wakati wa utekelezaji. Aidha, uchambuzi wa makadirio ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ulilenga kuliwezesha Bunge kupitisha bajeti ya Wizara hii kwa namna yenye mchango unaolingana.

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni hayo, sehemu hii inatoa matokeo ya uchambuzi wa mambo matano ambayo ni:

(i) Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(ii) Utekelezaji wa Kazi zilizopangwa;

(iii) Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(iv) Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; na

(v) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha za Bajeti.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi huo utajenga vigezo vya kutumika kufanya tathmini ya uhalisia wa makadirio ya mapato na matumizi. Hatua hiyo ni ya muhimu kwa uamuzi bora wa Bunge.

### 2.2.1 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, ili kutoa fursa kwa Bunge na umma kufahamu kama Serikali inazingatia ushauri uliotolewa Bungeni katika kuboresha matumizi ya rasilimali za umma, sehemu hii ya Taarifa inatoa mrejesho mbele ya Bunge. Kwa kufanya hivyo, Taarifa hii inapima dhamira ya Serikali katika kutekeleza mipango na miradi kwa kuzingatia maoni ya wawakilishi wa wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu mambo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba kwa sehemu kubwa ushauri wa Kamati ulizingatiwa na sehemu nyingine, utekelezaji wake ni endelevu kama inavyobainishwa katika **Kiambatisho Na. 2.**

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa ushauri uliozingatiwa ni kuhusu kupunguza changamoto ya uhaba wa walimu, wakufunzi na wahadhiri. Changamoto hiyo ilijitokeza zaidi katika masomo au fani za sayansi, hisabati na mafunzo ya amali katika kutekeleza mpango wa fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali (ufundi na ufundi stadi) kwa shule za sekondari za amali na vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa iliyotolewa kwenye Kamati inaonesha kwamba kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imefanikiwa kuajiri jumla ya walimu **13,942** kwa ajili ya shule za Msingi na Sekondari ambapo kati ya hao walimu **2,354** ni wa Masomo ya Sayansi na Hisabati, na walimu **451** ni wa masomo ya amali. Aidha, katika utekelezaji wa siku 100 za Ahadi za Mheshimiwa Rais kwa mwaka 2025/2026, Serikali imeajiri walimu **7,000** wa shule za msingi na sekondari. Serikali imeajiri watumishi **376** kwa Mamlaka ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ambapo walimu ni **304** na wasiyo walimu ni **72**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa, katika mwaka 2025, jumla ya wataalamu **1,427** katika masomo ya Amali na Biashara waliajiriwa na kupatiwa mafunzo ya mbinu za ufundishaji kabla ya kuanza kazi ili kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yao kwa ufanisi unaokidhi viwango vinavyotarajiwa. Vilevile, Serikali imetoa kibali cha kuajiri watumishi **500,** kati yao walimu ni **400** na wasiyo walimu ni **100** katika vyuo vya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kwa mwaka 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ushauri unaoendelea kutekelezwa ni kuhusu ruzuku ya uthibiti ubora inayotolewa kwa kila mwanafunzi *(Capitation grants)*. Utaratibu uliopo wa kutoa Shilingi 1,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kupitia fungu 56 TAMISEMI kwa shule za msingi na sekondari unakinzana na mgawanyo wa majukumu unaotambua wathibiti ubora kuwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kamati ilijulishwa kuwa Wizara inaendelea kufuatilia uhamishaji wa fedha hizo kutoka Fungu 56 – TAMISEMI kwenda Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**Mheshimiwa Spika**, hatua ya Serikali kusikiliza na kuzingatia ushauri unaotolewa Bungeni inastahili kupongezwa. Ni hatua ambayo inafanikisha lengo la Serikali kuwezesha ustawi wa watu kwa kuzingatia ushauri wa wananchi kupitia kwa wawakilishi wao. Kwa ufafanuzi wa kina kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati, **Kiambatisho Na. 2** kinaeleza zaidi.

### 2.2.2 Ukusanyaji wa Maduhuli


**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ililenga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **720,507,879,789.63**. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2026 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ilikuwa imekusanya shilingi **438,207,871,632.63** sawa na **asilimia 61** ya malengo yaliyokusudiwa. Muhtasari wa taarifa za ukusanyaji wa mapato unaonekana katika **Jedwali Na. 1** na picha ya hali halisi inatolewa kwenye **Chati Na. 1.**


**Jedwali Na 1: Makadirio na Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026**

| CHANZO | MAKADIRIO | MAKUSANYO | ASILIMIA |
|---|---|---|---|
| Idara/Vitengo | 8,402,257,000.00 | 5,751,137,370.00 | 68 |
| Taasisi | 712,105,622,789.63 | 432,456,734,262.63 | 61 |
| **Jumla** | **720,507,879,789.63** | **438,207,871,632.63** | **61** |

**Chanzo**: *Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027*

**Chati Na. 1: Taswira ya Uwiano wa Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Uwiano wa Makadirio kwa Wizara Uwiano wa kiasi kilichokusanywa na na Taasisi zake Wizara na Taasisi zake**




**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika**, taswira iliyojitokeza inaonesha kwamba:

(i) Hadi kufikia Februari, 2026 kiasi kilichokusanywa ni asilimia **61** ya lengo badala ya kuwa imefika asilimia **66.6**;

(ii) Kiasi kilichokusanywa kwenye taasisi zilizo chini ya Wizara hii ni asilimia **61;**

(iii) Kiasi kilichokusanywa kwa Idara na Vitengo vya Wizara ni asilimia **68** ikiwa imevuka lengo la asilimia **66.6** kwa kipindi hicho;

(iv) Katika Mpango wa makusanyo, Idara na Vitengo vilitarajiwa kuchangia kwa asilimia **1.** Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa mchango wake ni asilimia **1.**

(v) Katika mpango wa makusanyo, Taasisi zilitarajiwa kuchangia asilimia **99.** Taarifa ya makusanyo inaonesha kuwa Taasisi ilichangia kwa asilimia **99.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla Kamati imebaini kwamba upangaji wa lengo la makusanyo ulizingatia hali halisi. Hata hivyo, upangaji wa lengo la makusanyo kwa taasisi zilizo chini ya Wizara hii unahitaji tathmini kidogo. Kwa upande wa mchango wa makusanyo baina ya Idara na Vitengo kwa upande mmoja na taasisi kwa upande mwingine, hali halisi ilizingatiwa.

### 2.2.3 Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya usimamizi wa Kibunge wa bajeti ya Miradi ya Maendeleo, Bunge lilipitisha bajeti ya miradi ya maendeleo na inatarajia kuona mabadiliko yanayotokana na utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa uratibu wa Bunge la Tanzania ili kujua upatikanaji wa manufaa kutokana na miradi hiyo, kwa mujibu wa Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilifanya ziara ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa miradi hiyo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa sehemu ya ufuatiliaji wa miradi inayotekelezwa na Wizara hii, Kamati ilitembelea miradi sita (6) pamoja na kupokea taarifa ya upatikanaji wa fedha kwa ajili ya miradi na kuchambua utekelezaji wake. Ufafanuzi zaidi kuhusu miradi unaambatanishwa pamoja katika Taarifa hii **(Kiambatisho Na. 1).**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Waziri ilionesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2026 ambapo ni asilimia **66.6** ya kipindi cha utekelezaji, Wizara ilikuwa imepokea asilimia **42** ya fedha zote za miradi. Uchambuzi zaidi ulionesha mambo yafuatayo:

(i) Hali ya jumla ya upokeaji wa fedha za kugharimia miradi imekuwa hafifu, jambo linalochelewesha ukamilishaji wa miradi.

(ii) Msukumo mkubwa katika kukamilisha miradi unatolewa zaidi na Serikali kuliko wabia wa maendeleo na wahisani, jambo ambalo linapaswa kuzingatiwa kwa bajeti ya mwaka 2026/2027 ili miradi hiyo itekelezwe kwa fedha za ndani.

(iii) Mwenendo wa utekelezaji wa miradi hiyo unaendana na upatikanaji wa fedha. Kwa mfano, utekelezaji wa Mradi **Na. 4397** Ujenzi wa Chuo cha Elimu ya Ufundi Stadi (VETA – Gairo) unasuasua kutokana na kuchelewa kwa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa kuchelewa inaathiri ukamilishaji wa miradi kwa wakati. Aidha, usimamizi hafifu katika ujenzi wa vyuo 64 vya VETA ngazi ya Wilaya vinavyosimamiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kupitia Idara ya Elimu ya Ufundi unaathiri ubora, ukamilikaji na tija iliyokusudiwa.

### 2.2.4 Utekelezaji wa Majukumu

**Mheshimiwa Spika,** tarehe 24 Machi, 2026 Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Wakati wa uchambuzi Kamati ilizingatia vipaumbele vya Wizara, hatua iliyofikiwa, Bajeti iliyopitishwa na Bunge

na hali halisi. Lengo ni kujiridhisha na kiwango kilichofikiwa ili kulijulisha Bunge matokeo ya utekelezaji wa Bajeti iliyoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika,** maelezo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 yanapatikana katika Randama ya **Fungu 46 – Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (uk. 34-68)** na **Fungu 18 – Tume ya Taifa ya UNESCO (uk. 4-10)**.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi wa taarifa hizo yanaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Baadhi ya kazi zilizopangwa kwa Mwaka 2025/2026 zinaendelea kufanyika hadi sasa na kwa sehemu kubwa ni endelevu;

(ii) Baadhi ya kazi zimetekelezwa zikiwa zinakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile ongezeko la mahitaji ya miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu, ongezeko la mahitaji ya walimu hususan masomo ya Sayansi na Amali, wahadhiri na wakufunzi.

(iii) Sehemu kubwa ya kazi zilizotekelezwa zinaendana na vipaumbele vilivyoainishwa na Wizara.

**Mheshimiwa Spika**, mfano wa kazi zinazoendelea ni kuongeza fursa na kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali (Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi) katika shule za sekondari na vyuo vya amali. Maelezo ya Serikali yalionesha kuwa, Serikali inaendelea kuwezesha ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa katika shule 19 za amali kati ya shule 35 zilizolengwa kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali ilieleza kwamba imewezesha upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA katika shule tano (5) za sekondari za amali. Shule hizo ni Nyakato, Rugambwa, Maruku, Bukoba na Bwiru Wavulana. Aidha, imesajili jumla ya Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi 140. Kati ya Vyuo hivyo, Vyuo vya Elimu ya Ufundi ni 13 na Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi ni 127. Kati ya vyuo 100 vilivyopangwa kusajiliwa, Vyuo vya Elimu ya Ufundi ni 30 na Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi ni 70.

**Mheshimiwa Spika,** mfano wa kazi zilizokabiliwa na changamoto ni kuimarisha utoaji wa elimu katika ngazi zote. Taarifa ya Waziri ilionesha ongezeko la mahitaji ya miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama changamoto. Pamoja na hivyo, taarifa ilibainisha kuwa kazi hiyo iliendelea kufanyika. Ni maoni ya
Kamati kwamba utatuzi wa changamoto hizo ni jambo linalowezesha mwendelezo mzuri wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

### 2.2.5 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha

**Mheshimiwa Spika**, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoisha unalisaidia Bunge kufanya uamuzi sahihi kwa mwaka wa fedha unaokuja. Kwa kuzingatia hilo, Kamati ilitaka kubaini uwezo wa taasisi kutumia fedha, namna ya kuzuia makosa yanayojirudia kuhusu bajeti pamoja na kupima uhalali wa makadirio ya bajeti yanayowasilishwa Bungeni. Kufanikisha hayo, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kuangalia matumizi ya kawaida, matumizi ya mishahara, matumizi ya gharama za uendeshaji na matumizi ya fedha za miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** njia kuu iliyotumika kufanya uchambuzi ilijumuisha kuweka data katika jedwali, kukokotoa asilimia na kutafsiri ukokotozi. Kwa rejea rahisi, kazi hiyo inaonekana katika **Jedwali Na. 2**

**Jedwali Na 2: Mchanganuo wa Upatikanaji wa Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

| **UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 46 MWAKA 2025/2026** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | | **KILICHOIDHINISHWA** | **KILICHOPOKELEWA** | **ASILIMIA** |
| **KAWAIDA** | MISHAHARA | 635,249,992,000.00 | 407,410,082,886.86 | 64 |
| | OC | 53,364,242,000.00 | 33,597,226,516.79 | 63 |
| | **JUMLA** | **688,614,234,000.00** | **441,007,309,403.65** | **64** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **MAENDELEO** | NDANI | 1,186,987,965,000.00 | 634,233,227,661.90 | 53 |
| | NJE | 950,476,206,000.00. | 269,117,230,888.97 | 28 |
| | **JUMLA** | **2,137,464,171,000.00** | **903,350,458,550.87** | **42** |
| **JUMLA BAJETI** | | **2,826,078,405,000.00** | **1,344,357,767,954.52** | **47.6** |

**Chanzo**: *Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unabainisha kuwa Hadi kufikia mwezi Februari, 2026 yamejitokeza yafuatayo:


(i) Kiasi kilichopokelewa kwa ujumla ni asilimia **47.6** ikiwa ni pungufu kwa asilimia **66.6**;

(ii) Kiasi kilichopokelewa kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Wizara *(OC)* ni asilimia **63** kwa kipindi cha utekelezaji cha asilimia **66.6**;


(iii) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya mishahara ni asilimia **64** kwa kipindi cha utekelezaji cha asilimia **66.6**;

(iv) Kiasi cha fedha kilichopokelewa kwa ajili ya kugharimia miradi ya maendeleo ni asilimia 42 kwa kipindi cha utekelezaji cha asilimia **66.6.**

**Uwiano wa Makadirio kwa Aina za Matumizi**




**Uwiano wa Upatikanaji wa Fedha kwa Aina za Matumizi**




**Chanzo**: *Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027*

**Mheshimiwa Spika**, tafsiri ya data katika chati inaonesha yafuatayo:

(i) Kipaumbele cha Matumizi kwa ajili ya Mishahara kilikuwa asilimia **22** wakati wa makadirio na katika upatikanaji wa fedha kimekuwa asilimia **23**;


(ii) Kipaumbele cha matumizi kwa ajili ya matumizi ya uendeshaji *(OC)* kilikuwa asilimia **2** wakati wa makadirio na kimeendelea kuwa asilimia **2** kwa upatikanaji wa fedha; na

(iii) Kipaumbele cha matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo kilikuwa asilimia **76** wakati wa makadirio na kimekuwa asilimia **75** wakati wa upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa hali hiyo, Wizara imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kulingana na bajeti iliyopangwa. Aidha, msisitizo uliowekwa katika makadirio ya mishahara na upatikanaji wake unaashiria kuwa malengo yanayohusu masuala ya utumishi katika Wizara hii yamepata kipaumbele kwa asilimia iliyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika,** ili kujiridhisha na namna upatikanaji wa fedha ulivyoendana na makusudio ya Bunge, Kamati ilifanya ulinganisho wa makadirio kwa upatikanaji wa fedha hadi kufikia mwezi Februari, 2026. Kwa ajili ya kurahisisha taswira ya upatikanaji huo wa fedha, **Chati Na. 2** imetumika katika uchambuzi.

**Chati Na. 2: Ulingansho wa Makadirio kwa Upatikanaji wa Fedha hadi kufikia Mwezi Februari, 2026**




**Chanzo**: *Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027*

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa grafu hiyo inayohusu mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kama ifuatavyo:

(i) Kwa ujumla upatikanaji wa fedha ni pungufu ya asilimia **50** ilhali kipindi cha utekelezaji kimefikia asilimia **66.6**. Jambo hili si ishara nzuri ya utekelezaji wa bajeti;

(ii) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mishahara ulifikia asilimia **64** katika kipindi cha utekelezaji ambacho ni asilimia **66.6.** Ingawa tofauti si kubwa, jambo hili linaashiria kwamba upatikanaji wa fedha ungechelewa kidogo tafsiri yake kwa masuala ya utumishi ingekuwa tofauti;

(iii) Upatikanaji wa fedha kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Wizara ulikuwa ni asilimia **62** katika kipindi cha utekelezaji ambacho ni asilimia **66.6.** Hali hiyo haikuathiri uendeshaji wa Wizara kwa ujumla.

(iv) Upatikanaji wa fedha za kugharimia miradi ya maendeleo haukuwa mzuri kiasi cha kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla upatikanaji wa fedha kwa Wizara hii unahitaji juhudi za ziada za kuwezesha wastani wa asilimia **52.4** ya fedha ambazo hazijafika zipatikane ifikapo tarehe 30 Juni, 2026. Kwa kufanya hivyo, Serikali itakuwa imewajibika ipasavyo na Bunge litakuwa limetoa mwongozo wake inavyostahili.

## 2.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia masharti ya Kanuni ya 120 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilichambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa kuzingatia kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Wakati wa uchambuzi, Kamati ilijielekeza katika maeneo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na uzoefu uliopatikana kwa mwaka wa fedha 2025/2026; na

(ii) Makadirio ya Matumizi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ikilinganishwa na upatikanaji wa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati ulizingatia pia Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu 2025/2030, inayoeleza: **Nanukuu;**
*"CCM inaamini kuwa rasilimali watu ndio rasilimali kuu katika kuleta maendeleo. Ili kutumia rasilimali hiyo kikamilifu, Taifa halina budi kuinoa ili kuimarisha mchango wake katika kuchochea maendeleo. Nyenzo muhimu ya kuinoa rasilimaliwatu ni elimu. Hivyo, CCM itaendelea kuwekeza katika kupanua fursa na kuboresha elimu na mafunzo katika ngazi zote. Lengo ni kuhakikisha kuwa mfumo wa elimu unazalisha wahitimu wenye maarifa na ujuzi stahiki na uwezo wa kushindana kimataifa."* (uk.23).

**Mwisho wa kunukuu.**
**Mheshimiwa Spika,** kwa ahadi hiyo, tathmini ya Kamati inajenga msingi unaozingatia dhamira ya Serikali kuinoa rasilimali watu kwa kutumia elimu. Kwa sababu hiyo, taarifa hii inabainisha matokeo ya uchambuzi katika maeneo yafuatayo:

### 2.3.1 Makadirio ya Mapato

**Mheshimiwa Spika**, taarifa kuhusu lengo la ukusanyaji wa maduhuli ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2026/2027 iliwasilishwa kwa mujibu wa masharti ya Kanuni ya 118 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Baada ya kuipokea taarifa hiyo, Kamati ilichambua makadirio hayo kwa kuzingatia lengo lililokuwa limewekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika,** ukusanyaji wa mapato yanayotokana na shughuli za umma katika Sekta ya Elimu una uhusiano wa karibu na ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara hii. Ili kujiridhisha na namna Wizara ilivyojipanga, Kamati ilifanya uchambuzi kwa kutumia uzoefu

uliopatikana katika utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Uchambuzi ulifanyika kwa kutumia nyenzo kama vile jedwali, chati, ukokotozi na ulinganisho kadiri ilivyofaa.

**Mheshimiwa Spika,** rejea ya matokeo ya uchambuzi ni **Jedwali Na. 3 na Chati Na. 3.**

**Jedwali Na 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027**

| **ULINGANISHO WA UKUSANYAJI WA MADUHULI FUNGU 46 2025/2026 NA 2026/2027** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO/UPUNGUFU** | **ASILIMIA YA ONGEZEKO /UPUNGUFU** |
| **Idara na Vitengo Wizarani** | 8,402,257,000.00 | 9,311,892,000.00 | 909,635,000.00 | 11 |
| **Taasisi** | 712,105,622,789.63 | 770,217,295,341.06 | 58,111,672,551.43 | 8.2 |
| **Jumla** | 720,507,879,789.63. | 779,529,187,341.06 | 59,021,307,551.43 | 8.2 |

**Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi unaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Makadirio ya mapato kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 yameongezeka kwa **asilimia 8.2** ikilinganishwa na Mwaka wa fedha 2025/2026. Ongezeko hili lisipofanyiwa kazi vizuri linaweza kuwa takwimu zisizo na uhalisia. Sababu ya maoni hayo ni kuwa kwa kipindi cha utekelezaji cha asilimia **66.6** makusanyo yalikuwa nyuma kwa asilimia **5** hivyo ongezeko la asilimia **8** lingetarajiwa kuwa upungufu wa lengo kwa asilimia **5.**


(ii) Makadirio ya mapato ya Wizara yameongezeka kwa asilimia **11** lakini uzoefu hauonyeshi ongezeko hilo.

(iii) Makadirio ya makusanyo kwa Taasisi za Wizara hii yameongezeka kwa asilimia **8.2** ilhali uzoefu unaonesha hadi kufikia Februari, 2026 zilikuwa nyuma kwa asilimia **5.6** jambo linaloleta mashaka ya uhalisia wa lengo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa uchanganuzi huo, upo umuhimu wa Serikali kufanya tathmini ya vigezo vya upangaji wa lengo la makusanyo. Aidha, mipango yoyote ya ukusanyaji wa mapato unahitaji tathmini ya kina ili kuendana na uhalisia. Kwa vyovyote vile, kuweka lengo la makusanyo bila kuzingatia uhalisia kunaweza kuathiri utekelezaji bora wa majukumu ya Wizara. Hata hivyo, uchambuzi wa jumla unaonesha kiwango cha uzingatiaji wa uhalisia.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ajili ya kutambua maeneo yenye vyanzo vya uhakika vya mapato, Kamati ilifanya ulinganisho wa makadirio ya mapato kati ya Wizara, Idara na Vitengo vyake kwa upande mmoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa upande mwingine. Mlingano huo unaonekana katika **Chati Na. 3**

**Chati Na. 3: Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2026/2027**




***Chanzo**: Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026*

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya uchambuzi yameonesha kuwa uzoefu wa ukusanyaji wa mapato uliopatikana 2025/2026 umezingatiwa inavyostahili katika kupanga mchango wa mapato ya Wizara kwa Idara, Vitengo na Taasisi zake. Hali hiyo inaashiria taratibu bora za upangaji wa makadirio ya mapato.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi zaidi wa Kamati umeonesha kuwa makadirio ya Makusanyo yameongezeka kwa mwaka wa fedha 2026/2027 na vyanzo vyote vya mapato kwa mwaka wa fedha ulioisha vinaendelea kuwa vile vile. Hali hii inaonesha kuwa Wizara inaweka juhudi stahiki katika ukusanyaji wa mapato.

### 2.3.2 Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya **Shilingi 1,692,288,114,000** kwa ajili ya kugharimia Miradi ya Maendeleo kwa **Fungu 46** iliyokusudiwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2026/2027. Uchambuzi umeonesha mambo yafuatayo:-

(i) Bajeti inayoombwa imepungua kwa asilimia **21** kwa upande mmoja na taarifa ya utekelezaji ilionesha baadhi ya miradi inaelekea kukamilika kwa upande mwingine.

(ii) Ugharimiaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani umeongezeka kwa asilimia **12.**

(iii) Fedha za nje kwa ajili ya miradi ya maendeleo zimepungua kwa asilimia **62**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla uzoefu wa upatikanaji wa fedha za nje kwa mwaka wa fedha unaokwisha umezingatiwa inavyostahili. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutumia zaidi fedha za ndani katika Bajeti ya Miradi ya Maendeleo.

### 2.3.3 Makadirio ya Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, mapema asubuhi ya leo Mheshimiwa Waziri aliweka mezani hotuba yake inayoonesha kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inaomba jumla ya shilingi **2,388,398,284,000.**

Asilimia **29** ya fedha hizo ni makadirio ya matumizi ya kawaida na asilimia **71** ni matumizi ya kugharimia miradi ya maendeleo. Ili kuliwezesha Bunge kufanyia kazi makadirio hayo inavyostahili, Kamati imeweka muhtasari na mchanganuo wa fedha hizo katika **Jedwali Na 4**.

**Jedwali Na 4: Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027**

| ULINGANISHO WA BAJETI 2025/2026 NA 2026/2027 (FUNGU 46) | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **AINA YA MATUMIZI ('000')** | | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO/ UPUNGUFU** | **ASILIMIA** |
| **Kawaida** | **Mishahara** | 635,249,992 | 648,082,352 | 12,832,360 | 2 |
| | **OC katika** | 53,364,242 | 48,027,818 | -5,336,424,000 | 10 |
| | **Jumla** | 688,614,234 | 696,110,170, | - 10,665,252 | 1.5 |
| **Maendeleo** | **Ndani** | 1,186,987,965 | 1,333,177,000 | 146,189,035 | 12 |
| | **Nje** | 950,476,206 | 359,111,114 | - 591,365,092 | 62 |
| | **Jumla** | 2,137,464,171 | 1,692,288,114 | -445,176,057 | 21 |
| **Jumla Bajeti** | **Jumla kuu** | 2,826,078,405 | 2,388,398,284 | -437,680,121 | 15.5 |

***Chanzo:*** *Usanifu wa Kamati kutokana na Randama ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.*

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha mambo yafuatayo:-

(i) Bajeti ya mishahara imeongezeka kwa asilimia **2** jambo linaloashiria kipaumbele cha Serikali katika masuala ya utumishi.

(ii) Bajeti ya matumizi ya uendeshaji wa shughuli za Wizara imepungua kwa asilimia **10**.

(iii) Kwa ujumla bajeti ya matumizi ya kawaida imepungua kwa asilimia **10**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa matokeo hayo ya uchambuzi bado Wizara imejipanga kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa hati idhini.

Mpango huo unaendana na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050, Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu 2025/2030 na lengo la Serikali lililoelezwa kwa mujibu wa Katiba.

### 2.3.4 Makadirio ya Matumizi ya Tume ya Taifa ya UNESCO (Fungu 18)

**Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya UNESCO inakadiriwa kutumia jumla ya shilingi **2,866,993,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli na vipaumbele vya Tume hii. Kati ya fedha hizo, asilimia **46.6** inakadiriwa kutumika kwa ajili ya mishahara na asilimia **54.4** ni kwa ajili ya kugharimia uendeshaji wa Tume. Kiasi cha fedha kilichopangwa kwa ajili hiyo kinatokana na mtazamo wa shughuli za Tume pamoja na njia zitakazotumika kutekeleza shughuli zilizopangwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla dhima ya Tume ya Taifa ya UNESCO kushirikiana na wadau katika kuhamasisha amani na malengo ya maendeleo endelevu nchini imezingatiwa na kuwezeshwa kibajeti. Muhtasari wa mchanganuo wa fedha hizo unaonekana katika **Jedwali Na. 5**

**Jedwali Na 5: Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka 2025/2026 na Mwaka 2026/2027**

| **ULINGANISHO WA BAJETI FUNGU 18 KWA MWAKA 2025/2026 NA 2026/2027** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **AINA YA MATUMIZI** | **2025/2026** | **2026/2027** | **ONGEZEKO /UPUNGUFU** | **ASILIMIA** |
| **MISHAHARA** | 1,538,096,000 | 1,335,020,000 | -203,076,000 | 13 |
| **OC** | 1,702,192,000 | 1,531,973,000 | -170,219,000 | 10 |
| **JUMLA** | **3,240,288,000** | **2,866,993,000** | **-373,295,000** | **11.5** |

***Chanzo:*** *Usanifu wa Kamati kutokana na Randama ya Tume ya Taifa ya UNESCO kuhusu Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.*

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maelezo ya Jumla

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi, naomba kutoa maoni ya Kamati kwa kuzingatia matokeo ya uchambuzi. Maoni haya yanajenga msingi wa ushauri nitakaoutoa. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Kutokukamilika kwa ujenzi wa Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) 64 vya Wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe kutokana na mtiririko mdogo wa fedha ni jambo linaloathiri manufaa yanayolengwa kupatikana kutokana na ujenzi wa vyuo hivyo.

(ii) Kutokutolewa kwa fedha za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa ukamilifu kunaathiri lengo la Serikali la kutoa mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu ili kuwapunguzia vikwazo vya kiuchumi katika kupata elimu bora.

(iii) Baadhi ya Vyuo Vikuu vinavyotoa kozi za Afya kutokuwa na hospitali za mafunzo kwa vitendo (teaching hospitals) kunaathiri ufanisi wa elimu ya tiba na huduma za afya kwa ujumla kutokana na wanafunzi kukosa fursa kwa vitendo *(hands-on experience)* katika mazingira halisi ya hospitali.

(iv) Ongezeko la wanafunzi linalosababisha uwiano wa kitabu kimoja kwa wanafunzi ufikie 1:3 hadi 1:5 unaweza kurekebishwa. Marekebisho yanayowezesha uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja yatawezekana iwapo fedha za uchapaji zitapatikana kulingana na mahitaji pamoja na usimamizi mzuri wa usambazaji wa vitabu kwa wakati na kuwafikia walengwa.

(v) Utaratibu uliopo wa ruzuku ya shilingi 1,000 kwa kila mwanafunzi kwa mwaka kwa ajili ya wathibiti ubora (Capitation grants)

kupitia TAMISEMI kwa shule za msingi na sekondari unaleta urasimu usiyokuwa na sababu na kuathiri utekelezaji mzuri wa majukumu ya wadhibiti ubora.

(vi) Upungufu wa bajeti kwa ajili ya kuimarisha mafunzo ya walimu kazini hususan walimu wa lugha ya alama ambapo kwa sasa ni wachache na hawakidhi mahitaji halisi. Upungufu huo utaathiri ubora wa elimu inayotolewa katika ngazi zote hasa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

(vii) Utekelezaji wa tamko la kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali unahitaji ongezeko la bajeti ili kutengeneza mazingira wezeshi kulingana na mahitaji yao.

### 3.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maoni ya Kamati ambayo ni mtazamo wa jumla kuhusu mambo yaliyotajwa hapo juu, Kamati inashauri mambo yafuatayo:-

(i) Serikali itoe fedha kwa ajili ya ujenzi wa Vyuo vya Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) 64 vya Wilaya na kimoja cha Mkoa wa Songwe. Aidha, Kamati inashauri Serikali iajiri watumishi, inunue vitendea kazi na kujenga karakana. Hatua hii itawezesha vijana wengi kupata ujuzi stahiki wa ufundi na kuingia kwenye soko la ajira jambo litakalopunguza changamoto ya ajira nchini. Ushauri huu unaendana na mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais wakati wa Hotuba yake akizindua Bunge la 13:

**Nanukuu:**
*"Vilevile, tutasimamia mpango wetu wa kuhakikisha kila Wilaya ina chuo cha VETA chenye vifaa stahiki vya mafunzo kwa vitendo." (uk.12)*. **mwisho wa kunukuu.**

(ii) Serikali itoe fedha zote za Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kama zilivyoidhinishwa na Bunge kwa wakati na kwa wanafunzi wote wenye sifa za kupata mikopo hiyo ili kutimiza azma ya Serikali ya

kuwapunguzia vikwazo vya kiuchumi wanufaika wengi zaidi katika kupata elimu bora.

(iii) Serikali iandae mkakati wa kuviwezesha Vyuo kuwa na hospitali za mafunzo kwa vitendo *(teaching hospitals)* kwenye Vyuo Vikuu vyote vinavyotoa kozi za Afya nchini. Mfano, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kinaweza kutumia Hospitali ya Mloganzila kama hospitali ya mafunzo kwa vitendo.

(iv) Serikali iendelee kutenga fedha za uchapaji wa vitabu kulingana na mahitaji ili kuimarisha uwiano wa kitabu na mwanafunzi hadi kufikia uwiano wa kitabu kimoja kwa mwanafunzi mmoja (1:1). Aidha, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia isimamie kikamilifu usambazaji wa vitabu hivyo na kuhakikisha vinawafikia walengwa kama ilivyokusudiwa.

(v) Serikali ifanye jitihada za kuhamisha *capitation grants* ya Shilingi 1,000 kwa kila mwanafunzi wa shule ya msingi na sekondari kwa mwaka, kutoka Fungu 56 - TAMISEMI ambalo halihusiki na Uthibiti Ubora wa Shule na kupeleka Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, ambalo linahusika na Uthibiti Ubora wa Shule.

(vi) Serikali iendelee kutenga bajeti kwa ajili ya kuimarisha mafunzo kazini hususan walimu wa lugha ya alama ili kuwawezesha walimu hao kuwa sehemu ya kukuza ujumuishaji, mtazamo chanya, na mazingira rafiki kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum. Ushauri huu unaendana na mwelekeo alioutoa Mheshimiwa Rais wakati wa Hotuba yake akizindua Bunge la 13:

**Nanukuu,**

*"Tunapotekeleza maendeleo jumuishi, tutaendeleza jitihada tulizozianza za kuwekamiundombinu na vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; pamoja na hao,tutaendeleza fursa muhimu ya kuwasomeshana kujiendeleza kwa watoto wenye magojwa adimu (rare diseases) wanaohudumiwa majumbani."* (uk.12). **mwisho wa kunukuu.**

(vii) Bajeti iongezwe kwa ajili ya utekelezaji wa tamko la kuwarejesha shuleni wanafunzi waliokatiza masomo kutokana na sababu mbalimbali kwa kuzingatia uhamasishaji wa jamii, kuboresha mazingira rafiki ya ujifunzaji, miundombinu inayozingatia jinsia, pamoja na upatikanaji wa huduma za ushauri na unasihi.

## 3.3 Hitimisho

**Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi kwa ajili ya kuwasilisha Taarifa hii. Aidha, Nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa hii yaingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Mhe. Husna Juma Sekiboko, Mb | - | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Cornel Lucas Magembe, Mb | - | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Hamis Shabani Taletale, Mb | - | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Asha Ramadhan Baraka, Mb | - | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Asha Juma Feruzi, Mb | - | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Regina Henry Mikenze, Mb | - | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Asha Juma Kombo, Mb | - | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Dkt. Christine Christopher Mnzava, Mb | - | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Yumna Mmanga Omar, Mb | - | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Kijakazi Yunus Mohamed, Mb | - | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Mohamed Abdulla Makame, Mb | - | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Mabula Johnson Magangila, Mb | - | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Fagason Aron Nkingwa, Mb | - | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Juma Abdalla Juma, Mb | - | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Bakari Shingo Bakari, Mb | - | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Onesmo Merdson Mnkondya, Mb | - | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Baraka Ulimboka Mwamengo, Mb | - | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Isaya Moses Mngurumi, Mb | - | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Dkt. Doto Mashaka Biteko, Mb | - | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Kassimu Amari Mbaraka, Mb | - | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru Mhe. Prof. Adolf Faustine Mkenda (Mb), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia na Wasaidizi wake, Mhe. Wanu Hafidh Ameir (Mb), Naibu Waziri; na Prof. Carolyne Nombo, Katibu Mkuu wa Wizara hii, pamoja na Watendaji wengine wa Wizara kwa ushirikiano mkubwa walioipa Kamati katika kutekeleza majukumu yake na kwa usimamizi mzuri wa majukumu ya Wizara kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya kipekee napenda kuwashukuru watumishi wote wa Ofisi ya Bunge wakiongonzwa na Katibu wa Bunge *Ndg. Baraka Ildephonce Leonard,* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vema katika wakati wote ilipokutana na hata wakati wa utayarishaji wa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii ili liijadili na likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Husna Juma Sekiboko, Mb
**MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA ELIMU, UTAMADUNI NA MICHEZO**
7 Mei, 2026

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Asha Juma Feruz kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Elimu, Utamaduni na Michezo.

Waheshimiwa Wabunge tuwatambue wageni ambao tunao ndani ya ukumbi. Wageni waliokaa Jukwaa la Spika; hawa ni wageni wa Profesa Adolf Faustine Mkenda, Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia tunaye ndugu Alli Issa Alli, Naibu Katibu Mkuu, Wazazi Zanzibar. *(Makofi)*

Tunaye ndugu Kirumbe Ng'enda, Naibu Katibu Mkuu, Wazazi Bara CCM. Wote tunatambua kwamba Mheshimiwa Ng'enda alikuwa ni mmoja wa Wabunge kwenye Bunge la Kumi na Mbili na alikuwa Mbunge machachari sana. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye ndugu Wendi Mombo, yeye Afisa kutoka Benki ya Dunia. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye Profesa Joseph Msambichaka, Mwenyekiti wa Tume ya Nguvu za *Atomic* Tanzania. Karibu sana Profesa. *(Makofi)*

Tunao wageni wengine wa Profesa Adolf Faustine Mkenda, ambao ni Wakurugenzi mbalimbali ndani ya Wizara ya Elimu; Wakuu wa Vyuo na Taasisi zake; Wakuu wa Vyuo Binafsi; Waratibu wa Miradi ya Maendeleo; Viongozi wa Mashirika ya Maendeleo ya Kijamii; Viongozi kutoka Taasisi za Kifedha *CRDB*, *NBC* na *NMB*; Wadau wa Maendeleo katika Elimu; Wamiliki wa Shule na Vyuo vya Kati Visivyo vya Serikali; Wadhibiti Ubora wa Shule; Mwakilishi wa Vyombo vya Habari Nchini; Wanufaika wa Samia *Scholarship Extended;* na Wanachuo wa Vyuo vya Ualimu. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wengine ni wanafunzi kutoka Chuo cha *VETA,* sijui ni cha wapi; Wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM);* Wanafunzi kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Dodoma; Viongozi kutoka Jumuiya ya Taasisi za Elimu ya Juu Tanzania (*TAHLSO*); Umoja wa Wanawake Wamiliki wa Shule na Vyuo vya Kati Tanzania; Sheikh Abid Mahmood Bhatti kutoka Jumuiya ya Waislam wa Ahmadiyya Tanzania; Washindi wa Tuzo ya Taifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu; na Ndugu na Marafiki wa Mheshimiwa Waziri. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wageni sita wa Mheshimiwa George Nattan Malima, wapiga kura wake kutoka Mpwapwa, Mkoani Dodoma. Karibuni sana. *(Makofi)*

Karibuni sana kwenye ukumbi wetu wa Bunge wageni wetu wote kwa ujumla wenu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea sasa na uchangiaji. Tutaanza na Profesa Sospeter Mwijarubi Muhongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Juma Feruz na Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, ajiandae.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia muda wa kuchangia bajeti ya Wizara hii. Labda nianzie mwisho, wakati nikiwa ninachangia nina mapendekezo 14. Kwa hiyo, ukiniona ninafika la 10 unajua ninakaribia kumaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba, hii Wizara tunavyoongelea Dira ya 2050 tulionesha umuhimu wa Wizara ya Nishati na nishati kuhitajika, lakini sasa kuendesha uchumi na hayo tuliyoyatarajia kufika mwaka 2050, kila kitu kipo kwenye Wizara hii. Ni kwamba na watakumbuka kwenye mchango wangu niliwaeleza ile *formular* ya mafanikio na ustawi wa mataifa duniani. Sasa leo siwezi kuirudia kama wamesahau waningoje mpaka wakati wa bajeti ndiyo nitairudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa cha muhimu ni kwamba safari yetu ya 2050 ni lazima tuwe na uchumi unaokua kwa kasi zaidi ya 10% na ni lazima uendeshwe na watu wajuzi *(Knowledge Economy)* bila hiyo hatuwezi kuvuka na hiyo ndiyo China ilifanywa mwaka 1978. Ninakumbuka wakati ninaenda kusoma lugha kule Ujerumani ninakutana na Wachina wamemwagwa huko wengi, kumbe walikuwa wanajitayarishwa kwa ajili ya mapinduzi ya uchumi nchini mwao. Mheshimiwa Waziri unafanya vizuri hii ya kupeleka vijana kwenye vyuo vikubwa vikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni sisi wajibu wetu kutathmini mfumo wa elimu tuliopewa; mfumo wa elimu wa Tanzania mpya ambao tunaishia darasa la sita badala ya darasa la saba. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri nimemfanyia *homework* kumrahisishia majibu. Je, mfumo wetu tuliouchukua ni mzuri? Miaka sita shule ya msingi, miaka minne shule ya sekondari, miaka miwili *high school* na miaka minne chuo kikuu. Waheshimiwa Wabunge na sisi tutathmini. Sasa hiyo kazi

nimeifanya na Watanzania wengi walikuwa na wasiwasi kwamba kuishia la sita huenda ndiyo elimu yetu inaenda kudorora kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya hapo niongee ya jimboni mwangu kwamba, Jimbo la Musoma Vijijini tunaenda vizuri kwa sababu sisi tuna shule za msingi 120, tuna sekondari 32 halafu, tuna sekondari ya amali moja na sasa hivi tunajenga sekondari kila kijiji. Kwa hiyo, ninapeleka shukrani zangu nyingi kwa Serikali na kwa Mheshimiwa Rais kama kweli wanataka tutoe mfano wa elimu bora ni Musoma Vijijini. Tunajenga maabara kwenye kila sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Waheshimiwa turudi kwenye mfumo wa elimu; Tanzania tumeenda sita, nne, mbili, nne, kwa mwaka huu mifumo ya elimu ambayo ni bora kabisa duniani *(Top Performing Education Systems in the World, the best in the World)* ya kwanza ni Singapore yenyewe ina madarasa sita, matatu, matatu, manne (6,3,3,4). Kwa hiyo, mwanafunzi anasoma miaka 12 kabla ya kwenda chuo kikuu. Sisi Tanzania tuna sita, nne, mbili, nne. Kwa hiyo, Mheshimiwa Profesa Mkenda na timu yake hawajafanya vibaya ni sita ongeza nne ongeza mbili, 12. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi ya pili yenye mfumo bora kabisa duniani ni Japan. Yenyewe ina sita, tatu, tatu, nne (6,3,3,4). Ndugu zangu nisiwe ninarudia yaani sita ni *primary school*, mitatu ni *junior secondary school*, mitatu *senior secondary school* na minne *university*, kwa hiyo sitorudia nitaenda kwa hiyo tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Finland ni ya tatu duniani yenyewe ina tisa, tatu, tatu. Yenyewe miaka 12 kabla ya chuo kikuu. Ya nne duniani ni South Korea ina sita, tatu, tatu, nne. Ya tano, ni Canada wanafungana na Switzerland ina sita, sita, nne. Kwa hiyo, ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge na hata kule Musoma Vijijini ndugu zangu walikuwa wanasema Profesa hii ya darasa la sita, ninawathibitishia tuko sahihi, hatujaharibikiwa na kitu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya miaka sita kuna ile ya shule ya awali *kindergarten*. Hiyo inategemeana na umri wa mwanafunzi na ni kama Tanzania ni kati ya mwaka mmoja mpaka miwili kutegemeana

na umri wa huyo kijana anayepelekwa kwenye hiyo shule ya *kindergarten*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kipimo cha pili kama tunaenda vizuri. Hiki ndicho ninaomba Profesa na timu yake hiki hatujakifanya, tukifanye. *Last time* niliwaeleza, lakini ninadhani safari hii, yaani sasa kila mtu anasema ana mfumo mzuri. Sasa upi mfumo mzuri zaidi ya mwingine kimataifa, kuna kupimana na yanaenda kupitia mashindano ya wanafunzi duniani na sisi inabidi tukashindane huko, mfumo wetu hauna matatizo, sasa tuone ubora wake ili tuboreshe na mashindano haya yanafanywa na wanafunzi. Bado, bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya kwanza inaitwa *Program for International Student Assessment (PISA)* miaka 15 wanafunzi wanashindana kusoma hisabati na sayansi; ya pili, inaitwa *Trains in International Mathematics and Science Study*; na ya tatu, ni *Progress in International Reading Literacy Study*. Kwa hiyo, hizi tatu bajeti ijayo ninaomba Mheshimiwa Waziri akija atueleze vijana wetu wameenda huko wamefanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipimo kingine ni kipimo cha kila Taifa lilivyoelimika *(The Most Educated Countries in the World)*. Kwa mwaka huu 2026 ya kwanza ni Canada. Maana yake ni kwamba 65% ya watu wenye umri mkubwa wa Canada walimaliza masomo ya sekondari wakaenda kupata mafunzo, wakapata vyeti baada ya sekondari *(Tertiary Qualification);*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ya pili, ni Ireland; ya tatu, ni South Korea; na ya nne, ni Uingereza na ndiyo mtindo tunaoutumia. Uingereza 54% ya watu wenye umri kati ya miaka 25 na 64 wameenda kupata masomo zaidi ya masomo ya sekondari. Kwa hiyo, hii Watanzania nayo tujipime *Tertiary Qualification* kama tunazo, kwa hiyo, hatujaenda vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaanza mapendekezo; pendekezo la kwanza, kwa Mwaka huu wa Fedha 2025/2026, tuna wanafunzi kutoka *form one* mpaka *form six* milioni 3.43.

Ninapendekeza angalau 50% ya hawa wanafunzi wawe wanasoma masomo ya sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la pili, tujenge maabara kwenye shule zetu zote za sekondari; pendekezo la tatu, na hili ni muhimu. La tatu, hili kwenye kila maabara zetu za sekondari lazima tuwe na *Technicians* ambao ndiyo wanaendesha hizo *experiments* siyo walimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninasoma Mara Sekondari nilikuwa na *Technician*, wakati wote nitakayokwenda kufanya majaribio ananifungulia bila hata Mwalimu kuwepo; pendekezo la nne, tunapaswa kuwa na maktaba zenye kompyuta. Hizi kompyuta ni muhimu kwenye maktaba kwa sababu vinapatikana vitabu ambavyo hununui chochote viko *online* badala ya kung'ang'ana kuagiza vitabu; pendekezo la tano, ni uhusiano...

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ooh ninamalizia. Pendekezo la tano, ni uwiano kati ya walimu na wanafunzi yaani ukubwa wa madarasa yetu. Kwa kuwa fedha ni matatizo turudi ile ya zamani niliyosoma mimi, shule za msingi watu 45 darasani, sekondari 35 na *high school* 25. Hii sayansi ni lazima tutafute walimu wengi wa sayansi kwa sababu ukiangalia *Physics* yenyewe ina *branch* tisa, *Chemistry* ina *branch* 10, Hesabu ina *branch* sita, *Biology* ina *branch* nane. Kwa hiyo, ndugu zangu tunahitaji walimu wengi wa sayansi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pendekezo la sita, tunataka tuwe na *Technical Schools, Secondary Schools* kama ilivyokuwa Ifunda na Moshi. La saba, muhimu sana *VETA* ishuke, kila halmashauri iwe na *VETA* moja. Pendelezo la nane, ninakaribia kumaliza. Pendekezo la nane, tuwe na *Technical Colleges* ambazo tunaita *Polytechnics* ambayo mfano wake ni kama ile ya zamani *Dar es Salaam Technical College*. Pendekezo la tisa, tuwe na vyuo vya aina mbili, vyuo vya kawaida kama vya Dar es Salaam halafu tuwe na...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Profesa muda wako umekwisha.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia tu hapo.

**MWENYEKITI:** Ninaomba umalize.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mwisho kwenye kumalizia, mwisho tuweke hela kwenye utafiti na tutumie *percent* moja ya *GDP*. La kumi na moja, *course take* nilipendekeza lazima iwe *foundation*. La kumi na mbili, Wizara itusaidie Vyama vya Kitaaluma vimekufa nchini yaani kama Vyama vya *Chemists*, vya *Physicists* na *Mathematicians* vifufuliwe. La kumi na tatu, Profesa mhimize sekta ya *universities* zianze kuwa na *endowment*, yaani pesa zilizotunzwa kusaidia mambo ya utafiti na nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukichukua chuo kikubwa kama cha Harvard *endowment* yake (hela iliyotunza kwa matumizi yake) ni dola 55,000,000,000, halafu ukichukua cha Texas wana 45,000,000,000. Kwa hiyo, hivi vyuo viwili vya Marekani, Harvard na Texas vina 100,000,000,000 zimetunzwa zinazidi bajeti yetu ya 95,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ni kwamba Dira yetu ya Maendeleo ili tufanikiwe ni lazima tuwekeze kwenye masomo ya Sayansi. Ni lazima ...

**MWENYEKITI:** Profesa, ahsante sana.

**MHE. PROF. SOSPETER M. MUHONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru sana kwa mchango wako mzuri. Jamani nimemwongezea muda kidogo kwa sababu alikuwa anaongea mambo ya kitaifa.

Sasa ninamwita Mheshimiwa Asha Juma Feruz, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Zeyana Abdallah Hamid na Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera ajindae.

**MHE. ASHA J. FERUZ:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. Kwanza kabisa ninapenda kuchukua fursa hii kuipongeza sana Wizara kwa utekelezaji mzuri wa bajeti inayokwisha. Hakika Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wamefanya kazi nzuri sana na tunaendelea kuwapa ushirikiano tufikishe malengo ya Dira ya 2050.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, nielekeze pongezi zangu kwa Wizara na hasa kwa Mheshimiwa Rais kwa kuweza kutoa fursa kwa upatikanaji na utoaji wa ujuzi kwa vijana katika vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo. Tulikuwa tuna vyuo 1414, lakini sasa tuna vyuo 1446, hii ni hatua kubwa sana. Mheshimiwa Rais ametoa fedha nyingi, amewekeza ili vijana wetu waweze kupata ujuzi na kuweza kujiajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa tuna vyuo vya ufundi 532, lakini tuna vyuo vya ufundi stadi 914. Unaweza kuona ni kwa namna gani sasa vyuo vyetu vimeongezeka, hata *VETA* pia, kutoka *VETA* 80 hadi *VETA* 145. Hakika hii ni hatua kubwa sana, tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais amefanya uwekezaji mkubwa, ambao utakwenda kutatua tatizo la ajira kwa vijana wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipongeza pia Wizara kwa mpango niliouona kwenye bajeti ya 2026/2027, inakwenda kuwekeza fedha nyingi bilioni 250, kwa kuanzisha *polytechnical colleges* tano kubwa maeneo ya Morogoro, Kigoma, Mwanza, Mtwara na Unguja. Hakika wameyaishi maono ya Mheshimiwa Rais, tunawatakia utekelezaji mwema na kwa kutangulia tu niseme hoja hii mimi itaiunga mkono kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niielekeze mchango wangu wa ushauri na maoni katika eneo la Bodi ya Mikopo. Bodi hiyo wakati inaanza ilianza kwa 70,000,000,000 sasa tuna 917,000,000,000 tulikofikia. Mchango wangu ninauelekeza kuhusu mageuzi ya Bodi hii ya Mikopo.

Kweli bodi inafanya kazi kubwa, lakini uhitaji wa wanafunzi kupata mkopo ni mkubwa. Fedha ama ruzuku tunayoipata haitoshelezi kuwapa wahitaji wote. Sasa ninashauri nini kifanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Bodi hii tubadilishe kutoka kwenye Bodi ya Mikopo kwenda kwenye Mfuko, ili tuweze kuipatia sheria Bodi hii au Mfuko huu tutakaouanzisha, uweze kujitanua katika eneo la kupata mapato. Kitendo cha kuendelea kusubiri chanzo kimoja cha fedha kinafanya watoto wa wanyonge, watoto wa wakulima kukosa mkopo. Tukiifanya Bodi hii kuelekea katika Mfuko, kwanza tutaipa nafasi ya kuanzisha vyanzo vyake vingine vya mapato, kwa hali iliyoko sasa hivi bodi haijitoshelezi katika utoaji wa huduma na inategemea ruzuku ya Serikali. Pia, haitumii fursa za wawekezaji na ubunifu za kifedha zilizopo nchini. Hakuna *engagement* ya *private partnership*. Tukifanya hivyo kubadilisha kutoka kwenye Bodi kwenda kwenye Mfuko itatusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuangalie mfano, jana Mheshimiwa Aweso alitupa mfano wa namna Tanga walivyoweza kutumia maji na kuweka *bonds* wakapata faida. Sisi tunaweza kutumia kwenye elimu, lakini pia tuangalie Mfuko wa Bima ya Afya, watu wanawekeza baadaye anaweza kutibiwa. Pia, kwenye elimu mtu anaweza akawekeza kuanzia mwanzo, akaja akatumia mbele kule, lakini pesa ile inavyoingia itaendelea kusaidia watu wengine ambao wakati huo bado wanahitaji mkopo na wakasoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi ada yake ni shilingi milioni nne, lakini bodi inampa shilingi laki saba au laki sita. Mtoto huyu wa maskini anashindwa kuendelea na masomo, kwa sababu ule mkopo alioupata katika ada yake haujafika hata nusu na mzazi hawezi kuhimili hizo gharama. Tunaendelea kusisitiza wanafunzi wasome sayansi, akienda kusoma labda fani za udaktari, ada ni kubwa, kwa hiyo tunakuwa hatumsaidii huyu mtoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni heri sasa tujielekeze mkopo wa wanafunzi. Ninajua katika pesa ya kujikimu ile *boom* wanapata sawa, lakini kwenye ada pesa ni ndogo, wanafunzi wanashindwa kujikimu.

Kwa hiyo, ninashauri hapo kwenye pesa ya ada *atleast* tuwape nusu ya ada, hiyo ndiyo namna ya kumsaidia mwanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili niuelekeze kwa wahadhiri. Wahadhiri waliopo chini ya *TCU* na wahadhiri waliopo chini ya *NACTVET*, wahadhiri hawa wanatofautiana maslahi. Mhadhiri wa *TCU* na Mhadhiri aliyepo chini ya *NACTVET* wanatofautiana hata mshahara, lakini wote ni wahadhiri. Ninazungumza kwa upande wa Wahadhiri Waandamizi, madaktari, *associate professors* and *professors*. Hii siyo sawa, kazi ya hawa watu wote ni kazi tatu za msingi. Kazi ya kwanza ni kufundisha, kazi ya pili ni kufanya tafiti na kazi ya tatu ni kutoa machapisho. Wote waliopo *TCU* na walioko na *NACTVET* wanafanya kazi hizi, kwa nini, kwenye maslahi tuwatofautishe? Mimi binafsi ninaona iko haja ya Serikali kufanya marekebisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu hawa pia wanatofautiana hata kwenye muda wa kustaafu. Hawa watu waliopo chini ya *TCU* wanastaafu wakiwa na miaka 65, lakini yule aliopo chini ya *NACTVET* anastaafu kwa miaka 60. Kwa nini? Ninaomba Wizara ya Elimu washirikiane na Wizara ya Utumishi, kuona ni namna gani eneo hili linarekebishwa. Hii inawafanya watumishi hawa waliopo chini ya *NACTVET* wanakuwa wanyonge, tunawadogosha, lakini tunaamini kwamba taaluma zao zinaisaidia jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hawa wahadhiri ambao wapo chini ya *NACTVET* wakichapisha machapisho yao kwenye tovuti ambazo vyuo viko chini ya *TCU,* machapisho yao yanakataliwa yanakuwa *dropped*. Kwa nini? Si sawa, sisi wahadhiri tunaona hii haiendi sawa. Tuone haja na sababu sasa ya kurekebisha eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia kushauri Serikali itoe jicho la tatu, katika vyuo ambavyo vinatoa kozi ya afya. Nitatoa mfano Chuo cha *MUHAS*, hakina hospitali yake inayoimiliki na ni chuo cha Serikali. Ni kweli wanafunzi wa *MUHAS* wanategemea Hospitali ya Muhimbili na sote tunafahamu kuwa, Muhimbili ni taasisi inayojitegemea na *MUHAS* ni taasisi inayojitegemea. Kwa hiyo, iko haja sasa, ninashauri Serikali ione umuhimu wa kuipa *MUHAS*, Hospitali

ya Mloganzila kama hospitali yao ya mafunzo. Hii itasaidia kuwapa wanafunzi nafasi ya kujifunza kwa vitendo vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, wapo wanafunzi ambao hawawezi kufanya mitihani ya mwisho, wakizuiliwa na uongozi wa vyuo vyao kwa kigezo cha kukosa ada. Hii si sawa. Haki ya mwanafunzi ni katika kusoma pamoja na kufanya mitihani yake. Hili lipo Mheshimiwa Waziri. Vipo baadhi ya vyuo vinazuia wanafunzi kufanya mitihani ya mwisho, *end of semester exams* kwa kigezo cha kwamba hajamaliza ada. Upo mchakato mrefu katika kusoma, kuna *tests,* kuna *assignemts,* walikuwa wapi kuwabana kule. Mwanafunzi akajibana, anafika *end of semester* kufanya mtihani anazuiliwa. Kwa hili, tunaona haliendi sawa na wanafunzi pia waangaliwe, kwa sababu ndiyo wataalam tunaowazalisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine katika eneo hili la wanafunzi, vipo vyuo vinatoa kada ambazo hazipo kwenye Sekretarieti ya Ajira. Mwanafunzi ameomba chuo, Serikali imemkubalia, ameomba mkopo, akapewa mkopo, akasoma akamaliza. Matarajio yake ni kuajirika, anapoingia kwenye Sekretarieti ya Ajira, anakuta kada aliyoisomea haipo. Anayeidhinisha kada hizi ni sisi Serikali, kwa maana ya kwamba Wizara ya Elimu, ndiyo wanatoa ruhusa ya kwenda ku-*implement* ile kozi ambayo inafundishwa kwenye chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe Wizara ya Elimu pamoja na Wizara ya Utumishi washirikiane, zile kada ambazo hazipo kwenye Sekretarieti ya Ajira ziingizwe. Ni maumivu makubwa kwa mwananchi ama mzazi kule kijijini kwetu, ambako anamsaidia mwanafunzi, kuweza kusoma, anamaliza, ana matarajio makubwa, halafu mwanafunzi yule haajiriki inaumiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Dkt. Zeyana Abdallah Hamid, atafuatiwa na Mheshimiwa Ester Bulaya. *(Makofi)*

**MHE. ZEYANA ABDALLAH HAMID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nishukuru kwa kupata fursa hii kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Shukrani zangu nizitangulize kwa Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi Watanzania ni waungwana sana na uungwana anaotuonesha Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwenye kuwekeza kwenye elimu ya mtoto wa Kitanzania, inastahili shukurani za kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mengine yote tuliyoyatamania katika sekta zote hayatafanikiwa, kama hatutafanya kazi nzuri, ambayo Mheshimiwa Rais ametuonesha maono jinsi ya kupita, wapi pa kuwekeza na namna ya kufanikiwa. Niipongeze sana Wizara kwa kutupangia mpango mahususi, mipango endelevu, mipango inayokwenda kumgusa mwanafunzi wa kila rika toka wa chekechea mpaka wa vyuo na vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Wizara kwa kuwa na sisi, katika safari hii ya elimu na hasa tukiangalia mafanikio yaliyofikiwa kwa mwaka uliopita, ambao wametupa *summary* leo, lakini kutuwekea mipango inayokwenda kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027. Sisi Wabunge wa vyuo na vyuo vikuu, tuna jicho la ukaribu sana kuangalia vipi tutaweza kuwawasilishia wananchi na kuiwasilishia Serikali kwa ambayo yanabidi yafike kwa wananchi na sekta ya elimu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaambiwa kwenye vitabu vya Imani, kwamba hawatakuwa sawa, wanaojua na wasiyojua. Quran inasema: "*Qul hal yastawī al-ladhīna yaalamūna wa-al-ladhīna lā yaalamūn.*" Kwenye mafunzo haya tunajiambia, Taifa lililoelewa na lisiloelewa halitakuwa sawa. Nimemwelewa sana Profesa pale alivyotupeleka katika tathmini ya nchi tofauti. Tanzania katika awamu hii, nayo pia imejipelekea katika kuhakikisha tunahama katika Taifa lililokuwa halielewi, na nini tunataka tuelewe, wapi tunataka tuwekeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini, ninaunga mkono hoja hii ya Bajeti ya Elimu? Tumeona namna dira ya Wizara imekwenda moja kwa moja, kutoa Taifa lenye *skill transformation*. Hii nitapita katika vipengele tofauti, ambavyo leo Waziri ametuonesha katika mpango

huu. Tunaipongeza Wizara kwa kutuandalia mpango mahsusi wa vyuo viwanda na waajiri, kwa sababu huku ndiko tunakwenda kulijibu lile suala, vijana tunaowasomesha wataajirika vipi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia kwenye huu mpango, wamelenga kwanza moja kwa moja kwenda kuboresha *curriculums*. Mitaala itakapouliza au itakapohoji, waajiri wanataka nini? Ndiyo tutarudi kuhakikisha tunasomesha kwa malengo na tunawashirikisha vijana wetu, wajitayarishe kujitoa katika vijana wenye malengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango huu umetuletea mfumo mpya wa usomeshaji ambao ni *work based learning*. *Work base learning,* inabinua juu chini, chini juu, elimu kutoka kwenye nadharia kwenda kwenye vitendo na hizi zipo nyingi. Kuna ambazo tutakuja kuziona wakati wanazitekeleza, za *problem based learning* ambayo inachukua tatizo mahsusi kutoka kwenye sekta, linalileta darasani na vijana wetu wanali-*innovate and then* linarudi kwa waajiri kulitekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *learning based models* ambazo zinatestiwa, zinasomesheka vipi na tunachanganya taaluma kutoka nje pia, kuona hizi taasisi zinazoajiri zitawatayarisha vipi vijana wetu. Mpango pia umeona umuhimu wa *innovations* na hivi vitu ambavyo vinabidi vitengewe fedha, saa nyingine vinakuwa ni vya majaribio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Innovations* zinatumia *resource* kubwa za *labs* na tumeona vyuo vingi ambavyo vinahitaji *laboratory* za viwango vya juu, kuweza ku-*test* hizi kazi za wanafunzi, kuweza kupata *data* za namna mafanikio haya yanapatikana. Pia, *information decisiyon making* nazo tumezishuhudia kwenye huu mpango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha inayohitajika kuweka *sustainability* ndiyo ambayo Wizara inatuomba leo tuiwekeze. Sababu nyingine za kuunga mkono hoja, ni kuangalia namna vyuo, hasa vya kati, vya amali, vya mafunzo stadi, ambavyo vimekwenda kuwekezwa. Lile ongezeko la vyuo 32, ni sawa na 84% nayo inawekeza katika kuwajengea uwezo vijana kwa vitendo, namna vilivyotawanywa katika mikoa, wilaya na pia halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona ujenzi wa vyuo vikubwa vitano vya *Polytechnic* na tunaishukuru sana Wizara kwa kutuletea chuo kimoja Zanzibar. Vyuo hivi vya ki-*polytechnic,* siyo tu vinajenga uwezo wa vitendo na elimu stadi kwa ngazi ya kati, lakini kwa hali ya juu ambayo moja kwa moja inaweza kwenda kutumika katika sekta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatuomba shilingi bilioni 250, kwenda kuwekeza katika vyuo hii vya *polytechnic*. Ninaunga mkono hoja na kwa kuangalia zaidi miradi, kuna mradi wa *educational skill for productive jobs*, kuna miradi ambayo tumeiona katika *skills and transformation for regional integration* na miradi hii nayo inakwenda moja kwa moja kuwekeza *skills au study*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikirudia nasaha ambazo Rais, Mheshimiwa Dkt. Ruto alitupa kuhusu maadui wa nchi mbalimbali. Akatuambia kwamba, adui huyu ni ukosefu wa ajira na tukichanganya haya ambayo tumeyaona, ni wazi kwamba, adui siyo tu ukosefu wa ajira, lakini kukosa kutumia rasilimali zetu za nchini kuchanganya na elimu ambayo tunaisomesha ili kutengeneza ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba niunge mkono hoja, kwa sababu tuna kila uwezo wa kutengeneza ajira. Tuna kila uwezo wa kusomesha. Tuna kila uwezo wa kuwekeza na kuiunga mkono sekta hii kwa sababu ya kubadilisha *mindset* za elimu, kutoka elimu nadharia kwenda kwenye elimu ya vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ester Bulaya kama ukiweza kuchangia kwa dakika tano, malizia hizo dakika kama sita.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii ya elimu. Kwanza niwapongeze Mawaziri wanafanya kazi kubwa sana na ni wanyenyekevu akiwepo

na Naibu Waziri, Mjumbe mwenzangu wa Baraza la 2008. Mimi nimekuwa kwenye Bunge hili, nikimaliza hii ni *term* ya nne. Ninaomba niwaambie kama kuna mtu ameleta mapinduzi kwenye sekta ya elimu ni Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa alisema, adui yetu wa kupambana naye ni ujinga, maradhi na umaskini. Hayo yote misingi yake unaipata kwenye Wizara ya Elimu. Kwenye kipindi chote, bajeti hii haijawahi kufika 1,000,000,000,000. Leo tunazungumzia shilingi trilioni 2.3 kwenda kwenye sekta ya elimu. Tunatenga pesa hizi unataka kuelimisha watu wako, kwenye vyuo vikuu vya ndani na nje ya nchi, kwenye vyuo vya kati, kwenye vyuo vya ufundi na kwenye vyuo vya *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni maandalizi ya kujenga Taifa lenye weledi, Taifa litakalojenga nchi yao wenyewe. Kwenye hizi trilioni mbili, trilioni 1.6 ni kwenye miradi ya maendeleo kwenda kuwekeza kwenye elimu, kwenda kujenga Taifa la wasomi, kwenda kujenga vijana watakaojenga nchi yao. Bajeti hii tumesema tunataka kujikomboa kifikra, kwenye pesa zote 359,000,000,000 sawa na asilimia tatu ndiyo inatoka nje, lakini trilioni 2.3 zote ni pesa za ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe kupitia Wizara ya Fedha, tunataka kujenga Taifa letu, kuwekeza kwa watoto wetu kupitia pesa zetu za ndani. Bunge hili, tuiombe Wizara ya Fedha, kuhakikisha pesa hizi zinatoka ili watoto wetu tunaokwenda kuwapeleka kusoma nje ya nchi, kutengeneza wanasayansi, wawe na uhakika wa kwenda, ili mpango wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi, kujenga kampasi kila mkoa, iweze kutekelezwa na kwenye bajeti nimeona inaanza Mara, Tanga na Kagera. Mwanzo wa utekelezaji wa Ilani unaanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Wabunge tuhakikishe tunaibana Serikali itoe hizi pesa, ili dhamira ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kutengeneza Taifa lenye ujuzi, kutengeneza Taifa la wasomi, kutengeneza wanasayansi wetu, ambao ndiyo dunia ilipo.

Kujenga mifumo yetu, ambayo itaendeshwa na watu wetu, ndiyo maana pesa hizi zimetengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninazungumza kwenye mpango, mataifa yote yaliyoendelea yali-*invest* kwenye vyuo vya kati, yali-*invest* kwenye *VETA,* ndiyo bajeti hii inavyosema, ili ule mpango wetu wa Dira ya 2050 ndiyo unaanza kujengwa hapa, kutengeneza vijana watakaopelekwa kwenye viwanda, kuijenga nchi yao. Tunaenda kwenye soko la ushindani wa elimu. Soko la ushindani la kupeleka wataalamu duniani, huwezi ukatengenezwa na nchi nyingine, wanajengwa na Watanzania wenyewe. Ndiyo maana nchi hii, iliweza kutoa viongozi wazalendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Baba wa Taifa ni mtoto wa maskini kutoka pale Butiama aliandaliwa na nchi yake. Hayati Mheshimiwa Benjamin Mkapa ni mtoto wa maskini, kutoka kule Lindi, Mtwara, aliandaliwa na nchi yake, Mheshimiwa Dkt. Jakaya Mrisho Kikwete kutoka Msoga aliandaliwa na nchi yake. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Hayati Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli watoto wa maskini kabisa, waliandaliwa na nchi yao, ni misingi ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumepiga hatua, kwenye Bodi ya Mikopo tumetoka 70,000,000,000 mpaka zaidi ya 900,000,000,000 na kitu. Ninaungana na hoja ya mdogo wangu Asha. Lazima tubadilishe Mfumo wa Bodi ya Mikopo, tutoke kwenye Bodi ya Mikopo uwe mfumo maalum, tutakaoutungia sheria utakaokuwa na chanzo chake. Tuwe tuna uhakika wa kupata fedha, Mheshimiwa Waziri tulifanikiwa hayo kwenye Mfuko wa Maji, tulifanikiwa hayo kwenye Mfuko wa Barabara, tumefanikiwa hayo kwenye Mfuko wa *REA,* tumefanikiwa kwenye Bima ya Afya, tunaweza kwenye elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii hatutakuwa na kusema wale vijana wetu hawarudishi mikopo ya kwa wakati, hawarudishi mikopo kwa wakati kwa sababu walikuwa hawakupata ajira. Haitazuia Mfuko huu usiendelee, kutoa mikopo kwa watoto maskini, kwa sababu tutakuwa tuna uhakika wa kupata pesa nzuri, kupata pesa za kutosha bila kutegemea ruzuku ya Serikali peke yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wengi wa maskini kama hao ambao Mheshimiwa Dkt. Samia, anatoa Samia *scholarship,* wa Manyamanyama, wa Tanga, wa wapi, wote watapata fursa ya kusoma kwa sababu kutakuwa kuna Mfuko Maalum, siyo tu kuanza chuo kikuu na mpaka kumaliza masomo yao. Kwa unyenyekevu mkubwa Waheshimiwa Wabunge, tuiunge bajeti hii ndiyo mpango unaanza kutekeleza Dira, lakini tunatengeneza wataalam wetu watakaolijenga Taifa lao kwa uzalendo mkubwa, kwa sababu hawajasomeshwa wenyewe wamesomeshwa na Serikali yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ester Bulaya.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi hiki cha asubuhi. Tutakaporejea mchana, wachangiaji watakaoanza ni wafuatao:

Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera, Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe na Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima. Wengine tutawatangaza kadiri ambavyo tutakuwa tunaendelea.

Nina tangazo moja, ni tangazo kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, inawatangazia Wabunge wote watakaopenda kusoma kozi fupi ya Diplomasia ya Uchumi na Kikanda, *Regional Integration EAC na SADC,* kwa muda wa wiki moja. Kozi hiyo itatolewa baada ya kipindi hiki cha Bunge la Bajeti kuahirishwa, kama tarehe hazitabadilika, kozi hiyo itatolewa kuanzia tarehe 29 Jumatatu mwezi Juni, hadi Jumamosi tarehe 04 mwezi Julai, mwaka huu.

Itachukua Wabunge 30 tu, kwa hiyo ni *first come, first save,* unajiandikisha kwenye Ofisi ya Katibu wa Bunge. Kozi hii itafanyika kwenye Chuo cha Dkt. Salim Ahmed Salim, pale Kurasini. Mwisho wa kozi kutakuwa na vyeti vinavyotambuliwa kitaifa na kimataifa.

Baada ya matangazo hayo machache, ninasitisha Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.01 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)*

*Mwenyekiti (Mhe. Cecilia D. Paresso) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na majadiliano. Sasa ninamwita Mheshimiwa Dkt. Wilson Charles Mahera.

**MHE. DKT. WILSON C. MAHERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ya kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii ya leo. Kwanza kabisa ninaanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuleta mabadiliko na uwekezaji mkubwa katika sekta ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza pia, kwa kuendelea kumwamini Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Katibu wake Profesa Caroline Nombo na wasaidizi wao kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kusimamia utekelezaji wa sera na mitaala mipya iliyoboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwanza tuanze kwa kukumbushana mwaka 1967, Mwalimu Julius Nyerere alikuja na Sera ya Elimu ya kujitegemea, ambayo lengo lake ilikuwa ni kujaribu kufuta mfumo wa kikoloni tuliokuwa tumeurithi na kutaka Watanzania, Vijana wa Kitanzania, walioelimika waweze kuwa na ujuzi wa kuweza kujiajiri, Ndipo aliposema kijana anapomaliza darasa la saba awe angalau na ujuzi mmoja wa kuweza kuutumia akirudi nyumbani, lakini utekelezaji wa elimu hiyo ya kujitegemea haukuweza kufanikiwa kwa kiasi kikubwa na alipomaliza madaraka ndiyo ikafa kabisa tukarudi kwenye masuala ya nadharia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia malengo yake ya wakati ule ndiyo *valid* mpaka sasa hivi kwa sababu, tunataka kuwa na Dira hii ya Mwaka 2050; tunataka kuwa na Taifa la watu wanaojitegemea, walioelimika na wenye ujuzi mbalimbali na wanaochangia katika kuleta uchumi. Sasa Profesa Ishumi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam alifanya *analysis* hivi karibuni akasema ni kwa nini, kama Taifa, tulishindwa kutekeleza elimu ya kujitegemea. Hatukuweza kuwa na nyenzo iliyoweza kutu-*guide* vizuri tutoke wapi, twende wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani mwaka 2021 alikuta kuna malalamiko. Watanzania wengi walikuwa wanalalamika kwamba, elimu yetu haina msaada kwa vijana, hawapati ajira na hawezi kujiajiri. Ndipo alipoielekeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, chini ya Uongozi wa Mheshimiwa Profesa Mkenda na Katibu wake Profesa Carolyne Nombo, kutafuta nini kifanyike, ili Watanzania waweze kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Mkenda kwa kushirikiana na wataalam wengine wasomi Tanzania, walipitia ile Sera ya Mwaka 2014 iliyokuwa imeshindikana ndiyo wakaja na Sera iliyoboreshwa ya Mwaka 2023; hoja na mitaala imeboreshwa, ambayo inakwenda kuwa mwarobaini wa tatizo la ukosefu wa ajira, kwa hilo, tuwapongeze tuwape maua yao, wengi walishindwa kufanya hivyo. Ukiangalia hata Sera ile ya Mwaka 2014 ilishindwa kutekelezeka kwa sababu, inahitaji matumizi makubwa ya fedha, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kuweka fedha nyingi baada ya kuanza kutekeleza hii sera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninawapongeza hata Wizara hapa leo wamekuja na bajeti ya 2.3 *trillion* na ukiangalia kwa kiasi kikubwa inakwenda katika kutekeleza hiyo sera, wamesema ni miongoni mwa mambo ambayo wanayapa kipaumbele. Baada ya kukubali kuanza kutekeleza ile sera wamewekeza fedha nyingi sana; ile sera, pamoja na mambo mengine inaelekeza uhuishaji wa amali na pia, elimu ibadilike iwe ya miaka 10, lakini ime-*focus* zaidi katika masuala ya sayansi, TEHAMA na hisabati na hayo ndiyo mambo yanayotupeleka kwenye Taifa lenye uchumi. Baada ya kufanya hivyo tayari shule 103 za amali zimeshajengwa kwa zaidi ya shilingi bilioni 90, ambapo Watoto wetu sasa wanaenda kusoma kwenye shule za amali. Kuna shule 158 zinatekeleza mkondo wa amali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia sasa tunapokwenda kwenye hii dira ninatamani nione watu wa Wizara ya Fedha wakiwa humu ndani, pamoja na watu wa mipango kwa sababu, bila kusomesha hawa Watanzania hiyo Dira ya 2050 haitafanikiwa. Hatutaweza kutekeleza Dira ya 5020 kwa kutumia Wachina na Wahindi, tunatakiwa tutumie vijana wetu watakaosoma kwenye *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli Mwalimu Nyeyere aliwahi kusema mficha maradhi kilio kitamfichua kwa hiyo, tukiangalia Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipokuta *VETA* zinasuasua alielekeza shilingi bilioni 100 zipatikane, ili *VETA* hizi ziweze kukamilika. Mpaka sasa hivi tunavyokwenda *VETA* 64 zipo 67% na ile *VETA* moja ya Songea ipo 68%. Fedha bado zinahitajika, bila kufanya maamuzi magumu itafika tena mwaka kesho *VETA* itakuwa bado zipo vilevile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameonesha nia, basi wanasema *great leaders inspires everyone to take action,* kwa hiyo, tunaamini sasa hivi Mheshimiwa Dkt. Samia ametu-*inspire*. Waziri wa Fedha, Waziri wa Mipango na Tume ya Mipango, kama kweli, wanataka Dira ya 2050 iweze kutekelezeka, basi watenge fedha ziende kwenye *VETA*, ili tuweze kuongeza ajira kwa sababu, *five years development plan* inasema tuongeze ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana watenge fedha ziende kuongeza ajira, bila *VETA* kukamilika, ajira hazitapatikana, *VETA* ndiyo habari ya mjini, ujuzi na ajira. Sasa, ili tukamilishe hii awamu tunahitaji shilingi bilioni 38.9 tufanye maamuzi ya makusudi tutenge shilingi bilioni 38.9, ili *VETA* zikamilike, Vijana wa Kitanzania waweze kuzitumia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia Wizara ya Elimu kwa kujenga majengo mengi; madarasa mengi mapya, matundu ya vyoo mengi, kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Pia, maabara nyingi, shule nyingi mpya za msingi, za sekondari na za awali zimejengwa na hiyo imesababisha kuongezeka kwa ajira. Mheshimiwa Dkt. Samia ameajiri walimu wengi wa awali mpaka vyuo vikuu, tuwape pongezi zao kwa kweli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hiyo imesababisha pia, ufaulu na udahili umeongezeka kwa kiasi kikubwa sana. Ukija kuangalia uandikishaji kwenye ngazi ya vyuo vya juu, tumeongeza kwa 43%, lakini ukilinganisha na nchi za Afrika Mashariki, bado tupo chini kwenye *gross enrolment rate*. Sasa nini kifanyike?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuipongeze Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Wizara ya Elimu kwa kujenga *campus* 16 katika kila Mkoa, zitakapokamilika inasemekana zitaongeza *enrolment* ya wanafunzi 100,000. Hii itasaidia sana kuongeza *gross enrolment rate,* ambayo ni *direct repercussiyon* ya *GDP per capita,* kwa hiyo, watu wa Tume ya Mipango na Fedha ni vizuri tukawekeza sana kwenye Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi ni kama unavyojenga ghorofa, msingi wa fedha nyingi za miradi ya maendeleo kwenye Taifa hili miaka mitano hii tuwekeze kwenye Wizara ya Nishati, Wizara ya Elimu, Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Viwanda na *VETA* zetu lazima zisomeshe wataalam, ambao watakwenda kusaidia kutengeneza matrekta, kuwe na ufundi, kwa ajili ya stakabadhi ghalani na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia, Wizara ya Elimu kwa kuja na ubunifu wa kuanzisha *scholarships* mbalimbali; *Samia Scholarship,* wanafunzi zaidi ya 2,000 wanasoma. Hongera sana Mheshimiwa Profesa Mkenda na wenzako. *Samia Extended Scholarship* tumepeleka zaidi wanafunzi nje; Mataifa mengi yaliyoendelea katika kuendeleza *human capital* pia, yanapeleka wanafunzi wengi nje ya nchi. Ninaomba tuongeze fedha, ili wanafunzi wengi zaidi waweze kwenda huko. Pia, ninampongeza kwa kuanzisha *Samia Innovation and Commercialization Fund,* ambayo inasaidia kuboresha ubunifu. Nadhani hii nayo ikiendelea kupewa kipaumbele, italeta mafanikio makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, tunajua kutokana na utekelezaji wa sera, mwaka kesho, mwaka 2028, tunakwenda kuwa na wanafunzi 3,021,177 zinahitajika fedha shilingi *1.77 trillion*. Sasa nimeangalia kwenye Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mamlaka ya Serikali za Mitaa wanatenga shilingi bilioni 136, Serikali Kuu inatenga shilingi bilioni saba. Kwa hiyo, inabidi tujitahidi kuongeza kasi kubwa, ili hizi shule ziweze kukamilika, vinginevyo itakuwa ni tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuhakikisha kwamba, fedha zinapatikana, ili shule ziweze kujengwa. Kwa kufuatia hilo, katika Wilaya yangu ya Butiama, Shule ya Sekondari ya Isaba, Shule ya Sekondari ya Mwibagi na Shule ya Sekondari ya Misanga, tunaomba sana fedha zipatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninarudia kusisitiza kwamba, tuwekeze fedha nyingi kwenye *VETA*, itakuwa mwarobaini wa ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Timida Mpoki Fyandomo, atafuta Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe na Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima na Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, wajiandae.

**MHE. TIMIDA M. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi nami kuweza kuchangia katika hoja hii muhimu ya Wizara ya Elimu, Wizara ambayo kwetu sisi vijana ndiyo daraja katika kufikia ndoto, matarajio na maono yetu. Mnamo tarehe 26 Aprili, 2026, nchi yetu imesherehekea miaka 62 ya Muungano. Ni umri wa mtu mzima, ambaye katika utumishi wa umma anapaswa kustaafu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa miaka 62 nchi yetu imepiga hatua kubwa sana katika eneo la elimu. Tumetoka kuwa na chuo kikuu kimoja cha Dar es Salaam, mpaka kuwa na vyuo vikuu zaidi ya 50. Vilevile tuna vyuo vikuu vya kati zaidi ya 400.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule za msingi na shule za sekondari kuna ongezeko. Hapa ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, katika kipindi cha uongozi wake amejenga shule za sekondari zaidi ya 1,300 na katika kila mkoa amehakikisha kuna shule maalum ya wasichana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia ametutoa kutoka kuwa na shule za amali tano, ametufikisha kuwa na shule za amali 103. Katika shule hizo, shule 29 ni zenye mkondo au mchepuo wa uhandisi. Tunampongeza Mheshimiwa Dkt. Samia kwa sababu, licha ya hayo ameendelea kujenga Vyuo vya *VETA*. Mwaka 2025 kulikuwa na Vyuo vya *VETA* 1,414, lakini mpaka sasa kuna Vyuo vya *VETA* 1,446.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo ameendelea kujenga Vyuo vya *VETA*, sasa kuna ujenzi wa vyuo 64 ambavyo vitafanya idadi kuwa vyuo 145. Sambamba na hilo ninaomba niipongeze Wizara ya Elimu, ninampongeza Waziri, Naibu Waziri pamoja na watumishi wote wa Wizara hii kwa kumsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza maono yake kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mafanikio haya yamesababisha kuwa na ongezeko la wahitimu katika vyuo vya kati na pia, vyuo vikuu, lakini licha ya ongezeko hilo na mafanikio hayo, bado wahitimu wetu wana

changamoto ya ajira na sababu mojawapo inayochangia changamoto hii ni kukosekana kwa ujuzi unaotakiwa katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijaenda kuishauri Serikali yangu ninaomba nikipongeze Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kuja na *program* maalum inayofahamika kama, *Skillika*, ambayo imelenga kuwajengea uwezo wahitimu, ili wawe na ujuzi unaohitajika katika soko la ajira. Sambamba na hilo, ninaipongeza Serikali yangu kwa sababu, imewekeza kiasi cha shilingi 175,000,000,000 katika mradi wa kimkakati wa kukuza ujuzi unaofahamika kama *E-STRIP*. Mradi huu unatekelezwa katika Chuo cha *NIT, DIT* na *ATC*, ninaipongeza sana Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninajikita katika kuishauri Serikali yangu. Kama ambavyo Serikali na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimetuonesha njia ya kuanzisha *program* kama hizi, naishauri Serikali kuanzisha *program* kama hizi katika ngazi mbalimbali za elimu na pia, kutumia wataalam wenye uzoefu na taaluma katika kuwafunza watu ambao tunawategemea, wawe na ujuzi ambao unatakiwa kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea kama Jordan na Singapore wanatumia *industrial driven curricula,* ambapo wao wanafanya *review* ya kozi zao kila mara. Sambamba na hilo wameanzisha baraza la elimu la tathmini, ambapo linafanya kazi ya kutathmini na kutafiti kama ujuzi ambao wanautoa katika vyuo vyao unaendana na kile ambacho kinahitajika katika soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nchi za Ujerumani, Uswiss na Austria nazo zinaenda na *system* inaitwa *duos education model,* ambapo wao wanafunzi wao wanaenda darasani siku nne za wiki, lakini siku tatu wanaenda kufanya *practical.* Hii haiwaongezei ujuzi tu vijana, bali pia, inawasaidia kupata kipato, ili watakapotoka katika vyuo waweze kujiajiri. Sambamba na hilo ninaomba kuishauri Serikali yangu kuongeza asilimia za uwekezaji katika elimu inayotokana na *GDP* ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *UNESCO* inashauri na kupendekeza kwamba, Mataifa yawekeze asilimia nne hadi sita ya pato la Taifa, yaani *GDP,* katika elimu. Mpaka sasa Tanzania tunawekeza 3.3% hivyo, ninaomba kwa unyenyekevu mkubwa, Serikali yangu iweze kuongeza kiasi cha kuwekeza katika sekta yetu ya elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee suala zima la wahitimu wa shahada ya uzamili ambayo inatokana na *career path*. Tumekuwa na mtazamo wa kwamba, wahitimu au wataalam hawa wanatakiwa kuwa na taaluma moja kwa muda mrefu, lakini tumesahau kwamba, changamoto za kisasa zimekuwa zikijikita katika taaluma mbalimbali hivyo, ninawaomba waajiri na taasisi zetu, pale ambapo mtu anaenda kujiendeleza kupitia shahada ya uzamili, basi wasiyone kama amepoteza mwelekeo wa taaluma kwa sababu, tunahitaji watu ambao wako *multiskilled,* lakini pia, wako *multidisciplinary,* ili waweze ku-*solve* matatizo ya wananchi kwa mitazamo mipana zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipongeza Serikali kwa kuendelea kujenga Vyuo vya *VETA*. Ninazidi kuihimiza Serikali, ajira nyingi zinatokana na sekta ya uzalishaji, sekta ya ufundi na pia, sekta ya ujenzi; ajira hizi zinahitaji watu ambao ni ma-*technician,* watu ambao wana ujuzi wa vitendo na mafundi *study*. Hivyo tukiendelea na kufanya mchakato wa kujenga Vyuo vya *VETA* ndani ya muda mfupi tutasaidia vijana wetu kupata ajira za haraka kwa kipindi cha muda mfupi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, ninaunga mkono hoja na ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Cornel Lucas Magembe.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaanza kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi, ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii ya elimu, ambayo tunajadili kupitisha bajeti yake. Kwanza ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye kwa kweli, kwa kiwango kikubwa ameifanya Tanzania sasa imekuwa ni miongoni mwa nchi ambazo Kimataifa zinaonekana zinakwenda kasi katika hii sekta ya elimu. Tunamshukuru na kumpongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninaomba nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda Pamoja, Naibu Waziri wake, pamoja na watendaji wote wakiongozwa na Katibu Mkuu. Kwa kweli, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Elimu, Waziri pamoja na wasaidizi wake wamekuwa wakitoa ushirikiano mkubwa sana kwetu sisi Kamati, lakini kwa niaba ya Bunge zima ambalo sisi ni wawakilishi wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kazi yao wanayoifanya, ukienda kupitia mambo ambayo wameyaleta leo hapa Mezani kwa kweli, hata hizi fedha shilingi trilioni 2.3 ambazo wanaomba tuziidhinishe zikawe matumizi katika Wizara hii, mimi binafsi naona bado ni kidogo sana. Kama inawezekana, basi ninaomba Bunge lako hili Tukufu liangalie namna nyingine na kuishauri Serikali itafute fedha nyingine ya kuiongezea Wizara hii kwa sababu, ina mambo makubwa inayokwenda kutekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya Sita ilipoingia madarakani toka mwaka 2021 ukienda kule vijijini mabadiliko ambayo utakutana nayo kwenye vijiji vyetu na kwenye Kata zetu ni mambo ya kupigiwa mfano ambayo hayajawahi kutokea toka tumepata uhuru katika nchi yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kuangalia shule za msingi ambazo zimeanzishwa mpya bila *involvement* ya mwananchi mwenyewe kuchangia fedha yake ni shule nyingi sana huko tunakotoka. Ukienda pia kwenye shule za sekondari kwa maana ya sekondari mpya pamoja na madarasa ambayo yamejengwa na miundombinu mingine kwa kweli Serikali ya Awamu ya Sita imefanya kazi ya kutukuka na ya kupigiwa mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kikubwa zaidi ambacho kimefanyika ni kuja na mpango huu wa kuhakikisha kwamba kila wilaya tunakwenda kupata *VETA* na ambayo leo hapa tulikuwa tunaambiwa zaidi ya vyuo

64 ambavyo vinajengwa na vinaelekea kwenda kukamilika viko karibu 67%, viko kwenye hatua nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nikuhakikishie na kulidhbitishia Bunge lako Tukufu kama Mjumbe wa Kamati ile, tumekwenda tumeona kwa macho kazi nzuri ambayo inafanyika ika katika miradi hiyo na *insha Allah* inakwenda kukamilika, ninadhani baada ya kupata kazi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Chato ni moja ya Wilaya ambazo zimenufaika na mipango mingi ya Serikali ya Awamu ya Sita. Chato imepata shule nyingi za sekondari, imepata shule nyingi za msingi, lakini tumekwenda mbali zaidi sisi tumepata *VETA* kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule hizi za sekondari zilizojengwa nitoe ushauri kwa Wizara, ni kwamba tumejenga sekondari nyingi, wananchi maeneo mengine wamehamasika wameanzisha shule za sekondari, lakini katika sekondari hizo ambazo zimejengwa na wananchi pamoja na zilizojengwa na Serikali, sekondari hizi hazina maabara katika shule zenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niishauri Serikali na Wizara yenyewe kwamba tukitaka kufanya vizuri na kupata vijana ambao watakuwa ni wazuri watakaokwenda kwenye vyuo vyetu vile vya *VETA* ambavyo vimeanzishwa kwa wingi, tunaomba Wizara ijikite kwenda kukamilisha maabara zinazokosekana katika sekondari zile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika Jimbo langu la Chato Kaskazini, kwenye Kata 14 ninazo shule zaidi ya shule 19 za sekondari, katika shule 19 zile shule 12 hazina maabara kabisa. Shule zile zimekuwa zikifanya vizuri zimekuwa zimeanza kufanya kazi, leo ni miaka mingine takribani miaka mitano, miaka minne na kadhalika. Sasa ninaomba Wizara sana kwamba wakati inakwenda kupeleka pesa zile za matumizi kwenye shule hizi, kwenye sehemu ya sekondari. Ninaomba katika shule hizi zifuatazo katika Jimbo langu la Chato wazingatie kuziletea maabara ili watoto wale waweze kupata elimu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule ya kwanza ambayo ina tatizo kubwa la maabara ni Shule ya Sekondari Mwelani, Shule ya Sekondari Mkungo, Shule ya Sekondari Bukamila, Shule ya Sekondari Nyambiti, Shule ya Sekondari Itale, Shule ya Sekondari Rubambangwe, Shule ya Sekondari Katende, Shule ya Sekondari Ilyamchele, Shule ya Sekondari Buhingo, Shule ya Sekondari Kasenga, Shule ya Sekondari Nyambogo na Shule ya Sekondari Nyamirembe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wakati unakwenda kugawa fedha hizi na ninaomba kwenye shule zile tuweze kupata angalau tujenge maabara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu mwingine kwa Wizara ni kukamilisha ile miradi ambayo imeanzishwa na Wizara. Iko miradi mingi ambayo imeanzishwa imepeleka fedha nyingi. Kwa mfano, pale Chato kulianzishwa shule ya watoto wenye mahitaji maalum, ile shule imepeleka zaidi ya bilioni nne ambazo zimetumika, leo hii ni miaka mitatu shule ile imeshindwa kufunguliwa kwa sababu tu imekosa shilingi 900,000,000 lakini shilingi 400,000,000,000 imekwishatumika, shilingi 900,000,000 ndiyo imekosekana ya kwenda kukamilisha shule ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Waziri kwamba wakati unakwenda ku-*wind up* utueleze watu wa Chato, shule ile ni ya watoto wenye mahitaji maalum kwa Tanzania kwa sababu ziko shule tatu tu ambazo zilianzishwa katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale watoto wanahitaji kusoma, lakini leo ukienda kwenye shule ile majengo yameanza kuchakaa. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anakwenda ku-*wind up* ahakikishe kwamba anatueleza hiyo shule ya Chato inakwenda kuanza kufanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye miundombinu na kwenye maeneo ambayo ujenzi ulikuwa umeshaanza, Mkoa wa Geita hatuna tawi la chuo kikuu, lakini kulikuwa kumeanzishwa na Wizara kwenda kujenga Tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pale Chato kwenye eneo la Kasagara, lakini mpaka sasa hivi nikwambie yule

mkandarasi aliyekuwa amepewa kazi hiyo ya kwenda kuanzisha ujenzi wa chuo kikuu kile alishabeba mitambo, alishabeba kila kitu akaondoka, ameacha eneo lile. Eneo lile lilichukuliwa kwa wananchi na wananchi wakapata fidia yao, lile eneo sasa wanataka wananchi kuanza kuvamia na kwenda kuendeleza shughuli zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe sana Mheshimiwa Waziri kwamba, tawi la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam linapaswa lijengwe pale Chato, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja basi atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba yake pia Mheshimiwa Waziri amezungumza kwamba wanakwenda kuanzisha maktaba, Chato kulianzishwa ujenzi mkubwa wa Maktaba ya Taifa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja. Maktaba kubwa ya Taifa ilianzishwa pale, ambapo maktaba ile itakapokwisha itasaidia watu wengi na wanafunzi wengi kutoka kwenye shule nyingi ambazo zinazunguka Mji wa Chato na vyuo vikuu ambavyo tunatarajia kuvianzisha pale, kipo Chuo cha *IFM*, kipo Chuo cha Utumishi wa Umma.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ahsante kwa mchango wako.

**MHE. CORNEL L. MAGEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Nilimtaja Mheshimiwa Dkt. Regina Christopher Malima, ajiandae Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa.

**MHE. DKT. REGINA C. MALIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia hotuba muhimu sana katika Wizara ya Elimu na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kabisa kupongeza wasilisho ambalo limefanywa na Mheshimiwa Waziri. Hongera sana kwa Mheshimiwa Waziri Profesa Mkenda pamoja na Msaidizi wake, Mheshimiwa Wanu na timu yote ya wataalam katika Wizara hii. Zaidi ninamshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuleta mageuzi makubwa katika sekta ya elimu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna uwekezaji mkubwa ambao wananchi wanapaswa kufahamu ambao umefanyika katika sekta ya elimu, basi ni Wizara hii kuchukua jukumu kubwa la kuleta mageuzi katika sekta ya elimu nchini. Mengi yamesemwa na Wabunge wenzangu na sintotaka nirudie sana, lakini niendelee kupongeza juhudi za Wizara hii katika kupanua miundombinu kupitia Mradi wa *HEET (Higher Education for Economic Transformation)*. Mradi huu unatekeleza ujenzi wa *campus* mpya 16 katika nchi yetu. Hili ni jambo la kupongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo hivyo tu, kuna kozi maalum ya kuwainua wanawake wanaotoka kwenye mazingira au kaya maskini kupitia Mradi huu wa *HEET*. Mradi huu katika kuendesha programu hii wanashirikiana na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Mpaka sasa wanafunzi zaidi au vijana zaidi ya 711 wamenufaika na 137 wanatokea Zanzibar, jambo hili ni la kupongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nina hoja mbili tu na kama muda hautaruhusu nitaleta hoja binafsi kwa ajili ya haya ambayo ninataka kuyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza kabisa ninatambua Wizara hii ipo katika kupitia Sera ya Elimu ya Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023 pamoja na mapitio ya sheria na mitaala. Kama tunavyofahamu nchi yetu iko katika changamoto ya mmomonyoko wa maadili, jambo hili linapaswa kuchukuliwa kitaifa, ajenda hii ni ya msingi sana kuitazama katika jicho la kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba tu Wizara hii kupitia wataalam wake pamoja na taasisi nyingine zilizoko chini ya Wizara

kuanzishwa rasmi kwa somo la maadili kama somo linalojitegemea katika mfumo wa elimu. Kwa nini ninasema hivyo? Tafiti zinaonyesha kabisa kwamba nchi yetu iko kwenye mmomonyoko mkubwa wa maadili, tunafanya nini kunasua kizazi chetu kutokana na changamoto hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya juhudi kubwa sana katika kutengeneza miundombinu, katika kuboresha mambo muhimu katika sekta ya elimu, lakini haya yote yatakuwa bure kama maadili tuliyonayo katika Taifa hili kwa sasa yataendelea kubaki hivyo. Kwa hiyo, niseme tu kwamba kuna mwenendo wa maadili ambao siyo mzuri katika jamii na tafiti zinaonyesha, lakini pia tunaona nidhamu, vitendo vya rushwa, vitendo vya rushwa hivi haviji kwa bahati mbaya, hivi ni mwendelezo tu wa tabia ambazo yumkini mtu hakupata malezi katika utoto wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masuala ya uadilifu na uzalendo yote haya yamekosekana katika nchi, elimu bora bila maadili ni bure. Kwa maana hiyo, ninapendekeza katika Wizara hii rasmi tuweke somo la maadili kama somo linalojitegemea. Niombe Wabunge wenzangu waniunge mkono katika hili kwa sababu bila maadili nchi yetu itaendelea kupata shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia vitendo mbalimbali ambavyo Serikali inatengeneza miundombinu, lakini vijana wanaharibu, hili siyo jambo la kufumbia macho. Niombe Wizara ya Profesa Mkenda iliangalie jambo hili kwa umakini na somo hili liwe ni somo la lazima katika ngazi ya elimu ya msingi, awali lakini pia sekondari na hata vyuo lijitegemee, liwe na maudhui maalum ambayo yataonesha namna ambavyo jamii au vijana wetu na jamii kwa ujumla wanaopaswa kuwa na kuna faida nyingi tu katika kuweka somo la maadili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi ambazo zimeendelea sana baada ya kuwa na mifumo kama hii, Profesa Muhongo aliongelea habari ya nchi kama Japan, Singapore, South Korea, kuna Finland. Nchi hizi ni nchi ambazo zimeendelea, wana somo la maadili katika

mitaala yao na linajitegemea kwa namna fulani na limeleta heshima kwa hizi nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mifano Barani Afrika tunayo Nchi ya Rwanda, Nchi ya Rwanda sasa hivi wana somo linaloitwa *values and ethics*. Pia tuna Nchi ya Kenya wana somo linaitwa *life skills education*. Tuna Nchi ya *South Africa* wana somo linaitwa *life orientation*, Nchi ya Ghana hawa wana somo linaitwa *religious and moral education*. Yote haya yametengeneza msingi wa maadili katika nchi yao na tumeona namna ambavyo wanapiga hatua katika masuala ya maadili na namna ambavyo vijana wameendelea kuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipendekeze somo la maadili liwe ni somo, lazima katika mfumo wetu wa elimu na kuanzia sasa Wizara ijipange tu, nitaleta hoja binafsi kama ambavyo nimesema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la ubora wa elimu. Ubora wa elimu uko katika nyanja mbalimbali, lakini tumeona namna ambavyo Serikali imejipanga au imeboresha miundombinu na mambo kama hayo, lakini bado kuna changamoto kwa wahadhiri au wakufunzi wetu. Wabunge wenzangu walielezea hiyo kwa upana zaidi, lakini niendelee tu kusisitiza, bado tunahitaji motisha kwa wahadhiri na wakufunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini ninasema hivyo? Hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonyesha namna ambavyo *enrollment* ya wanafunzi imeongezeka, lakini bado hatuoni namna ya ku-*balance workload* ya jambo hili. Kwa hiyo, niombe Mheshimiwa Waziri na hili nalo alifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niunge hoja hii mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Agnes Mathew Marwa, ajiandae Mheshimiwa Kassim Haji Kassim.

**MHE. AGNES M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Nianze moja kwa moja kwa kumpongeza sana Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa jambo zuri analolifanya la kutoa *scholarship* kwa masomo ya vyuo vikuu nje ya nchi na ndani ya nchi kwa watoto na hasa watoto wa maskini wasiyojiweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, ninampongeza sana Waziri Profesa Mkenda na Naibu wake pamoja na Wizara nzima kwa kazi nzuri wanayoifanya na hasa kwa ubunifu walioufanya wa huu mpango wa *SIS (School Information System)*. Hiki ni kitu kizuri kilichofanyika cha kwamba mifumo inasomana, kila shule nchi nzima wanakuwa wanaona kwamba hapa kuna walimu kiasi fulani, hapa kuna jambo fulani linalohusiana na elimu, huu ubunifu kwa kweli ni mzuri sana na ni ubunifu unaostahili kuendelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe kutokana na ubunifu huo, Mkoani kwangu Mara imekuwa ni sehemu ambayo tuna malalamiko ya muda mrefu ya walimu, walimu ni wachache sana na hasa kule Jimbo langu la Musoma Vijijini, kwa kweli walimu ni wachache sana wanafunzi ni wengi mno. Naamini kabisa hiki kilio yawezekana kwa vijijini ni maeneo mengi nchi nzima, kwa hiyo niombe jambo hili lifanyiwe kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika masomo ya biashara pia kumekuwa na wimbi la ukosefu wa ajira. Ni ukweli usiyopingika ni kwamba hawawezi watu wote wakaajiriwa Serikalini, kutokana na hili ningeomba somo la biashara liwe ni somo muhimu sana kuanzia chini mpaka juu kwa maana ya kuwajenga Watanzania au vijana wetu wa Kitanzania kwenye soko la ajira wanapomaliza elimu za juu basi wanaweza kujiajiri wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hili ninamshukuru sana Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kutoa ajira nyingi sana kwa walimu, kwa kweli ametoa ajira nyingi sana kwa walimu, Mwenyezi Mungu ambariki sana. Ninaomba Wizara iangalie kwa undani zaidi kuna vijana ambao wamesoma masomo ya biashara na wako mtaani hawana kazi, basi waangalie mpangokazi wa

kuwatengenezea ajira vijana hawa, wawashindanishe hili na wao sasa waende kufundisha somo hili la biashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa walimu, kuna changamoto kubwa sana ya kupandishwa madaraja, kupewa posho zao, lakini pia walimu wanacheleweshewa mishahara. Niombe suala hili Wizara ilifanyie kazi. Kwa kweli walimu hawa jamani ni watu ambao tunapaswa kuwajali sana. Tunapaswa kuwa-*motivate* kwa kila hali kwa sababu ni watu ambao wanatutunzia watoto wetu, tena kwa kipindi hiki kwa karne hii, Walimu wamekuwa sasa kama walezi, mtoto wa miaka mitatu anapelekwa shule. Kwa hiyo, niombe Wizara iwaangalie walimu kwa jicho la ziada.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walimu hawa mazingira wanayoishi na hasa kwa jiografia ya Mkoa wangu wa Mara, kwa kweli jiografia imekaa vibaya, wanakaa mbalimbali. Mwalimu anafundisha Nyamitwe B, lakini anakaa umbali wa kilometa 10 kutoka pale anapofundishia. Kwa hiyo niombe Serikali iangalie jinsi gani ya kuwakopesha usafiri wa bei nafuu ili na wao waweze kufika kwa wakati, lakini wanapofika shuleni angalau na wao wanakuwa tofauti na wanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwalimu akifika shuleni ukimwangalia miguu ana vumbi ndugu zangu, tuwaonee huruma walimu hawa kwa sababu wanafanya kazi ngumu sana. Pia tuwakumbuke kwenye *hardship allowance* yaani posho inayotakiwa katika kufanya kazi kwenye mazingira magumu. Walimu wao wamekuwa wakituomba na hasa mimi pale Musoma Mjini katika Jimbo langu pendwa, walimu nilikaa nao siku moja wakaniomba, wakaniambia Mheshimiwa nenda katuwakilishie hili jambo kwamba na sisi tunaomba basi japo watujali tunapofanya kazi kwenye mazingira magumu na sisi kama walimu tupate angalau *allowance* kwa ajili ya mazingira magumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hili jambo la Sera ya Elimu ya Mwaka 2023 la kuongeza ufaulu, ni jambo zuzuri sana na limekwenda vizuri sana lakini kuna mikoa kama Mkoa wa Simiyu, Mkoa wa Mara, Mkoa wa Geita kwetu bado watoto wanarudi mchana nyumbani na jioni wanarudi tena shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili kwa kweli limekuwa likishusha sana ufaulu wa watoto wa shule; ukizingatia huko njiani, na hasa kwa wale ambao walinichagua mimi, wanawake; watoto wetu wa kike, wanapata majaribu mengi sana kutokana na hali hii kutokana uwepo wa bodaboda huko njiani. Hivyo, watoto wengine wanaweza wakashawishiwa kwa chipsi huko njiani kabla hawajafika nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Serikali iangalie namna ya kukaa na wazazi, wazazi wachangie kiasi fulani; lakini pia na Serikali i-*top-up* ili kusudi watoto hawa wapate chakula, wasiwe wanarudi nyumbani mchana na kurudi jioni. Kwa hiyo niombe sana sana sana, niombe sana Serikali iwaangalie walimu hawa kwa jicho la kipekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia kwa kusema, Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa kweli ni mama mzazi, ni mama ambaye ametuonyesha kwamba anapenda sana kuipandisha elimu ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niwaombe sana, ndugu zangu, ndugu zangu, Wizara husika, ninaamini kabisa liko pale jembe letu; Mheshimiwa Wanu, mchapakazi kabisa, anaonekana kila siku kazini; vilevile yupo kaka yetu Profesa Mkenda, kwa kweli ni wachapa kazi kwelikweli. Ninaomba waliangalie hili jambo ili wamsaidie mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuipandisha elimu hii walimu waangaliwe wapewe kipaumbele. Walimu wakipewa kipaumbele angalau wakawa vizuri na wao, ninaamini kabisa hata watoto watakuwa wanawaangalia vizuri, hawatakuwa wanawaza mawazo ya *tuition* na vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishukuru sana Serikali yangu ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali sikivu; ninaamini kabisa kupitia mpango huu wa mama yetu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan elimu itakwenda juu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja asilimia mia kwa mia. Mungu awabariki sana, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Kassim Hassan Haji; Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila na Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga wajiandae.

**MHE. KASSIM HASSAN HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia Wizara hii yenye dira na taswira ya wanafunzi wenzetu; wanafunzi ambao tunaamini katika bajeti hii wanakwenda kupata maendeleo makubwa zaidi, hususan katika trilioni ambazo ameziweka Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshauri Mheshimiwa Waziri. Bajeti hii ni kubwa sana na bado katika maeneo ya vijijini tuna majengo ambayo hayajamalizika, majengo ambayo hayana ubora. Kwa hiyo nimwoombe sana Mheshimiwa Waziri, kwamba fedha hizi zitakapoingizwa aende akakamilishe majengo yale ili wanafunzi hawa waweze kusoma katika maeneo ambayo yatakuwa mazuri na maeneo ambayo yatawasaidia hata walimu kufanya kazi zao vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru kwanza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametoa nafasi za walimu 12,678, si jambo dogo katika kuboresha mambo ya elimu. Lililobaki sasa kwao Mheshimiwa Waziri ni kwenda kuboresha mambo mazima ya walimu wenyewe. Waende wakawaboreshee posho zao, waende wakawaboreshee angalau na wao wapate motisha ya kwenda kutembea katika maeneo mengine, ili haya mambo yaweze kwenda vizuri na watoto wetu wapate elimu nzuri ili na wao waweze kuwa na nguvu ya kufanya kazi zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo moja leo inabidi hapa nilizungumze kidogo. Mimi na Mheshimiwa Waziri tunakaa jirani pale, hebu kesho au kesho kutwa, atoke saa kumi na mbili. Sisi tunaokwenda mazoezi huwa tunawaona watoto wale wa *kindergarten,* wanatolewa majumbani na mabasi saa kumi na mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende tukaangalie hii sera kwa kweli. Hawa watoto wadogo ambao wako *KG 1, KG 2* kutoka saa 12.00, hata kama ndiyo tunatengeneza watu wazuri, lakini kwa wao ninaona

bado. Twende tukaangalie hii sera ya kuona wao angalau waweze kutoka saa 4.00 kwenda shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ninaomba nigusie suala dogo tu; ninaomba twende tukaangalie sana, twende tukawashauri wenzetu wa Zanzibar, katika sera nzima ya kwao ya elimu ya amali iweze kuungana na *VETA*. Kuna tatizo, bado watoto ambao wanamaliza katika vyuo vya amali Zanzibar, wanapokuja kufanya *application* katika sehemu za kazi bado ni tatizo katika vyeti vyao. Vyeti havisomani na mifumo ya vyeti bado haijawa sawa. Nimwombe sana Mheshimiwa, wafanye kama *memorandum* au jambo lingine lolote ambalo linaweza likawasaidia na wao waendane na elimu hii elimu ya *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeanzisha vyuo vya amali. Vyuo vya amali hivi kwetu tunaona ni taswira nzuri, vilevile vitaleta tija kwa sababu wengi wao ambao wanamaliza katika vyuo hivi wanaenda kujiajiri wenyewe bila kupitia katika ajira za Serikali. Nimwombe sana Mheshimiwa wavisaidie vyuo hivi. Wamezungumza hapa, hapa, na wamesema kwamba wanakwenda kuvijenga, na wanakwenda kuvimalizia. Siyo kuvijenga na kuvimalizia, tuviwekee na vifaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi dunia iko katika utandawazi, watu wanaenda katika *TEHAMA;* twende tukawasaidie hawa, angalau wanapomaliza katika vyuo hivi basi na wao waweze kujiajiri bila kutegemea Serikali hizi ziwape ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine la msingi kabisa; kuna watoto ambao wanafanya michezo ya UMISETA na UMITASHUMTA. Tumezungumza hapa, kwamba tunatengeneza shule nyingi za vipaji, shule nyingi za mikoa, na shule nyingi za wilaya; Mheshimiwa Waziri hebu akajikite sasa kuweka shule hizi za vipaji maalum kwa watoto hawa ambao tunawategemea katika michezo katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano imeanzishwa shule ya Malya, kuna watoto ambao wanakwenda katika michezo ya UMISETA na UMITASHUMTA wako ambao tunawapa zawadi kwa sababu wao ni watoto waliofanya vizuri. Watoto hawa tuwachukue, kutokana na

vipaji vyao tutengeneze kanda ambazo zitakwenda kusaidia vipaji hivyo ili na wao waweze kujiajiri baada ya kumaliza katika shule hizo na waendeleze vipaji vyao. Kama tunavyojua sasa hivi vipaji ni ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia, kwa kuzingatia hoja hizi ninaomba bajeti hii, Waheshimiwa Wabunge wenzangu, ipewe kipaumbele cha kutosha ili kwenda kuweka mfumo mzima wa elimu katika ubora. Vilevile, tumsaidie Mheshimiwa Rais ili maono, dhamira na matakwa yake ya kusema kwamba, sasa hivi tunakwenda kulifungua Taifa letu na kwamba elimu ndiyo iwe kila kitu, basi twende tukaipitishe bajeti hii kwa nguvu zote na kwa umoja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ninakushukuru Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa namwita Mheshimiwa Mabula Johnson Magangila.

**MHE. MABULA J. MAGANGILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii. Nami ninaomba nianze kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan; vilevile Waziri, Mheshimiwa Profesa Mkenda pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Wanu Hafidh; kwanza kabisa kwa kuamua kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa sera hii, ni mageuzi makubwa yanayomgusa kila Mtanzania; na hii inathibitisha kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania humgusa kila Mtanzania. Utekelezaji wa elimu ya lazima ya miaka 10, kwa kweli hatuwezi tu kujua ni kwa namna gani Mheshimiwa Rais amekwenda kutatua tatizo la watoto waliokuwa wakifika darasa la saba wanakwenda kuolewa; tatizo la watoto waliokuwa wanashindwa kumaliza sekondari kwa sababu ya umbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunapokwenda kutekeleza elimu ya lazima, maana yake ni kwamba Mheshimiwa Rais Samia amekwenda kukubaliana na kutekeleza sera ya sekondari kila kijiji.

Awamu ya Nne ilitekeleza sekondari kila kata, leo hii kwa sera hii tunakwenda kutekeleza sekondari kila Kijiji; ambapo mtoto akiingia darasa la kwanza, anatoka akiwa *form four.* Jamani! haya ni mageuzi makubwa mno. Mheshimiwa Rais amechukua maamuzi makubwa mno ya kuwasogezea huduma watoto wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kule jimboni kwetu bado watoto wetu wanasafiri kilometa 10 hadi 15 kwenda kutafuta sekondari. Mtoto kutoka Matinje kwenda Butondoro; kutoka Nyangarata, Kalole, aende Lunguya. Kutoka Mwankima, Igungu aende Mwaruguru ni umbali mrefu mno. Mtoto huyu kwa mazingira ya kawaida hawezi kumaliza shule. Wanaanza 100 wanamaliza 60. Kwa mazingira haya na kwa mageuzi makubwa haya tuna uhakika wa watoto wetu wengi sasa wanakwenda kupata elimu ya sekondari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mageuzi ya kuamua kujenga *VETA* kila wilaya; ujenzi wa *VETA* kila wilaya; na Waheshimiwa Wabunge ninaomba niwaambie, kwamba *VETA* hizi si zile *VETA* ambazo zilipendwa; ni *VETA* ambazo zimewekewa miundombinu ya kisasa. Mimi ni mjumbe wa Kamati hii, nimetembelea hizo *VETA* hata mimi nilikuwa siamini, lakini ukifika VETA zetu sasa hivi zinachukua watoto wa aina zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekwenda kwenye *VETA* unakuta mtoto ni mlemavu hana mikono yote, lakini leo ni *architecture,* anachora ramani za majengo. Haya yanawezekana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kwa hiyo kwa kweli niipongeze sana Serikali hii ya Awamu ya Sita kwa kuamua kutekeleza sera hii ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa kampasi za vyuo vikuu katika mikoa yote ambayo haina vyuo vikuu; jamani, haya yanawezekana kwenye awamu ya sita pekee yake. Idadi hii ni kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwetu sisi Jimbo la Msalala tumepata angalau *Training Center* ya wachimbaji wadogo pale Segese ambayo inatokana na Serikali hii hii. Kwa hiyo, niseme tu kwamba

tuendelee kuipongeza Serikali na kuendelea kupitisha bajeti hii kwa kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wito wangu sasa, TAMISEMI wauchukue utekelezaji huu. Kwetu sisi ukizungumza, tuna shule za msingi 122, tuna sekondari 26 pekee yake. Kwa utekelezaji wa sera hii wa sekondari kila kijiji, tunahitaji madarasa mapya 166, ambayo leo hii kwenye shule za msingi tuna watoto 92,000, sekondari tuna watoto 15,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea na utekelezaji wa sera hii, sekondari mwaka 2028 kuna watoto 17,000 wanaingia *form one*. TAMISEMI wasikie na waanze utekelezaji sasa, tusisubirie mwaka 2028, tutafeli. Idadi hii ni kubwa mno, mageuzi haya ni makubwa mno, ni lazima tuone umuhimu wake. Jambo hili haliwezekani likarudi nyuma, haya ndiyo maendeleo na hii ndiyo kazi na utu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokuwa na Taifa lililoelimika kuanzia chini Taifa linaloajirika; mageuzi haya yanakwenda kutoa ajira kwa vijana wetu waliohitimu fani ya ualimu ambao walikuwa wamekata tamaa; mageuzi haya yanahitaji walimu 40,000, ni ajira za kutosha kwa Watanzania ambao walikuwa wanajiuliza hivi tulisoma ualimu kwa ajili ya nini. Hata ikitokea walimu tukaona kama vile hawatoshi, sasa hivi sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge hapa ni mashahidi, tumejifunza mambo mangapi kupitia simu zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa bahati nzuri na sera hii inataka somo la biashara liwe ni somo la lazima kwa watoto wetu wa sekondari; itakapotokea upungufu wa walimu Wizara iangalie *topic* ambazo zinaweza kufundishwa kwa kutumia *AI*. Kwani *balance sheet, book keeping, trial balance* haiwezi kufundishwa jamani na *AI*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, twende tukaanze kufundisha wafanyabiashara tusifundishe wahasibu, tuwafundishe wanasayansi, tusifundishe walimu wa sayansi, tukafundishe wafanyabiashara kwa wingi kuliko wahasibu ili wafanyabiashara hawa wawaajiri wahasibu. Tukiendelea kufundisha wahasibu wengi kuliko wafanyabiashara watakwenda kufanya kazi wapi? Kwa hiyo mitaala yetu iende ikajikite huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, atafuata Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka; Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo na Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele wajiandae.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti ninakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kutoa mchango wangu. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na naibu wake kwa kazi nzuri ambayo kwa kweli wanaendelea kuifanya. Wamefanya vizuri na wanaendelea kufanya vizuri. Pia niwapongeze Katibu Mkuu na watendaji wa taasisi zote zilizoko chini ya Wizara yake; kwa kweli wanafanya vizuri, hongera sana kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ninachangia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu nilitamka nikasema kwamba maadui wakubwa wa Tanzania wako wanne, na nikawataja. Juzi Mheshimiwa Rais wa Kenya ametutajia maadui hao. Leo ninasema maadui wale wameongezeka, sasa wako sita na nitawataja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adui wa kwanza wa nchi yetu ni umaskini mkubwa, adui wa pili ni ujinga, adui wa tatu ni maradhi, adui wa nne ni ukosefu wa ajira, adui wa tano ni uchumi mdogo wa nchi yetu, adui wa sita ni rushwa kwenye nchi yetu na maeneo mbalimbali na wa saba ni ukosefu wa uwajibikaji na uadilifu katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maadui hawa tutaweza kupambana nao vizuri ikiwa Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia itatusaidia sana kwenye hili. Hatuwezi kuondokana na maadui hao bila kuwa na maarifa ya kutosha, bila kuwa na ujuzi wa kutosha, bila kutumia elimu kubadilisha tabia zetu na mienendo yetu. Mienendo yetu inaweza

ikabadilika kama tutakuwa na maarifa ya kutosha. Kwa hiyo kazi hii ni ya Wizara hii. Tutapambana na rushwa kwa kuwaelimisha watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kazi ya Wizara hii wanaweza kutupa ujuzi kuhusu namna ya kupambana na rushwa, namna ya kupambana na umaskini, namna ya kupambana na maradhi, namna ya kutengeneza ajira na namna ya kutumia teknolojia mbalimbali. Ndiyo maana Wizara hii inaitwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunajua, kwamba hakuna nchi inayoweza ikaendelea bila hivyo vitu kutiliwa mkazo. Kwa hiyo ninasema kwamba wanafanya vizuri sana. Kutokana na hilo ninampongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa kuongeza bajeti ya Wizara ya Elimu. Sasa hivi bajeti ni zaidi ya 2,000,000,000,000 inayokwenda Wizara ya Elimu ili kutekeleza sera mbalimbali. Huu ni ujasiri mkubwa, haya ni maono makubwa. Tuna kila sababu ya kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa maamuzi haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema vyuo vitapambana na hao maadui; ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Wamekuwa wakijibu maswali na wamekuwa wakitueleza; sisi Mkoa wa Songwe tumekuwa tukiomba vyuo; na ni mkoa wa mwisho kuanzishwa, ni mchanga. Bahati mbaya hatuna chuo lakini wanasema tuna chuo kimoja kiko kule chini mpakani, kilometa 130 kutoka pale Vwawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri, ametuambia tunajenga Chuo cha *VETA* cha Mkoa, tunashukuru sana. Tunaomba basi kile Chuo sasa kikamilike. Kisipokamilika kile chuo, vijana wetu wataendelea kukosa ujuzi, vijana wetu hawataweza kujitegemea, umaskini utaendelea kuwepo na maarifa yataendelea kukosekana. Tunaomba kije haraka. Mheshimiwa Waziri ajitahidi akamilishe kile chuo ili angalau kitoe mchango mkubwa na sisi Wanasongwe na Wanavwawa tuondokane na hao maadui ambao nimewasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapotaka vyuo kwamba tunahitaji vyuo, wengi wanasema ni huduma, lakini kwa tafsiri yangu ninasema vyuo siyo huduma. Ninasema vyuo vinatupatia maarifa, ujuzi na

umahiri wa kuweza kufanya mambo mbalimbali hapa duniani. Vyuo ni uchumi, vyuo ni biashara, vyuo ni ajira na vyuo ni viwanda kwa sababu utawatayarisha watu na utawachakata. Kile chuo ni kiwanda cha kuwachakata na kutengeneza ile malighafi ili wawe na maarifa ya kutosha na ndiyo maana, kasi ya maendeleo ya nchi yetu itakuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji hao ili wale Wanambozi wanaozalisha mahindi kwa wingi, wanaozalisha kahawa kwa wingi na wanaozalisha maparachichi kwa wingi waondokane na kuuza kama malighafi bali watengeneze viwanda vya kuongeza thamani ili tupate uchumi mkubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji na tumetenga maeneo. Kata ya Ipunga tuna ekari 308 tumetenga kwa ajili ya chuo, bado hatujapata. Kata ya Nyimbili tumeweka eneo zuri pale Sasanda kuna ekari 700 tumetenga ekari 200 kwa ajili ya vyuo. Pale Kata ya Hasamba tumetenga maeneo zaidi ya ekari 125 zipo, maeneo yapo. Tunahitaji na tunaamini tukijenga vyuo kwenye maeneo yale, tutaweza kupata fedha za kigeni nyingi. Wazambia, Wamalawi, Wakongo na wengine watakuja kusoma kama sisi tunavyokwenda kusoma Ulaya na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tufike mahali vyuo vilivyopo katika nchi yetu hii, watu watoke katika maeneo mbalimbali waje kusoma hapa kwetu. Mazingira ni mazuri, tuboreshe maeneo. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye ubora wa maeneo...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga, kuna taarifa.

## TAARIFA

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba kumpa taarifa mzungumzaji ndugu yangu

Mheshimiwa Hasunga asiwe na wasiwasi na Mheshimiwa Rais kukamilisha hizo *VETA* kwa sababu amekuta shule za amali ziko tisa nchi nzima. Leo zimekamilika shule 103. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Japhet Hasunga unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaipokea kwa mikono miwili. Ninataka kuzungumzia mabadiliko makubwa ambayo Wizara wameanzisha. Hii ya mitaala ambayo wameibadilisha (mitaala ya elimu ya shule ya msingi na sekondari). Wamefanya jambo nzuri sana, lakini mitaala hii tunataka hata kwenye vyuo, vyuo wavisimamie navyo vibadilishe viwe na mitaala inayokidhi mahitaji ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyuo pale bado pana changamoto. Wakati tunakwenda tunahitaji kwenye vyuo tuboreshe mitaala. Nilikuwa ninaangalia vyuo bora Tanzania, ambavyo kwenye dunia ni vya ngapi ambacho ni chuo bora Tanzania ni cha ngapi duniani. Sitaki kusema na sitaki kutaja vyuo hapa maana yake nikitaja itakuwa aibu na itakuwa kama ninatangaza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niseme ukiingia kwenye *website* ukatafuta vyuo bora Tanzania ni vya ngapi duniani tuko mbali sana, tuko mbali sana. Ni kwa nini? Kwa sababu hatujaweka mkazo namna ya kuviendesha vyuo vyetu ili tuhakikishe kwamba *professors* na wahadhiri wafanye machapisho ya kutosha, wafanye utafiti wa kutosha, watunge vitabu na mambo mengine yote ili yasaidie katika kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya muda ninataka niseme wanafanya kazi nzuri na sisi tutawaunga mkono na tutaendelea kuiunga mkono kuhakikisha maendeleo makubwa yanapatikana kupitia Wizara yetu ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Waheshimiwa Wabunge, ninaomba niwatambulishe kwenu wageni waliotembelea Bunge jioni ya leo.

Kwanza, ni wageni wa Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia ambao ni wanafunzi 34 washindi wa *Samia Scholarship* ambao wataenda kusoma *degree* ya kwanza kwenye *artificial intelligence* nchini Ireland. Karibuni sana na hongereni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wapo pia Umoja wa Wanawake Wamiliki wa Shule na Vyuo vya Kati Tanzania *(TAWOSCO)* ambao ni Ndugu Krista Rweyemamu, Ndugu Aisha Shamte Mzee, Ndugu Juliana Asey, Ndugu Mercy Makamu, Dkt. Anjelina Bijura, Dkt. Rachel Mwalukasa, Ndugu Anna Tarimo na Ndugu Ruth Sabaya. *(Makofi)*

Yupo pia mgeni wa Profesa Adolf Mkenda ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa mabasi ya Tilisho bwana John Tilisho. *(Makofi)*

Wapo pia wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ambao ni wanafunzi 155 na walimu nane wa Shule ya Sekondari *Kings Modern* kutoka jijini Dar es Salaam. Karibuni sana wageni wetu hapa Dodoma. *(Makofi)*

Sasa ninamwita Mheshimiwa Kassimu Amari Mbaraka.

**MHE. KASSIMU A. MBARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, shukran sana kwa kupata fursa hii nami kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Elimu. Awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kutujalia kuwepo hapa Bungeni na kuendelea kulitumikia Taifa letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika nukta ya pili ninapenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ndani ya Taifa letu la Tanzania kwenye kuisimamia na kuleta mageuzi makubwa chanya hususan mageuzi ya kielimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona miaka mingi sana tumepita na kauli mbalimbali za elimu, lakini leo ile azma ya kauli kubwa ya Taifa hili ya elimu ya kujitegemea inaenda kutimia kwa kuona mabadiliko makubwa yaliyofanyika kwenye mitaala ya elimu ambayo inawawezesha vijana kuhitimu kidato cha nne akiwa pia amehitimu masomo yanayosimamiwa na *NACTVET* na kuweza kupata cheti na kuingia kwenye soko la ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, atakuwa na ujuzi ndani ya umri mdogo au hata kuendelea katika vyuo vya kati na kuweza kupata elimu. Hili ni jambo kubwa sana kwa sababu soko la dunia ya leo linahitaji watu wenye ujuzi na si nadharia tena. Kwa hiyo, wataweza kushindana katika soko la ajira hapo baadaye. Hilo ni jambo kubwa sana. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa hiyo aliyoifanya kuisimamia mageuzi ya mitaala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Profesa Adolf Mkenda pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Naibu Waziri, Wanu Hafidh Ameir kwa kazi kubwa wanayoifanya kwenye Wizara hii ya Elimu pamoja na watendaji wao Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara ya Elimu. Kwa kweli wanafanya kazi kubwa sana kuisimamia maono mapana ya Taifa hili pamoja na maono mapana ambayo yamo katika Dira yetu ya 2050 kuhusiana na masuala elimu ndani ya Taifa letu la Tanzania. Ni jambo jema kabisa hilo na mambo yote yanakwenda vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuongea hayo kwa muhtasari sasa nijikite kwenye jambo la msingi. Ukichunguza zaidi utakuja kugundua kwamba Wizara ya Elimu 100% maisha yake inagusa maisha ya vijana wa Taifa la Tanzania na katika Taifa la Tanzania vijana katika *population* ni takriban 68% hadi 70%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tafsiri yake ni nini? Tafsiri yake ni kwamba idadi ya ongezeko la watu inakua Tanzania, lakini ukiacha hivyo idadi ya vyuo vikuu vinaongezeka Tanzania. Maana yake ni nini? Ni lazima tujifunge mkanda vizuri kuhakikisha tunaihudumia vizuri elimu ya juu kupitia *Higher Education Students' Loan Board* kwa kuhakikisha mikopo ya vyuo vikuu (elimu ya juu) na ya kati inayotolewa na *Higher*

*Education Students' Loan Board* inatoka kikamilifu na bajeti ile inatoka kama vile ilivyopitishwa na kuidhinishwa na Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatolea mfano, ukiangalia bajeti ya Mwaka wa Fedha 2023/2024, 2024/2025 na 2025/2026 kuna kitu utakigundua. Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge katika jumla ya vipindi hivyo vitatu ni shilingi 2,442,851,755,519.98. Hii ndiyo bajeti iliyoidhinishwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2023/2024, 2024/2025 na 2025/2026. Iliidhinishwa hii iende kwenye *Higher Education Students' Loan Board,* ifike pale watoto wale wakopeshwe, vijana wetu waweze kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiasi kilichopokelewa *Loan Board* ni shilingi 1,788,017,499,927.58. Hiyo ndiyo fedha ambayo imepokelewa takriban shilingi bilioni 654 na ushee bado haijapokelewa. Tafsiri yake ni nini? Ni kwamba kampasi zinaongezeka, kampasi zinakuwa nyingi zinazidi kutanuliwa, idadi ya *enrolment* inakua vyuo vikuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake ni kwamba tunaishauri Serikali fedha tunazozipanga hapa Bungeni kuhusiana na *Higher Education Student Loan Board* na tunazoziidhinisha katika bajeti hii ikishapitishwa na Bunge Tukufu fedha hizo ziende kama zinavyohitajika. Watoto wetu wapate mikopo kwa sababu ukiangalia takwimu hii Bodi ya Mikopo inafanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, takribani 70% ya pesa wanayotoa wanaikusanya takribani 70%. Afrika Mashariki, Afrika kwa ujumla na duniani ni moja katika *organ* muhimu na inafanya kazi vizuri sana. Kwa nini fedha hizi tusiziidhinishe zote zikafika zikapokelewa zikaingia kwenye matumizi vijana wetu wakapata elimu tukawa tunawasaidia kikubwa zaidi? Hilo ni jambo la msingi kwenye *Higher Education Students' Loan Board.* Fedha tunazoidhinisha hapa Bungeni ziende Bodi ya Mikopo kama tulivyoidhinisha, vijana wa Tanzania wakanufaike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninalotaka kuchangia ni kuhusiana na Wadhibiti Ubora. Ukiangalia wale Wadhibiti Ubora ni

kama *CAG* katika elimu. Yaani ni wakaguzi ambao wao wanakagua masuala yote yanayohusiana na elimu ndani ya nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hebu ifike mahali tuwaondoe kwenye Fungu 56 - TAMISEMI tuwapeleke kwenye Fungu 46 la Bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwa nini ninasema hivyo? Mkurugenzi wa Halmashauri ndiye anasimamia karibu shule zote katika eneo lake. Mkurugenzi anaposimamia mwisho wa siku ndiye anayelipa ile *capitation grant fee* kwa ajili ya wale Wadhibiti Ubora kufanya kazi zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa siku zote anayemlipa mpiga zumari ndiye anayechagua wimbo. Hii maana yake ni nini? Tuwafanye Wadhibiti Ubora wawe huru wafanye kazi zao vizuri. Wakipita kule wakiona hakuna madawati, hakuna miundombinu mizuri ya matundu ya choo au shule zina hali mbaya waweze kuandika ripoti na kushauri vizuri ili tuweze kupata matokeo bora kwenye shule zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachoshauri hawa moja kwa moja wasimamiwe na Wizara ya Elimu, TAMISEMI wasihusike nao. Malipo yao yote yatoke Wizara ya Elimu waje kwenye Fungu - 46 la bajeti. Hili ni jambo muhimu sana kwa sababu hili ndilo jicho letu katika majimbo ili wafanye kazi zao kiweledi na vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine la msingi zaidi ni kuhusiana na suala zima la *VETA*. *VETA* ndiyo inajenga taswira kubwa ya kutengeneza ujuzi wa nchi hii, ndiyo *masterplan* ya ujuzi kwa vijana wetu ndani ya Taifa la Tanzania. Fedha zinazotengwa kwa ajili ya *VETA* zitoke, *VETA* zikatengenezwe zisimame ili vijana wetu waweze kuingia katika *enrolment* hiyo na kuweza kupata tija kubwa ya kupata ujuzi hapo baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka unaokuja mbeleni, darasa la sita wanamaliza, hali kadhalika wanamaliza na darasa la saba, kutakuwa na *double cohort*. Maana yake huko mbeleni kutakuwa na *enrolment* kubwa ya wanafunzi kuingia vyuo vya kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini kinachohitajika? Kinachohitajika vyuo vya *VETA* vijengwe kwa haraka viwepo nchi nzima ili vijana hao waingie hapo waweze kupata ujuzi. Wakitoka pale wana ujuzi kamili wataweza kujiendeleza hapo baadaye katika shughuli zao mbalimbali za ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VETA* isiishie kujengwa, tuvilinde kwa thamani kubwa. Kwa nini tuvilinde kwa thamani kubwa? Nitatolea kesi moja ya Tanga. Nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu. Tanga tuna Chuo cha *VETA* kizuri sana. Pale panatolewa mafunzo ya udereva *(Passenger Service Vehicle)* na *HDV (Heavy Duty Vehicle)*. Palitokea kidogo purukushani lakini baada ya muda kuna mtu alitokea akalala, akaamka, akasema hii kozi nimeifuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Mheshimiwa Waziri wa Elimu, mtu bingwa kabisa, Profesa Mkenda. Nilikaa naye nikazungumza naye akamtoa *Director* wa *VETA*, akamtoa na Naibu Katibu Mkuu wa Elimu, waende Tanga. Leo hii *Alhamdulillah* Chuo cha VETA Tanga kinatarajia kurudisha kozi ya *PSV* na kozi ya *HDV* waweze kusoma pale *VETA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, isiishie kuvijenga hivi vyuo tuvisimamie kwa ari kubwa na kuvitolea jicho. Ndivyo vilivyoshikilia mhimili wa vijana wa Tanzania. Mheshimiwa Rais Dkt. Samia ameweka mtazamo mkubwa sana kwenye suala la *VETA* kwa sababu ndipo ujuzi wa vijana wetu utapatikana hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo sasa nitoe pongezi zangu za dhati kabisa kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kupitia Mradi wa *HEET (Higher Education for Economic Transformation)* na sisi Tanga tumenufaika kupitia *Mzumbe University Mkinga Campus;* mradi wa dola milioni saba. Haya ni mabadiliko makubwa na ni mageuzi makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka niliambie Bunge hili Tukufu, Tanga ndio chemichemi ya elimu ya Taifa hili. Shule ya kwanza ya Msingi ilikuwa Magila na Shule ya kwanza ya sekondari ni Tanga. Sisi ndiyo watu wa mwanzo kusoma na kuwa na mwanga wa elimu.

Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya awamu yake kuileta *Mzumbe University, Mkinga Campus* ameiongezea ladha na utamu fahari ya elimu ndani ya Mkoa wa Tanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Wizara kwa kuisimamia Miradi hii ya *HEET*. Tumeitembelea miradi hii *value for money* unaiona na wakandarasi wazawa wamepewa nafasi. Mfano Mradi ule wa Mloganzila pale mkandarasi mzawa kama *Mohamed Builders* ameufanya mradi vizuri na unamalizika kwa wakati. Miradi ile iko takriban 70%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kusema hayo, ninaunga mkono hoja, bajeti hii tuipitishe kwa kishindo. Shukrani sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Taska Restituta Mbogo, ajiandae Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi kuchangia bajeti ya Wizara ya Elimu. Kwanza, kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu muumba mbingu na dunia kwa kutujalia afya na leo hii tunachangia Wizara ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mkenda, Waziri wa Elimu na Naibu wake Mheshimiwa Wanu kwa kazi nzuri ambazo wanazifanya kwenye Wizara hii ya Elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jinsi ambavyo amelichukulia kwa uzito suala la elimu nchini kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais ameweza kujenga madarasa ya kutosha kwenye Nchi yetu ya Tanzania. Pia, ameweza kujenga shule kwa watoto wa kike wasichana shule kwa ajili ya kusoma masomo ya sayansi. Hii ni hatua kubwa kwa watoto wa kike nchini kwetu Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijikite kwenye mchango wa Wizara ya Elimu. Niliwahi kusimama hapa tarehe 7 Mei, 2023 na tarehe 8 Aprili, 2026 na leo tarehe 7 Mei, 2026, nikisema kwamba kwenye Mkoa wangu wa Katavi tumeachwa nyuma kwa sababu mkoa una matatizo ya uhaba wa madarasa, madawati na matundu ya vyoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nirudie takwimu ambazo nilizitaja humu Bungeni nilipochangia Wizara ya TAMISEMI. Mkoa wangu wa Katavi una upungufu wa madarasa 3,205, uhitaji wa madarasa 6,071, yaliyopo ni madarasa 2,866 tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wangu wa Katavi una upungufu wa madawati 27,348, ina uhitaji wa madawati 87,681 yaliyopo ni madawati 61,332. Mkoa wangu wa Katavi una upungufu wa matundu ya vyoo 5,360, unahitaji matundu ya choo 9,122 yaliyopo ni matundu ya vyoo 3,662.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nimetoa takwimu hizi? Nimeitoa takwimu hizi kwa kuwa tunakwenda sasa kwenye Elimu ya Msingi ya lazima ya madarasa kumi. Kwa maana kwamba darasa la kwanza mpaka la sita, tunakwenda sekondari madarasa manne. Sasa watoto watakuwa wanasoma madarasa 10. Kwa upungufu huu wa madarasa, madawati na matundu ya vyoo, Mkoa wangu wa Katavi utafikaje huko kwenye shule za msingi lazima miaka 10?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivi kwa sababu Wizara ya Elimu ndiyo msimamizi wa sera, lakini mtekelezaji wa sera ni TAMISEMI. Hakuna *connection*, kutoka Wizara ya Elimu kwenda TAMISEMI kule kwenye halmashauri, kusimamia kuona vyoo vipo, madarasa yapo na matundu ya choo yapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ijaribu kuliangalia hili kwa kuwa inapelekea sera TAMISEMI azitekeleze lakini haiwa-*control* hawa TAMISEMI kuhakikisha kwamba wanajenga hayo madarasa, wanatengeneza madawati na wanachimba hayo matundu ya vyoo. Nini maana yake? Maana yake ndiyo ukosefu wa matundu ya choo, madarasa na madawati kwenye Mkoa wangu wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Serikali ijaribu kuangalia, je, itaweka kanuni kwenye Wizara ya Elimu ambazo zitakuwa zina-*foresee* huku kwenye TAMISEMI? Kwa sababu Mkurugenzi anaripoti kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu, haripoti kwa Waziri wa Elimu. Asipochimba choo, asipoongeza darasa, asipotengeneza dawati, Mheshimiwa Mkenda hawezi kumwajibisha yule Mkurugenzi. Maana yake nini? Maana yake sera zile ambazo Mheshimiwa Mkenda anazisimamia zinashindwa kutekelezwa huku chini na wale wanaozitekeleza hawako *answerable* kwa Mheshimiwa Mkenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia mwaka 2028 tukijaliwa uhai tutakuwa na wanafunzi 21,177 ambao watakuwa wanakwenda kwenye shule za sekondari. Nini maana yake? Tutakuwa na wanafunzi ambao watakuwa wamefika darasa la sita wanahitaji kwenda sekondari, lakini tutakuwa na wanafunzi ambao wako darasa la saba ambao watakuwa wanakwenda pia sekondari. Jumla nchini kwetu Tanzania tutakuwa na wanafunzi 3,021,177 na tutahitaji madarasa 23,266, tutahitaji walimu 40,192, tutahitaji maabara 9,366 na tutahitaji matundu ya vyoo 46,632. Hizi ni takwimu zilizosomwa hapa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaiomba Wizara ya Elimu iweze kuangalia ni jinsi gani tutaweza kutekeleza hayo mambo. Kwa sababu ninavyoona kwenye Mkoa wangu wa Katavi, tunashukuru kweli Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Mheshimiwa Rais kweli imejenga madarasa, imetengeneza miundombinu lakini utekelezaji kwenye mkoa bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, sisi wananchi wa Mkoa wa Katavi watoto wetu watapataje hii Samia *Scholarship*? Leo hii umewaonyesha wanafunzi hapo kuna hii *Samia Scholarship extended* ambayo wanafunzi wanakwenda kusoma nje. Je, wale wanafunzi watoto wetu, lakini wajukuu zangu kule Katavi watapataje hii *Samia Scholarship* wakasome nje kama wanakaa chini? Darasa moja kwenye Mkoa wa Katavi wanakaa wanafunzi 200. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, je, nikitoa mfano, hata Mheshimiwa Waziri akituma mtu akaangalie, kuna shule pale Mpanda Mjini, Shule

ya Msemulwa, watoto wanakaa darasani 200. Hawa watoto kutoka darasa la kwanza mpaka la tano wanakaa chini. Je, hii *scholarship* ya Mheshimiwa Rais, Mama Samia, ambaye ametupenda akatoa hiyo *scholarship* watoto wakasome nje, wale wajukuu zangu Mpanda wataipataje? Kama wanakaa chini kutoka darasa la kwanza mpaka la tano, wataipataje hii *scholarship*? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia pia watoto ambao wanakwenda kusoma *gender equality* walivyokuwa wanatambulishwa hapo, nimejaribu kuangalia *gender* nimekuta kuna wasichana wanne. Ninaomba hizi *scholarship* ambazo Mheshimiwa Rais ametoa zizingatie pia *gender balance*. Kama *scholarship* ziko 30, basi 15 wawe wasichana, 15 wawe wavulana ili tuweze kwenda sambamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ambalo ningependa kulizungumza leo ni lugha ya kufundishia. Mheshimiwa Profesa. Mkenda anafahamu kwamba, sera ya nchi yetu watoto wanafundishwa kwa Kiswahili kutoka darasa la kwanza mpaka la saba. Wanapokwenda sekondari ndiyo wanakwenda kupambana na Kiingereza. Yeye amesoma vizuri kwa kufundishwa na walimu wa zamani na ndiyo maana ame-*excel* mpaka akawa profesa wa kusoma darasani. Je, una utaratibu gani au tunawaangaliaje hawa watoto kuweka lugha ya kufundisha ya Kiingereza kutoka darasa la kwanza? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. TASKA R. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja. Kwa nini ninasema hivi? Ninasema hivi kwa sababu *English is official language, but Swahili also is official language. Why don't we use two languages?* Kwa sababu watoto wetu wanapokwenda kwenye *interview* nje ya Nchi ya Tanzania wana-*feel inferiority* mbele za watu kujitetea japo kile kitu wanakifahamu. Sisi sote humu ndani watoto wetu wamesoma *English Medium*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba hili suala niliache hapo na nimwachie kama kitendawili Mheshimiwa Profesa Mkenda. Iko haja ya kuweka Kiingereza kufundishwa kutoka darasa la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Paschal Inyasi Chinyele; Mheshimiwa Ado Shaibu Ado, Mheshimiwa Saashisha Elikinyo Mafuwe na Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa wajiandae.

**MHE. PASCHAL I. CHINYELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa fursa hii. Ninaomba nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza Profesa. Mkenda pamoja na msaidizi wake, Wanu Ameir kwa bajeti hii nzuri waliyotuletea siku hii ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niongelee mambo mawili tu; la kwanza, nitaongelea kuhusiana na Bodi ya Mikopo. Tumeelezwa katika bajeti hii kwamba mwaka 2028 tutakuwa na vijana wa *Form One* ambao wanakaribia 3,000,000 wanaingia kwenye shule zetu. Hii maana yake nini? Kuanzia mwaka 2038 tutakuwa na waombaji wa mikopo wanaokaribia 1,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa, waombaji wa mikopo tunao kati ya 190,000 hadi 200,000 ambao ni wa mwaka wa kwanza. Kwa hiyo, hapa tunachokisoma ni kwamba Serikali yetu kupitia Wizara ya Elimu, ijipange sawasawa kufikia miaka ya 2038 na kuendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa bajeti iliyosomwa, pesa iliyopangwa kama nimesikia vizuri kwa mwaka huu ni shilingi bilioni 292, hivi imepangwa kwa ajili ya Bodi ya Mikopo. Sasa, ushauri wangu tu kwamba Serikali ijipange ifikapo miaka hiyo, ihakikishe kwamba Bodi ya Mikopo inakuwa na fedha ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikibidi, Bodi ya Mikopo ibadilishwe iwe kama Mfuko kama zilivyo *NSSF* au *PSSSF*, ziwe na fedha na zijendeshe ili kupata fedha nyingi. Ikiwezekana Serikali inaweza hata ikafanya

tozo kwenye miamala ya simu kupata fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia elimu ya vijana wetu. Kwa sababu kwa suala la elimu na hasa hasa maamuzi haya mazito yaliyochukuliwa ya kuboresha mfumo wa elimu tutakuwa na wanafunzi wengi wanaotaka mikopo, *almost a million* au laki nane hivi. Sasa hivi tunahangaika na watoto 200,000 au 300,000. Je, itakuwaje mwaka 2038 na kuendelea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali ianze kufikiria kutafuta fedha za kutosha kwa ajili ya kugharamia elimu ya vijana hawa, tunahangaika. Tumesikia kijana yule aliyekuwa analia mtaani amesaidiwa, hata hivyo, ninataka kuwahakikishia yule yule aliyesaidiwa hayuko peke yake. Wako wengine ambao vyombo vya habari havijawafikia, wanalia hawajapewa mikopo na wako mtaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninaloomba kuchangia siku ya leo, katika ukurasa wa 97 wa kitabu cha bajeti, kimetajwa Chuo cha Ufundi cha Dodoma kinaitwa *Dodoma Technical College*. Chuo hiki kimejengwa katika eneo la Kata ya Mbalawala. Kama unakwenda Singida ukifika Nala upande wa kulia utaona kipo kinaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii kuwasilisha shukrani za wakazi wa Kata ya Mbalawala kwa ujenzi wa Chuo kile cha Ufundi, *Polytechnic College,* ambacho kimejengwa. Chuo kile kwa taratibu zilizowekwa na Mheshimiwa Waziri ni kwamba mwaka huu kitachukua watoto 1,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watoto wale ni wengi kwa lile eneo na niseme tu kwamba eneo lile na hatua hii ya kujenga kile chuo inataka kufanana na mwaka 1970 pale Chuo cha Dar es Salaam kilipojengwa pale Ubungo. Wakati ule palikuwa ni pori hivi, kile chuo kikachechemua uchumi wa maeneo ya Msewe, Ubungo yenyewe, Sinza na maeneo ya Mlalakuwa yakawa ni maeneo ya miji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi pia panaenda sasa kuchangamka, maeneo ya jirani na Mbalawala, maeneo ya Chigongwe, maeneo ya Ilindi katika Wilaya ya Bahi na maeneo jirani yanakwenda sasa kupata uchumi. Ninachukua nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa

maamuzi haya aliyoyafanya ya kuanza sasa kukifanya chuo hiki kianze kuchukua watoto na kuanza kutoa elimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nisisitize tu kwamba chuo kile ni cha Watanzania na bado kuna miundombinu ambayo haijakamilika. Zinahitajika shilingi 3,000,000,000 ili chuo kile kianze kuchukua wanafunzi kuanzia mwaka huu wa masomo. Ni ombi langu kwa Serikali, Mheshimiwa Profesa Mkenda, ninaomba sana pesa inayotakiwa karibu shilingi 3,000,000,000 iweze kutolewa, kwa sababu mpaka sasa hivi miundombinu ya maji safi na majitaka bado haijakaa sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana miundombinu hiyo ikae sawa ili mwezi wa kumi watoto waanze kuingia na kusoma pamoja na kupata ujuzi wa kusaidia nchi yetu, lakini pia chuo hiki kinaweza kuchechemua uchumi wa eneo lote la Jiji la Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ado Shaibu Ado.

**MHE. ADO S. ADO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti ya Wizara ya Elimu. Ninaomba hoja zangu tatu za mwanzo ambazo nitazisema kwa muhtasari zielekezwe kwa mabosi wangu wananchi wa Tunduru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninafanya hivi kwa sababu wananchi wa Tunduru wamenipa heshima kubwa sana na wanaendelea kunipa heshima kubwa sana kwa kuniunga mkono kisiasa na kuniamini. Kama inavyofahamika hakuna kitu azizi, hakuna kitu cha thamani kubwa ambacho mwanasiasa anapaswa kukipigania kwa nguvu zake zote isipokuwa imani ya umma. Kwa hiyo, hoja zangu tatu zitaelekezwa kwao kwa ajili ya kuilinda imani yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazitaja tu, Wanatunduru wamenituma jambo la kwanza, pale Tunduru tuna Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha *VETA*; tulihoji hapa Bungeni, tunarudia tena Wanatunduru wanataka jibu, wanataka kauli ya Serikali ni lini watapata chuo kamili cha *VETA* cha Serikali? Ninataka kusema ninakubaliana na Kamati ya Bunge ya Elimu kwamba kama tunataka kuwakomboa vijana wetu, tuwekeze kwenye elimu ya ufundi. Hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Wanatunduru wamenituma nikukumbushe kwamba wao walitoa ardhi yao, wakatoa na majengo yao, wakaikabidhi Wizara ya Elimu kupitia Chuo Kikuu cha *SUA*. Vitu hivi vina thamani inayofikia shilingi 1,000,000. Ahadi ya *SUA* ikawa watajenga kampasi kamili pale Tunduru ya Tawi la *SUA*. Hivi sasa tunahesabu miaka, tunaona wenzetu ambao hawajatoa chochote vyuo vinajengwa katika maeneo yao. Wanatunduru wamenituma nimhoji Waziri na kwa hili nitaishika shilingi yake mpaka watakapotueleza chuo kitajengwa lini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, wapiga kura wangu viziwi na hiki ni kilio cha viziwi wote Tanzania. Wamenituma nikueleze kwamba, wakati umefika kwa Lugha ya Alama kutambuliwa rasmi, kuwekewa kinga ya kisheria kama ambavyo Kenya lugha hiyo imo kwenye katiba yao na ifundishwe kwenye mitaala ya elimu katika nchi yetu. Hayo nimeyasema upesi ili kulinda imani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninalotaka kulisema na hasa ikizingatiwa kwamba mengine yanayohusu elimu ya awali, ya msingi, ya sekondari na elimu ya vyuo vya kati yamepata mjadala mkubwa hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda nijielekeze kwenye ufanisi kwa elimu ya juu; nitarejea nyaraka ambayo Waziri na mimi tunafahamu, ninarejea azimio ama tamko la Kampala juu ya wajibu jamii pamoja na haki ama uhuru wa wanazuoni ama wana-*academia*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilisoma azimio lile utakuta kwamba viko vipengele muhimu viwili vya kujipima. La kwanza ni lazima Serikali

i-*commit* rasilimali kwa ajili ya elimu ya juu. Azimio lile linatamka hakuna ufanisi vyuo vikuu, hakuna uhuru vyuo vikuu kama Serikali haija-*commit* rasilimali za kutosha kwa ajili ya elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Azimio la Kampala linasema lazima wanazuoni wafanye kazi kwa uhuru bila kutishwa, bila kuingiliwa, vipengele viwili na Waziri anafahamu, *that was way back* 1990. Tukifanya *assessment* leo kipengele cha rasilimali kwa maoni yangu, nikitazama hali ya wahadhiri wa vyuo vikuu, hitimisho langu kwa Waziri wa Elimu, tumewasahau, huo ndiyo ukweli wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitampa mifano michache Waziri, yeye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ni nyumbani, aende nyumbani awatembelee ma-*comrade* wake majumbani, wako wahadhiri nyumba zao zinavuja na ushahidi upo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, atembelee madarasani akaone jinsi *whiteboard* zinavyobadilika kuwa *blackboard*. Atembelee maofisini *University* haina *Wi-Fi*, haina *Wi-Fi* ya uhakika. Zamani ilikuwa ukiwa mhadhiri ni jambo la fahari, leo hii hali ni ngumu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam pale nimefanya utafiti wahadhiri wanadai zaidi ya shilingi 6,000,000,000 za posho ya malazi kwa miaka minne mfululizo. Tutapata fahari ya wahadhiri wetu? Wanadai malimbikizo ya mishahara zaidi ya shilingi 1,000,000,000. Kuna fahari gani tena ya kuwa Profesa, ya kuwa daktari wa chuo kikuu? Hili la rasilimali bado tuna mlima mrefu wa kuukwea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele cha pili, uhuru. Kama tunataka kupata kilicho bora kutoka kwa Wanazuoni wetu, tuwaache wafanye kazi yao kwa uhuru na uhuru wa Mwanazuoni unaanzia katika chumba cha kufundishia, Mwanazuoni aachwe afanye kazi yake kwa uhuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viko visa kwa karibuni vya kuwatisha, vya kuwashughulikia Wanazuoni. Sina muda, Chuo Kikuu cha Dodoma yuko Mhadhiri ametoa maoni yake kwenye *lecture*, ameitwa Polisi na

akawekewa dhamana na *UDOMASA*. Pale *SUA* iko mifano ya namna hiyo. Ushahidi upo, Iko mihadhara inashindwa kuendelea katika vyuo vikuu kwa sababu wanapata mbinyo wa Dola. Kama tunataka Wanazuoni wetu watupe matunda mazuri, tuwaache wafanye kazi kwa uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuyasema hayo, ninashukuru sana na nimemaliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, ajiandae Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia Bajeti yetu ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninamshukuru sana Mungu kwa kunipa nafasi hii kuweza kushiriki tena hapa. Kabla sijasema lolote, ninaomba kumshukuru sana Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kumwamini kaka yetu Mheshimiwa Profesa Mkenda na sisi watu wa Kilimanjaro. Niwaambie tu kaka yetu sisi tunamwamini na tunaendelea kumwombea amtumie kwenye mambo magumu kama haya kipindi ambacho tunafanya mabadiliko makubwa ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza pia wasaidizi wake Mheshimiwa Naibu Waziri, jirani yangu, dada yangu lakini pamoja na Katibu Mkuu Profesa Nombo na Naibu Makatibu Wakuu Hussein pamoja na ndugu yangu Mushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna kila sababu ya kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mambo makubwa aliyoyafanya kwa kipindi chake kwenye mabadiliko ya elimu. Itakumbukwa kipindi hiki cha Mheshimiwa Profesa Mkenda na Mheshimiwa Dkt. Samia na wasaidizi wake, yametokea mabadiliko mengi sana kwenye mfumo wetu wa elimu. Leo hapa tunavyozungumza, wanafunzi wa Kitanzania wamepata *Samia Scholarship* na tumewashuhudia pale. Haya ni mapinduzi makubwa

sana, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kazi hii kubwa aliyoifanya kwa wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yametokea mabadiliko ya kimfumo, kubadilisha mfumo wetu wa Elimu ya Awali. Leo tunazungumza Elimu ya Amali na Mafunzo na vyuo vinajengwa na wanafunzi wanapata taaluma, hayo ni mapinduzi makubwa sana. Hili kubwa ambalo Mheshimiwa Profesa Muhongo ameongea kwa undani sana sitarudia na mabadiliko kutoka kwenye mfumo wetu wa elimu kwa maana ya saba, nne mbili halafu *three plus.* Leo tuna Mfumo wa Elimu wa *six* kwa maana ya *four*, *two* na *three plus,* haya ni mapinduzi makubwa sana. Mheshimiwa Profesa Muhongo ameeleza nchi zilizofanikiwa kwenye mfumo huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, sasa ni wakati sahihi wa kwenda kubadilisha mawazo ya kwamba, ukimchukua mtu wa darasa la nane wakati wa Mkoloni na ukimchukua mwanafunzi wa *Masters* sasa hivi, yule wa Mkoloni anaonekana ni bora kuliko sisi. Kupitia mfumo huu ninaamini tunaenda kubadilisha mtazamo huo. Watoto wetu, wanafunzi wetu wawe na elimu ambayo akija mtaani, inapimika na inakuwa na ubora na ubora zaidi. Kwa mfumo huu, tunakwenda mahali, Profesa Mungu akubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuzungumza kwa uchache tu kuhusiana na ujenzi wa Vyuo vya *VETA*. Ndugu yangu na kaka yangu Mheshimiwa Profesa Mkenda, Mama Samia amefanya kazi kubwa sana kwenye Jimbo la Hai na Wanahai wamenituma leo kumshukuru sana. Kule kwetu amejenga barabara, amejenga masoko. Sasa hivi ninamtaarifu Mheshimiwa Profesa Mkenda akiwa anaenda nyumbani, amwambie dereva wake akifika pale Hai tuna taa za kuongoza magari. Muda si mrefu ninaamini tutapata na *flyovers*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hili la *VETA* atakapoanza, Mheshimiwa Naibu Waziri ametuahidi hapa kufikia mwezi Desemba zitakuwa zimekamilika, ninakuomba sana uanze na Chuo cha Wilaya ya Hai kwa jirani zako. Pale tumekutengea eka 52, ukitaka kujenga Chuo cha *VETA* cha Kanda, njoo pale Hai tuna eneo la kutosha.

Ninakukumbusha, Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara kutembelea Chuo cha Kikuletwa pale, ile barabara ya mkoa Mheshimiwa Naibu Waziri ninakumbuka alisema neno, akasema ninalichukua, ninapeleka kwa kaka yao Mheshimiwa Profesa Mkenda na mama yao Mheshimiwa Samia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile barabara ya kuelekea kwenye chuo siyo rafiki. Tumepata kilometa tatu lakini ninajua, wale waliotuwezesha kwenye kile chuo wanaweza kutusaidia Barabara ya Bomang'ombe – Chekimaji – *TPC*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuzungumza jambo moja kuhusiana na watumishi wanaotoa elimu kwetu. Ninawashukuru sana walimu wa Tanzania. Profesa umeweza haya yote magumu, hebu ninaomba hili, Mheshimiwa Mama Sitta amekuwa akizungumza mara nyingi sana, sisi tuna Taasisi *TSD* inayohusika na walimu, kwa nini walimu wa nchi hii wanakuwa na mabosi kila mahali? Ninamwomba, kama ameweza la mitaala, hili aliweze, walimu wawe na msimamizi mmoja ili waweze kupata stahiki zao kwa wakati kama ilivyo Nchi ya Ghana na maeneo mengine. Yuko *expert* Mheshimiwa Mama Sitta pale, atamweleza kwa sababu ya muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, ameeleza kwenye hotuba yake, vyuo vikuu vya nchi hii vinafanya utafiti ngazi ya *Masters*, ngazi ya *PhD* na ngazi nyingine. Wanaandika wanayajaza kwenye makabrasha ya vyuo vyetu vikuu. Ninaomba ifike mahali Profesa sasa, waanze kutumia tafiti zinazofanywa na wanafunzi wa vyuo vikuu, kuvileta viweze kuwasaidia Watanzania wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ninaomba kusema, nilisema wakati ninauliza swali hapa, liko jambo ambalo limeanza hivi karibuni kwamba Mhadhiri anayefundisha Chuo Kikuu kwenye kozi fulani, anatakiwa sifa za ajira yake ziwe *specific* kwenye eneo lile na nilitoa mfano kwenye kozi ya *Political Science*. Mhadhiri aliyesoma *Political Science*, anasoma *International Relations*, anasoma *Public Relations,* lakini inapofika kwenye kufundisha anakataliwa. Matokeo yake Chuo cha *UDOM* wamefunga baadhi ya kozi kwa sababu ya hilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamwomba Profesa hebu aingilie kwa haraka jambo hili, vinginevyo tutakosa kozi nyingi ambazo ni mahitaji. Ni sambamba na lile ambalo wanafunzi wanasoma kozi ambayo ukija mtaani, *yes* mwajiri namba moja tunaamini ni Serikali, ninaamini pia sekta binafsi, lakini huyu mwajiri namba moja kwa nini mtoto asome kozi ambayo akija mtaani, akiingia kwenye Sekretarieti, haipo. Nimefanya utafiti mdogo nikagundua, vyuo hivi vinafanya mawasiliano na Sekretarieti ya Ajira, lakini na Utumishi, kunakuwa na *delay* hapa katikati. Ninaomba Waziri atusaidie kuondoa hilo haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema kabla kengele ya kwanza haijalia, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha, chondechonde hii Bajeti ya Elimu ni ya kimkakati, tunaomba fedha zote tunazozipitisha hapa ziletwe kwa 100% ili hii mipango iweze kutekelezeka. Tumeambiwa hapa 2028 watoto wetu wanaenda kuhitimu darasa la sita, lazima tuanze kuweka bajeti zinazotekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo ambalo tunapanga mipango, tunashusha kwenye *level* ya halmashauri, tunasema halmashauri wakajenge madarasa. Halmashauri hizi ninaomba waziweke kwenye *cluster*. Halmashauri zina uwezo tofauti, huwezi kulinganisha Halmashauri ya Kinondoni na Halmashauri ya Wilaya ya Hai. Ukiwaambia hawa waende wajenge vyoo ndani ya miezi sita, hawa wakajenge madarasa, hili jambo hatutafanikiwa. Lazima tufanye tathmini ya mahitaji ya walimu wanaotakiwa, madarasa yanayotakiwa na vifaa vya kufundishia ili inapofika 2028, tuwe tumejiandaa lisiwe ni jambo ambalo limetokea kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla muda haujakwenda, sikupata nafasi ya kuchangia Wizara nyingi kidogo kwa sababu ya matatizo niliyokuwa nayo. Wanahai wameniambia Ndugu Chongolo ni rafiki yako, kule Hai alituahidi kutujengea Bwawa la Kilanya, ninaomba sana anisaidie kumkumbusha. Hata hivyo, alituambia atatueletea fedha kwa ajili ya Bwawa la Mbatakero kwa maana ya Skimu ya Umwagiliaji. Anisaidie kumkumbusha na zile za Metrom na Bolutu, haya ni mahitaji makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ni shida, tatizo la mbolea. Wakinisikia watu wa Hai nimesimama hapa sijazungumza mbolea, mbolea imekuwa ni changamoto kwenye wilaya yetu. Anisaidie kuongea na *senior* mwenziwe, amwambie tuna hiyo changamoto ya mbolea, watu hawapati mbolea, matokeo yake sasa hivi wamelima, mashamba mengi mbolea haijapatikana, achukue hatua za kidharura ili tuweze kupata mbolea kwa wakati na iuzwe kwa bei rafiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, anisaidie kumwambia Profesa hapo ambaye ni jirani yake kwamba, kule kwetu tuna shule chakavu, ninajua na Rombo zipo, tumeandika andiko maalum la Mkoa wa Kilimanjaro, tumeshawasilisha TAMISEMI, tunaomba watusaidie kuleta fedha hizi za shule chakavu ili na sisi tuondokane na shule ambazo hazifanani na sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ninamshukuru sana, sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa heshima anayotupa katika Jimbo letu la Hai. Leo Jimbo la Hai ninapowaambia taa zinawaka barabarani, barabara zinapitika. Na yale machache yaliyokuwepo ambayo tunajua atayafanya, kwa kweli sisi tunaendelea kumwombea Mheshimiwa Rais, tunampenda sana na tunasema Mama Samia ni mama wa Hai, karibu sana Jimbo la Hai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako ambao umejumuisha mpaka mambo mengine ambayo hayapo kwenye Wizara.

Nilimtaja Mheshimiwa Zainab Abdallah Issa, atafuata Mheshimiwa Selina Henry Kingalame na ajiandae Mheshimiwa Fatma Ally Rembo.

**MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii kuchangia Bajeti ya Wizara ya Elimu. Ninaanza na hadithi ya Mtume wetu Muhammad *(SAW)*

ambayo alisema: "*Twalabul 'ilmi fariidhatun 'alaa kulli Muslimin wa Muslimat*" kwa maana kuitafuta elimu ni faradhi kwa kila Muislamu mwanamke na mwanaume. Pia, ukisoma Mithali 4:13 inasema: "Mkamate elimu usimwache aende zake, mshike kwa maana huo ndiyo uzima wako."

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha huo ninachukua fursa hii kumpongeza sana Waziri wetu wa elimu Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, mtu bingwa kabisa aliyefanya mageuzi makubwa sana kwenye sekta ya elimu nchini Tanzania na msaidizi wake Naibu Waziri Mheshimiwa Wanu Hafidh Ameir, mwanamke mchapakazi, mnyenyekevu, mtulivu, hodari, anayepambana kuhakikisha Sekta ya Elimu inapiga hatua kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kuwaambia nchi hii katika Makatibu Wakuu waliowahi kutokea katika Wizara hii, ni Profesa Nombo. Huyu mama mpigie simu mpaka saa nane usiku, atapokea simu kuhakikisha anahudumia wananchi kwa masilahi mapana ya elimu ya Taifa hili. Profesa Nombo popote alipo apokee maua yake, Mwenyezi Mungu ambariki sana. Ninawapongeza Naibu Katibu Mkuu, Menejimenti ya Wizara na hapa wapo vijana wanaofanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda pale *VETA,* Mkurugenzi wa *VETA CPA* Anthony Kasore, kaka yangu apokee maua yake, *VETA* wanafanya kazi kubwa na kazi nzuri sana. Pia, tunampongeza Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu Tanzania, Profesa Aneth Komba, hongera sana kwa mama yangu anafanya kazi kubwa sana. Ninaomba pia kumpongeza Katibu Mtendaji Mkuu wa Baraza la Mitihani la Taifa, Profesa Said Mohamed, hongera sana, anafanya kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee Mkurugenzi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania *(TEA),* hongera sana kwao, tunatambua na kuthamini kazi yao. Tunataka kuwaambia, elimu ni ibada. Kama sisi hatutawapa malipo basi malipo watayakuta kwa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kwa upekee kabisa kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye ndiye suluhu ya matatizo kwa Watanzania. Tumeona mageuzi makubwa sana aliyoyafanya kwenye sekta ya elimu. Kwenye historia ya nchi hii tumeenda kufanya maboresho ya Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 ambayo kwa sasa hivi elimu ya lazima itakuwa miaka 10 kwa maana kutoka darasa la kwanza mpaka kidato cha nne.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *KPI* ya *development index*, moja ya maeneo ni *literacy rate*. Leo hii tunaenda kupata uhakika kwamba watoto wetu wote nchini Tanzania watafika kidato cha nne. Haya ni mageuzi makubwa na ya kuungwa mkono. Hongera sana kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amezindua Mpango Mkakati wa Kisayansi wa *KKK,* kwa maana sasa watoto wetu mpaka watakapofika darasa la tatu watakuwa wana uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu. Haya ni mageuzi makubwa. Ninampongeza Mheshimiwa Rais kwa kuja na mpango wa pamoja kati ya waajiri, vyuo vyetu vya ufundi stadi pamoja na vyuo vikuu ili kuhakikisha kwamba vijana wetu wanaokwenda kwenye elimu ya vitendo, wanapata ujuzi, wanapata uzoefu waende kupambana kwenye soko la ajira, hongera sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote, Mheshimiwa Dkt. Samia amefanya mageuzi makubwa kwenye miundombinu ya elimu. Kwa mfano, kwenye shule zetu za sekondari mwaka 2021 tulikuwa na shule 18,000, sasa hivi tuna shule 20,889, sawa na ongezeko la 11.2%. Kwenye elimu ya sekondari tulikuwa na shule 5,000 tu, sasa hivi tuna shule 6,488, sawa na ongezeko la 18.5%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa vyuo vikuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya mageuzi makubwa sana. Mwaka 2021 bajeti ya mikopo ya vyuo vikuu ilikuwa ni shilingi 700,000,000,000, leo ninavyozungumza hapa bajeti ya Vyuo Vikuu ni shilingi 839,000,000,000. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye historia ya nchi hii, Mheshimiwa Rais Samia anaweka rekodi kuwa Rais wa kwanza kutoa mikopo kwa vyuo vya kati, haijawahi kutokea kwenye historia ya nchi hii. Mwaka 2021 waliokuwa wanapata mikopo ya vyuo vya vya kati ni 10,200, sasa hivi wanaopata mikopo ni 18,473 kutoka shilingi 10,000,000,000 mpaka shilingi bilioni 18.7, nani kama Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kubwa kuliko yote, kupitia uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia, sasa hivi tuna *Samia scholarship* ambazo zinawainua vijana wetu kwenye masomo ya sayansi kutoka wanafunzi 1,407 mpaka wanafunzi 2,630, sawa na ongezeko la 46.5%. Ametoa mikopo kutoka shilingi 7,000,000,000 mpaka shilingi bilioni 13.7% sawa na ongezeko la 40%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumtia moyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, *Madam President, thank you for promoting Educational Policies, thank you for strengthening Diplomacy, thank you for fighting up for this country, thank you for your untouched victory.*

*Sayyidat Raisat Samia anjariyatun wa hawiyatun wa mutawadhiatun, wa nastamirru bijiddatin. Nahnu nad'u jami'a al-mustathmirin, wa nad'u jami'a aswihab al-maslahat. Tanzania hiya mawtinuhum. Son excellence la Présidente Samia on lit les trés fort le trophe determinér visiyonner aujourd'hui nous a pris notre avertissements nous appelons touts les parties prénomes la Tanzanie votre maison moi je suis.* Mheshimiwa Rais tuko pamoja na wewe, tunakuunga mkono na Mwenyezi Mungu atakulinda na kukubariki Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumwambia Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, Hayati Sheikh Abed Karume aliwahi kusema: "Huwezi kuwa mwana wa nchi kama huna uchungu na nchi yako." Leo hii tuna kizazi cha *Generation Z,* asilimia kubwa ya watoto hawa hawana Uzalendo, hawana Utaifa. Ninamwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Elimu, ipo haja ya ku-*integrate* elimu yetu na kuhakikisha vijana wetu…

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab Issa kuna Taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Saashisha Mafuwe.

**TAARIFA**

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kumpa Taarifa dada yangu mpendwa na shemeji yangu kwamba Bunge letu tuna lugha mbili rasmi, Kiingereza na Kiswahili. Akitusaidia kurudia yale maneno aliyosema na sisi tuweze kuyaelewa tuweze kufurahia alichokuwa anakisema. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab unaipokea Taarifa hiyo?

**MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeipokea lakini niliweka msisitizo ili ujumbe hii dunia ijue na Tanzania ijue kwamba tunaye daktari wa matatizo ya Tanzania Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizia kwa kumwambia…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Zainab, kwa mujibu wa kanuni tuna hizo lugha mbili, sasa hicho ulichokisema ni kizuri sana. Ili tuweze kuwa na uelewa wa pamoja, utusaidie kututafsiria.

**MHE. ZAINAB ABDALLAH ISSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuzungumza, nimewaambia Watanzania kwamba Mheshimiwa Rais wetu, kipenzi chetu sisi tunampenda sana, furaha yetu yeye mwenzetu hakika anapambana. Uchumi wetu, Diplomasia yetu imeimarika sana, Utalii wetu, vivutio vyetu dunia imeviona. Tunawakaribisha wawekezaji, wadau wote, karibuni tuijenge Tanzania yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuhitimisha, ninamwomba sana Mheshimiwa Profesa Adolf Mkenda, tunaenda kwenye kizazi cha *Generation Z,* pamoja na kwamba tunawekeza kwenye elimu na amali, kama hatujawekeza kwenye maadili, uzalendo na utaifa, bado

tutakuwa hatujafikia malengo. Ninamwomba ashirikiane na wenzetu wa Jeshi la Kujenga Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miaka ya 60 na 70 wazee wetu wanajua, kwenda Jeshini ilikuwa siyo suala hiari, ilikuwa suala la lazima. Ipo haja ya watoto wetu kwenda kupata mafunzo ya ukakamavu na uzalendo ili wanapotoka kurudi uraiani, waweze kuwa na uzalendo wa kulipambania Taifa lao. Ninakuomba sana hili jambo lifungamanishwe na masuala ya uzalendo kwa kushirikiana na Jeshi la Kujenga Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Selina Henry Kingalame; Mheshimiwa Fatma Ally Rembo na Aisha Mshantu Mduyah wajiandae.

**MHE. SELINA H. KINGALAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi ili niweze kuchangia katika hii Wizara ya Elimu. Kwanza kabisa ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima, afya na kibali. Pili, ninapenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mapinduzi makubwa ya sekta ya elimu, hasa elimu ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mradi Mkubwa wa *HEET*. Mradi huu ni wa miaka mitano, ulianza Mwaka 2021 mpaka Mwaka 2026. Mradi huu wa Dola za Kimarekani 425, unafanya mapinduzi makubwa sana katika marekebisho na ujenzi wa vyuo vikuu mbalimbali nchini Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipomshukuru tena Mheshimiwa Rais. Siku anahutubia Bunge hili la Kumi na Tatu alikuja na akasema azma ya Serikali ni kujenga matawi ya vyuo vikuu katika mikoa yote ya Tanzania. Sisi ni mashahidi, tunaona kabisa wameanza kwa ujenzi wa vyuo 16 kwenye mikoa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nichukue nafasi hii pia, kumpongeza Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Profesa Mkenda. Hongera sana kwake, kazi yake tunaiona na ameonesha yeye siyo Waziri wa ofisini ni Waziri wa *field.* Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii pia kumpongeza Naibu Waziri wa Elimu, hongera sana Mheshimiwa Wanu, kwani kazi yake tunaiona, ziara zake tunaziona. Nimekuwa mmoja wa watu ambaye ninapeleka kero nyingi sana na amekuwa akizitatua kwa wakati. Hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nijikite sasa kwenye mchango wangu, nitazungumzia vitu viwili. Kwanza ni udahili wa wanafunzi wa elimu ya juu ni wazi kwamba, umeongezeka. Tukiangalia kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ambapo ni wanafunzi 137,000 na Mwaka wa Fedha 2025/2026 wanafunzi 170,000. Hii ni wazi kwamba, ongezeko hili la udahili kuna mazingira rafiki na mazuri katika vyuo vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ni moja, tunadahili wanafunzi hawa, lakini vyuo vingi havina uwezo wa kuwapa hosteli. Hii inasababisha wanakwenda kutafuta hosteli nje ya kampasi, ambapo sasa usalama wao na mali zao inakuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu na ushauri kwa Serikali ni waangalie namna ambayo wanaweza kujenga hosteli maeneo ya vyuo. Kama maeneo ya vyuo siyo rafiki sana, labda ni madogo, waangalie ni namna gani ambavyo wanaweza wakatafuta maeneo mengine yakasimamiwa vizuri, ili vijana wetu wa vyuo na vyuo vikuu wawe salama. Pia, muda mwingine gharama za usafiri kutoka hosteli mpaka eneo la chuo imekuwa ni changamoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa pili ni Mikopo ya Elimu ya Juu. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa ongezeko la bajeti ya mikopo mpaka kufikia shilingi bilioni 917. Ni ukweli usiyopingika, siyo wanafunzi wote ambao wanapata

mkopo wanapata na ada pia, changamoto hii imekuwa ni kubwa sana kwa wanafunzi wa vyuo na vyuo vikuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwanafunzi inabidi atumie *boom* lake kulipia ada, ili asiweze kukosa masomo au mitihani yake. Ombi langu kwa Serikali, najua Serikali yangu ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni sikivu sana, lakini pia, nina imani kubwa sana na Waziri, baba yangu Mheshimiwa Profesa Mkenda, ukishirikiana na Naibu wako hakikisheni vijana hawa wanapata *boom,* basi wazingatiwe na ada pia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siyo lazima wakapata asilimia yote mia, lakini angalau asilimia ambazo zitakuwa na unafuu kidogo, ili waondokane na hii adha ya kulipa ada. Nawahakikishia siyo kwamba, wataleta tu tabasamu kwa vijana hawa wa vyuo na vyuo vikuu, bali mtaleta utulivu wa nafsi na akili katika masomo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Fatma Ally Rembo.

**MHE. FATMA A. REMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango Wangu. Awali ya yote, kwanza ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunipa afya njema, siku ya leo kwa mara ya kwanza kuchangia hoja, lakini pia, kuchangia Bajeti ya Wizara ya Elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda pia, kutoa pongezi kwa dhati ya moyo wangu kwa Jemedari wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kazi ya mageuzi makubwa anayofanya katika sekta ya elimu ya nchini. Pia, ninapenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara ya Elimu nchini kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kuendelea kuchagiza maendeleo ya elimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kusema, elimu ndiyo msingi wa maendeleo ya Taifa lolote duniani na sote tunafahamu hilo. Taifa lenye elimu bora hujenga uchumi imara, teknolojia, ajira na pia, ustawi wa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kitabu cha *Quran* kinaanza kwa amri ya kusoma, *Surah Al Ala,* Aya ya 96, mstari wa kwanza. Unasema: *"soma kwa jina la Mola wako mlezi aliye kuumba",* lakini pia, kwenye Biblia, Hosea 4:6 inasema: *"watu wangu wanaangamia kwa kukosa maarifa"*. Tunaona kabisa hii inaonesha wazi kuwa, elimu ni msingi wa maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kujikita sasa moja kwa moja kwenye mchango wangu. Ninajikita zaidi kwenye mafunzo ya ufundi stadi na pia, elimu ya ufundi stadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza Serikali kwa kuongeza Vyuo vya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi kutoka 1,414 mpaka 1,446 mwaka 2026. Pia, ninapenda kusema na kuongezea uzito kuwa, *VETA* imekuwa ni daraja kubwa sana la kuwavusha vijana na wanawake. Wanawake wengi wameweza kujiajiri kupitia *VETA,* wengi wamekuwa wakifungua biashara ambazo wamejiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano ni karakana, kuna gereji, kuna wanaofungua *saloon,* kuna wengine ambao wanafungua *catering,* lakini wapo ambao wanafungua kampuni ndogo za TEHAMA. Tunashuhudia vijana wenzetu wakipambana katika kuchangia maendeleo ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na shughuli mbalimbali za uzalishaji mali kupitia elimu ya ufundi stadi, kwa hakika tunaona *VETA* ni sehemu ambayo ni uwekezaji mkubwa wa moja kwa moja kumsadia kijana au mwanamke kuweza kujiajiri na kuchagia uchumi wa nchi hii, lakini bado tuna changamoto ambayo inatukabili ukiachana na haya maendeleo ambayo tunayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wetu wa elimu nchini umejikita katika nadharia kuliko vitendo; dunia ya sasa inahitaji watu wenye ujuzi mbalimbali na ubunifu. Zaidi ya kuwa na vyeti pekee ni lazima mtu awe na ujuzi na kwanza kujua kutumia teknolojia kwenye kuchagiza na kutatua changamoto za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa mfano, zipo nchi ambazo zimeendelea kiuchumi, kama Ujerumani, China, Singapore, South Korea; hizi nchi zimewekeza sana kwenye ufundi stadi, lakini pia, kwenye teknolojia na ubunifu pamoja na *practical skills* kwa wananchi wake, vijana na wanawake. Ninaomba kuishauri Serikali yangu kwa unyenyekevu mkubwa waweze kufanya maboresho yafuatayo, kwa ajili ya mustakabali wa maendeleo ya elimu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, waendelee kubadilisha mfumo wa elimu kutoka kwenye nadharia kwenda kwenye vitendo, ili kuweza kusaidia wahitimu wetu wawe na uwezo na ujuzi. Wakitoka katika mafunzo waweze kwenda moja kwa moja kujiajiri au kuwa na utayari wa kuajirika kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kuimarisha elimu ya sayansi, TEHAMA, *coding,* kwa maana ya *programming* na pia, ubunifu kuanzia elimu ya msingi. Yaani *coding,* TEHAMA na *programming* zianzie kwenye ngazi ya msingi na siyo tu kwenye vyuo vikuu, ili watu waweze kujifunza mapema nyanja hizi za teknolojia na tukizingatia sasa hivi tunaishi kwenye uwanda mkubwa wa teknolojia, ndiyo maisha ya sasa na ndiyo maisha ya baadaye. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuimarisha ushirikiano kati ya vyuo vya ufundi na viwanda, ili wahitimu watoke wakiwa tayari kwenye soko la ajira. Kwa maana ya kwamba, vyuo vya ufundi viweze ku-*intergrate* na viwanda, ili wahitimu wetu wawe tayari wamejiandaa wakiwa kwenye masomo, wakitoka wawe tayari kwenda kuajirika, lakini pia, kuajiri na wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda piakusisitiza vyuo vikuu na taasisi za utafiti zipewe fedha za kutosha, kwa ajili ya *innovation*. Zipewe fedha kwa ajili ya *medicine,* zipewe fedha kwa ajili ya

*scientific research,* zipewe fedha kwa ajili ya *agriculture technology* na *renewable energy*. Vyuo hivi vina uhaba wa fedha za kufanya haya, kwa ajili ya kuleta maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na teknolojia na maarifa tunahitaji elimu inayojenga maadili. Tunaona Taifa letu sasa ambavyo limekuwa na mmong'onyoko mkubwa wa maadili. Vijana wengi wamekuwa wakifanya mambo mengi ya hovyo na wengine ni wanafunzi kwa hiyo, tunakumbushwa kwamba, tunatakiwa tuanze kuwapa elimu wakiwa huko huko shuleni, elimu ya maadili, uzalendo wa nchi yao, nidhamu, lakini pia, uwajibikaji na utu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi nilivyosema sasa ndiyo msingi wa maendeleo yote tunayoyatafuta kwa sababu, elimu bora siyo vyeti peke yake, bali kujenga Taifa lenye wananchi wenye maadili na maono katika nchi yao. Ninapenda kusema Tanzania ina vijana wengi sana wenye ujuzi mkubwa, lakini lazima tuendelee kuboresha mfumo wetu wa elimu, ili kuwekeza zaidi katika sayansi, teknolojia, ubunifu na ujuzi wa vitendo, ili Taifa letu liweze kuwa miongoni mwa nchi zenye uchumi mkubwa na pia, ushindani wa Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninapenda kwanza kunukuu *quote* ya Nelson Mandela. Alisema, *"Education is the most powerful weapon which, you can use to change the World"*, akimaanisha, elimu ni silaha yenye nguvu zaidi unayoweza kuitumia kubadilisha dunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *quote* hii tunaona ni namna gani elimu ndiyo msingi mkuu wa maendeleo katika nchi na Taifa lolote katika dunia hii. Namalizia kwa kusema, napenda pia kutoa pongezi tena na tena kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ndugu zangu tumeona ni namna gani ambavyo ameleta mageuzi makubwa, wananchi tuendelee kumpa moyo, lakini sisi kama Wabunge, tuendelee kumwombea Mheshimiwa Rais, ili aweze kuendelea kufanya mambo makubwa na mageuzi katika Taasisi hii ya elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba kusema ninaunga mkono hoja na ninashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Aisha Msantu Mduyah.

**MHE. AISHA M. MDUYAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi hii. Ninaanza kwa kuwapongeza Wizara, Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, Menejimenti ya Wizara, pamoja na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake. Kubwa zaidi ninapenda kumpongeza na kumshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mageuzi makubwa sana aliyofanya katika elimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata Sera ya Elimu ya Mwaka 2014, Toleo la 2023, Sera ambayo imeleta maono makubwa katika nchi yetu. Kwanza tumeona tuna Mtaala unaojumuisha masomo ya amali, lakini pia, tumeona tumeongezewa lugha; mbali ya Kiswahili na Kingereza, Lugha ya Alama pia, inatambulika kama lugha rasmi ya kujifundishia na kujifunzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna lugha nyingine kama *brail*, pamoja na lugha ya mguso kwa wenzetu wenye uziwi na kutoona; hongera sana na shukrani sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Mbali na hiyo tumeona pia, sera imekuja na miongozo minne, ikiwemo Mwongozo wa Shule ya Nyumbani. Ninapongeza kwa sababu, inawapa nafasi wanafunzi wenye mahitaji maalum ambao hawawezi kufika shule nao waweze kupata fursa sawia za kusoma, kama wenzao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatoa pendekezo katika utekelezaji huu, bado jamii kubwa sana haijaweza kuufahamu huu mwongozo. Tunao wanafunzi wengi wenye mahitaji maalum ambao wako nyumbani, lakini hawapati fursa ya kujifunza. Hivyo basi, ninashauri Wizara iweze kuangalia ni kwa namna gani uelewa unazidi kuendelezwa kwa jamii ikiwemo walimu ambao ndiyo watekelezaji, lakini pia, wazazi na walezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hiyo pia, Wizara ione ni kwa namna gani wataweza kuwawezesha walimu hawa usafiri na posho, kwani tunajua mwongozo huu unatekelezwa nje ya muda wa shule. Pia, kwa mapenzi mema ya Rais wetu ameweza kuruhusu wanafunzi kurudi shuleni, wakiwemo wale ambao walisitisha masomo kwa changamoto za ujauzito, tukapata *re-entry guideline*. Bado uelewa wa mwongozo huu haujafika kwa jamii kwa ukubwa wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona kwamba, kuna urasimu mkubwa sana ambao mabinti hawa wanaupata pindi wanapotamani kurudi shule. Mbali na hapo kwa wale wanaorudi shule bado mazingira ya shuleni hayapo sawa, kuna ubaguzi kutoka kwa wanafunzi wenzao, lakini pia, sehemu salama ambayo wanaweza kuwahifadhi watoto wao kipindi wao wako shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea pia, kuipongeza Wizara kwa nafasi nyingine ambazo wanaendelea kufanya. Ninaomba nichangie pia katika suala la teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona kwamba, Wizara ya Mawasiliano inafanya kwa ukubwa wake kuendeleza huduma ya *internet* katika jamii, lakini ninaishauri Wizara ione ni kwa namna gani teknolojia inafika shuleni. Hii itapunguza gharama za uchapaji wa vitabu, wanafunzi watapa vitabu kwa njia ya *E-books* na pia, itaharakisha upatikanaji wa vitabu hivi, hasa kwa wale ambao wako pembezoni mwa miji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la elimu jumuishi, ninajivunia tumepiga hatua kubwa sana, hasa katika masuala ya miundombinu. Tumeona ni kwa namna gani Serikali inaboresha miundombinu, ninaomba bajeti iweze kuongezwa katika elimu jumuishi, hasa kwenye vifaa saidizi vya kujifunzia na kufundishia. Tuone ni kwa namna gani wanafunzi hawa wanapata vifaa hivi ambavyo vinaendana na uhitaji wao, vifaa ambavyo havitowaongezea wenyewe ulemavu, bali vitawasaidia katika kupata elimu yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiwa ninahitimisha ninaiomba Serikali, pamoja na kushukuru kwamba, Mheshimiwa Rais ametoa ajira mpya za walimu, lakini pia, ione ni kwa namna gani walimu hawa wanakwenda kuongezwa, hasa walimu wa masomo ya sayansi, masomo ya amali na masomo jumuishi. Hii inaenda sambamba na kuona ni kwa namna gani walimu hawa wanapatiwa mafunzo ya elimu jumuishi ili waweze kwenda kufundisha wanafunzi hawa ambao wengi wao hawana changamoto na wale ambao wana changamoto katika shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kumalizia ninaomba kuunga mkono hoja. Ninawatakia Wizara kila la kheri katika utekelezaji wake. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ahsante kwa mchango wako. Sasa ninamwita Mheshimiwa Morris Joseph Makoi, ajiandae Mheshimiwa Lucy Damas Kombani.

**MHE. MORRIS J. MAKOI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kuniona. Ninaomba nichangie katika eneo la uangukaji wa taaluma kwenye elimu ngazi ya chini kwa sababu, ninaona wachangiaji wengi wameongea zaidi katika ngazi ya juu, ambayo Waziri, Mheshimiwa Mkenda, anaisimamia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuwe na wanafunzi wenye elimu nzuri katika shule za sekondari na vyuo ni lazima tuangalie taaluma katika ngazi ya chini kuanzia shule ya msingi mpaka, pengine *form four, form five* na *form six.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule zetu za sekondari za Kata nyingi kwa kweli taaluma inaanguka sana kutokana na ukosefu wa ufuatiliaji wa wale Waratibu Elimu na wale wengine ambao wanatakiwa kusimamia elimu katika ngazi hiyo. Kwa hiyo, ninaomba nimwambie Kaka yangu Waziri Profesa Mkenda pamoja na kazi kubwa sana ambayo anaifanya, pamoja na uwekezaji mkubwa sana ambao Rais Samia Suluhu Hassan amewekeza, bado kuna kazi kubwa sana ya kuangalia ngazi ya chini ili tuweze kwenda sambamba na malengo ambayo tunayatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, iko changamoto katika upande pengine wa mitihani ya darasa la saba, ambapo wanafunzi darasa zima wanaambiwa kwamba wame-*pass* na wanakwenda kujiunga na *form one*, lakini ukifuatilia wakati mwingine ukiwakuta *form two* kuna mwanafunzi ambaye hajui kusoma na kuandika. Sasa, katika mazingira haya huko mbeleni tunakwenda kutengeneza watu ambao hawawezi kuleta tija na pengine kutuletea matokeo ambayo tunatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninamwomba Waziri, pamoja na kwamba hili eneo pengine ni la TAMISEMI, lakini kama Wizara zinatakiwa zisomane, kwa sababu TAMISEMI wanamtengenezea ngazi ya chini na yeye anatengeneza ngazi ya juu, kama wanasomana wanaweza wakatengeneza wanafunzi ambao wanaweza wakaleta matokeo ambayo pengine tunayatarajia ama tunayahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni chakula, ninapenda kuzungumza habari ya upatikanaji wa chakula kwenye shule zetu kuanzia shule ya msingi na hata sekondari zetu hasa za Kata. Kumekuwepo na utaratibu wa Serikali wa wananchi ama wazazi kuchangia mchango wa chakula katika shule zetu. Katika hili jambo maelekezo yanayotolewa na Serikali lakini yamekuwa hayana nguvu sana, kwa hiyo kumekuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa vyakula katika shule za msingi na sekondari katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile Wakurugenzi hawawajibiki kuingilia au kufuatilia, wanafunzi wengi wamekuwa wakikaa wakiteseka na njaa na mwanafunzi yeyote ambaye ana njaa hawezi kujifunza na kuweka kitu kichwani. Ninatoa ushauri, kama itampendeza Waziri na anaweza kushauriana na Waziri wa TAMISEMI, kuna baadhi ya shule ambazo zina mashamba ama ardhi ya kutosha ambayo inazunguka shule, basi, Serikali ingeweza kuweka utaratibu yale mashamba yakalimwa rasmi kwa ajili ya kusaidia uzalishaji wa chakula kwa wanafunzi wa zile shule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaweza kusaidia kupunguza gharama ya michango kwa wazazi kwa mfano, kama mzazi alikuwa

anachangisha shilingi 100,000 kwa msimu, anaweza akachanga labda shilingi 20,000 ambayo inaweza ikawa rahisi kuipata, hasa wale wananchi wa maeneo ya vijijini. Uko utaratibu ambao mwanafunzi kabla ya kujiunga anatakiwa kuchangia moja kwa moja kwenye ile fomu anapojiunga shuleni, siyo wazazi wengi ambao wana uwezo wa kuchangia moja kwa moja, wengine wanashindwa kuchanga, lakini Serikali inaelekeza kwamba wanafunzi wote wawe darasani ama awepo shuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo walimu wakuu wanatii yale maelekezo, lakini mwishoni mwa siku kunakuwa na wanafunzi waliolipa na ambao hawakulipa. Kwa hiyo, kinachotokea ni kwamba, chakula kinanunuliwa kinatumika, kikiisha wanafunzi wanabakia hawana chochote, kwa sababu wale walioshindwa kuchangia mchango wao haukupatikana, kwa hiyo, kama kuna uwezekano basi mashamba ya shule yangetumika kusaidia kupunguza tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali inaweza kuweka utaratibu maalum ambao zile fedha zinaweza zikalipwa pengine kwa *control number* au moja kwa moja kwa Mkurugenzi na Mkurugenzi akawajibika kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapata chakula shuleni wakati wote, kuepusha kuunda Kamati za Vyakula za Shule ambazo na zenyewe zinasemekana kwamba zinajihusisha na uharibifu wa fedha na vyakula ambavyo vinapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo niongelee uchakavu wa miundombinu wa shule zetu za msingi na sekondari. Ninaomba nitoe shukrani nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais pamoja na Mheshimiwa Waziri Profesa Mkenda kwa kazi kubwa ambayo imefanyika katika Halmashauri ya Moshi, kwa ukarabati wa shule mbalimbali za msingi na sekondari na nyingine zimejengwa upya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama unavyojua shule nyingi za msingi na sekondari katika Wilaya ya Moshi zimejengwa miaka mingi zaidii ya miaka 50, zote zimefikia mahali zimekuwa na uchakavu wa wakati mmoja, kwa hiyo, ninaomba Waziri anapokuja kuhitimisha atuambie ni mpango gani, mkakati gani upo wa kuhakikisha shule zote za msingi

au sekondari ambazo ni chakavu zinaboreshwa, kwa sababu Serikali imepeleka fedha imejenga baadhi ya madarasa na baadhi ya shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unakuta tumekuwa kama tuna ubaguzi. Wapo wanafunzi wanaosoma kwenye vyumba vizuri na wanaosoma kwenye vyumba vya zamani ambavyo vingi vinavuja. Sasa, inakuwa kama pengine inakuwa ni ubaguzi na wale wanafunzi wengine wanaona kama wamepewa madarasa mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba wakati Waziri anakuja ninamwomba sana na ninajua anatoka Kilimanjaro, anafahamu hali ilivyo kule, atuambie Serikali inatusaidiaje kwa kweli katika hii hali kwa sababu ni jambo ambalo limekuwa sugu na tumejaribu kuangalia njia mbalimbali za wafadhili, wanatusaidia lakini bado tatizo ni kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunahitaji kabisa nguvu ya Serikali na nguvu ambayo inahitajika hasa wakati huu maeneo ya milimani mvua nyingi zilizonyesha zimesababisha uharibifu na ule uchakavu umezidi kwa sababu ya mvua ambazo zimenyesha kubwa. Kwa hiyo, ninaomba sana Waziri atakapokuja atusaidie kuangalia hilo jambo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia tuangalie utaratibu wa kuwepo na walimu. Tunajua kwamba ngazi ya sekondari walimu wako wa kutosha maeneo mengi, lakini kwenye ngazi ya elimu msingi walimu ni wachache sana. Unakuta shule moja ina walimu watatu au walimu wawili, unakuja mradi wa ujenzi wa darasa wanateuliwa kusimamia darasa, mwishoni anabakia mwalimu mmoja katika shule, sasa ufundishaji wa namna hiyo hauwezi kutoa matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kama inaonekana kwamba shule ina mradi na hakuna wasimamizi, basi hakuna sababu ya kumteua mwalimu aliyeko pale, ni bora akatafutwa mtumishi kutoka halmashauri akaja kusimamia ule ujenzi ili wale walimu wachache wawili watatu waliobaki shuleni waendelee kufundisha wanafunzi badala ya kuwekwa katika mazingira yale ambapo wanafunzi wanabakia kwenda shuleni wanazunguka kuanzia asubuhi mpaka jioni, wanarudi na hakuna ambacho kinaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, ninaomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri Profesa Mkenda, Naibu wake na wale wote wanaomsaidia katika majukumu haya. ninamshukuru vilevile, Rais Samia pamoja na Wasaidizi wake na hata washauri wake ambao wanamshauri kwa jinsi ambavyo anatusaidia kuhakikisha kwamba suala la elimu limepata kipaumbele na wanafunzi wetu wale ambao wamekuwa katika yale madarasa mapya na shule mpya ziizojengwa wanaendelea kunufaika na mchango huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Lucy Damas Kombani, ajiandae Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka. *(Makofi)*

**MHE. LUCY S. D. KOMBANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia. Kwanza ninawapongeza sana Wizara kwa harakati wanazoendelea kufanya kuhakikisha kwamba elimu ya Tanzania inazidi kukua siku hadi siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, ninapenda kumpongeza na kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa kufadhili walimu 150 kwenda India ili wakajifunze mafunzo ya ufundi stadi. Hili ni jambo kubwa sana kwa sababu tunajua kama tunataka kuendelea kwenye mambo haya ya sayansi na teknolojia, lazima tujifunze kwa nchi ambazo zimeendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda Waziri atakapotoa majibu yake atwambie uwiano wa kimkoa. Hawa watu 150 mikoa mingine imeshirikishwaje, kama yote imeshirikishwa ni walimu wangapi walioenda hususan Mkoa wangu wa Morogoro? Kwamba, kati ya walimu 150, hawa ni wangapi wamekwenda kupata haya mafunzo India? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuongezea kwenye hili, tunaelewa kwamba sayansi, teknolojia tunajifunza kwa nchi ambazo zimeendelea, ninamwomba Waziri ashirikiane na Mabalozi wa

Tanzania wa nchi mbalimbali kutafuta *exchange programmes*. Tunajua programu hizi zinawawezesha walimu na wanafunzi waende nje ya nchi kujifunza vitu mbalimbali na mara nyingi hizi programu wanagharamia zile shule husika za nje ya nchi. Kwa hiyo, ili kupeleka hili zoezi kwa uharaka na kuokoa gharama, basi wasaidie kufanya hivyo. Pia, hili zoezi la *exchange programme* mara nyingi huwa motisha kwa walimu na wanafunzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nililokuwa ninataka kuchangia ni suala la msawazo wa walimu. Walimu wengi sasa hivi wako mijini wanakimbilia mjini. Hali za vijijini siyo nzuri kabisa, utakuta kuna mwalimu mmoja na mwalimu huyu labda kasomea Kiswahili na *English,* lakini kutokana na uhaba, huyu mwalimu analazimika afundishe hisabati au sayansi, hiki kitu siyo kizuri kwa ustawi wa mwanafunzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kinaleta *stress* kwa mwanafunzi kinaleta *stress* kwa Mwalimu, Mwalimu ili afiche ile *weakness* yake sasa ana-*develop ego defence mechanism*. Utakuta likifika somo la hesabu anaingia na fimbo nyingi mno, kwa hiyo, yule mtoto akiona zile fimbo hata kuelewa kwenyewe inakuwa ngumu. Tuangalie huu msawazo wa walimu, walimu wapelekwe vijijini ili kila mwalimu afundishe somo alilolisomea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sula lingine ninalotaka kuongelea ni ustawi katika elimu kwa mtoto wa kijijini. Tunahimiza udahili wazazi wanaandikisha watoto, lakini kwa hali ilivyo kwa kijijini kwa kweli inakatisha tamaa. Utakuta mtoto kaanzishwa darasa la kwanza, inaanza kwanza mzazi hana hata uwezo wa kumnunulia viatu, lakini huyu mtoto utakuta anatembea umbali mrefu kwenda shuleni, akifika shuleni anakaa chini, hajamaliza kukaa chini anashinda na njaa siku nzima. Tujiulize je, huyu mtoto ndiyo mtu mzima ambaye atafikia vizuri hii dira tunayoiongelea ya 2050? Wizara iangalie namna ya kumrahisishia maisha huyu mtoto wa kijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ninataka kumaliza nalo na kushauri Wizara, Profesa ninatamani sana, katika mitaala yetu ifike mahali mitaala iendane na mazingira ya shughuli za

kiuchumi za jamii husika. Ninatokea Ulanga, kule tunayo madini mbalimbali tunachimba, lakini leo hii ukichukua rubi ukanichanganyia na chupa ninashindwa kutofautisha na Ulanga ni kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatamani sana, kwa mfano sisi Ulanga tunachimba madini, basi mtoto kuanzia elimu ya msingi afundishwe vile vitu vya pale. Ninatamani sana mkulima wa mpunga Malinyi, huyu mtoto aanze kufundishwa kuanzia umri mdogo. Mimi siyoni haja ya kuendelea kulisoma sikio na sehemu zake zote za ndani ambalo hadi leo hii halijawahi kunisaidia, hicho kitu basi tungejifunza kwenye kutambua labda mbegu ya mpunga imekaaje na inafanyaje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye sehemu za wafugaji hivyo hivo, watoto wajifunze kuanzia wadogo, kwamba ufugaji unakuwaje, ng'ombe huyu anatoa vitu gani, anatoa nyama. Ng'ombe huyu hatakiwi kuchapwa sana ngozi itaharibika na hizi ngozi tunatumia kwenye kutengeneza mabegi. Huyu mtoto afundishwe kwamba ng'ombe huyu hatakiwi kwenda kumlisha kwenye shamba la mtu mtatafuta ugomvi. Hivi vitu vingetusaidia sana zaidi ya kusoma vitu ambavyo ni vya sehemu ambazo hazituhusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ifikie mahali tusiwe na wananchi ambao vichwani tumelishwa vitu vya kigeni, halafu wale wageni wanatoka kule wanakuja kutumia rasilimali zetu ili kuendelea kimaisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufikia hapo, ninaomba niunge mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako na mchangiaji wetu wa mwisho kwa jioni ya leo, ni Mheshimiwa Asha Ramadhani Baraka.

**MHE. ASHA R. BARAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Kwanza kabisa ninamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, pia ninawashukuru wote, Mwenyekiti wa Kamati ya Elimu, Utamaduni na Michezo, ninamshukuru Waziri wa Elimu

Profesa Mkenda na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Wanu Ameir. Mawaziri wetu kwenye Wizara hii wametupa mchango mkubwa sana, tumeongozana nao sisi Wajumbe wa Kamati na tumeona ufanyaji kazi wao ni wa hali ya juu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia Chuo cha Usafirishaji - *NIT* halafu baadaye nitakwenda na *VETA* na nitakwenda na shule za *primary*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara ya kwanza Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya Rais wetu, Dkt. Samia Suluhu Hassan imeweza kusomesha marubani kwa mara ya kwanza pale chuo cha usafirishaji. Hawa marubani ambao tunategemea watakuwa wanarusha ndege zetu pamoja na Shirika la Ndege la Tanzania, lakini hapo nyuma marubani walikuwa wakisoma Nchi kama *South Africa*, Marekani, Uingereza na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yetu ni sikivu na imeangalia upande wa usafiri wa anga ikaamua kwamba waweze kusomesha marubani. Unajua kusomesha marubani nje ni gharama kubwa sana, lakini Serikali yetu ikafanya mchakato kwamba marubani wawe wanasoma hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitembelea kwenye kile chuo utakuta kuna ndege ziko pale, lakini ni ndege kwa ajili ya mafunzo. Kwa hiyo, marubani wanapata elimu na marubani hao tayari wameanza kurusha ndege. Tunaishukuru sana Wizara yetu ya Elimu kwa jambo hili ambalo ni kubwa sana kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitakwenda kwa upande wa *VETA*, nimetembelea baadhi ya vyuo vya *VETA*. Ukiangalia vyuo vya *VETA* Serikali inategemea kujenga vyuo vya *VETA* Wilaya zote nchi nzima, lakini hivi ambavyo vimejengwa sasa hivi vinapokea watoto wetu vijana tofauti tofauti. Kuna vyuo vya *VETA* vinapokea watoto mpaka vijana wenye ulemavu, utakuta kijana mwenye ulemavu labda hana mikono kabisa, lakini anatafutiwa mafunzo ya kuendesha maisha yake na kuweza kujikimu yeye binafsi pamoja na familia yake. Kwa hiyo,

ninatoa pongezi sana kwa Mawaziri wetu na ninatoa pongezi sana kwa Serikali yetu kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ninataka kuongelea kuhusu watoto. Utakuta watoto wetu wanaosoma shule hizi za *primary* au shule za awali, wanaamka alfajiri saa 11.00. Mimi huwa ninapishana nao wakati ninaenda kufanya mazoezi. Utamkuta mtoto amebeba begi kubwa lina madaftari mengi halafu yuko peke yake, wakati mwingine unamkuta mtoto wa kike anatembea barabarani umbali mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda tu kuishauri Wizara ifanye mchakato, hawa watoto kama wanaingia darasani wawe wanabebeshwa madaftari ambayo wanatumia kwa siku hiyo hiyo kuogopa kwamba yule mtoto amebeba mzigo mkubwa mgongoni na unakuta labda anakaa Kinondoni, shule yake ya *primary* anaenda kusoma Temeke, mfano kwa Dar es Salaam, au kwa hapa Dodoma labda yuko Dodoma Mjini shule yake anayosoma ni Chamwino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa, unamkuta yule mtoto anatembea kwenda kungoja basi, akienda kungoja basi halafu anakuwa amechoka begi limemlemea kabisa huku mgongoni. Ninaomba tu Wizara ifanye mchakato kwamba wale watoto wawe wanasoma shule jirani na sehemu wanayokaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishukuru sana Wizara ya Elimu kwa mambo makubwa ambayo wameyafanya katika nchi yetu kuhakikisha kwamba tunakuwa na elimu nzuri na bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa siku ya leo, kwa jioni ya leo, ninawatakia Wabunge wenzangu wote jioni njema kwa sababu mimi ndiyo mchangiaji wa mwisho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako.

Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa shughuli zetu katika Mkutano wetu wa Tatu, Kikao chetu cha Ishirini na Nne, tunawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliopata fursa ya kuchangia siku ya leo.

Waheshimiwa Wabunge, sasa ninaahirisha Bunge hadi kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.38 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 8 Mei, 2026 Saa Tatu Asubuhi)*

PARLIAMENT OF TANZANIA
BUNGE LA TANZANIA